

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Pili – Tarehe 1 Februari, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI

Na. 16

Ujenzi Usiokidhi Viwango Hospitali ya Wilaya ya Himo- Moshi Vijijini na Mawenzi

MHE. BETTYE. MACHANGU aliuliza:-

Kwa kawaida Mkandarasi anayejenga hospitali au jengo lolote lile hupewa ramani za michoro ya majengo husika lakini ni jambo la kushangaza kwamba majengo ya hospitali ya Wilaya inayojengwa Himo imeonesha upungufu mwingi, kwa mfano, vyumba vya maabara vilitakiwa kuwa saba (7) lakini vimejengwa vyumba viwili (2), idara ya macho vilitakiwa vyumba vitatu (3) lakini kimejengwa chumba kimoja (1) na katika hospitali ya Mkoa, Mawenzi jengo la *operation* la hospitali hiyo limejengwa katika viwango duni:-

(a) Je, Serikali itafanya nini kwa ujenzi huo ulio chini ya viwango uliokwishajengwa kwenye hospitali hizo mbili?

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kwa wahusika wa matatizo haya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya - Himo inatokana na kupandishwa hadhi kwa kilichokuwa Kituo cha Afya cha Himo. Ujenzi unaoendelea unalenga kuongeza majengo katika Hospitali hiyo kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ujenzi unafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza imegharimu shilingi milioni 175.

Awamu ya pili itagharimu shilingi milioni 319 ikihusisha ujenzi wa jengo la Utawala, Huduma ya Mama na Mtoto, jengo la X-Ray na uzio wa choo cha nje. Kwa mantiki hiyo ujenzi utakapokamilika jengo litakuwa na vyumba saba vya maabara na vitatu vya idara ya macho kwa kuzingatia ramani iliyotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Oktoba, 2011 Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilifanya ziara katika hospitali ya Mkoa wa Mawenzi akiwemo Mheshimiwa Grace Kiwelu Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kilimanjaro. Ziara hiyo ilibaini upungufu kadhaa ukiwemo ujenzi wa jengo la upasuaji kutozingatia michoro iliyotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kusababisha jengo kufanyiwa marekebisho kukidhi vigezo vilivyowekwa na Wizara. Mshauri wa ujenzi huo alikuwa ni Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA).

Baada ya kubaini upungufu huo Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilitoa maelekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro kuhakikisha upungufu uliojitokeza unafanyiwa kazi haraka. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilimuagiza Katibu Tawala huyo awasiliane na Katibu Mkuu, TAMISEMI ili awasiliane na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi ambayo wakala wa majengo iko chini yake.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na usimamizi mbovu wa Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) katika ujenzi wa jengo hilo, Wizara ya Ujenzi ilifahamishwa kuhakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya Mhandisi Mshauri aliyeshindwa kusimamia ujenzi wa jengo hilo kwa kuzingatia michoro iliyoidhinishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imejiwekea mkakati wa kuzifanya hospitali za Mikoa ziwe za rufaa na kwa kuwa hali ya kuzidiwa wagonjwa katika hospitali ya Mawenzi ni kubwa sana na kwa kuwa hospitali ya KCMC inazidiwa kutokana na ubovu wa tatizo la hospitali ya Mawenzi. Kwanza, je, Serikali iko tayari sasa kuharakisha mpango wake wa kuifanya hospitali ya Mawenzi kuwa ya rufaa katika mpango wake wa maendeleo 2012/2012?

Swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa wodi ya wanawake na majengo mengine ya hospitali ya Mawenzi umechukua muda kwa sababu ya kujengwa vipande vipande na kwa kuwa wanawake wengi wanaotaka kujifungua wanasongamana katika vitanda na hata kulala chini, Serikali haioni kwamba inapata hasara kwa sababu ya mfumuko wa bei yaani *inflation* na kwamba wanawake hawa hawatendewi haki?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, hili la hospitali za Mikoa kuwa hospitali za rufaa wala sio jambo la kujadiliana hapa kwa sababu kisera lilishakubalika kwamba hospitali zote za Mkoa ziwe hospitali za rufaa katika Mikoa kwa maana ya kwamba, tumeanzisha vituo vingi vya afya na zahanati na kadhalika. Kinachotakiwa tu hapa sasa ni kuingiza katika mipango ya Mkoa kwa maana ya *Regional Consultative Committee* ili tuweze kuona sasa *operationalisation* ya mawazo hayo mazuri ambayo anayazungumzia Mheshimiwa Betty Machangu.

Mheshimiwa Spika, la pili hili analozungumza la wodi hii na kwa bahati mbaya sana wakati ule tulipokwenda pale katika hospitali ya Mawenzi tulikuwa tumemuomba Mheshimiwa Betty Machangu pia aweze kufika, lakini kwa kweli kwenye majukumu aliyokuwa nayo alishindwa kufika, lakini ni kweli kabisa kwamba tumeiona hiyo wodi ya akinamama, ni wodi ambayo ukiangalia utafurahi wewe mwenyewe. Ni kubwa lakini nazungumza habari ya bilioni 12, sasa bilioni 12 na hela zinazopitishwa hapa ni hela kidogo sana, hela tunazojua kwamba zimepelekwa katika ile hospitali ni bilioni 1.3 sasa unaweza ukaona kwamba ni kweli kabisa anavyosema vifaa vitapanda bei lakini tatizo ninaloliona hapa ni ufinyu wa bajeti.

Hata hivyo, tuko tayari kukaa na Mheshimiwa Betty Machangu tufikirie wote kwa pamoja kwamba tufanye nini. Tatizo lililoko la msingi pale ni kwamba, kuna miradi mingi pale, kwa hiyo inafika mahali sasa una-*scatter* sasa *resources*, kwa hiyo, unashindwa kufika mahali. Nadhani ana mawazo wazuri na tunaweza tukakaa naye, tukaona kwamba tupeleke labda upande mmoja ili tuweze kuondoa tatizo hilo na ndivyote tulivyoliona na Mheshimiwa Grace Kiwelu wakati tulipokwenda pale.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Naibu Waziri kuhusu ujenzi wa hospitali ya Wilaya iliyopo Himo.

SPIKA: Hospitali gani tena?

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Himo ameitaja hapa kwenye swali la msingi la Betty Machangu, hiyo ni hospitali iliyoko katika Jimbo langu. Mwaka jana mwezi Januari nakumbuka niliuliza swali kuhusu ujenzi na kazi inayofanyika pale kwenye hospitali ya Himo na nikauliza hospitali hiyo itakamilika lini. Waziri alijibu kwamba ikifika mwezi wa Mei mwaka jana itakuwa imekamilika, lakini juzi nimepita pale nimekuta hakuna kinachoendelea, ningemwomba Waziri kama ana maelezo ni kwa nini hospitali ile haijaanza kazi?

Swali la pili...

SPIKA: Huwezi kuuliza maswali mawili Mheshimiwa, ni swali moja tu kwa sababu sio swali lako.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Lyatonga Mrema ni kweli kabisa kwamba, ndivyo tulivyokuwa tumedhania, kile kituo ni kituo ambacho kimekuwa *transformed*, ilikuwa sio kazi ambayo imeanza moja kwa moja, ni kwamba tulisema kituo hiki kibadilishwe matumizi, kiwe hospitali ya Wilaya. Pale kumekuwa kuna matatizo pia kwamba Mkandarasi na nafikiri labda ndiyo swali alilotaka kuuliza na hivi asubuhi, nimezungumza na DED na nikamwambia kwamba ni hatua gani zinazochukuliwa. Kesho watakwenda kwenye PMU watazungumzia zaidi kwa undani hii hali ya kusuasua ambayo Mheshimiwa Lyatonga Mrema anaizungumzia hapa.

Matumaini yangu ni kwamba, sasa Halmashauri kwa kutumia sheria na taratibu zilizowekwa watatafakari upya mkataba ambao wameingia pale kwa sababu ni kweli kama anavyosema kwamba *speed* inayokwenda pale ni ndogo na kwa hiyo, kushindwa kufikia lengo lile la kwamba sasa kituo kiwe kimeanza kazi.

MHE. ANNA K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi. Namwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa nimekuwa nafuatilia sana ziara yake aliyokuwa anaifanya katika baadhi ya Mikoa na kwamba yeye mwenyewe aliona kwamba majengo mengi yanajengwa chini ya kiwango na akawa anafoka. Je, Serikali leo inatoa tamko gani zito hapa ili hii tabia ya kujenga majengo mengi chini ya kiwango iachwe mara moja?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwamba amekuwa anafuatilia na pia nimetoka kule kwako, wanakusalimia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu hapa tulipofikia hatutaki hata siku moja tumsikilize Mbunge anazungumza hapa halafu tukampuuza, hatutampuuza kabisa Mbunge yeyote. Hiyo tunasema kabisa, Mbunge yeyote atakayeleta habari yoyote nataka niwathibitishie, hatutampuuza hata kidogo. Ni kweli kabisa kama anavyosema, hali tuliyoikuta katika *field* kule inasikitisha na inatisha. Hela zilizopitishwa hapa za TAMISEMI zilikuwa trilioni 2.5 ndizo zilizopelekwa kule, kwa nchi changa kama Tanzania ni kweli kabisa kwamba fedha hizi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa yeye anataka kujua kwamba tunasema nini. Wale watu wote ambao wamehusika na mambo haya ya ujenzi ambayo ni hafifu, tumetoa maelekezo kwa Tawala za Mikoa kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na tumewaandikia barua na tumeipeleka ripoti hiyo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mkuchika yuko hapa anasikia tunazungumza habari hiyo, wote wale ambao wamehusika na ujenzi hafifu tutawachukulia hatua kwa misingi ya sheria zilizowekwa. Hilo ndiyo tamko letu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Nilitaka kuwaeleza tofauti ya maswali ya nyongeza wanayouliza wengine na hili alilouliza Mheshimiwa Anna Kilango. Yeye amezungumzia jumla sasa, angeweza kuuliza habari ya Same kule, huyu hakujianda juu ya Same, lakini la ujumla analiweza kwa sababu ndiyo Sera yenyewe. Kwa hiyo, ndiyo utofauti wa maswali ya nyongeza. Nakushukuru kwa hilo swali. (*Makofi*)

Na. 17

**Fedha za CDCF Katika Halmashauri
za Tanzania Zanzibar**

MHE. AHMED JUMA NGWALI aliuliza:-

Mbunge kutoka Tanzania Zanzibar sio Mjumbe katika Halmashauri na Mabaraza ya Miji kwa mujibu wa Sheria za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar:-

Je, ni taratibu gani zilizotumika kupelekea fedha za CDCF kwenye Halmashauri hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mujibu wa Sheria za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinazohusu Halmashauri, yaani *The District and Town Councils Acts No. 4 of 1995 and The Zanzibar Municipal Councils Act No. 3 of 1995* Waheshimiwa Wabunge siyo miongoni mwa Wajumbe wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kupeleka fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwenye Halmashauri uko wa aina mbili; kwa upande wa Tanzania Bara Hazina hupeleka fedha hizo moja kwa moja kwenye akaunti ya Jimbo husika iliyofunguliwa kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Mfuko huo na fedha hizo husimamiwa kwa kufuata utaratibu kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 22 cha Sheria hii. Utaratibu huo umefafanuliwa katika kifungu cha 5(1) na 2(a) na (b) cha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Na. 16 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Zanzibar ambako ndiko swali la Mheshimiwa Mbunge linalenga, fedha kutoka Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hupelekwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais ya Tanzania ambaye naye huzipeleka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar kupitia Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano na hatimaye kwenda Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetathmini utaratibu wa kupeleka fedha kwenye Majimbo ya Tanzania Zanzibar na kubaini kuwa utaratibu huo ni mrefu na unawanyima Wabunge wanaotoka Zanzibar fursa ya kusimamia utekelezaji kwa kuwa wao siyo Wajumbe wa Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo Serikali itawasilisha Muswada wa kurekebisha Sheria hiyo ili kuweka utaratibu mbadala wa kupeleka fedha katika Majimbo ya Tanzania Zanzibar.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiwajibiki katika mamlaka ya fedha ya Zanzibar; je, Mkguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano anawajibikaje katika kukagua fedha hizi za CDCF Zanzibar?

Swali langu la pili; kwa kuwa ukaguzi wa fedha hizo za CDCF, Zanzibar haupo kikatiba wala kisheria, taratibu gani za sasa za kiharamu ambazo zinatumiwa katika kuzikagua fedha hizo?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri umeelewa swali lake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hiyo sehemu ya mwisho sikuisikia.

SPIKA: Ni ukaguzi, zinakaguliwaje hizo hela, *Controller and Auditor General* anazikaguaje wakati kule ni Zanzibar na huku vingine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali yote mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo *center* ya *controversy* yenyewe, tatizo lenyewe linalozungumzwa hapa ndilo hilo analoliulizia swali. Hapa nilieleza mlango unaotumika ni kwamba, inakwenda kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo akizungumza habari ya *accountability* pale Mheshimiwa Samia ndiye atakayesema kwamba hela hizi zimetumikaje pale. Kwa maana anachozungumza *Controller and Auditor General* ha-cross over akaenda upande wa pili kwa sababu hili ni suala la Muungano na kule kuna Hazina kwa maana ya Zanzibar, kwa hiyo inaishia hapo. Kwa hiyo, pale ndipo watakaposema kwamba hela zimetumikaje. Kwa kuona hilo la kwamba sasa Mbunge anashindwa kusimamia vizuri matumizi haya, ndiyo maana sasa hoja ni kwamba, tutafakari upya, Sheria irudi tena hapa Bungeni ili sasa tumpe Mheshimiwa Mbunge fursa ya kusimamia hela hizi na katika namna ambayo ni ya uwazi zaidi, lakini kwa sasa ndivyo tunavyofanya.

SPIKA: Ahsante, Muswada unakuja safari hii, kwa hiyo tunaendelea.

Na. 18

**Upungufu Mkubwa wa Watumishi Kwenye
Vituo Vya Afya Nchini**

MHE. SUZAN L. KIWANGA aliuliza:-

Ingawa viko vituo vingi vya afya vilivyojengwa vijijini lakini vimeshindwa kuanza kufanya kazi kutokana na upungufu wa watumishi wa kutoa huduma kwenye vituo hivyo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi na mrefu wa kukabiliana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wananchi wake, imefanya jitihada kubwa za kujenga Vituo vingi vya Afya na Zahanati Vijijini. Aidha, ni kweli kuwa upungufu wa watumishi ambao umesababisha baadhi ya vituo vya afya na zahanati zilizojengwa na kukamilika katika maeneo ya Vijijini kushindwa kuanza kutoa huduma. Katika kukabiliana na upungufu huo Serikali imefanya yafuatayo:-

(a) Kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi wa fani mbalimbali za afya mwaka hadi mwaka kuanzia mwaka 2007 hadi 2011. Mfano, fani ya uuguzi, udahili uliongezeka kutoka 1,645 mwaka 2007/2008 na kufikia 3,136 mwaka 2010/2011 na fani ya sayansi shiriki, udahili umeongezeka kutoka 450 mwaka 2007/2008 na kufikia 2,257 mwaka 2010/2011.

(b) Kuondoa urasimu katika ajira kwa kuwapangia vituo wahitimu kutoka vyuoni kwa kuwapeleka katika Halmashauri kulingana na mahitaji na vibali vinavyotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hivi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inawapanga watumishi wa fani za afya moja kwa moja kulingana na mahitaji ya watumishi hao na uwepo wao katika soko la ajira. Tangu mpango wa MMAM uanze mwaka 2007, jumla ya wataalam 11,000 wa kada mbalimbali za afya walipangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Mfano, idadi ya wataalam waliopangiwa vituo vya kazi iliongezeka kutoka 4,812 kwa mwaka 2007/2008 na kufikia 6,000 mwaka 2010/2011.

(c) Kuweka vivutio zaidi katika maeneo ya vijijini ambako kuna mazingira magumu ya kazi.

(d) Sekretarieti za Mkoa na Halmashauri kuwahamishia watumishi kutoka maeneo yenye watumishi wengi na kuwapeleka katika maeneo yenye upungufu wa watumishi ili kupunguza tatizo hili la watumishi.

(e) Kuhimiza waajiri kuwasilisha mahitaji ya rasilimali watu wakati wa kuandaa bajeti na kupata kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi ameweka kipengele si kwamba ataongeza vivutio zaidi katika maeneo ya vijijini ambako kuna matatizo na mazingira magumu ya kazi. Je, ni vivutio gani ambavyo vimewekwa angefafanua hapa ambavyo vinatoa au ni nyongeza ya posho au ni vivutio gani kwa watumishi hao kwa sababu bado kuna mazingira magumu ya kazi? Kwa kuwa niko katika Kamati ya LAAC na naona hali halisi kule vijijini, kwa hiyo, ni bora angeainisha hivyo vivutio.

Pili, hivi sasa kuna wimbi kubwa la watumishi ambao wakipangiwa vijijini au tayari wako vijijini wanahama kutokana na sababu za msingi ama mazingira magumu, kwa mfano, barabara hamna, maji hamna, umeme hamna, hamna huduma za simu na vile vile watumishi hawa wanapenda kujiendeleza. Kwa kuwa katika maeneo haya hakuna huduma hizo, je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka huduma hizo ili kuzuia wimbi la watumishi hao kutokua katika maeneo hayo kuwahudumia wananchi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hapa Waheshimiwa Wabunge tumeelezwa Mkoa ule wa Rukwa, jinsi ambavyo wao wenyewe waliji-*mobilize*, wakakaa, wakaangalia utaratibu. Daktari akipelekwa pale kwenye ule Mkoa, wao wenyewe kwa Mfuko wao, nisije nikaulizwa hapa iko wapi kwenye bajeti. Daktari akienda pale anapata shilingi milioni moja. Hili jambo si jambo dogo hata kidogo. Akienda Mkunga pale anapata shilingi laki saba kwa kuanzia tu. Wale wananchi wanaweza wakamsaidia mahindi ya kuanzia na chakula cha kuanzia. Hilo jambo si dogo hata kidogo kwa mtumishi anayeanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaweza tu wakampa moyo wa ushirikiano na mshikamano pale, wakamsaidia kubeba masanduku yake wakati anapokwenda kijijini pale. Hilo jambo si dogo hata kidogo. Namna tu mnavyompokea pale, Daktari wetu karibu hapa, hilo jambo si dogo hata kidogo wala halihitaji kuingia kwenye bajeti hapa. Kwa hiyo, tunayo mifano mingi sana na hivi ndivyo ambavyo tunasema na sisi tunajitahidi. Lakini nimetoka Ludewa, Filikunjombe yuko hapa, tumepeleka boti pale kwa sababu kwa kweli ni matatizo makubwa sana kupeleka dawa pale na Madaktari na nini. Kupeleka boti pale si jambo dogo hata kidogo, Ndugu yangu Kiwanga ni jambo kubwa sana hilo.

Mheshimiwa Spika, habari ya *social services* zinazozungumzwa hapa, barabara tumezijenga mnaona zinapitika, sasa hivi tumeweka *morum* mle, hilo si jambo dogo hata kidogo. Sasa hivi tunatumia redio zile, tunatumia redio za mkono tunazungumza kama zahanati kule kuna mama anataka kujifungua amezidiwa, kuna *complication* imetokea pale, tunapeleka *ambulance* inakwenda kumchukua kwa kutumia simu za upepo hilo jambo si dogo. Yapo mambo mengi ningeweza nikaeleza hapa ambayo tunayafanya. Lakini namshukuru Mheshimiwa Kiwanga kwamba ametuambia hivyo, tutajitahidi kwa kadri tunavyoweza kuona kwamba mazingira ya kazi kwa Madaktari wetu, mazingira ya kazi ya Manesi na watumishi wengine wote wa Serikali yanakuwa mazuri ili kuwa kivutio kule wanakokwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwaomba sana hawa Madaktari, walimu wote, watumishi wanaokwenda kule, wawahurumie watu wetu. Pia kule kuna matatizo, wawasaidie kule na sisi wakati huo tukiendelea kuboresha mazingira ya kazi. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI. Pia nataka kuongezea kwamba Serikali kwa kuona umuhimu wa watumishi ambao wanakwenda katika Wilaya zile ambazo tunazona ni za pembezoni, imeanza ujenzi wa nyumba kumi kumi. Kwa kuanzia, tumeanza na Wilaya 18 na pia tumetoa maelekezo kupitia sera yetu ya malipo na motisha. Tumetoa maelekezo kwa mamlaka za ajira kuangalia

ni vivutio gani. Tumetoa *package* ambavyo wao wanaweza wakazitoa katika maeneo hayo na pia tumeanzisha Bodi ya Maslahi na Tija ambayo itatushauri kwamba ni *incentive* ipi tutoe katika maeneo husika. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Jibu limejitosheleza. Sasa naingia Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla atauliza swali hilo.

Na. 19

Shamba Lenye Mgogoro Mvomero

MHE. AMOS G. MAKALLA aliuliza:-

Shamba lililokuwa la ushirika na kumilikiwa hivi sasa na Mheshimiwa Fredrick T. Sumaye, lililoko Kijiji cha Mvomero lina mgogoro ambapo wananchi wanataka wagawiwe kwa ajili ya makazi na kilimo:-

(a) Je, ni utaratibu gani uliotumika kumuuzia Mheshimiwa Fredrick T. Sumaye, shamba hilo badala ya kuwapa kipaumbele wananchi mwaka 2010?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kutokana na ukweli kwamba Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kuahidi kushughulikia kero hiyo?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Jimbo la Mvomero kwa jitihada anazofanya kufuatilia na kuzitafutia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi wa Jimbo lake.

Baada ya pongezi hizo napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa shamba lenye hati Na. 21919 lililoko katika Kijiji cha Mvomero, Wilaya ya Mvomero lenye ukubwa wa ekari 326 linalomilikiwa na Bibi Esther Sumaye. Kabla yake shamba hilo lilikuwa linamilikiwa na ndugu Onasaa Waryaeli Kisanga na Mesaki Josiah Ndanshau wakitumia jina la *Mvomero Rover Farm Limited* kwa hati Na. 21919.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizoko kwenye Wizara yangu zinaonesha kuwa awali shamba hilo lilikuwa likimilikiwa na *Mvomero River Farmers Limited* ya Morogoro kuanzia 1978 hadi Julai 1985 lilipohamishiwa kwa Kampuni ya *Wami & Magole Farmers Cooperative Society Limited* ya Morogoro. Mnamo Machi 1996 Kampuni ya *Wami & Magole Farmers Cooperative Society Limited* ilibadili jina na kuitwa *Morogoro Farmers Primary Society Limited*. Aidha, tarehe 27 Novemba, 2001 *Morogoro Farmers Primary Co-operatives Limited*. Walimuuzia Ndugu Esther Sumaye shamba hilo na baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru kwa Serikali uhamishaji wa miliki (*Transfer*) ulikamilishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa Kifungu cha 61 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bibi Esther Sumaye anamiliki shamba hilo kwa mujibu wa Sheria na kuliendeleza kwa kuzingatia masharti ya hatimiliki, Serikali inaheshimu haki zake na hivyo haitaweza kumnyang'anya kwani itakuwa ni ukiukaji wa haki za kumiliki mali zilizoainishwa kwenye Ibara ya 24(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa shamba hili liliombwa mwaka 1999 na Kijiji cha Mvomero

chenye wakazi 12,000 na walikuwa tayari pale pale Makao Makuu ya Wilaya na makazi kwa wananchi wale 12,000. Ni taratibu gani zilizotumika kuwakataa wananchi 12,000 na akapewa Esther Sumaye? (Makofi)

Swali la pili, kwa kuwa katika kampeni za uchaguzi Rais mwaka 2009 ambaye Kikatiba ndiyo mwenye mamlaka ya kufuta hati yoyote ile na umiliki wowote. Awaahidi wananchi wa Mvomero kwamba tukichaguliwa atashughulikia suala hilo. Majibu ya Waziri ndiyo kumaanisha kwamba, anapingana na kauli ya Rais juu ya kushughulikia tatizo hili? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba mwaka 1988 wananchi wa Kijiji cha Mvomero waliomba kwamba shamba hilo wapewe wao. Yaani lichukuliwe kwa mmiliki na kukabidhiwa wao. Hata hivyo, maombi yale yaliwasilishwa na Mbunge aliyekuwepo wakati huo na katika kumbukumbu zetu hazioneshi kwamba baada ya hapo ni hatua zipi zilichukuliwa na Mheshimiwa Mbunge. Sasa kama kuna pia ombi lililotolewa mwaka 1999, kwa bahati mbaya Ofisi yangu haina taarifa ya kwamba kuna ombi lililofuata baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kusema kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaheshimu haki ya mtu yeyote katika nchi hii kumiliki mali, kwa sababu hiyo ni haki yake ya msingi. Sasa kama wananchi waliomba kwamba wapewe shamba hilo na mwenye mali hakupenda kuwapa badala yake akamwuzia mtu mwingine, ulikuwa ni uamuzi wake mwenyewe ambao hatuwezi kuingilia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba angelishughulikia suala hilo. Wizara yangu haipingani na kauli ya Mheshimiwa Rais. Tunachosema ni kwamba Mheshimiwa Rais katika kulishughulikia suala hilo, moja ya hatua anazochukua ni kupata taarifa juu ya hali ya shamba hilo. Kama akithibitisha kwamba mwenye shamba anamiliki kihalali na kwamba analiendeleza kwa mujibu wa sheria huwezi kumnyang'anya kwa sababu hajakiuka kifungu chochote. (Makofi)

Na. 20

Kufuta Hati za Mashamba ya Mkonge Kibaranga

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Mwaka 2008/2009 Serikali iliahidi kufuta hati za mashamba ya mkonge yasiyoendelezwa kwa kuanzia na shamba la Kibaranga na kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imekamilisha taratibu zote husika:-

Je, hatua ya kufuta hati hizo imefikia wapi?

SPIKA: Swali gani, mbona hujataja?

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Swali langu Na. 20 Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inathibitisha kuwa ilipokea mapendekezo ya kufuta Hatimiliki za mashamba ya mkonge yasiyoendelezwa kwa muda mrefu kutoka Wilaya ya Muheza likiwemo shamba la Kibaranga lenye hati Na. 4856 na ukubwa wa ekari 5,730. Baada ya kuyachambua mapendekezo hayo,

Wizara iliridhika kuwa yalikiidhi vigezo vya ufutaji hatimiliki kwa mujibu wa Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 inayoruhusu Serikali kubatilisha miliki ya ardhi yoyote ambayo mmiliki ameshindwa kutimiza masharti ya kuendeleza. Baada ya uhakiki kukamilika mapendekezo yaliwasilishwa Ikulu kwa Mheshimiwa Rais kwani kwa mujibu wa Sheria ndiye mwenye mamlaka ya kuidhinisha ufutaji wa hati miliki ya ardhi. Tunayo matumaini kuwa muda si mrefu mchakato huo utakamilika na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kujulishwa uamuzi wa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nimshauri Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Muheza kuwa wawe na subira wakati Serikali ikishughulikia mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kero ya wawekezaji kutwaa ardhi na ama kubadilisha matumizi bila kuzingatia Sheria na wakati mwingine kugawa vipande na kuuza imeanza kushamiri hapa nchini. Utaratibu huo unakwenda kinyume kabisa na malengo ya Serikali ya kutenga ardhi kwa ajili ya kuvutia wawekezaji ili kuzalisha mali na hivyo kuinua pato la Taifa. Natoa wito kwa Viongozi wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya kufanya uhakiki wa matumizi ya ardhi kwenye maeneo yao na pale wanapobaini ukiukwaji wa masharti ya hati miliki walete mapendekezo Wizarani kwangu ili Serikali itwae ardhi hiyo na kumilikisha wawekezaji wenye nia thabiti ya kuendeleza kwa manufaa ya Taifa.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya uhakika ambayo kwangu mimi ni kama mwongozo. Pia naomba nimshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Tanga kwa jinsi alivyojituma kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi hasa katika shamba la Kibaranga.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa ya migogoro inatokana na hili ambalo Mheshimiwa Waziri hapa amesema la wawekezaji kutoa ardhi na kujichukulia madaraka hata kabla hawajapewa hati ya kumiliki ardhi. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri akubali pendekezo kwamba jibu hili alitoe kama mwongozo kwa Halmashauri, kwa Wakuu wa Wilaya na Bodi ya Mkongwe kwa sababu wao ndio wasimamizi lakini wanawaachia wawekezaji wanafanya fujo na kuhatarisha maisha ya wananchi; je, atalipokea hilo?

La pili, ni mgogoro ambao umezuka hivi karibuni katika shamba moja la Kumburu, hapo hapo jirani na shamba la Kibaranga. Maisha ya watu yalikuwa yapotee pale, lakini Mkuu wa Mkoa amesaidia kutuliza. Kinachotushangaza ni kwa namna gani shamba hili la Kumburu liliweza kufutiwa hati na ikatolewa hati mpya mwaka 2005 kinyume cha utaratibu huo ambao sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Muheza tumekuwa tukiufuata. Wamepataje hati hiyo Mheshimiwa Waziri unaweza ukatuambia na wametumia utaratibu gani kuweza kufanikisha kupata hati mpya?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kwa kupokea majibu yetu na ushauri wake wa kwamba jibu hili litolewe kama mwongozo kwa uongozi wa Mikoa na Wilaya pamoja na Viongozi wa Mashamba ya Mkongwe litatekelezwa ipasavyo:-

Ushauri wake huo Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba unakwenda sambamba kabisa na maelekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi yaliyotolewa kwetu baada ya mkutano wake uliomalizika hivi karibuni.

Swali la pili, ni kwamba, shamba la Kumburu lilifutiwa hati mwaka 2005 bila kufuata taratibu na kummilikisha mtu mwingine, tutafuatilia kutafuta taratibu zilizotumika na majibu tutampatia Mheshimiwa Mbunge na tutachukua hatua ipasayo ikiwa itabainika kwamba taratibu za utoaji ardhi ile na kummilikisha mmiliki mwingine hazikuzingatia sheria.

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa wa Korogwe.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Ndiyo Mheshimiwa Spika, naitwa Ngonyani.

SPIKA: Ngonyani!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Naam. Kwa kuwa tatizo la Kibaranga, Muheza linafanana kabisa na la Korogwe Vijijini hasa kwenye mashamba ya Mswaha, Gomba, Kerenge Kibaoni, Magunga pamoja na Hale. Je, Serikali ina mpango gani ili wananchi wa mashamba hayo wapewe maeneo ya kulima?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini ningeomba arudie sehemu ya mwisho ya swali lake.

SPIKA: Kasema kwa nini utaratibu wa wananchi wapewe mashamba ya kulima, hayo aliyoyataja.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imefanya kwamba wao ndiyo wameanzisha hatua hiyo ya utoaji wa ardhi ile kutoka kwa mwekezaji ambaye ameshindwa kuiendeleza. Tunamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya pamoja na Mkoa ili kuhakiki matumizi ya mashamba hayo kwa kuoanisha na masharti yaliyoko katika hati miliki za mashamba na ikiwa wataridhika kwamba hayatumiki ipasavyo, basi walete mapendekezo Wizarani ili Mheshimiwa Rais aweze kushauriwa kwamba mashamba yale yatwaliwe na Serikali na kumilikishwa wananchi.

Na. 21

Ulinzi na Usalama wa Nchi

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Ulinzi na usalama wa nchi yetu unajumuisha ulinzi wa majini ambao Tanzania Zanzibar kupitia kikosi chake cha ulinzi wa maji kinafanya kazi ya kulinda Bahari ya Tanzania.

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itasaidia vipi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vifaa kwa kikosi cha KMKM ili kufanikisha kazi hiyo muhimu kwa nchi yetu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatibu Kai Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tisa (9), Ibara ya 147(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaruhusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuunda na kuweka majeshi ya aina mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania. Ulinzi huu unajumuisha maeneo ya bahari na maziwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jukumu la ulinzi wa majini katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekelezwa na JWTZ kupitia Kamandi ya Jeshi la Wanamaji (Navy). Inapotokea tishio lolote la kiulinzi au kiusalama katika maji ya Tanzania JWTZ huweza kuvijumuisha vyombo vingine kama KMKM au *Police Marine* katika kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutoa mafunzo kwa maafisa na askari wa KMKM kupitia kozi mbalimbali zinazotolewa katika shule ya Ubaharia (*Navy Training School*) iliyopo Makao Makuu ya Kamandi ya Wanamaji Kigamboni, Dar es Salaam. Vile vile kikosi cha KMKM wamekuwa wakipata nafasi ya kutumia cherezo (*slip way*) iliyopo Navy Kigamboni kutengeneza meli zao pasipo gharama yoyote isipokuwa kugharamia vipuri.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Naomba sasa nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa Zanzibar ni nchi iliyozungukwa na maji pande zote na kwa kuwa usalama wa Zanzibar unatokana na Bahari. Je, Serikali ya Muungano haioni umuhimu wa kuiondolea ugumu SMZ kwa kununua vifaa vya ulinzi ili kuimarisha usalama wake zaidi?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa usalama wa Baharini umekumbwa na changamoto kubwa ya maharamia wa Kisomali na kwa kuwa, maharamia hawa wamekuwa wakifika hadi bahari ya Tanzania. Je, Serikali ya Muungano ina mikakati gani ya makusudi ya kusaidia kikosi cha KMKM?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba, jukumu la ulinzi wa maji ya nchi yetu ni jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa maana hiyo basi, Kamandi yetu ya wanamaji, yaani Navy, inafanya jukumu lake la ulinzi kote. Sio upande wa Tanzania Bara peke yake. Pia kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, uwezo wa Navy kwa sasa kuisaidia KMKM uko katika nyanja hizo mbili; moja, ni kuwapa mafunzo pale Kigamboni katika chuo chake na la pili ni kuwasaidia kutumia chelezo ili kutengeneza vifaa vyao. Uwezo wa Navy kwa sasa kuwasaidia KMKM kivifaa bado ni mdogo kwa sababu Navy yenyewe ina changamoto ya kupata vifaa vya kujitosheleza wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa mapambano dhidi ya uharamia tunao na kama taarifa ilivyotolewa ni kwamba, mapambano hayo sasa yanakwenda vizuri kwa sababu, tumepata uwezo wa kuiboresha Navy zaidi kivifaa ili iweze kutimiza jukumu lake hili la msingi. Vilevile tuna makubaliano ambayo tumeingia na nchi rafiki ikiwemo Msumbiji na Afrika Kusini ya kusaidiana katika mapambano dhidi ya uharamia, jambo ambalo kwa kweli litatusaidia sana katika mapambano ya uharamia.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kurudia kusema kwamba, sio rahisi kwa Navy kuwapa KMKM vifaa kwa sababu Navy yenyewe bado haijitosheleza, lakini tutaendelea kusaidiana nao katika upande wa mafunzo na hatimaye uwezo utakapokuwa mzuri zaidi tutaangalia uwezekano wa kuwasaidia.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa linahusu maharamia wa Kisomali. nashukuru, limejibiwa.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi akisema kwamba, mamlaka ya kuunda vikosi vya kijeshi ni mamlaka ya Jamhuri ya Muungano. Ningependa kujua ni mamlaka yapi yaliyoiruhusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuunda kitu kinachoitwa Vikosi Maalum na kumfanya Rais wa Zanzibar kuwa Kamanda Mkuu wa Vikosi Maalum, hivyo, kuifanya nchi yetu kuwa na Maamiri Jeshi wawili nchi moja? *(Makofi)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina Maamiri Jeshi Wakuu wawili. Nchi yetu ina Amiri Jeshi Mkuu mmoja tu ambaye, ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba ya Zanzibar, ndio inayompa Mamlaka Rais Wa Zanzibar, kuunda Idara Maalum ambazo ndizo hizo KMKM, Mafunzo, na kadhalika. Kutokana na mamlaka aliyopewa Rais wa Zanzibar ya kuunda Idara Maalum, hakufanya kosa kwa sababu ametumia Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Na. 22

JWTZ Kufanya Kazi za Jeshi la Polisi

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Je, ni wakati na mazingira gani Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) linawajibika kufanya kazi za ndani badala ya Jeshi la Polisi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna wakati au mazingira yatakayolifanya Jeshi la Ulinzi wa Tanzania, kufanya kazi za ndani badala ya Jeshi la Polisi. Bali Jeshi la Ulinzi la Tanzania linaweza kusaidia pale Jeshi la Polisi linapoelemewa na kuombwa kufanya hivyo. Msaada wa JWTZ kwa shughuli za ndani, si katika masuala ya usalama wa ndani tu bali jeshi linaweza kuombwa kusaidia katika shughuli nyingine inapobidi kama vile shughuli za uokoaji, ujenzi, hususan nyakati za dharura na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Majeshi ya Ulinzi yanatumika pale panapotokea uvunjifu wa amani, dalili za uvunjifu wa amani na inapodhihirika na Mamlaka za kiraia kuwa Polisi wameelemewa. Majeshi ya Ulinzi yanapotoa msaada huo, hayachukui nafasi ya mamlaka za kiraia, isipokuwa yanasaidia kudumisha sheria na amani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu namba 21 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 2002, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaruhusiwa kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia pale ambapo kuna machafuko, ghasia au uasi, pindi linapooombwa na mamlaka za kiraia pale ambapo mamlaka hizo haziwezi kuzuia au kumaliza vurugu, machafuko au maasi hayo. Utaratibu unaotumiwa na JWTZ katika kutoa msaada kama hiyo, umebainishwa kwenye Kanuni ya 15 ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya Kwanza (Utawala) inayozungumzia majukumu ya Majeshi ya Ulinzi katika kusaidia mamlaka za kiraia.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa, Mtanzania yeyote ana haki kufanya kazi popote Tanzania kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa, wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe, walikuwepo *Mbezi Beach* kwa shughuli za uvuvi mnamo mwishoni mwa mwezi wa Tisa na wakavamiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kitendo hiki kinawadhililisha wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe na kwenda kinyume na Sheria Nambari 21, Kifungu 21, Sheria ya mwaka 2002, Sura ya 192?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri, haoni kitendo hiki cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kuwavamia wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe, kinakwenda kinyume na taratibu za ulinzi wa Taifa letu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba, Jeshi kuna wakati linaombwa na Mamlaka nyingine ziwe za kiraia au majeshi mengine kusaidia katika *operation* maalum. Ninazo taarifa kwamba Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, liliwahi kuombwa kusaidia mamlaka hizo katika kupambana na wavuvi haramu. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge, nitamwomba sana, yanapotokea matukio kama hayo kama anathibitisha kwamba wavuvi hao hawakuwa wanatumia zana haramu, alipaswa kutoa taarifa kwetu na tungezuia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukweli unabaki palepale, sidhani kama wanajeshi wa Tanzania wanaweza wakawavamia wavuvi tu ambao hawana kosa lolote na kuwanyang'anya mali zao bila sababu. Napenda nirudie kusema kwamba, endapo matukio kama haya yanatokea na tunao ushahidi kwamba wameonewa, basi ni vyema tupate taarifa ili tuchukue hatua. Lakini kama wanatumia nyenzo za uvuvi haramu, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane naye katika kuwaelimisha wavuvi hawa kuacha kutumia nyenzo kama hizo. (*Makofi*)

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi swali la nyongeza. Kwa kuwa, katika vurugu zilizotokea Mbeya mwishoni mwa mwaka jana, Jeshi la Polisi lilishindwa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba lilielemea. Kwa kuwa pia, Jeshi la Ulinzi kupitia JKT nalo pia lilielemea. Je, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi pamoja na

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, wata kubaliana na mimi sasa kwamba, kumbe suluhu ya migogoro yote sio kutumia nguvu bali ni kushirikisha wananchi katika njia za amani? *(Makofi)*

SPIKA: Swali lako liko nje kabisa, lakini Waziri naomba ujibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, inapotokea machafuko ambapo Jeshi la Polisi linaona limeelemewa, wanao wajibu wa kuomba msaada kutoka Jeshi la Ulinzi kwa taratibu ambazo zipo kisheria. Baada ya tukio lile la Mbeya, Mkuu wa Mkoa alitumia utaratibu huo wa kuomba msaada kwa kuniandikia barua ya kuomba msaada wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, huwezi kwenda katika mazungumzo wakati tayari kuna fujo zinazotokea. Wananchi walikuwa wananyang'anywa mali zao, maduka yalikuwa yanataka kuchomwa moto, magari yanataka kuchomwa moto, huwezi kusema sasa utatumia mazungumzo. Ni lazima utulize kwanza, halafu ndio muanze mazungumzo. Kama ilivyokuwa, baada ya kupata ombi hilo tulitumia JKT tu kabla ya Jeshi la Wananchi halijaingia na wao waliweza kuzuia, waliwasaidia Polisi kuzuia machafuko yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, waliofanya machafuko yale yaweze kutulia ni hao JKT. Baada ya hapo ilikuwa sasa ni jukumu la mamlaka za kiraia kupitia Mkoa, kuendelea na mazungumzo ili kuona kwamba, mambo kama hayo hayatokei tena.

Na. 23

Utendaji Kazi wa Bohari Kuu ya Dawu (MSD)

MHE. HENRY D. SHEKIFU aliuliza:-

Yapo malalamiko makubwa kuhusu utendaji wa MSD hususan uhaba wa dawu, uharibifu wa dawu na vifaa vya hospitali, urasimu wa kupata dawu, kuhodhi fedha za hospitali za Wilaya na Mikoa na kadhalika:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa muundo wa MSD (*Organisation Structure*) umepitwa na wakati na unapaswa kutazamwa upya?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Bohari ya dawu na Halmashauri zote nchini, imeendesha zoezi la makadirio ya mahitaji ya dawu, vitendanishi na vifaa tiba. Lengo ni kuboresha upatikanaji wa mahitaji hayo kwa wakati muafaka. Vilevile Serikali inatekeleza mpango wa kusambaza dawu na vifaa tiba hadi ngazi ya zahanati na vituo vya afya. Mpango huu ulifanyiwa majaribio katika Mkoa wa Tanga na katika mwaka wa fedha 2011/2012 mpango huo unatekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Lindi, Dar-es-Salaam, Pwani, Shinyanga, Manyara, Rukwa na Ruvuma. Mpango huu utaenezwa nchi nzima kwa awamu. Aidha, katika kuboresha huduma ya uhifadhi na usalama wa dawu, Bohari ya Dawu (MSD) inajenga maghala manne katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mbeya, Dodoma na Tabora kwa msaada wa wafadhili.

(b) Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wadhamini wa Bohari ya Dawu, imetekeleza ushauri wa Serikali wa kurekebisha muundo wa utendaji wa Shirika kwa kuanzisha usimamizi wa huduma Kikanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kurugenzi ya Huduma kwa Wateja na Mauzo katika Kanda ya Mashariki inayosimamia Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mtwara na Tanga. Kanda ya Kaskazini inayosimamia Mikoa ya Mwanza, Tabora na Kilimanjaro na Kanda ya Kusini inayosimamia Mikoa ya Dodoma, Iringa na Mbeya.

Kurugenzi nyingine ni pamoja na Kurugenzi ya Mahusiano ya Kitaasisi, *Corporate Affairs*, Kurugenzi ya Fedha na Kurugenzi inayoshughulikia ununuzi, ugomboaji wa bidhaa, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa ni kwamba, dawa hazipatikani zinapoagizwa kutoka *Central Store*, yaani Bohari Kuu, matokeo yake ni kwamba, MSD wanahodhi fedha za Halmashauri pamoja na Hospitali. Kwa utaratibu huu ulioelezwa naamini tatizo linatokana na ukiritimba wa MSD. Kwa nini, Serikali haichukui hatua ya kujenga ushindani kule MSD ili dawa zipatikane kwa urahisi na ziagizwe kwa wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upo uharibifu mkubwa kwa kuagiza dawa ambazo hazifikii viwango na vifaa ambavyo havifikii viwango. Je, Serikali imeshafanya tathmini kuona athari zilizotokana na jambo hili? Kwa kuwa, waliogiza, waliogiza kwa makusudi, je, baada ya kutambuliwa wamechukuliwa hatua gani kwa kuagiza bidhaa hafifu ambazo zina madhara kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, la kwanza aliuliza, kwa sababu kumekuwepo na ukiritimba wa MSD kuuza dawa peke yake na kusambaza kwenye Sekta ya Serikali; je, hatuwezi tukaanzisha ushindani?

Mheshimiwa Spika, naomba nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na kwamba, dawa zinatoka MSD ambazo tunalipia sisi kama Serikali katika Vituo vyetu vya Afya kuna pesa ambazo zinatokana na michango mbalimbali. Kwa hiyo, hizi pesa ambazo zinatokana na michango mbalimbali kwa mfano Bima ya Afya, mchango wa papo kwa papo pamoja na Bima ya Afya ya Jamii tunashauri kwamba, wanaruhusiwa kununua dawa kutoka kwenye sehemu nyingine. Pamoja na kwamba, sasa hivi hakuna huo ushindani, lakini ushindani ambao wanaanza kuupata sasa hivi ni huo ambao kwamba, Hospitali zinakuwa na pesa nyingi sasa kwa hiyo, wataanza kununua dawa, hivyo, biashara yao inaweza ikapata athari kidogo.

Kwa hiyo, ndio sababu tuliamua kwamba, tuanze kufanya kwanza uchambuzi wa kujua mahitaji ya Hospitali, halafu pamoja na kuhakikisha kwamba MSD inapeleka dawa mpaka kwenye Vituo vya Afya na Zahanati, ili tuangalie kama kutakuwa na maboresho na tutakuwa tayari kufanya marekebisha jinsi ambavyo tunaona matokeo ya huu mpango mpya.

Mheshimiwa Spika, la pili, kumekuwepo na malalamiko kwamba kuna vifaa pamoja na dawa ambazo hazikidhi viwango. Hilo tumelipata na tumeanza kulifanya kazi. Tutakapopata jawabu kwamba, ni kweli ni vitu gani ambavyo vimeagizwa, wale wahusika ambao walifanya makosa haya tutawachukulia hatua. Lakini mpaka sasa hivi hatujaweza kuona mahali popote ambapo tumerejeshewa dawa, tukarejeshewa na vifaa kwa mfano, *BP Machines* kwamba, hazifanyi kazi ili tuweze kutumia kama ushahidi wa kufuatilia na kuwachukulia wahusika hatua. Naomba pale ambapo kuna tatizo kama hili, basi Waheshimiwa Wabunge, wawahamasishe Viongozi wa Hospitali zao wavikusanye, watulettee pamoja na ushahidi kwamba vilipelekwa lini kutoka MSD ili tuweze kufuatilia tatizo hilo.

Na. 24

Matatizo ya Kuona

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE aliuliza:-

Tafiti zinaonesha kuwa Watanzania walio wengi hasa walimu na wanafunzi wana matatizo ya kuona:-

- (a) Je, ni sababu gani zinazosababisha tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali ina mipango gani katika kupambana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Kwa niaba ya Waziri ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamidu Salehe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na Shirika la Afya duniani inakadiriwa kuwa Tanzania ina wasioona asilimia moja ya watu wake wote. Idadi hii inaongezeka kuwa mara tatu zaidi watu wenye uoni hafifu. Makadirio hayo yanamaanisha kuwa Tanzania ina takriban watu 450,000 wasioona kabisa na watu milioni 1,350,000 wenye uoni hafifu. Sababu zinazosababisha kutokuona ni pamoja na zifuatazo: Mtoto wa jicho asilimia 50, makovu kwenye kioo cha jicho kinachotokana na upungufu wa vitamini A, au maradhi ya surua asilimia 20, shinikizo la jicho asilimia 10 na asilimia 20 nyingine inasababishwa na magonjwa ya retina kama vile kisukari, shinikizo la damu na umri mkubwa na matatizo ya kuzaliwa yaani kwa *congenital reasons* na maambukizo ya Usubi pamoja na ajali mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu imeweka mikakati ya upimaji wa awali wa wanafunzi shuleni na wale wanaobainika kuwa na matatizo wanapelekwa kwenye vituo vya afya kwa ajili ya vipimo zaidi na matibabu. Aidha, jamii inahamasishwa juu ya umuhimu wa kuwapeleka watoto wenye matatizo ya macho kwenye vituo vya afya ili kupata vipimo na tiba sahihi. Vilevile kuhusu tatizo la uoni kwa watu wazima imeboresha huduma za macho ambazo zinatolewa kwenye vituo vya tiba, lakini kutokana na uhaba wa Wataalam wa macho nchi, huduma za mkoba za macho zinatolewa kwa wananchi walio mbali na vituo vya kutolea huduma za macho. Pia, Wizara imeweza kushawishi Shirika la Taifa la Bima ya Afya ili kuwezesha upatikanaji wa miwani kama moja ya mafao kwa wachangiji wakiwemo walimu. Hii ni katika kutekeleza Mkakati wa Shirika la Afya Duniani wa Dira 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara yangu napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wadau mbalimbali wakiwemo *Lions Club* kwa kugharamia na kuendesha huduma za upimaji na matibabu ya macho kupitia mfumo wa huduma za mkoba yaani *Outreach*.

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya Watanzania wanaamini kuwa kusoma sana makaratasi na vitabu hasa karatasi nyeupe zinasababisha uono hafifu na hatimaye upofu, je, Serikali inawaelimisha nini Watanzania hao.

La pili, Mheshimiwa Naibu Waziri atujulishe tu ni mikoa gani hapa Tanzania iliyoathirika sana kwa tatizo hili?

SPIKA: Atajua kweli, haya!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kushauri tu kwamba kusoma sana karatasi nyeupe kwa muda mrefu hakuna mahusiano ya moja kwa moja na upofu, ila inaweza tu ikasababisha macho kuchoka kwa haraka. Upofu unatokana na sababu ambazo zinaharibu jicho au sehemu ya jicho na kufanya jicho lishindwe kuona. Kwa hiyo, kusoma hakuna mahusiano ya moja kwa moja labda tufanye utafiti kwa sababu hakuna mtu ambaye amefanya utafiti huo, siwezi kukataa wala kukubali, lakini tunahitaji utafiti ila naomba kushauri kwamba Watanzania tuendelee kusoma, kusoma hakuna mahusiano na upofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameuliza kwamba, ni mikoa ipi inayoongoza kwa upofu. Ukweli ni kwamba, Dodoma imekuwa inaongoza ndiyo sababu na Hospitali ya Mvumi ilikuja kujengwa hapa mapema, lakini mkoa wa pili na watatu na wa nne naomba Mheshimiwa Mbunge univumilie, nitakwenda kuangalia *statistics* zetu na takwimu ili nikupe jibu kwa usahihi zaidi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Msalato – Dodoma

MHE. AGNESS E. HOKORORO - (K.n.y. MHE. OMARY A. DADWEL) aliuliza:-

Serikali imetenga eneo la Msalato kwa muda mrefu sasa ili kujenga Kiwanja cha Ndege cha Kisasa hapa Dodoma:-

- (a) Je, ujenzi huo utanza lini?
- (b) Je, kiwanja hicho kinatarajiwa kuwa na ukubwa gani kulingana na mahitaji ya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na kiwanja kikubwa na cha kisasa cha ndege katika Makao Makuu ya Nchi, Mkoani Dodoma. Hatua za awali za ujenzi wa kiwanja hiki zimeanza. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato kwa gharama ya shilingi milioni 715.5 kupitia msaada wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika (BADEA).

(ii) Kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi wanaozunguka eneo hili ambapo wananchi 1,432 wamekwishalipwa. Aidha, kazi ya kusafisha maeneo yatakayojengwa miundombinu ya kiwanja, kama vile barabara ya kurukia ndege, jengo la abiria na miundombinu mingine ya kiwanja imekamilika.

(iii) Sasa tunaendeleza majadiliano na washirika wa maendeleo ya Taasisi mbalimbali ya kifedha kama vile Serikali ya Ufalme wa Saudi Arabia, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika (BADEA), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) pamoja na wawekezaji binafsi katika kutafuta fedha za ujenzi ambazoshilingi bilioni 166.95.

Hivyo ujenzi utanza mara fedha zitakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, kiwanja kitakuwa na ukubwa wa kuhudumia ndege za ukubwa wa Boeing 747 kwa usalama na kitakidhi mahitaji ya Mji wa Dodoma kwa muda mrefu ujao.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ametuhakikishia kwamba, mara fedha zitakapopatikana uwanja huo utanza kujengwa. Je, uwanja wa zamani utakuwa na matumizi gani?

Pili, upo mpango gani madhubuti wa kujenga miundombinu mbalimbali kando kando ya uwanja mpya wa Msalato kama vile hoteli, maduka na vitu vingine muhimu kwa ajili ya huduma muhimu kwa watumiaji wa uwanja huo? (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana wewe ni mwaminifu kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Agness Hokororo.

SPIKA: Haya ya nyongeza ni ya Agness Hokororo, siyo ya yule bwana.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Ndiyo. Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo: Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kitaendelea kutumika kwa ndege ndogo ndogo na pia kitaendelea kutumika kwa ajili ya mafunzo ya urubani kwa sababu kitakuwa na miundombinu yote inayohitaji. Kuna maeneo mengi Wilson Airport na Nairobi Jomo Kenyatta ipo pale, Saint Clara iko pale, Saint Francisco Airport iko pale, kwa hiyo, hizi hali ni za kawaida tu kuwa na kiwanja kidogo na kiwanja kikubwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali kupitia viwanja vya ndege itatengeneza mpango kabambe (*master plan*) ambao utaaanisha maeneo ya hoteli maduka ya kisasa kama vile *duty free* ili sekta binafsi ziwe kushiriki. Hata hivyo, Wizara inashauri mamlaka ya ustawishaji wa Mji wa Dodoma CDA, kutenga maeneo ya kuzunguka kiwanja kwa matumizi ya kibiashara kama ilivyo viwanja vya Dubai na vinginevyo duniani badala ya kufanya maeneo hayo kuwa ya makazi.

Na. 26

Maeneo Yanayomilikiwa na Shirika la Reli

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Shirika la Reli la Taifa lina maeneo mengi ya ardhi katika Mkoa wa Dar es Salaam ambayo hayaendelezwi na matokeo yake maeneo hayo yamekuwa maficho ya majambazi na vibaka wanaowapora wananchi mali zao wanapopita kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na Keko Darajani na BP.

Je, Serikali ina mpango gani na maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli (RAHCO) ilianzishwa mnamo mwaka 2007 kupitia Sheria ya Reli (*Railway Act No. 4*) ya mwaka 2002. Kwa mujibu wa Sheria hiyo niliyoitaja, moja ya jukumu kubwa la RAHCO ni kuendeleza rasilimali na miundombinu ya reli nchini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya reli ambayo hayaendaendelezwa katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na za Jiji la Dar es Salaam, zikiwemo sehemu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, yamegawanyika katika aina kuu mbili zifuatazo:-

(i) Kuna maeneo ambayo yapo kwenye eneo la hifadhi ya njia ya reli ambayo yapo kwa mujibu wa Sheria ya Reli ya mwaka 2002.

(ii) Pia kuna maeneo ambayo yalitengwa kwa shughuli za kiutendaji za reli lakini bado hayaendaendelezwa ipasavyo. Maeneo hayo ndiyo yale aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo ni kwa RAHCO kuendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa maeneo ya aina zote mbili yanawekewa uzio imara ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za reli kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara ya Uchukuzi itafuatilia kwa karibu na kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanawekewa uzio na kusafishwa na pia ulinzi shirikishi nafikiri utasaidia sana ili sehemu ziwe salama na kupitika pia.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali ya nyongeza mawili. Kwa kuwa maeneo haya hayaendaendelezwa zaidi ya miaka 50 sasa na Mkoa wa Dar es Salaam unakadirwa na upungufu wa maeneo kwa maendeleo ya wanawake, vijana na hata kujenga vituo vya kulelea watoto wachanga ambao mama zao wanakwenda makazini katikati ya jiji. Kwa kuwa maeneo hayo bado yako wazi mpaka leo, je, Serikali iko tayari kutoa maeneo hayo kusaidia makundi hayo ya jamii?

Maeneo ya Shirika ya Reli kuanzia Keko, Ubungo Maziwa, Ilala, Gerezani, Gongolamboto na Pugu, ni maeneo ambayo yametetelekezwa, hayafanyiwi usafi wa aina yoyote na matokeo yake yanakuwa makao makuu ya majambazi na vibaka katika Jiji la Dar es Salaam je, Mheshimiwa Waziri unanihakikishiaje, au unanisaidiaje haya maeneo yafanyiwe usafi wa haraka na kuwekewa ulinzi ili kuondoa tatizo la wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuporwa hovy hovy simu zao na vibaka wanaokimbilia maeneo mengine?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufasaha kabisa, Serikali pamoja na RAHCO ambao ndiyo wana jukumu ya kuangalia sehemu hizo watazitunga sehemu hizo na kuhakikisha kuwa zinasafishwa ili maghala hayo ambayo ameyataja yasiwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa sehemu hizo ili zitumike kwa matumizi mengine, sasa hivi tuko katika hatua za kuboresha sana usafiri wa reli na tunahitaji sehemu nyingi kuliko hizo ambazo zipo. Tunapoangalia miaka 50 kutoka sasa reli itahitaji sehemu nyingi kwa ajili ya shughuli nyingi, siyo kireli tu pamoja na shughuli zile ambazo zinaambatana na usafiri wa reli. Kwa hiyo, Serikali siyo tu inaweka sehemu hizo lakini tuko katika jitihada sehemu mbalimbali ikiwezekana kuongeza sehemu kama hizo badala ya kuzitua. Ahsante sana.

Na. 27

Ahadi ya Kuupatia Maji Mkoa wa Tabora

MHE. MUNDE T. ABDALLAH aliuliza:-

Serikali iliahidi kuupatia maji ya uhakika Mkoa wa Tabora kutoka bomba kubwa la Kahama linalotoa maji yake Ziwa Victoria.

Je, Serikali ina mkakati gani juu ya ahadi hiyo ya muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya awali ya kutekeleza ahadi ya kupeleka maji safi na salama Mjini Tabora kutoka Ziwa Victoria. Hadidu za Rejea kwa ajili ya kumwajiri Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa kina wa mradi zimeandaliwa na kupeleka Benki ya Dunia kupata kibali cha kutangaza. Kazi ya usanifu itaanza katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 na itahusisha kupeleka maji katika Miji ya Nzega, Igunga, Isaka hadi Tinde.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2011/2012, Serikali imetenga shilingi milioni 637.5 kwa ajili ya kazi ya usanifu. Mradi huo utatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP).

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini niishukuru pia Serikali kwa kuanza mchakato huo wa kupeleka maji katika Wilaya ya Igunga na Nzega angalau sikusikia Tabora Manispaa imetajwa kwenye mradi huo unaoanza.

Kwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu na ndiyo kwanza Serikali imeanza usanifu kama jibu la msingi linavyosema na kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Tabora hususan Wilaya ya Tabora Manispaa hususan akinamama wamekuwa wakiteseka sana na tatizo la maji, je, Serikali ina mpango gani sasa wa

kuharakisha mikakati yake ya muda mfupi ili akinamama hawa na wananchi wote wa Mkoa wa Tabora waepukane na adha hii ya maji? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikuhakikishie kwamba katika mipango ya muda mfupi unaoendelea sasa hivi katika Mji wa Tabora Manispaa kwa kupitia ushirikiano wa Shirika la Maendeleo la Uswisi, kuna miradi miwili kwanza kulikuwa na mradi wa kuanza upanuzi na ukarabati wa Mji Manispaa ya Tabora na pili kumekuwa na upanuzi na ukarabati wa maji safi pamoja na maji taka katika Mji wa Tabora, ambapo Shirika hili la SECO limeahidi kutoa dola milioni 4.8 na kazi ya usanifu imekamilika na mkandarasi tayari ameshapatikana na kazi itaanza hivi karibuni.

Pia katika kuuboresha upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Tabora, Serikali katika mradi wa WSDP pia imekamilisha usanifu katika Miji Midogo ya Urambo, Sikonge na Uyui na tatu kuna Shirika la JICA limeahidi kusaidia vijiji 20 katika Halmashauri zote katika Mkoa wa Tabora ambazo ni Igunga, Nzega, Sikonge, Urambo, Uyui pamoja na Manispaa. Kwa hiyo, baada ya hii miradi yote katika muda huo mfupi nakuja kuunganisha maji ya kutoka Ziwa Victoria na uhakika kabisa Mkoa wa Tabora utaboreka katika huduma ya maji safi. (Makofi)

Na. 28

Kuondolewa kwa Hitaji la Visa kwa Watanzania Afrika Kusini

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU) aliuliza:-

Kutokana na kuondolewa kwa hitaji la visa kwa Watanzania wanaokwenda Afrika ya Kusini:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na wimbi la wananchi wa nchi jirani wanaoghushi uraia wa Tanzania ili waingie Afrika Kusini bila vikwazo vya Visa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festu Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inasimamia masuala ya uraia kulingana na Sheria ya Uraia Na. 6 mwaka 1995 na Kanuni zake za mwaka 1997. Serikali inaendelea na misako ili kudhibiti ugushaji wa hati za uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Uhamiaji ipo katika hatua za kuboresha mfumo wa uombaji wa uraia pamoja na vyeti vya uraia viwe vya ki-electronic ambavyo vitakuwa imara, bora na vigumu kughushiwa.

MHE. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Nashukuru kwa majibu mazuri, lakini ni wiki iliyopita tu tumeshuhudia Watanzania vijana zaidi ya 100 wamerudishwa kutoka Afrika ya Kusini. Je, kati ya hao ni wangapi ambao walithibitika kuwa na hati za kusafiria za kughushi?

(ii) Katika kipindi hiki cha mpito kama Waziri alivyosema, kuna utaratibu wa kuboresha mfumo wa kupata hati za uraia kwa njia ya elektroniki; ni utaratibu gani ambao utatumika katika kipindi hiki cha mpito?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Kebwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wamekuwepo vijana ambao walirejeshwa kutoka Afrika Kusini, lakini pia wamekuwepo vijana ambao wamerejeshwa kutoka maeneo mengine mbali na Afrika Kusini. Tatizo, kumekuwepo na vijana ambao wanakwenda kutafuta maisha bora na kadhalika na wengi wao siyo kwamba wanakwenda na hati za kughushi, lakini wanakwenda bila hata hati isipokuwa tu wanakwenda kujaribu maisha wanakamatwa kule. Niseme tu kwamba, hili ni suala ambalo halitukabili Tanzania peke yetu, linazikabiri nchi karibu zote ulimwengu mzima.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo tunalifanya ni kwamba, tunafanya maandalizi ya kuhakikisha kwamba hati za kusafiria na hati za Kitanzania zinakuwa imara zaidi ambazo zitakuwa ni ngumu kwa watu kuweza kughushi.

Kuhusu swali la pili kwamba ni kitu gani ambacho kinafanyika; sasa hivi tumeingia katika mchakato, naomba nitumie neno hili "mchakato", la kitaifa na ninafikiri ni zoezi ambalo tutakwenda nchi nzima, ni zoezi gumu kidogo lakini kwa sasa hivi tumeanza na Wafanyakazi wa Serikali. Bado tuna changamoto kubwa sana ya kuhakikisha kwamba, tunakwenda katika nchi nzima, elimu iwe ya kutosha, lakini pia kuweza kuwatambua na kuwabaini nani Watanzania na nani wasiokuwa Watanzania.

Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba, hili zoezi litatakiwa ushirikiano mkubwa na wewe Mheshimiwa Mbunge ukiwemo, Halmashauri zote zikiwemo na Viongozi wote mpaka Wenyevidi wa Mitaa wakiwemo katika zoezi hili.

Na. 29

Udhaliishwaji wa Wanawake Wafungwa Nchini

MHE. MHONGA S. RUHWANYA aliuliza:-

Kumekuwa na matendo ya kikatili na uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu katika magereza nchini ikiwemo Gereza la Bangwe Kigoma, upande wa wanawake kuvuliwa nguo zote anapoingia mfungwa mwanamke gerezani hapo na kupewa adhabu za kuruka kichura akiwa uchi kama alivyojaliwa:-

Je, Serikali itawachukulia adhabu gani Askari hao wa Magereza wanaowadhaliisha wafungwa wanawake?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndiyo mara ya kwanza tunapata taarifa za kushtua kama hizi kuhusu Gereza la Bangwe. Tumefuatilia bila kupata ushahidi wa jambo hili. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ana ushahidi wa jambo hili anipatie mara moja. Bila kuwabaini askari wanaofanya vitendo hivi ni vigumu kuwaadhibu kama aelezavyo Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, wahalifu wanapoingia na wawapo magerezani, zipo kanuni na taratibu zinazolinda na kuthamini haki za utu wao chini ya Kanuni za Kudumu za Uendeshaji wa Jeshi la Magereza za Mwaka 1968. Kanuni hizi hazimruhusu askari kutothamini, kumdharau au kumdhaliisha mfungwa na kumtesa mmfungwa. Endapo askari yeyote anakiuka Kanuni na Sheria hizo, hatua kali za kinidhamu huchukuliwa mara moja dhidi ya askari mhusika.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuli za maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nasikitika kwa majibu haya ya Serikali, inaonesha kabisa waliohojiwa ni askari ambao wanatenda vitendo hivyo, *obviously* majibu ni lazima yaje kama yalivyo.

(i) Pamoja na kwamba, askari hawa wamekataa, naitaka Serikali itoe tamko kali kwa askari wote wanaofanya vitando vya kinyama kwa mahabusu wa jinsia zote pamoja na watoto.

(ii) Ushahidi uliopo siyo wa picha ni wa moja kwa moja; je, Serikali itakapokutana na wanawake hao au hata mmoja aliyeathirika na matendo kama hayo tena wanayofanyiwa na wanawake wenzao ambao ni askari; itachukua hatua gani kwanza kwa askari hao kudanganya; na pili kwa kufanya vitendo hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ruhwanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotamka, masikitiko ni makubwa, kama kweli mambo haya yanafanyika. Tunataka tuwe na ushahidi wa kutosha na lazima tuwe na mahali pa kuanzia, ndiyo hapo ninakuomba kama wewe mwenyewe una ushahidi wa kutosha ama mahali, unaweza kutupelekea tukapata ushahidi wa kutosha nikuhakikishie hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mbunge kasema kwamba, anasikitishwa na jibu la Serikali, jibu haliwezi kuwa tofauti na hapo kwa sababu tumejaribu kutafuta ushahidi hatukuupata lakini kama utaweza kuwa nao ukatusaidia kuupata, tutakuwa tayari kuchukua hatua kwa sababu tunasema huo ni ukiukwaji wa haki za mfungwa aliyepo gerezani.

Kuhusu swali la pili, mimi nasema nipo tayari kama utanionesha mama mwathirika au akina mama waathirika na tutachukua hatua zinazostahili bila mashaka, bila kigugumizi na bila woga wowote, kwa sababu haki za mfungwa zinabaki pale pale kama Mtanzania, isipokuwa yeye anatazamwa tu kwa makosa ambayo ameyafanya.

MHE. MADGALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mfungwa yeyote anapoingia gerezani haimwondolei haki yake ya kibinadamu; na kwa kuwa kwenye swali la msingi mambo yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Mhonga yametokea mimi ni shahidi namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku ya Mungu wanawake gerezani wanavuliwa nguo zote mpaka nguo ya mwisho na wanasachiwa na wanawake ambao ni Maafisa Magereza. Kwa kuwa huu ni udhalilishaji mkubwa wa haki za binadamu na hasa kwa akina mama; Serikali sasa kwa kupitia mimi ambaye ni shahidi namba moja; wapo tayari kuondoa taratibu hizi zilizopo Magerezani ambazo ni ukiukwaji wa haki za binadamu haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge, nimekusikiliza na unasema kwamba wewe ni mwathirika katika walioathirika na mambo kama hayo. Sina uhakika kama kweli Mheshimiwa Mbunge alivuliwa nguo akaachwa uchi wa mnyama, lakini kama kweli hiyo imetokea sidhani kama hilo ni jambo la fahari ama la kufurahia. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazungumza vizuri na askari waliokufanyia hivyo watakuwepo na tutatazama ni hatua gani za kuchukuliwa, kwa sababu kweli mambo ya kufanyiwa

searching na kadhalika, yapo ili kuhakikisha kwamba kila kitu kipo salama; yaani vitu ambavyo havihitajiki kuingia gerezani.

Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu ni kwamba, Serikali inalichukulia suala hili kwa uzito wake ingawa Waheshimiwa Wabunge mnacheka na mnatabasamu, lakini tunalichukulia kwa uzito wake na tutalifuatilia kadiri tuwezavyo ili tuhakikishe kwamba haya yanayosemwa kama kweli yapo, hatua stahiki zinachukuliwa. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuwa mfungwa ama kuwa mahabusu, hakukuondolei haki zako za ubinadamu.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, atauliza swali hilo.

Na. 30

Ucheleweshaji wa Mikopo ya Wanafunzi

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Kumekuwapo na ucheleweshwaji mkubwa wa fedha za mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Hazina:-

Je, Serikali ina mikakati gani mahususi ya kutatua tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kutoa fedha zinazotosha kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Hazina hutoa fedha kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu pamoja na Wizara, Idara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea, baada ya bajeti husika kupitishwa na Bunge. Vilevile naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Hazina hutoa fedha hizi kulingana na hali ya makusanyo ya mapato kwa vile tunaendesha kwa *Cash Budget*.

Mheshimiwa Spika, napenda ifahamike kwamba, utoaji wa fedha za mikopo ya elimu ya juu huhusisha taasisi nyingi ili kuhakikisha taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria zinazingatiwa. Kweli kuna wakati hujitokeza ucheleweshaji au upungufu. Haya mara nyingi hutokea pale ambapo makusanyo ya mapato yanakuwa madogo kuliko mahitaji yaliyooombwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna changamoto za msingi ambazo ni pamoja na kuwepo kwa wanafunzi wengi kuzidi uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji ya wanafunzi hao na urejeshwaji mdogo wa mikopo baada ya wanafunzi kuhitimu elimu ya juu na kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hizi na pia ili kujibu malalamiko yaliyojitokeza na kuweka mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo, Mheshimiwa Rais, aliteua Kamati Maalum ili kudurusu mchakato wa utoaji mikopo na utendaji wa taasisi zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mikakati ya Serikali ni kuongeza vianzio vya mapato ili kuimarisha uwezo wa Serikali kumudu mahitaji yaliyopo. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume iliyotajwa na ambayo Serikali imeyaridhia.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa majibu ya Naibu Waziri yanaonesha kwamba mikopo ya wanafunzi hutegemea *cash budget*, lakini Ripoti ya CAG kwa Mashirika ya Umma kwa mwaka 2009/2010 inaonesha kwamba katika *quarter* ya Julai mpaka Septemba, pesa zilizotolewa kwenda Bodi ya Mikopo zilitolewa zaidi kwa shilingi 21.1 bilioni. Kwa *quarter* ya Desemba 2011, pesa zilizotakiwa kutolewa zilitolewa pungufu kwa shilingi 85.3 bilioni. Je, Serikali inataka kuwahakikishia wanafunzi na W atanzania kwa ujumla kwamba makusanyo ya Serikali yanaongezeka kipindi kile tu ambapo kunakuwa ni wakati wa uchaguzi na wakati wa miaka mingine makusanyo yanapungua?

(ii) Utaratibu wa kupeleka fedha za mikopo vyuoni kwa wanafunzi wanaoendelea, yaani *continuing students* umeonesha kwamba kuna udhaifu mkubwa kwa Wahasibu vyuoni ambao siyo waaminifu na huandaa majina hewa na kuyapeleka Bodi ya Mikopo na matokeo yake huwasababishia wanafunzi usumbufu mkubwa wa kutokupewa mikopo wale ambao wanastahili. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kurudisha utaratibu wa zamani kwa Bodi kupeleka fedha za mikopo moja kwa moja kwenye akaunti za wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza na wale ambao wanaendelea baada ya kufanyika uhakiki katika vyo vyo ili kuondoa usumbufu, migomo na maandamano kwa wanafunzi bila sababu?

WAZIRI WA ELIMU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la pesa kuongezeka tu kipindi cha uchaguzi lakini siyo miaka mingine, suala hili siyo kweli; tumeendelea kuwa na mtiririko mzuri wa makusanyo ya fedha na wakati wowote tunaendelea kuwahudumia wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwa kadiri ya bajeti inavyoruhusu.

Kuhusu suala la pili la kutokupitishia mikopo katika vyo kwa ajili ya wanafunzi hao wa mwaka wa kwanza na wale wanaoendelea, mtindo huu wa kupitisha vyuoni tumefanya miaka yote lakini miaka ya nyuma tulikuwa hatupitishi pesa za kujikimu za wanafunzi kupitia vyo na baadhi ya vipengele lakini mwaka huu tumeanza kufanya hivyo. Tumefanya hivyo kwa sababu ya upotevu mkubwa sana wa fedha za Serikali kupitia majina hewa na kupitia vijana ambao hawapo shuleni na pesa inakwenda moja kwa moja kwenye akaunti. Tayari taarifa ambazo tumezipata Serikali na mimi Waziri nimeziona, imesaidia sana kwa sababu wale ambao hawapo vyuoni, pesa zao safari hii zimebanwa pale pale chuoni na kurudishwa kwenye Bodi kuliko mtindo wa zamani ambapo ingekwenda moja kwa moja kwenye akaunti mwaka mzima pesa inakwenda kumbe mwanafunzi hayupo chuoni na tutaendelea hivyo ili tulinde pesa za Wananchi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba muwe mnaangalia muda umekwisha. Nina matangazo machache na tunaanza na wageni.

Wageni tulionao katika Jukwaa la Spika ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Mheshimiwa Jaji Mstaafu Damian Lubuva na pia yupo Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ambaye pia ni Jaji Mkuu Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Mahmoud Hamid, amefuatana pia na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Ndugu Julius Mallaba. Nadhani mnakumbuka Viongozi hawa wameteuliwa hivi karibuni baada ya Mheshimiwa Rais kuwatangaza na wamekuja hapa kuweza kutoa heshima kwa Ofisi ya Spika. *(Makofi)*

Wageni wengine waliopo katika Jukwaa la Wageni wamekuja kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye. Wageni hao wanatoka Uingereza, wamekuja kuhamasisha maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, nao ni Ndugu Andrew Brown; *if you can stand please wherever you are*. Pia tunaye Ndugu Christopher Taylor, yupo pia Ndugu Alexandra Bamboye na Ndugu Lesly Graham. Kwa hiyo, hawa ni wageni wanaokwenda Wilaya ya Arumeru kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri.

Baada ya hapo tuna matangazo machache ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo baada ya kipindi cha maswali saa tano, nimewaruhusu hawa wafanye saa tano, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao cha kuchambua Azimio leo; na wao pia nimewaruhusu saa tano, ambapo kikao kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa B. Kwa hiyo, Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria kikao hicho.

Katibu wa *Caucus* ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anasema niwatangazie Kamati ya Uongozi ya CCM siyo ya kwangu kwamba, kutakuwa na kikao saa saba katika Ukumbi wa Spika. Hii ni Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi.

Pia nimeombwa na Kaimu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, nitangazie kwamba, Wabunge wa CHADEMA watakuwa na Kikao cha Kamati ya Wabunge leo tarehe 1 Februari 2012, saa nane mchana katika Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene, anipokee kazi kwa sababu ya wageni tulionao.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu kwa hatua inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 (The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2012)

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni
kwa Mara ya Kwanza)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu umesomwa kwa mara ya kwanza, kwa hiyo, utaendelea kwa hatua zake nyingine zinazofuata na kwa sababu hiyo basi, nikuombe Katibu utueleze shughuli inayoendelea.

HOJA ZA SERIKALI

M A A Z I M I O

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika (The African Youth Charter) wa Mwaka 2006

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo ya kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika (*The African Youth Charter*) wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kibali chako, naomba niungane nawe na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania katika kuwakumbuka na kuwaomba ndugu zetu Marehemu Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Regia Mtema na Mtumishi wa Bunge, Ndugu Nicodemus Senge, waliofariki hivi karibuni. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa maelekezo na michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili wakati wa vikao vilivyofanyika

baina ya Kamati na Wizara yangu kati ya tarehe 19 na 20 Januari, 2012. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba, michango yao tumeithamini na pia tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu mapendekezo ya kuridhia Mkataba uliokusudiwa ambao ninaliomba Bunge lako Tukufu liweze kuuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Nchi Huru za Afrika ulibuni Mkataba wa Vijana wa Afrika (*African Youth Charter*), kwa lengo la kutoa msisitizo na Mwongozo wa Kiseru na Kisheru kwa Nchi Wanachama kuhusu umuhimu wa kuwashirikisha na kuwahusisha vijana katika nyanja zote za maendeleo na ustawi wa Bara la Afrika. Mnamo tarehe 2 Julai, mwaka 2006, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika waliridhia kubuniwa kwa Mkataba huu na kutoa wito kwa Nchi Wanachama kuukubali kwa kuweka saina, kuuridhia na kuuvumisha (*popularisation*).

Tanzania kama Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika (AU), ilisaini Mkataba huo tarehe 13 Novemba, mwaka 2008 na sasa tuko kwenye mchakato wa kuuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maudhui ya Mkataba wa Afrika: Mkataba wa Vijana umegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu hii inaeleza wajibu wa Umoja wa Afrika katika utekelezaji wa Mkataba huu. Wajibu huo ni kurejea sheria zinazounda umoja wenyewe, dira, matarajio, imani na utashi wa umoja huo na ule wa Wakuu wa Nchi wa Afrika. Aidha, sehemu hii pia imeeleza umuhimu wa kuutekeleza Mkataba huu kwa kufuata maadili, mila, desturi na ustaarabu wetu wa asili ya Afrika ambao umejengwa katika misingi ya haki za watu.

Sehemu ya pili ni haki na wajibu ambayo ni Ibara ya 1 – 28 ya Mkataba huu. Sehemu hii inaeleza majukumu ya Nchi Wanachama ambayo ni kutambua haki, uhuru na kazi zilizohifadhiwa kwenye Mkataba huu na kuchukua hatua za lazima kulingana na michakato ya Kikatiba katika kulinda Mkataba wenyewe. Aidha, Mkataba huu unahimiza ushirikishwaji wa Vijana bila kujali uzawa, ukabila, rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au hali nyinginezo. Katika sehemu hii, Mkataba pia unahamasisha nchi maridhiwa kuwaruhusu vijana kutoa mawazo yao, kwenda wanakotaka bila kuvunja sheria, kushiriki katika ulinzi wao binafsi na familia, kuwawezesha vijana kumiliki mali na kujiletea maendeleo yao na ya Taifa lao. Aidha, Mkataba huu unahamasisha nchi kuwapatia vijana elimu bora na maendeleo ya ujuzi, maisha endelevu na ajira, afya bora na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu wa Vijana wa Afrika pia unaeleza kuhusu wajibu wa vijana kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 26. Wajibu huo ni pamoja na wajibu wa vijana kwa familia zao na jamii wanamoishi, wajibu kwa nchi yao na Jumuiya za Kimataifa. Aidha, vijana wanahimizwa kuwa wasimamizi wa maendeleo yao wenyewe, kushiriki katika shughuli za kiraia, kuchangia katika ukuzaji wa maendeleo ya uchumi wa nchi yao, kutetea demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu na uhuru wa msingi wa mtu, kukuza, kuhifadhi na kuheshimu desturi za Kiafrika na urithi wa kiutamaduni na kurithisha haki hii kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni hitimisho ambayo ni Ibara ya 29 – 31. Sehemu hii inaweka msisitizo katika maeneo makuu yafuatayo: Utaratibu wa kuridhia Mkataba, Utekelezaji wa Mkataba na Jinsi ya kuufanyia Mkataba marekebisha au maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika ni pamoja na:-

Kwanza ni kuwezesha nchi yetu kushirikiana kwa karibu na nchi nyingine za Afrika katika masuala yanayohusu Maendeleo ya Vijana. Pili, kuwa na mfumo wa kisheru wa kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika vyombo vya juu vya utoaji wa maamuzi katika maendeleo ya Bara la Afrika. Tatu, kuwawezesha Vijana kubadilishana teknolojia katika masuala ya maendeleo, kuibua vipaji walivyo navyo na kuwawezesha kukabiliana na changamoto za utandawazi katika masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mikataba ya Kimataifa ya aina hii inapaswa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusoma azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU);

NA KWA KUWA Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika katika Mkutano uliofanyika Banjul (Gambia) mwezi Julai 2006 waliazimia kila Nchi Mwanachama kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika ili kuwezesha Mkataba huu kutekelezwa kwa ajili ya Maendeleo ya Vijana;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama zinatambua kuwa Vijana kama rasilimali kubwa ushiriki wao kikamilifu katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini utawezesha Nchi za Bara la Afrika kuwa na umoja utakaowezesha kukabili mabadiliko ya nchi;

NA KWA KUWA pamoja na mambo mengine Mkataba wa Vijana wa Afrika:-

- (a) Una lengo la kuondoa dhana ya ubaguzi baina ya Vijana kwa misingi ya rangi, jinsia, lugha, dini na mitazamo ya kisiasa miongoni mwa Vijana;
- (b) Unatambua uhuru wa vijana kwenda nchi yoyote wanakotaka kwa kuzingatia sheria za nchi husika, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kuungana na uhuru wa imani watakayo;
- (c) Unatambua na kulinda maisha ya mtu binafsi, familia, mali na thamani za vijana wa Nchi Wanachama; na
- (d) Unatambua ushiriki na umuhimu wa vijana katika kuleta maendeleo katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

NA KWA KUWA Mkataba wa Vijana wa Afrika unatambua na kusisitiza ushiriki wa vijana katika shughuli mbalimbali za kijamii na hivyo kuzitaka nchi wanachama pamoja na mambo mengine:-

- (a) Kuwawezesha vijana kushiriki katika Shughuli za Bunge na vyombo vingine vya utoaji wa maamuzi kwa mujibu wa sheria za nchi husika;
- (b) Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na usawa baina ya vijana wa kike na wa kiume katika kushiriki kufanya maamuzi;
- (c) Kuwawekea vijana mazingira mazuri ya kupata habari na huduma mbalimbali zitakazowawezesha kufahamu wajibu na haki zao katika jamii;
- (d) Kuhakikisha vijana wanapata elimu bora na endelevu ambayo hatimaye itawezesha kupata ajira zenye staha na hivyo kujikomboa kiuchumi, kiutamaduni na kijamii;
- (e) Kuhakikisha kuwa vijana wana afya nzuri kimwili na kiakili ili waweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;
- (f) Kuwawezesha vijana kuishi na kufanya kazi mahali popote katika nchi zilizoridhia Mkataba huu kwa kuzingatia sera na sheria za ajira za nchi husika;
- (g) Kuhakikisha kuwa marekebisho mbalimbali pamoja na mapitio yanaweza kufanywa na nchi wanachama pale inapoona kuna upungufu au matatizo; na
- (h) Kuwapa uhuru vijana kuingia katika ndoa kwa kuzingatia sheria ya nchi husika.

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Mkataba wa Vijana wa Afrika kutatoa fursa ya mambo yafuatavyo:-

- Tanzania kushirikiana kwa karibu na nchi nyingine za Afrika katika masuala yanayohusu maendeleo ya Vijana;
- Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kubadilishana uzoefu katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa zinazowahusu Vijana; na
- Kuwepo mfumo wa kisheria wa kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika vyombo vya juu vya utoaji wa maamuzi katika maendeleo ya Bara la Afrika.

NA KWA KUWA katika mchakato wa kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika uchambuzi wa kina umefanyika na kubaini maeneo ambayo kimsingi hayakubaliki katika mazingira ya Tanzania na hivyo kutoyazingatia katika kuridhia ikiwa ni pamoja na maeneo yafuatayo:-

- (a) Masharti ya Ibara ya 12(1)(h) inayozitaka Nchi Wanachama kuandaa Sera ya Taifa ya Vijana itakayotungwa na kupitishwa na Bunge na hatimaye kutungiwa sheria tofauti na utaratibu wa Tanzania ambapo Sera hutungwa na Serikali; na
- (b) Masharti ya Ibara ya 13(4)(h) ikisomwa pamoja na Ibara ya 23(1)(g) zinazohusu watoto wenye ujuzito au waliwolewa kuendelea na masomo ni kinyume na Sera yetu kwa sasa.

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba wa Vijana Afrika na manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Sita, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika, yaani *African Youth Charter of 2006*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iam uliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kuwasilisha hoja ya azimio hilo na limeungwa mkono na tundaendelea na hatua nyingine. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii iliyoshughulikia Azimio hili, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, sasa naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vijana wa Afrika *(The African Youth Charter)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Nyongeza ya 8 chini ya Kanuni ya 115, Kifungu cha 9(1), naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Vijana wa Afrika *(The African Youth Charter)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuchukua fursa hii kutoa Salamu za Heri ya Mwaka Mpya kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Wananchi wote kwa ujumla. Vilevile kwa namna ya pekee, naomba niwatakie kheri ya mwaka mpya Wananchi wote wa Jimbo la Peramiho. Pia naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati yangu, kuwapongeza sana Wachezaji wa *Twiga Stars* kwa ushindi mkubwa dhidi ya Timu ya Namibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa Bunge letu Tukufu kwa kuondokewa na Wabunge wetu wapendwa wawili katika kipindi cha mwezi mmoja; Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari.

Pamoja na hayo, naomba kuipa pole ofisi yako kwa kuondokewa na Mtumishi wa Bunge, ndugu yetu Nicodemus Senge. Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi; Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilipata fursa ya kufikiria na kuchambua Mkataba wa Kimataifa wa Vijana wa Afrika (*The African Youth Charter*) na kutambua madhumuni ya Serikali kuhusu Mkataba huu. Maelezo na ufafanuzi kuhusu Mkataba huu yaliwasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, tarehe 19 Januari, 2012 na tarehe 20 Januari, 2012 ambapo wadau mbalimbali walitoa maoni yao. Aidha, Kamati inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia katika kuboresha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, Mikataba ya Kimataifa na Maazimio, kabla ya utekelezaji wake kuanza huridhiwa na Bunge. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta mbele ya Bunge Azimio kwa ajili ya kuridhia Mkataba huu, kwani miaka kadhaa imepita toka Nchi Wanachama wamalize kukubaliana kuridhia Mkataba huu kwa makubaliano ya kuleta maendeleo ya vijana katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Mkataba huu wa Vijana limetokana na mambo yafuatayo:-

Sheria na Katiba ya Umoja wa Afrika, Mpango Mkakati wa Tume ya Umoja wa Afrika wa Mwaka 2004 - 2007, Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (1948), Mapatano ya Kimataifa ya Haki za Kiraia na Kisiasa (1976), Mapatano ya Kimataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (1976), Vipambebe vya Programu ya Utekelezaji ya Dunia ya Umoja wa Mataifa kwa Vijana kwa Mwaka 2000 (*The World Plan of Action for the year 2000 and beyond*) na juhudi zinazoendelea kufanywa na Umoja wa Mataifa katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs).

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wa ujana ni umri unaofurahisha na kuvutia sana na ni umri muhimu katika maendeleo ya jamii ambapo vijana hufurahia kipindi cha mpito kutoka katika umri mdogo na kuingia katika ujana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanafalsafa aitwae Collins aliandika hivi: "Katika maisha, jamii imejiingea mifumo miwili ya maisha. Mfumo wa kwanza ni mfumo wa kijamii ambao huhusisha utaratibu wa kisheria kuchukua nafasi dhidi ya mfumo uliopo. Mfumo wa pili ni ule unaotawaliwa na amani na demokrasia kwani ushirikishwaji wa hiyari kupitia nyenzo ya mahitaji ni kitu muhimu katika mfumo huo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya hali halisi ya dhana na mantiki ya Mkataba huu, mifumo yote miwili ni muhimu kwa vijana wetu tulionao kupata nafasi ya kuchangia maendeleo ya nchi yetu. Sasa ni wakati wa nchi yetu kuyapa kipaumbele mahitaji ya vijana na kuwawezesha kielimu, kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bara la Afrika linajulikana kwa umaskini na uwepo wa Ugonjwa sugu wa VVU/UKIMWI, migogoro, vita vya wenyewe kwa wenyewe, njaa na majanga mengine mengi. Bado Bara letu lina kazi ya kujenga utawala bora kwa kuwajengea vijana wetu mwelekeo wa maisha ya sasa na kuleta maendeleo katika nchi zao. Hakika, vijana ndiyo wameshika mhimili wa maendeleo ya Bara letu na nchi yetu kwa ujumla katika karne hii ya ishirini na moja. Ni dhahiri kabisa, baada ya kuridhiwa kwa Mkataba huu wa Vijana, utafunguka ukurasa mpya wa kuweka misingi ya kushughulikia masuala ya vijana kwa wakati na hatimaye Taifa kunufaika na nguvu kazi hii ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa rasilimali kubwa ya Taifa letu ni vijana. Kwa kutumia vijana tunaweza kupiga hatua kubwa za maendeleo japokuwa zipo changamoto kubwa zinazoweza kuwepo baada ya kuridhiwa Mkataba huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

Utayari wa Sekta nyingine mtambuka kuoanisha Sera za Kisekta na mahitaji ya Mkataba huu kwa maendeleo ya vijana; umuhimu wa ukusanyaji wa takwimu kuhusu hali halisi ya maisha ya vijana na changamoto zao nchini mwetu; vitendea kazi na upatikanaji wa rasilimali kwa maendeleo ya vijana; ufahamu wa vijana wa mambo yahasuyo Mkataba wao pamoja na kuwa tayari kuyatekeleza na

kutekelezewa; Wizara husika kuongezewa bajeti ili kukidhi mahitaji ya kutekeleza Mkataba huu; na mwingiliano wa Mkataba na baadhi ya mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitasoma maoni ya Kamati kuhusu Mkataba wa Vijana wa Afrika. Mkataba huu umegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: Sehemu ya utangulizi, sehemu ya ufafanuzi wa maneno na tafsiri mbalimbali, sehemu ya haki na wajibu wa vijana na Nchi Wanachama na hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza, utangulizi. Sehemu hii ya kwanza inaelezea sheria, dira, matarajio na mambo mengine muhimu yaliyopelekea chimbuko la Mkataba huu. Eneo hili halikuwa na utata kabisa katika Kamati yetu, lipo wazi na Kamati ilipokea maelekezo hayo imeyatolea maelekezo katika sehemu ya utangulizi wa Ripoti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Mkataba inatoa ufafanuzi wa maneno husika yaliyojitokeza ndani ya Mkataba. Maneno kama vile Mwenyekiti, Tume, Nchi Wanachama na Kijana, yametolewa ufafanuzi katika eneo hili. Kijana ametafsiriwa kuwa ni mtu mwenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Katika hili Kamati inashauri kuangalia Sheria zetu nazo zinamtaja vipi kijana kiumri ili kuondoa utata na kuendana na Mkataba kama ulivyojielekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, inafafanua ibara mbalimbali zilizopo ndani ya Mkataba. Kamati ilipata nafasi ya kupitia Ibara moja hadi nyingine kwa kushirikiana na wadau. Yafuatayo yalijitokeza katika uchambuzi wa Ibara hizo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya kwanza ilikuwa inazungumzia majukumu ya Nchi maridhiwa. Katika Ibara hii ya kwanza, Kamati haikuwa na tatizo lolote na inakubaliana na jukumu la Kimkataba kwa nchi maridhiwa kwamba zitatambua haki, uhuru na kazi zilizohifadhiwa katika Mkataba huu. Nchi hizo pia zitachukua hatua za lazima kulingana na michakato ya Kikatiba na Kanuni za Mkataba huu, kukubali hatua za kisheria au nyinginezo zitakazokuwa za lazima ili kuzipa nguvu Kanuni za Mkataba. Kamati haikuwa na tatizo na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2 inahusu kuepuka ubaguzi. Kamati inakubaliana na ibara hii kwani inaondoa ubaguzi wa utafaifa, rangi, jinsia na kadhalika katika kufaidi haki na uhuru. Ibara hii inawapa vijana ulinzi dhidi ya ubaguzi katika maoni yao na imani walizo nazo. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuona mipaka ya uhuru huu inazingatia sheria za nchi tulizonazo na vilevile inazingatia Sehemu ya Tatu ya Katiba ya nchi yetu tuliyonayo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3 inazungumzia Uhuru wa mtu kwenda anakotaka. Kamati haikuwa na tatizo na ibara hii ihusuyo uhuru wa kwenda popote ilimradi vijana wetu wasivunje sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4 inazungumzia uhuru wa kutoa mawazo. Kifungu kidogo cha (1) kinampa kijana uhuru wa kusambaza mawazo au maoni yake kutegemea ukomo au mipaka inayoelekezwa na sheria. Kamati imeridhika kabisa na kifungu hiki kwa kuwa msisitizo wa uhuru huu unaendana na mipaka ya kisheria ya nchi husika ili kutunza maadili na utu wa vijana wenyewe na jamii nzima. Ibara ya 5 inahusu uhuru wa mtu kushirikiana na wengine. Ibara ya 6 ni uhuru wa maoni, dhamira na kuamini dini mtu aitakayo. Kamati haikuwa na tatizo na ibara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7 inazungumzia ulinzi wa maisha ya mtu binafsi. Ibara hii inawataka vijana kutoingiliwa katika mambo yao binafsi, makazi, mawasiliano ya kiholela kinyume na sheria, kuvunjiwa heshima au hadhi yao. Hili ni jambo jema lakini Kamati inazidi kushauri, kwa kuwa Mkataba unasisitiza umuhimu wa mila na tamaduni katika maendeleo ya vijana, basi vijana waelimishwe kupokea ushauri ulio mwema na wenye lengo la kuboresha maisha kwa kadiri ya utamaduni wa Taifa letu la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8 inazungumzia ulinzi wa familia na umiliki wa mali. Kamati haikuwa na tatizo na Ibara hizi kwani umiliki wa mali na haki kamili ya vijana na maamuzi ya kuingia katika ndoa bila kushawishiwa ni jambo jema sana. Kamati inawakemea vikali wale wote wanaowalazimisha vijana wao kuoa au kuolewa na wenza wasiokuwa chaguo lao na kwamba tabia hii isipate nafasi ya

kuendelea ingawa wazazi na walezi wanaweza kuwa washauri katika kuwapa miongozo vijana wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 10 inazungumzia Maendeleo na Ibara ya 11 Ushiriki wa vijana. Ibara ya 11 kifungu kidogo cha (2) kinaeleza wazi ushiriki wa vijana katika nyanja zote lakini nchi ndiyo itatakiwa kutoa kipaumbele na kuwapa motisha vijana kuwa wadau muhimu katika maeneo ya maendeleo kama vile:-

Moja, ushiriki wa vijana katika Bunge na vyombo vingine vya maamuzi kufuatana na sheria. Kamati inaona suala hili ni muhimu sana kwa vijana katika nchi yetu kwa sasa kwani idadi ya vijana ni kubwa na inazidi kuongezeka. Hivyo, umuhimu wao katika maendeleo ya nchi ni jambo la msingi sana na hasa ushiriki wao katika vyombo vya maamuzi; ushirikishwaji wa vijana katika Vyama vya Siasa na katika nyanja za siasa na hasa wakati wa uchaguzi ni jambo la kutiliwa nguvu na ni jambo muhimu sana kwa sasa. Kamati inasisitiza na kushauri kuwa, Katiba za Vyama vya Siasa zitamke wazi umuhimu wa ushiriki wa vijana wa kike na wa kiume katika siasa na hata wakati mwingine nyadhifa za juu za uongozi ndani ya vyama vya siasa, vijana wapewe kipaumbele ili waweze nao kushiriki katika maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 sehemu (j) inasisitiza uwakilishi wa vijana kama sehemu ya ujumbe kwenye mikutano ya kawaida na isiyo ya kawaida ndani na nje ya nchi.

Kamati inasisitiza kuwa, kwa kuwa Serikali imekuwa ikialikwa na kushiriki katika mikutano mingi ndani ya nchi na nje ya nchi ni vyema sasa ukaratibiwa utaratibu wa vijana kuwepo na kushiriki katika mikutano hiyo. Aidha, vigezo vya ushiriki viwekwe wazi na uwakilishi wa uwiano wa vijana upatikane na uonekane wazi. Kamati inasisitiza jinsia izingatiwe katika ushiriki na uwakilishi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 inazungumzia Sera ya Taifa ya Vijana. Kamati haikuona tatizo katika Ibara hii kwa ujumla wake, lakini Kamati iligundua kuwa kifungu kidogo cha (h) kisemacho Sera itapitishwa na kukubaliwa na Bunge na kufanywa sheria, kina utata kwani kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu, Sera hupitishwa na Baraza la Mawaziri na sheria hutungwa na Bunge. Hivyo, Kamati inashauri kifungu hiki kisiridhiwe ili kuendelea na utaratibu uliopo mpaka hapo utaratibu wa kutunga Sera utakapobadilika au kwa ushauri mwingine wowote ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 inaelezea elimu na maendeleo ya ujuzi na Ibara ya 14 inazungumzia utokomezaji wa umaskini na mfungamano wa vijana kiuchumi na kijamii. Hizi ni ibara za msingi sana kwani kwa ujumla wake, zinazungumzia masuala muhimu ya vijana katika maeneo yafuatayo:-

1. Elimu ya maendeleo ya ujuzi na ufundi;
2. Uondoaji umaskini na ushiriki wa vijana katika uchumi wa jamii;
3. Maisha endelevu ya vijana na ajira zao; na
4. Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya manne kama nilivyosema hapo awali ni muhimu sana kwa Vijana wa Tanzania. Kama inavyofahamika, mpaka sasa idadi ya vijana katika Bara la Afrika ni takriban bilioni 1.3, wakati katika nchi yetu vijana kuanzia miaka 15 - 35 ni asilimia 35 ya Watanzania wote kwa mujibu wa sensa iliyopita, lakini mpaka sasa ongezeko linazidi kuwa kubwa. Aidha, inakadiriwa kuwa takriban asilimia themanini ya Vijana wote wa Tanzania wanaishi vijijini na wanakabiliwa na matatizo mengi sana kama vile:-

- (i) Hawana nyumba bora na za kisasa;
- (ii) Hawana zana bora za kazi za uzalishaji mali na huduma;
- (iii) Hakuna miundombinu rafiki kama umeme, maji, usafiri, viwanda vidogo vidogo, mabenki, ajira binafsi na elimu za ujasiriamali;

(iv) Wanakabiliwa na mfumko mkubwa wa bei na maisha magumu kwa ujumla wake; na

(v) Hawana sheria nzuri na rafiki za kuwawezesha kujiendeleza katika maisha yao wanapoishi huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya yakiendelea, takriban asilimia ishirini ya vijana wote wanaishi mijini na wao wanakabiliwa na changamoto nyingi na chache ni kama zifuatazo: Kukosa ajira; gharama za elimu zipo juu; kukosa malazi na chakula stahili; gharama kubwa za huduma za msingi kama za afya na huduma nyinginezo; unyanyasaji wa kijinsia; uvutaji na ulaji madawa ya kulevya; ukahaba na matendo ya mapenzi kwa wenye jinsia moja; kukosa vituo vya kuwashauri katika masuala mbalimbali; kukosa uwezo wa kupata mikopo ya elimu na pia biashara; kukosa ufahamu wa fursa za ajira binafsi na ajira rasmi; athari za migomo yenye mahitaji muhimu kwao; na pia wanakabiliwa na janga la maambukizi ya VVU/UKIMWI ambapo vijana wengi wameathirika na VVU/UKIMWI kwani kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI kwa Mwaka 2008, asilimia saba ya vijana wetu wote katika Nchi yetu ya Tanzania wameshaathirika na kukosa habari za maisha mapya ya kuishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu sasa unaiagiza nchi yetu kutekeleza na kupanga kwa makini Sera na Sheria zitakazowatoa vijana wetu katika matatizo haya makubwa na ya msingi. Mfano, mkataba unazitaka nchi ridhia kufanya mambo yafuatayo:-

1. Kuwaandaa vijana kuishi maisha ya uwajibikaji kwenye jamii zilizo huru zinazokuza amani, uelewa, uvumilivu, kujadiliana, kuheshimiana na urafiki miongoni mwa makundi yote;
2. Kuwapatia vijana haki ya kupata elimu iliyo bora (elimu iliyo rasmi na isiyo rasmi na hasa elimu ya stadi za kazi na maisha);
3. Nchi Wanachama watatakiwa kutoa elimu bure na elimu ya lazima kwa kuchukua hatua za kupunguza gharama za elimu zisizo za moja kwa moja kwa vijana; na
4. Kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaoacha shule inapungua na hapa Kamati inashauri Serikali kuongeza bidii ya kuimarisha miundombinu ya shule zetu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabweni kwa wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13(4)h inaeleza kuhusu elimu na maendeleo ya ujuzi.

Mkataba unataka wasichana na vijana wa kike wanaopata ujauzito au kuolewa kabla ya kumaliza elimu zao, kupewa fursa ya kuendelea na masomo kama vijana wengine. Kamati inaridhia kwa stara kwa kuwa sheria za nchi yetu bado haziruhusu watoto waliiolewa au kupata ujauzito kuendelea na masomo katika shule zao. Hivyo basi, Kamati inaona sasa ni wakati mwafaka wa Serikali kushughulikia suala hili kwa makini. Aidha, Kamati inashauri yafuatayo:-

Vijana wa kiume ambao huachishwa masomo kwa sababu mbalimbali, sababu hizo zipimwe na wanaoweza kurudishwa shule warudishwe haraka ili kumaliza masomo yao.

Serikali kuanza kuyafikiria upya masharti ya ajira kwa kuondoa vipengele vya uzoefu ambavyo mara nyingi huwanyima vijana fursa za ajira kwa kuwa ni dhahiri kwa sasa vijana wengi wanamaliza Vyuo Vikuu wana uwezo hivyo ni muhimu kupitia Mkataba huu, Serikali itafute njia ya kusaidia kutengeneza mazingira bora ya ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi kwa vijana wetu.

Ili kuendana na Mkataba huu na hasa katika Ibara ya 13, kifungu kidogo cha (d) na (e), Kamati inaomba sasa Serikali ione umuhimu wa kukuza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini kwani vitasaidia sana kukuza maendeleo ya ufundi vijijini na kukuza teknolojia nchini kwani hata maendeleo ya Mataifa Makubwa na hasa yale ya Ulaya, yalitokana na maendeleo ya viwanda vidogo vidogo. Aidha, Kamati inasisitiza vijana wenye ulemavu wasiachwe nyuma katika maendeleo ya nchi yao.

Vijana watumie elimu walizonazo ili kujishirikisha katika tafiti kwa maendeleo ya nchi yetu katika kutokomeza umaskini. Serikali iangalie upya mifumo na hatimaye iweze kuwasaidia vijana kuzalisha, kukuza uchumi na kujipatia ajira kwani vijana wengi toka vijijini wamekuwa wakitoroka maeneo yao na hasa ya

vijijini kwa kukosa miundombinu fasaha ambayo ingeweza kuwaendeleza kiuchumi. Kwa kuwatumia vijana, Serikali inaweza ikapiga hatua za kiuchumi kwa haraka zaidi.

Mikopo ya Elimu ya Juu itengenezewe utaratibu rafiki wa kuwafanya vijana kulipwa kwa wakati na kwa urahisi. Vilevile Sheria ya Mikopo hiyo itazamwe upya ili mikopo hiyo iwe endelevu na iweze kuwasaidia vijana wetu kupata elimu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17 inahusu masuala ya ulinzi. Katika Ibara hii Mkatoba unasisitiza umuhimu wa vijana katika uendeshaji wa usalama na vitendo visivyokuwa vya kimabavu na maumivu yasiyokwisha ya kimwili na kisaikolojia, yanayotokana na kujihusisha katika vurugu na mapambano ya silaha pamoja na vita. Kamati inaunga mkono vifungu vyote katika Ibara hii na kukemea tabia za wanajamii kuwatumia vijana katika uvunjifu wa amani kwa kuleta vurugu, migomo isiyo na tija na vikundi vya ushabiki wa kuvuruga amani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 inazungumzia usimamizi wa sheria. Kamati inaaifiki kifungu hiki na Ibara hiyo. Hata hivyo, inashauri Serikali kuwapa misaada ya kisheria vijana wanaoshtakiwa ili kuwapa utetezi na hasa pale ambapo mazingira ya kesi zao yanaonesha unyanyasaji wa ujana wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19 inazungumzia maendeleo endelevu na ulinzi wa mazingira. Kamati inakubaliana na Ibara hii na haikuwa na tatizo na Ibara hii. Ibara ya 20 inazungumzia Vijana na Utamaduni. Ibara ya 22 inazungumzia mtawanyiko wa vijana nje ya Afrika. Kamati inakubaliana na Ibara hizo na haikuwa na tatizo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 23 inazungumzia wasichana na vijana wa kike. Kamati imetambua umuhimu wa vifungu hivi na kifungu kinasisitiza uwiano sawa kati ya vijana wa kike na vijana wa kiume katika kupata taaluma. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwani mpaka sasa uwiano wa wasichana na wavulana katika elimu ni wa kuridhisha. Kwa mujibu wa Ripoti ya *Basic Education Statistics in Tanzania 2007-2011*, katika shule za msingi uwiano kati ya wanafunzi wa kike ni asilimia 50 na wanafunzi wa kiume ni asilimia 50; sekondari wanafunzi wa kike ni asilimia 45 na wanafunzi wa kiume ni asilimia 55; elimu ya ufundi wanafunzi wa kike ni asilimia 45 na wanafunzi wa kiume ni asilimia 55, Vyuu Vikuu wanafunzi wa kike asilimia 34 na wanafunzi wa kiume ni asilimia 66. Kwa uwiano huu, pamoja na kazi nzuri ya Serikali, kuhakikisha watoto wa kike wanapata elimu, bado msisitizo unatakiwa kuongezwa katika eneo la Vyuu Vikuu na Vyuu vya Ufundi ili uwiano huu uwe sawa kati ya watoto wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha (g) bado kinasisitiza wasichana na vijana wa kike kuendelea kuhudhuria masomo wakiwa wajawazito kama kilivyoenezwa nyuma lakini kilijirudia tena. Kamati inashauri kifungu hiki kiridhiwe kwa stara mpaka sheria zetu zitakaporuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha (L) kinaendelea kukemea ukatili dhidi ya wasichana na hasa ukeketaji lakini kifungu (M) kinaziomba nchi wanachama kusaidia kutunga na kusimamia sheria za kulinda wasichana na vijana wa kike. Aidha, Kamati inashauri Mashirika ya Dini, Wanasiasa na Viongozi wa Jamii, kukemea vikali tabia ya kukeketa watoto wa kike bila kuona aibu ya madaraka ambayo yako katika mikono yao. Udhaliishaji huo ni mkubwa na bado umekuwa ukiendelea katika Taifa letu na hivyo Serikali haina budi kuendelea kusimama imara kuhakikisha udhaliishaji huo unakoma na kukemewa.

Ibara ya 24 inahusu vijana wanaokabiliwa na changamoto za ulemavu wa kiakili na kimaumbile. Ibara hii inawazungumzia vijana wenye ulemavu wa kiakili na kimaumbile. Kamati inakubaliana na eneo hili lakini inashauri sheria za kuwalinda vijana hawa zizingatie Sheria na Mikatoba ya Watu wenye Ulemavu na hasa Mkatoba wa Mwaka 2010 kwani katika Mkatoba na Sheria hiyo, Ibara ya kwanza inayohusu madhumuni imetoa tafsiri pana ya watu wenye ulemavu na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 25 mpaka 28, Kamati haikuwa na tatizo na Ibara hizi. Ibara ya 29 mpaka 31 iliyohusu hitimisho, Kamati haikuwa na tatizo na Ibara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa jumla; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Mkatoba wa Vijana wa Afrika ili sasa Bunge liweze kuuridhia kwa kuwa Mkatoba huu ni nyenzo na silaha muhimu ya

maendeleo ya vijana kama tulivyosema mwanzo, vijana kwa hakika ndiyo Taifa la leo na mhimili au nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi japo wanakabiliwa na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri mambo ya jumla yafuatayo yafanyike ambayo ni:-

Sheria zote ambazo bado hazitoi fursa kwa vijana kujajiri au kuajiriwa zifanyiwe marekebisho na baadhi ya sheria hizo nazo zifanyiwe mabadiliko kama zifuatazo:-

- (a) Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi Na. 7 ya Mwaka 1999. Sheria hii inawanyima vijana wengi wasanii kupata haki zao; kwa hiyo, Kamati inaomba ifanyiwe mabadiliko;
- (b) Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Vyuo Vikuu;
- (c) Sheria na Sera za Elimu zinazoweza kumruhusu kijana wa kike kuendelea na masomo apatapo ujauzito nayo iangaliwe;
- (d) Sheria ya Ndoa nayo iangaliwe kwa sababu inaruhusu watoto wenye umri mdogo kufunga ndoa; na
- (e) Sheria ya Mirathi nayo iangaliwe ili kuwapa haki vijana kupata mirathi na haki zao wanapofiwa na wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo tatizo kubwa la vijana kutumika na kutumia madawa ya kulevya; tunaomba sana Serikali ilianganalie. Kutopatikana kwa ajira kwa vijana limezidi kuwa tatizo kubwa sana, Serikali sasa ioneshe juhudi za dharura kushughulikia tatizo hili au kwa kuwafanya vijana waajiri au waajiriwe wao wenyewe. Lipo tatizo kubwa sana linalojitokeza ambalo bado halionekani kufanyiwa kazi lakini linaathiri sana vijana wengi, nalo ni tatizo la mapenzi kwa wenye jinsia moja. Kamati inashauri Serikali kuanza kushughulikia suala hili kwani linaenda kinyume na imani, maadili na utamaduni wa nchi yetu. Serikali sasa ianze kutenga bajeti kwa shughuli za vijana. Serikali ianze sasa kuwa na benki ya taarifa zinazowahusu vijana, wako wapi, wanafanya nini na wana matatizo gani (*Youth Data Bank*). Mwisho, Serikali ianze kazi ya kuwajengea vijana uzalendo mfano, kuanzisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa kila kijana anaemaliza elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Mch. Getrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi, Mheshimiwa Peter Siomon Msigwa, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Abdallah Haji Ally, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na mimi mwenyewe Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasilillah, kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake ya kikanuni. Vilevile naomba niwashukuru Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Sethi Kamuhanda na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa Azimio hili. Kamati inamshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kuamua kulileta Azimio hili katika Kamati yangu ili lifanyiwe kazi. Aidha, Kamati inawashukuru Wadau na Mashirika yaliyofika mbele ya Kamati na kutoa maoni kuhusu kuridhiwa kwa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio ambalo liko mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, kwa Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge iliyoshughulikia hoja iliyoko mbele yetu ya Azimio la Kimataifa la Vijana wa Afrika.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naomba niwataje watakaanza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ili wajiandae. Msemaji wetu baada ya huyu wa Kambi ya Upinzani, atakayeanza atakuwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyariba Nyangwine, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na baadaye wengine wataendelea.

Sasa nimwite Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, a.k.a. Mr. Sugu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMaji MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami kabla sijaendelea, naomba nimwombe Mungu awalaze mahala pema peponi Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Sumari, maana mkataba huu umekuja wakati nyota ya Regia imezimika lakini kuridhiwa kwa Mkataba huu ni tunu kwake pamoja na Vijana wa CHADEMA na vijana wengine walioungana bila kujali itikadi za vyama kwani toka mwaka 2006 wamekuwa wakiudai uje Bungeni na hatimaye leo umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu azimio tajwa hapo juu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kwa mwaka huu wa 2012, naomba kutoa Salamu za Mwaka Mpya kwa Waheshimiwa wote waliopata bahati ya kuingia mwaka huu salama na pia kuwapa pole wale wote waliopatwa na maswahibu ambayo yako nje ya uwezo wao. Aidha ninawashukuru Wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya hasa wale wa Jimbo la Mbeya Mjini, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kujenga upya Mbeya yetu. Nawaomba mwaka huu ushirikiano uzidi ili maendeleo yapatikane kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio hili ni muhimu sana hasa wakati huu ambapo Vijana wa Taifa hili wanakabiliwa na changamoto nyingi sana za maisha katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tupo kwenye mchakato wa maandalizi ya kupata Katiba Mpya na bora kwa maslahi ya Watanzania wote bila kujali itikadi za kisiasa, kidini, kikanda au ubaguzi wa aina yoyote ule ni vizuri sasa kuwe na utaratibu wa kufanya Mikataba ya Kimataifa kama huu wa leo kuanza kutumika pale tu Serikali inapousaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu utawezesha Serikali kujipanga na kufanya tathmini ya kina juu ya Mikataba hii kabla ya kuisaini na pia utasaidia kuondoa utaratibu unaolalamikiwa kila mara kwa Serikali kuchelewesha Mikataba ya Kimataifa ambayo ni muhimu kwa ustawi wa jamii yote. Hii inadhihirika katika Mkataba huu ambao umesainiwa Novemba, 2008 na leo ni zaidi ya miaka mitatu imeshapita bila Mkataba huu kuletwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inayo maoni yafuatayo kuhusu Mkataba wa Vijana wa Afrika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; haki ya kumiliki mali. Haki hii ipo katika Ibara ya 9 ya Mkataba huu ambapo kila kijana ana haki ya kumiliki au kurithi mali na kuhakikisha kuwa vijana wote wa kike na wa kiume wana haki hiyo kama ilivyoainishwa bila ubaguzi wa aina yoyote ule. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa, Serikali inazingatia masharti ya Ibara hii kwa sababu ipo tabia ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana na vijana ambapo mamlaka za Serikali za Mitaa wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa sana Wamachinga ikiwa ni pamoja na tuhuma za baadhi ya askari kuwapora au kuharibu bidhaa za vijana wanaojihusisha na biashara ndogondogo na hata baadhi ya vijana hao kupoteza maisha.

Hali hii inajitokeza sana katika miji mikubwa hapa nchini kama Jiji la Mbeya ambapo kulitokea vurugu kubwa kati ya wafanyabiashara wadogo wadogo na Mamlaka za Serikali. Pia katika Jiji la Dar es Salaam hali kama hii hujitokeza mara kwa mara mathalani pale Manispaa ya Kinondoni ilipobomoa Soko la Big Brother usiku wa manane na kusababisha mali nyingi kupotea na mpaka leo vijana wale hawajalipwa fidia kwa uharibifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuheshimu matakwa ya Ibara hii ikiwa ni pamoja na kuboresha na kutenga maeneo rasmi kwa kuwashirikisha kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo ambao kimsingi wengi wao ni vijana ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara ambayo imekuwa ikitokea katika sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; maendeleo ya vijana. Changamoto za vijana kimaendeleo ni nyingi sana na juhudi za kupunguza na hatimaye kuziondoa zinaonekana kutokuwekewa mkazo na Serikali. Hii ni pamoja na kuwepo kwa wimbi kubwa la vijana mijini na vijijini kutokuwa na ajira na kushindwa kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuja na Mpango Mkakati wa Dharura hapa Bungeni kuhusu tatizo la ajira kwa vijana kwa kuwa huu sasa si wakati wa porojo za maisha bora kwa kila Mfanzania wakati kila kukicha vijana wengi wanashinda vijiwani bila ajira. Hili ni bomu linalosubiri kulipuka kama Serikali haitachukua hatua za dharura kuwanusuru vijana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka mkazo wa kufufua viwanda vingi ambavyo vilikabidhiwa kwa wanaoitwa wawekezaji ambao wameathiri moja kwa moja uzalishaji wa awali na hivyo kufanya ajira nyingi sana kupotea, mathalani, Kiwanda cha Zana za Kilimo (ZZK) Mbeya, Kiwanda cha Nguo cha Mbeya (*Mbeya Textile Mill*), Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Kiwanda cha Mbaao cha Mkumbara na viwanda vingi Mkoani Tanga ambavyo vimezorota sana kama siyo kufa kabisa na vingine kugeuzwa maghala ya kuhifadhi pombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na mpango mkakati wa kuunusuru uchumi wetu kwa kuongeza uzalishaji katika viwanda, kilimo na sekta zingine ni wazi tatizo la ajira halitapungua na litazidi kuongezeka. Katika mpango mkakati huo ambao tunaitaka Serikali kuuleta ni vizuri wazingatie ndani yake ni namna gani ya kuleta mabadiliko ya uchumi yanayoendana na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, haki ya kupata taarifa. Ibara ya 10(3)(a) ya Mkataba huu inaitaka Serikali kuhakikisha vijana wanapata habari kila wakati kuhusu mambo mbalimbali yanayotokea hapa nchini na Kimataifa. Hili linahitajika kwa kuvishirikisha kwa karibu vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoitaka Serikali kuacha vitisho kwa vyombo vya habari kwenye hotuba yetu mbadala wakati wa Bunge la Bajeti mwaka jana kwa Wizara hii, Kambi Rasmi ya Upinzani tunarudia tena kuwa ni wazi masharti ya Ibara hii hayatatimbia kwa sababu pamoja na kueleza sikitiko letu kwa Serikali kulipa Gazeti la Mwananchi vitisho, bado Serikali imekwenda mbali zaidi kwa kuwakamata wahariri wa vyombo vya habari pamoja na maandishi wa makala ambao kwa namna moja au nyingine walikuwa wanatimiza wajibu wao wa kuwapa taarifa Wananchi wakiwemo vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta au kufanyia marekebisho sheria zote ambazo siyo rafiki kwa vyombo vya habari kama vile Sheria ya Usalama wa Taifa na pia Sheria ya Magazeti ambayo imekuwa ikipigiwa kelele siku hadi siku na wadau wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, masuala ya elimu. Mkataba huu pia unaitaka Serikali kuwapa elimu vijana na kuwawezesha kujua haki zao za msingi, lakini kubwa zaidi ni kuwapa elimu hiyo katika mazingira ya kidemokrasia ili kupata ujuzi na pia kuwajengea uwezo wa kujiamini katika masuala mbalimbali kama inavyoelezwa katika Ibara ya 10(3)(d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo tabia ya Serikali kutumia nguvu kubwa na kufanya maamuzi ambayo siyo mazuri kujenga mazingira ya kidemokrasia katika taasisi zetu za elimu hususan Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mamia ya wanafunzi wa elimu ya juu wapo nyumbani kwa kusimamishwa au kufukuzwa vyuoni kwa sababu ambazo kwa namna moja au nyingine zinaendeleza tabia ileile ya Serikali kushughulikia matokeo badala ya kiini cha matatizo. Kwa sababu badala ya kutatua matatizo yanayowakumba wanafunzi kama vile kukosa au kucheleweshewa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo na matatizo ya malazi; bado Serikali imekuwa ikiwafungulia mashtaka na pia kuwafukuza wanafunzi kwa sababu za kisiasa huku wakisingizia baadhi ya vyama vya siasa kuwa ndiyo chanzo badala ya kuzingatia uhalali wa madai ya vijana hao wanavyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Elimu kuwarudisha wanafunzi wote waliofukuzwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Dodoma na Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili, kwa sababu kwa kuwaacha wanafunzi hao mtaani siyo suluhisho la matatizo katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini lakini pia ni kinyume na Mkataba huu ambao unataka mazingira ya kidemokrasia katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu pia unaitaka Serikali kutoa elimu bora ambayo itawapa vijana ujuzi baada ya kuipata kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 13(1). Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuondoa dhana iliyojengeka ya ubaguzi wa kitaasisi katika shule zetu za sekondari na msingi, kwa sababu kwa sasa hivi kuna tofauti kubwa sana kati ya shule za sekondari maarufu kama shule za kata na shule za watu binafsi katika ubora na ufaulu. Tatizo hili la ubora wa elimu pia lipo katika shule za msingi ambapo ni kawaida kwa maeneo mengi hapa nchini kukuta watoto wetu wanakaa chini kwa kuwa shule zetu hazina madawati. Serikali inatakiwa kuzingatia masharti ya Ibara hii kwa kufilia mkazo kutoa elimu bora na siyo bora elimu ili kutoa elimu inayokidhi ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutenga rasilimali za kutosha kwenye elimu kama ambavyo inaelekezwa katika Ibara ya 13(4)(i) ya Mkataba huu na kuhakikisha rasilimali hizo zinasimamiwa vilivyo ili kuweza kukidhi malengo yake na kuondoa ufisadi katika Miradi mbalimbali katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Azimio la Serikali kuhusiana na Mkataba huu imeelezwa kuwa katika mchakato wa kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika, Serikali imebaini kwamba masharti ya Ibara ya 13(4)(h) hayakubaliki katika mazingira ya Tanzania; ni sawa. Masharti hayo ni yale yanayoruhusu vijana wajawazito au walioolewa kuendelea na masomo na kwamba Serikali imeeleza kuwa masharti hayo ni kinyume cha Sera za Nchi ya Tanzania na mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya ziada kuhusu sababu ambazo Serikali imezieleza kwa Umoja wa Afrika (AU) pamoja na Bunge kupatiwa nakala ya vielelezo vilivyowasilishwa. Aidha, Serikali ieleze iwapo katika kufanya uchambuzi juu ya kifungu husika, ilipata maoni ya wadau wa msingi wanaosimamia masuala ya haki za vijana wa kike nchini. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza Bungeni kuhusu maandalizi ya mfumo maalum kwa ajili ya kuwawezesha vijana wa kike waliojifungua kuweza kupata haki ya elimu na kulinda haki zao za kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ushirikishwaji wa vijana. Mkataba huu katika Ibara ya 11(2)(a) umeweka mkazo na sharti kwa Serikali kuwashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali za kila siku, hii ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha vijana ambao hawapo kwenye mfumo rasmi wa ajira au elimu kutoa mawazo yao moja kwa moja na hivyo kuwa sehemu ya maamuzi ya mambo mbalimbali yanayowahusu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa ushiriki wa vijana Bungeni utakuwa na tija kwa mujibu wa Ibara tajwa kama Serikali itazingatia kubadili mfumo wa uchaguzi ili kuwa na mfumo wa uwakilishi wa uwiano (*Proportional Representation*) na hivyo kupanua wigo wa uwakilishi wa vijana Bungeni na kwenye vyombo vingine vya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Benki ya Vijana. Kwa kuwa kwenye Mkataba huu Ibara ya 11(2)(g) inaitaka Serikali kuwawezesha vijana kifedha na kuwajengea uwezo; ni wakati mwafaka sasa kwa Serikali kuzingatia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuanza rasmi mchakato wa kuanzisha Benki ya Vijana ili kukidhi masharti haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunatoa msisitizo kwa Serikali kuwa, Benki hiyo ya Vijana itakayoanzishwa iwe ya vijana wote kama jina linavyosadifu na ambayo haitawabagua vijana kiitikadi ili kuweza kuwajengea uwezo kifedha na hivyo kuwakwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Sera ya Vijana. Sera ya sasa ya Vijana ya Mwaka 2007 ina utofauti mkubwa sana na masharti ya Mkataba huu ambao unaridhiwa na Bunge lako Tukufu. Pamoja na Serikali kukataa masharti ya Ibara ya 12(1)(h) kuhusu Bunge kutunga Sera na baadaye kuwa na Sheria itakayoendana na Mkataba huu kuhusu Sera ya Maendeleo ya Vijana; Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ifanye mapitio (*review*) ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ili iendane na hali halisi ya vijana na Taifa kwa sasa pamoja na masharti ya Mkataba wa Vijana tunaoridhia. Aidha, Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo pamoja na masharti ya Mkataba wa Vijana Afrika. Bila Sheria, matamko ya Sera na Mkataba huu yatabaki kuwa maneno matamu bila matendo ya kubadili maisha ya vijana hapa nchini na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Baraza la Vijana. Umepita muda mrefu sana toka Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Wanaharakati wa Masuala ya Vijana kuitaka Serikali kuanzisha Baraza la Vijana ambalo kwa namna moja au nyingine, litawapa fursa vijana kuwa pamoja na kuweza kutoa maoni yao kwa pamoja bila kuingiliwa na itikadi za vyama vya siasa. Kwa kuwa Ibara ya 12(i) ya Mkataba huu wa Vijana inataka Serikali kuanzisha mpango utakaoratibu namna ya kuwaunganisha vijana, basi ni wakati mwafaka kuanzisha Baraza hilo ili kuwapa vijana chombo watakachotumia kujadili mambo yao mbalimbali kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, ahsante sana kwa Hotuba hiyo ya Kambi ya Upinzani. Sasa nitamwita mchangiaji wetu anayefuata na wa kwanza hapa atakuwa Mheshimiwa Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Silinde.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuwa wa kwanza kuchangia Azimio hili linalohusu vijana. Kabla sijaanza na mimi niungane na waliotangulia kutoka rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wameaga dunia; Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Regia Mtema, kijana mwenzangu ambaye tumezaliwa mwaka mmoja, tumepishana mwezi mmoja na ninaamini kabisa angekuwepo leo tungeshiriki pamoja katika kuchangia Azimio hili ambalo lina manufaa kwa Vijana wa Afrika na Vijana wa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelipitia Azimio limeeleza mambo mengi ya msingi yanayohusu vijana; kumwezesha kijana kupata elimu, kujijiri au kuajiriwa, kijana kuondokana na umaskini, kijana kuepukana na matumizi ya madawa ya kulevya, lakini je, kwa hapa tulipo hivi vyote Vijana wa Tanzania wanavipata? Hilo ndilo swali langu kubwa. Je, mazingira ya elimu yaliyokuwepo yanamtengenezea mazingira mazuri Kijana wa Kitanzania kupata elimu bora? Yanamtengenezea mazingira mazuri Kijana wa Kitanzania anapomaliza Elimu ya Chuo Kikuu kupata ajira au kijijiri mwenyewe? Kwa masikitiko makubwa, jibu ni hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuona changamoto ambazo zinawakabili vijana wenzetu, hawapati elimu bora na hasa wale vijana ambao wanatoka familia za maskini kule vijijini kama Manyamanyama Bunda, tunaona vijana wanavyopata changamoto za elimu. Pia wanapojikongoja kusoma katika mazingira magumu na kufikia Elimu ya Juu anakutana na changamoto za Bodi ya Mikopo, hapati mikopo anasoma kwa tabu; lakini pia anapomaliza Chuo Kikuu, hakuna ajira kama ambavyo tumesikia hapa kuna mazingira magumu ya kupata ajira. Leo kijana anaambiwa kigezo kimojawapo cha kupata ajira ni uzoefu kazini; huyu kijana ambaye ametoka Chuo Kikuu uzoefu huo anaupata wapi? Nayo inatengeneza mazingira magumu ya kijana kukosa ajira. Je, Serikali imetengeneza mazingira ya kijana huyu kujijiri mwenyewe? Hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huko kote kijana ameshindwa kufanikiwa lakini hata rasilimali za nchi yetu kijana ameshindwa kunufaika nazo na tegemeo kubwa lililobaki ni ardhi. Katika Azimio hili, Ibara ya

14(2) imeeleza kabisa, inamtaka kijana apewe nafasi ya kumiliki ardhi na imesema kabisa Nchi Wanachama zitoe *grants* kwa vijana au *organizations* za vijana kuweza kumiliki ardhi itakayowasaidia kijamii na kiuchumi. Leo sina uhakika kama nikimuuliza hapa Waziri wa Ardhi kuna eka ngapi ambazo zimetengwa kwa ajili ya kumsaidia Kijana wa Kitanzania ili kujikwamua na umaskini; nikimuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo katika ardhi inayofaa kilimo ni eka ngapi ambazo zimetengwa ili kumsaidia kijana aweze kujijiri mwenyewe hakuna. Kama mnavoyoua, sisi Wabunge Vijana kupata tu kiwanja ni kazi je, kijana aliyekuwa kule mtaani anaweza kumiliki ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashukuru Azimio hili, limekuja kwa wakati muafaka. Ni vyema sasa Wizara husika ziangalie ni jinsi gani zitawasaidia vijana katika kunufaika na ardhi yao. Kama maeneo mengine huko yameshindikana, lakini ardhi ni muhimu sana. Hili lisishe kwenye makaratasi tu, naiomba sana Serikali, hii ndiyo rasilimali pekee ya kumkomboa kijana wa Kitanzania. Kati ya asilimia 15 ya Watanzania wasiokuwa na ajira, asilimia 60 inatengenezwa na vijana. Ni hatari! Nami naamini kabisa, mpaka Umoja wa Afrika kuleta Maazimio haya, wameona kabisa kuna hatari kwamba kutakuwa na mgogoro baina ya vijana Afrika na Dunia nzima na Serikali zao kwa sababu ya kutotimizwa matatizo yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wamekuwa na changamoto nyingi, lakini haionekani dalili yoyote ya kutatua matatizo yao. Ndiyo maana nimesema nashukuru nikiwa kama Mbunge ninayewakilisha vijana, limeletwa Azimio hili humu ndani na mimi nikiwa mmojawapo nalijadili leo. Vijana wenzetu wana malalamiko mengi sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwa upande wa ardhi, tuache kugawiana tu sisi wenyewe vigogo. Hawa vijana maskini na wenyewe wana haki ya kumiliki ardhi, ndiyo mtaji wao uliobaki. Ajira hakuna, huko kwenye migodi imeshindikana, viwanda vimekufa, ardhi hii naamini haifi, haozi. Tunaomba vijana wa Kitanzania wapewe nafasi ya kumiliki ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye hili hili Azimio, kuna kipengele kimenifurahisha sana kinachosema kijana wa Kitanzania naye apate fursa ya kufanya kazi zenye staha. Lakini, hebu tujiulize, kwenye migodi yetu, ni kazi gani ambazo vijana wa Kitanzania wanazifanya? Je, zile kazi za staha, vijana hawa ambao wamemaliza vyo wanapata hizo nafasi za kuzifanya kwenye migodi? Jibu, hakuna! Twende kwenye hoteli; angekuwepo kaka yangu Mheshimiwa Maige hapa ningemwuliza; Je, vijana wa Kitanzania wanapata kazi za staha kwenye hoteli au ndiyo wanaishia kuwa wafungua vizibo, watandika vitanda? Ndiyo kazi ambazo vijana wenzetu wanafanya. Lakini, Je, hawana elimu ya kutosha ya kushika nyadhifa ambazo kila siku tumechoka! Tumezoea kuona wageni ndiyo wanaozishika kwenye hoteli, wageni wanazishika kwenye migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya tu kwa upande wa hoteli, leo hii Meneja akiwa mgeni, baada tu ya miaka miwili yule akiondoka, anayechukua nafasi ni mzawa. Sisi hapa kwetu tunashindwa nini? Hatuwezi kuwajenga vijana wetu au ndiyo tayari tumeshazoea kwamba kila kitu kizuri lazima kifanywe na wageni, tunajidharau wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa Azimio hili likitekelezwa kwa vitendo, vijana wa Kitanzania watanufaika na rasilimali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye migodi kule kwetu Nyamongo - Mara, ukienda kule utalia! Vijana wanavyohangaika kule. Lakini, kazi ambazo hazitoi jasho ndiyo wanapata wageni, kisingizio utaambiwa hawajasoma. Tuna Vyo vya Madini na tunajua kuna vijana wenzetu wengi tu wame-graduate na wana sifa: kwa nini, wasifanyiwe mpango huo wakanufaika na rasilimali zao wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndiyo kama nilivyosema, mazoea. Tunaamini kabisa jambo zuri ndiyo lifanywe na wageni. Matokeo yake vijana wa Kitanzania wanabaki wanahangaika, wamekuwa tu mashuhuda wa kuona rasilimali zao zinavyowafaidisha wengine, wao wamebaki wanataabika. Nami nasema kweli, vijana ni bomu litakalolipuka na wala siyo uongo. Siku hadi siku vijana wanazidi kuongezeka. Leo tuko zaidi ya asilimia 60, mwaka 2015 hapa tutafika asilimia 80. Tusije tukatengeneza chuki ya vijana na wazee na wala tusije tukatengeneza mazingira ya sisi pia kujipendelea kwa sababu waliokuwepo hawataki kutushirikisha vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Azimio hili, Ibara ya 11 imezungumzia ushiriki wa vijana wa kike na wa kiume kwenye vyombo vya maamuzi. Nashukuru pia suala hili limekuja kwa wakati muafaka. Tunakwenda kwenye mchakato wa Katiba Mpya. Katiba yetu ya zamani, mbali na kwamba inatambua sifa ya mgombea, mbali ya kwamba inatambua nafasi ya Viti Maalum kwa akina mama, imewasahau kabisa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sehemu yoyote ambayo inaongelea nafasi ya vijana, aidha Bungeni, Udiwani, Serikali za Mitaa wala za Vijiji. Sasa huu ndiyo wakati muafaka. Akina Ester leo tupo hapa, ni kwa ajili ya huruma ya UWT tu. Akina mama, Sofia Simba na mama Anna Abdallah, laiti wasingekuwa na huruma hiyo, leo tusingekuwepo hapa. Lakini hata vijana wenzangu walioshinda kwenye Majimbo, wanajua kazi waliyoifanya bila kujali itikadi zetu hapa za vyama. Wameshinda kutokana na wingi wetu wa kujiandikisha kupiga kura, hatukuwa na hela. Leo hii kijana wa Kitanzania hawezi kushinda Ubunge kama hana hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nalo lazima tuliangalie. Tunaweza tu tukaleta mapendekezo na ikatambulika ki-Katiba, jumla ya idadi ya Wabunge tuliopo, aidha iwe ya Viti Maalum au Majimbo, *at least* asilimia kadhaa au 40 wawe vijana. Au labda kule kwetu Mara tuna Majimbo 10, basi sema tu Majimbo manne Mkoa wa Mara watakaopatikana wawepo vijana. Lakini hapa vijana wanapata taabu. Yaani mpaka kijana ameingia humu Bungeni, cha moto amekiona! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusitengeneze mazingira hayo, na sisi tukijua wapigakura wengi, tukasema mwaka 2015 hakuna mzee atakayeingia humu! Eeh!, Kwa hiyo, tusitengeneze mazingira hayo kabisa! Tunaomba tusaidiane ili kuhakikisha kila uwakilishi unakuwepo kwa usawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naamini kabisa hakuna kijana ambaye ataacha kuunga mkono. Lakini nasisitiza Maazimio haya yafanywe kwa vitendo na yasiishie kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Bulaya kwa mchango mzuri wa kisomi. Hongera sana.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia Azimio hili kuhusu vijana, kwa sababu ukiacha tu kwamba Azimio linataka vijana, mimi mwenyewe ni kijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa jambo la kwanza, kwa kuwa wenzangu wote wamezungumzia kwamba tumeondokewa na wenzetu, wapendwa wetu, Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, pamoja na baba yetu Mheshimiwa Jeremiah Sumari, tunachoweza kusema tu ni Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Nasi tunaamini huko waliko wataendelea kutuombea na ipo siku na sisi tutafika. Lakini, leo wajue kwamba tunajadili vijana, kama mzee na yeye alikuwa kijana, mzee Sumari na Regia bado alikuwa katika umri wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wazi kabisa kwamba ujana ni mapito kwa sababu nitakapozungumzia ujana wa leo, haina maana kwamba Silinde maisha yake yote ya milele atakuwa ni kijana. Naamini kabisa miaka kama 15 ijayo nitakuwa katika umri wa watu wazima nikielekea uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana katika Taifa letu ndiyo kwa sasa walio wengi kuliko idadi nyingine yoyote. Tunapozungumzia vijana, tunaposema Taifa bila vijana ni sawasawa na Jeshi bila askari, hapo ndipo unakuwa unazungumzia masuala ya vijana. Unapozungumzia vijana, unazungumzia nguvu kazi ya Taifa letu, watu ambao kwa kiwango kikubwa ndiyo wanaoingiza pato la Taifa hili kwa ajira zilizo kamili na ambazo siyo rasmi. Kwa hiyo, hii inaeleweka wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, nimefurahishwa sana na kuletwa kwa Azimio hili. Lakini nilitaka angalau hata Serikali itueleze ni kwa nini Azimio hili limecheleweshwa tangu mwaka 2006 ambapo Rais alilisaini mpaka mwaka huu? Kwa sababu mimi nakumbuka mwaka 2006 ndiyo nilikuwa naingia mwaka wa kwanza Chuo Kikuu cha Dar es salaam, tunahitaji sasa Serikali itueleze, kwa nini limechelewa kwa

kiwango hiki? Nikiwa mwanafunzi, lilisainiwa; nikiwa Mbunge, nalipitisha! Ni nini hapa katikati kilitokea? Kulikuwa na tatizo gani? Kwa hiyo, tunahitaji Serikali mtujibu hili. Miaka sita ni mingi sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye upande wa elimu, pamekuwa na matatizo makubwa sana kwa kipindi cha sasa. Asilimia kubwa ya vijana wa Tanzania ndiyo walioko katika Vyuvo vya Elimu ya Juu na Sekondari kwa sababu Shule za Msingi ni watoto. Sasa unapokuta Sera ya Elimu ya Juu inashindwa kuwasaidia vijana kupata elimu bora hususan kwenye kupata mikopo ambayo itawawezesha wao kuendesha masomo yao, maana yake unaona kabisa kwamba hapa pana walakini na mwenendo mzima wa Serikali kwamba Serikali haitendi haki, Serikali haiwasaidii vijana kwa ajili ya kujenga Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojenga mazingira ya kuwabagua Watanzania kwa mikopo kwa makundi yao, kwamba huyu apate *grade "A"*, huyu apate *grade "C"* na wote ni Watanzania, maana yake ni kwamba tunajenga ubaguzi wa Taifa lijalo. Ndiyo maana aliyepata daraja "A" atasema mimi nimependelewa na Serikali, na aliyepata "D" atajutia ile nafasi yake na hata siku za baadaye akija akipata ajira katika sekta yoyote ile na yeye atafanya kama alivyotengwa kwa sababu mfumo wa makundi katika elimu ya juu maana yake mnawatenga Watanzania. Ni bora ikaeleweka wazi kabisa kwamba kuna wanafunzi wa binafsi kwa maana ya *private* na kuna wanafunzi wa *public* kwa maana ya Serikali, watu ambao wanasomeshwa kwa asilimia mia moja. Ingefurahisha zaidi kwamba Serikali ingewekeza zaidi katika elimu. Hili sisi tungeweza kuwaunga mkono. Lakini sasa hivi migogoro ya elimu ya juu imekuwa ni mikubwa na wanaoteseka na migogoro hii ni vijana kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu gani tunayohitaji kuizungumzia? Vijana wa vijiji wametengwa sana kwa sababu asilimia kubwa ya watu wanaopata elimu ni wa maeneo ya mijini. Sisi ambao Majimbo yetu ni ya vijijini tunafahamu hiyo adha. Ukiangalia matokeo ya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita, vijana walioathirika kwa kufeli zaidi ni vijana wa vijijini na hao ndiyo tunasema asilimia kubwa ndiyo wamekuwa wanaathirika sana na mfumo mzima wa elimu. Lakini haya ni makosa ya nani?

Mimi siamini kabisa kwamba ni makosa ya wananchi wetu, haya ni makosa ya mfumo mzima ambao ulitengenezwa tangu awali. Tunachopaswa wote kwa ujumla, Serikali lazima isikilize, na sisi kama wadau ambao tunatoa maoni yetu, lazima myafuate kwa sababu hawa ndio watu ambao tunategemea kabisa kwamba Taifa la baadaye ndiyo litakuwa linaongozwa nao. Mimi siamini kabisa katika dhana ya kwamba vijana ni Taifa la kesho, mimi naamini kabisa katika dhana kwamba vijana ni Taifa la sasa, wazee ndiyo wanaopaswa kutushauri kwa wakati huu kwa sababu sisi ndiyo nguvu ukazi ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye masuala ya ajira. Vijana ndiyo wamekuwa waathirika Wakuu katika hii *issue*. Hii ni kwa sababu gani? Ukiangalia ajira zote za msingi, Makatibu Wakuu utaona pana *limit* ya umri. Ukiangalia Wakurugenzi, utaona kabisa hakuna vijana. Haina maana kwamba tunahitaji kwamba vijana ndiyo wachukue nafasi zote, hapana. Tunachohitaji ni kwamba pawepo na mchanganyiko na ndiyo maana Mheshimiwa mwenzangu aliyetangulia amejaribu kuzungumzia changamoto ambazo baadhi ya sisi vijana tulizipata wakati wa uchaguzi ambao tuligombea katika Majimbo mpaka kushinda. Tunajua adha ya kwa nini tulikuwa hatuaminiwi. Kiuhalisia, jamii yetu tangu awali ina mtazamo wa kwamba kijana sio mtu mwenye uwezo, lakini sasa hivi imedhihirika wazi kwamba kweli hata vijana tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilipokuwa nagombea, watu walikuwa wanasema: "Sasa pamoja na kwamba ana uwezo wa kujenga hoja, ana watu wanamfuata, na nini, lakini bado ni kijana! Bado ni kijana. Kwa nini asisubiri miaka mitano/kumi ijayo ndiyo tumpeleke Bungeni." Sasa hii ndiyo dhana ya Taifa. Sasa dhana hii inajengwa na nani? Ukikuta kama unagombea kwa upande wa *opposition*, watu wa upande wa pili ndiyo wanazungumza, kweli ni kijana anayefaa! Lakini jamani, bado ni kijana tumpe muda! Sasa hii dhana ni lazima iondoke kwamba kila mtu ana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha kwenye suala la umri, ujana vile vile ni mtazamo. Unaweza kuwa mzee, lakini vilevile ukawa na mtazamo mzuri wa ujana. Lakini kwa Azimio la leo linataka vijana kwa mtazamo wa umri. Ninachoamini kabisa ni kwamba kijana yeyote unapokuwa kijana maana yake unakuwa na nguvu, na ndiyo maana hata leo hapa ukisema mimi na mzee Pinda tupange ngumi kidogo, naweza nikamsumbuasumbua sana kwa sababu nguvu zangu kidogo ziko imara. Lakini wao kwenye

busara wako juu zaidi kuliko mimi. Ndiyo maana ya ujana. Ujana ni ufahari kidogo na hili ni lazima mlijue. Kwa hiyo, tunalohitaji katika hili, lazima mwazingatie vijana kwa kiwango kikubwa, siyo kama ambavyo imekuwa inazingatiwa kwa wakati huu uliopo. Hii kama tutaendelea kufanya vizuri, ndiyo itakayotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia machafuko yaliyotokea Misri yalikuwa ni mienendo midogo tu kwamba kijana wa Chuo Kikuu alikuwa anafanya shughuli za kimachinga, askari mgambo wakaenda wakamnyang'anya, vurugu zikaanzia pale pale. Matokeo yake, Rais akang'oka na utawala mzima wa nchi ya Tunisia ukatoka, ni kwa sababu waligusa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pamekuwa na malalamiko makubwa sana na hii Serikali lazima mmfahamu kwamba vijana kwa kiwango kikubwa wamekuwa wakilalamika kila mahali ukienda. Ukienda, vijana wanasema Serikali inatutenga, Serikali haitupi ajira, Serikali haituhusishi katika masuala ya kilimo, Serikali haituhusishi katika masuala ya siasa. Karibu katika kila jambo vijana wamekuwa wakilalamika. Mbaya zaidi, wazee wetu mmekuwa mnaziba masikio. Sijui niseme!

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua, Afrika ni tofauti sana na wenzetu wa Ulaya. Ulaya kijana anakuwa na nguvu ya kuweza kumwambia hata mzee wake, "ni lazima unisomeshe." Lakini kwa upande wa Afrika haya mambo ni tofauti. Afrika unachotakiwa, mzee akishasema, inabidi ukubali tu hivyo hivyo. Lakini, hii tabia tutaendelea nayo mpaka lini? Maana kama wote tutaendelea kufikiri kama miaka ya zamani, basi kwa utaratibu huu hatutafika. Kwa hiyo, ajira lazima zizingatiwe kwa vijana wote kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwenendo mzima huu ambao umekuwa ukiendelea siku zote kwamba lazima kijana ajiriwe kwa uzoefu, hili liondoke. Uzoefu ataupata kule kule anakokwenda kufanya kazi. Hata sisi mgetuambia kwamba ili ugombe Ubunge, lazima uwe na uzoefu, maana yake usingekuwa hapa. Lakini leo tuna uzoefu mzuri, na tunaamini tunakoeleka mbele, tutakuwa wazuri zaidi na tutaweza kulisaidia hili Taifa. Kwa hiyo, hili liondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana katika siasa, hili nalo limekuwa ni tatizo. Lakini tatizo lake ni katika miaka hii iliyopita. Mwaka 2015 nafikiri utakuwa ni mwaka wa kipekee sana na wa kihistoria katika nchi hii kwa sababu sasa hivi ari ya vijana katika siasa imeamka na wazee hili lazima mlifahamu kabisa kwamba kweli vijana sasa hivi wameamka na wengi wamesema kabisa mwaka 2015 watajitokeza na mifano halisi ni mimi Silinde. Mheshimiwa Ester Bulaya alisema kwamba kijana ili ushinde ni lazima uwe na fedha. Siyo kweli. Mimi kusema ukweli, Silinde nilishinda, nilikuwa na Sh. 25,000/= tu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyonirudisha Jimboni, na *at the end of the day* nilishinda bila gharama yoyote. Kwa hiyo, hata vijana wanaweza kushinda bila gharama yoyote. La msingi wawe majasiri na wawe na nia thabiti ya kuweza kulitetea Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Katiba yetu inasema kijana wa umri wa miaka 18 ndiye anayeruhusiwa kupiga kura. Lakini kijana wa umri wa miaka 21 na kuendelea ndiye anayeruhusiwa kugombea. Sasa unamrusu kijana wa miaka 18 lakini hana haki ya kugombea. Wakati huo huo unawatenga, miaka 18, 19 na 20 hawa wanaruhusiwa kupiga kura tu, hawaruhusiwi kuongoza.

Nafikiri hapa palikuwa na mantiki. Ukitaka kuruhusu, basi ruhusu kama ni miaka 21 kuendelea wote wapige kura. Ukitaka kusema kwamba miaka 18, basi apewe vile vile ya kugombea. Kuna nafasi mbalimbali za kugombea; Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji, Ubunge, Udiwani na Urais vilevile lazima mtuzingatie safari hii. Kwa hiyo, kidogo mshushe, maana mkiweka miaka 40 ni mingi. Mshushe kidogo hata iwe 30 hivi mwone kazi itakavyokuwa. Kwa hiyo, nafikiri mambo yatakwenda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Kitanzania kwa nyakati za sasa kusema kweli maendeleo yao kwa ujumla yako chini. Vijana wa Vijijini kwetu sisi tunakotoka ndiyo ambao wengi ni masikini kupita maelezo. Sasa kinachohitajika sasa hivi, mmekuwa na utaratibu mzuri, mnahitaji kuanzisha Benki ya Vijana. Lakini, hii Benki ya Vijana mimi ninachotaka, isianzishwe na Chama cha Siasa wala Taasisi fulani. Kama ni kuanzishwa, ianzishwe na Serikali yenyewe. Maana ikishaanzishwa ndani ya Serikali, tunaamini kabisa kwamba Serikali pamoja na kwamba inaongozwa na Chama fulani, lakini ikishaingia madarakani, tunaamini kwamba haifuati milengo ya Vyama vya Siasa.

Kwa hiyo, tunachohitaji kutoka kwenu, Serikali ndiyo ianzishe Benki, siyo kama sasa hivi tunaambiwa kabisa kwamba sijui wale wanaoanzisha Benki, mmoja sijui ni Katibu Mwenezi wa Chama fulani! Ile haiteti picha nzuri kwa Watanzania kwa ujumla. Kama mnaweka hata ile *Board of Directors*, watu wanaokuja kuanzisha ile Benki, wahusishwe Watanzania mbalimbali kutoka maeneo mbalimbali, mchukue watu kutoka Mikoa, Mara, Mbeya na maeneo mengine, hii itasaidia na hatimaye tutakuwa tunajenga Taifa ambalo sisi wote tunalihitaji ambalo naamini kabisa kwamba ninyi wazee wetu ndiyo mnakotaka tufikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania ni maskini, maana yake kulikuwa na kipindi mlituambia kuna mabilioni ya JK ambayo yalielekea maeneo ambayo yalikuwa hayafai. Kwa ujumla watu ambao ni wazee, siyo wazee ni makampuni ndiyo ambayo yalipatiwa hii kitu.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, mimi naomba kuwasilisha na ninakubaliana na Azimio la Vijana, lakini haya niliyoyazungumzia yafanyiwe kazi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunapoendelea kuchangia pamoja na uzuri wa michango hii, lakini ninaomba niwakumbushe Kanuni yetu ya 151 na ili iweze kueleweka. Basi niirudie tu kwa kuisoma, inasema hivi: "Endapo itatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge, basi Spika atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote."

Pili, inasema: "Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa wamusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni."

Tatu, inasema: "Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali."

Nne, inasema: "Baada ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Waziri yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni."

Ingawa kwa kweli, naamini watu wengi wameguswa na mambo mbalimbali yaliyotukuta na hasa misiba, lakini basi umuhimu wa kufuata Kanuni na wenyewe unatutaka tujaribu kuokoa muda kwa sababu hiyo. Naamini Spika na Kiongozi wa Serikali wamefanya hayo, kwa hiyo, tuendeleo na mijadala na haya mengine basi tutatumia fursa nyingine kuweza kuwapa pole ndugu zetu hawa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, sasa namwita Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyariba Nyangwine atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na baadaye Zainab Kawawa.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianza kwa kutoa shukrani kwa Waziri pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani na yule Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii hususan katika suala hili la Mkataba wa Vijana wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wasiwasi wangu pamoja na kuunga mkono hoja zote ambazo zimeongelewa na Wajumbe waliotangulia na mwasilishaji, lakini wasiwasi ni kwamba haya tunayoyazungumza ni kweli yatatekelezwa? Kama haya yatatekelezwa, ina maana tutakuwa tumeondoa matatizo yote ya vijana. Kwa hiyo, vijana wa Tanzania na vijana wa Afrika watakuwa katika hatua nzuri sana ya kupata maendeleo, kupata elimu, maana mkataba umeongelea vitu vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri alisikie hili na kwamba afanye kazi ya ziada akihusisha Watanzania wote kuhakikisha kwamba yote yanayojadiliwa katika mkataba huu yatatekelezwa, na zaidi

vijana wapewe mkataba huu wausome. Nafikiri kama vijana wakiusoma watapata changamoto nyingi sana za kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuongelea maudhui yaliyomo katika mkataba huu, mkataba huu unajadili mambo mengi, unajadili wajibu, unajadili haki, na mambo mengine mengi tu. Lakini nianze na Ibara ya 14 ambayo inasema uhuru wa kutoa mawazo. Kijana wa Afrika, kijana wa Kitanzania anatakiwa atoe mawazo katika jumuiya mbalimbali, katika uzalishaji mali na hata katika Mikutano ya kisiasa, lakini hayo mawazo nasisitiza, yawe ya kujitegemea, yasiwe mawazo tegemezi. Sana sana, sasa hivi tunaangalia vijana wa Tanzania wanatumika katika siasa, wanatumika katika fani mbalimbali hata katika uzalishaji wanakuwa ni watumwa.

Nawaombeni vijana wa Tanzania wasiwe watumwa, wajitegemee kimawazo na sana ukienda hata katika mfumo wa siasa ukipita vijiwani, vijana wanalalamika; ukipita kwa mfano Sinza, Ubungo, vijana wanalalamika, wanasema kwamba, (samahani naomba nitumie neno moja ambalo vijana wanatumia vijiwani lakini siyo rasmi). Wanasema kwamba vijana wa sasa hivi wanatumika kama *condom*. Naombeni Vijana wa Tanzania wasitumiwe kama *condom*, vijana wa Tanzania watumike kuendeleza nchi ya Tanzania, vijana wa Tanzania wawe wazalendo na sana utakuta hata baadhi ya watu wanaokimbilia nafasi mbalimbali za uongozi kila mmoja anasema kwamba nitatutua matatizo ya vijana. Vijana wamekuwa ndiyo mtaji wa kujipatia umaarufu kiasiasa. Mimi naomba hilo likome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili litakoma endapo vijana wa Watanzania tutajitegemea katika fikra na katika mawazo yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ajira kwa vijana. Katika ibara ya 15 ambayo inaongelea ajira kwa vijana, vijana wa Tanzania na vijana wa Afrika hususan, wanasema kwamba uzalishaji wa vijana upatiwe kipaumbele katika kupata ajira. Vile vile wamesema mara nyingi sana kijana akitaka ajira anaambiwa awe na uzoefu wa miaka 15. Mimi nasema kwamba kwa sababu vijana wengi wamesoma na wanakwenda *field*, nasisitiza kwamba katika uajiri kwenye Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali hata katika maeneo ya watu binafsi au uwekezaji, jambo la kuajiri vijana liwe asilimia 60, asilimia inayobaki kama 40 iwe ya watu ambao wamevuka umri wa vijana. Hiyo itasaidia sana kuwawezesha vijana kiuchumi. Lakini sasa hivi kijana anaambiwa kwamba ili apate ajira, uzoefu wa miaka mitano, miaka 10 au miaka 15 ina maana anapata ajira akiwa na miaka 26 wengine mpaka miaka 30, akipata sasa hivi miaka 15 ina maana anapata ajira akiwa na miaka 45. Akianza na miaka 45 baadaye miaka 50 anaambiwa astaafu. Sasa hivi umri wa Mtanzania kuishi haizidi hata miaka hamsini. Hili jambo kwa kweli linahitaji kuangaliwa sana katika utekelezaji wa mambo mengine ambayo yatakuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri suala hilo lifanyiwe kazi na sana sana vijana wawezeshwe kujijiri wenyewe hasa kwa kuanzisha hiyo benki ya vijana. Mimi nashauri, hakuna haja ya kuwepo na *Board of Directors* kutoka sehemu mbalimbali kama wenzangu walivyokwisha sema, wawe ni vijana wenyewe, kuna vijana ambao wamesoma, wana shahada nzuri za uchumi, hao vijana wakiendesha hiyo benki wenyewe na mtaji wakajiweka wenyewe, Serikali ikawawezesha, mimi nafikiri tutaweza. Lakini tukisema kwamba Bodi ya Wakurugenzi ni wazee wa miaka 60, 70, wastaafu, hakuna chochote kitakachofanyika. Hilo tulisahihishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika ibara ya 12 Sera ya Taifa ya Vijana, kweli Taifa la Tanzania halina sera ya vijana ambayo inawawezesha ndiyo maana kila kijana anajisemea mambo ovyo, vijana wengine hawana maadili, na sana vijana wamekosa mwongozo.

Nikinukuu inasema kwamba: "Sera ianzishwe haraka iwezekanavyo na kuletwa hapa Bungeni ili tuiipitishwe haraka na hii ndiyo itakayokuwa dira kwa vijana. Sera ifafanue zaidi juu ya changamoto zinazowakabili vijana na namna ya kukabiliana na changamoto hizo na sera ya maendeleo kuhusu vijana na wamesema kwamba kutakuwepo na uteuzi wa watalaam ambao wataunda dawati la vijana." Hilo dawati la vijana naomba kwamba hawa watalaam wawepo vijana wenyewe na hao vijana wengine watoke vijijini, wengine watoke mijini, maana tunapongelea mambo kama hayo, tunasahau vijana wa vijijini. Vijana wa vijijini wana shida, ukiacha vijana wa mjini ambao kwa kweli wana ujanja wa kupata namna ya kuishi, lakini vijana wa vijijini kule wana shida sana. Naomba hilo jambo tuliangalie katika

kuanzisha sera ya vijana na hasa dawati la watalaam la vijana, vijana wahusishwe kutoka pande zote za nchi na sana watoke vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya maendeleo na ujuzi, kijana apate elimu bora kama huu mkataba unavyositiza. Sasa hii elimu ni ya aina gani ambayo kijana ataipata? Nchi ambayo sasa hivi ina matabaka mengi, nchi ambayo elimu inatolewa kulinga na wenye uwezo na wasiokuwa na uwezo, hili jambo naombeni siyo kwamba ni Wizara ya Vijana tu yenyewe itakayoweza kusamehe hili suala, pamoja na Wizara nyingine na sisi Watanzania kwa ujumla, kwa sababu sasa hivi imegawanyika katika matabaka makubwa sana. Wenye nacho na wasiokuwa nacho. Wenye nacho, wanasomesha watoto kwenye shule ambazo zina kila kitu, na zaidi watoto wetu wanalazimishwa kusoma lugha nyingine za kigeni, analazimishwa asome Kiingereza na Kifaransa.

Sisi tunaajivunia Kiswahili, hao vijana wengi ambao sasa hivi wanasomesha katika shule hizi za academia, mimi naona tunajenga tabaka ambalo kwa kweli litakuja kutugarimu huko siku za usoni. Tusitize umuhimu wa vijana wetu kusoma na wapate elimu katika lugha ya Taifa, vile vile hatutasahau lugha nyingine za mawasiliano kama Kiingereza, Kifaransa na lugha nyinginezo. Lakini katika hizo shule zinazofundisha masomo ya kimataifa, tusitize somo letu la Kiswahili lifundishwe, hapo tutakuwa tunaondoa matabaka katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile elimu ya ujasiriamali ifundishwe hadi vijijini. Vijana wajitokeze wafundishwe na vile vile washirikishwe namna watakavyoweza kuanzia mitaji mbalimbali itakayowawezesha kujimudu kimaisha.

Pia elimu ya uzalendo pia ifundishwe mashuleni. Mtoto anapoanza kusoma aanze kujifunza Mtanzania ni nani? Mtanzania anafanya kazi gani? Mtanzania ana wajibu gani katika nchi yake? Kwa nini Mtanzania amezaliwa Tanzania? Kwa nini aitwe Mtanzania? Mambo kama hayo tukiyafanya na tukiyatilia maanani tutajenga uzalendo katika vijana wetu, na sana nasisitiza Wizara hii iangalie namna itakavyowawezesha vijana wawe wazalendo. Zitungwe nyimbo za kizalendo za kuenzi na kuheshimu utukufu na historia ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 14 inazungumzia utokomezaji wa umaskini kuwawezesha vijana kiuchumi. Hapa nitaongelea suala la madini ambalo limeongelewa katika ibara hii, kwamba vijana watawezesha kumiliki madini. Mimi kwa upande wangu kule Nyamongo kila siku nagombana na wawekezaji kwamba wawezeshwe wale vijana, kuwe na mfuko maalum wa wachimbaji wadogo wadogo ili hao wachimbaji ambao wengi ni vijana wanaofanya kazi hatarishi waweze kujitegemea. Wasiishie katika kuzalisha tu, kila siku wanazalisha na wanachozalisha hakiwanufaishi, kinawanufaisha watu wanaotoka nchi wekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo naomba hata katika sera hii mtakapokuwa mmetunga mwangalie namna kijana atakavyoweza kumiliki rasilimali za Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwepo viwanda vidogo vidogo hasa *SIDO*. Vijana waajiriwe na elimu ya *VETA*, Vyuho vya *VETA* visaidie sana kuimarisha vijana wapate ujuzi. Tumesema kwamba vijana wawezeshwe kisayansi na kiteknolojia, lakini haya mambo yanakuwa ni nadharia tu. Tuangalie namna tutakavyoweza kufanya elimu ya *VETA* ifike hadi vijijini. Kila Wilaya tunaweza kujenga Chuo cha *VETA*. Naamini katika kufanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia vijana kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nisisitize wajibu wa kijana. Kijana wa Tanzania anatakiwa atoe mchango mkubwa katika nchi yake. Wajibu wa kijana wa Tanzania asiishie kulalamika tu kwamba kila siku anapokaa analalamika kwamba Serikali imfanyie hivi, Serikali ifanye hivi, hayo mambo yanatuponza. Wajibu wa kijana ni kuhakikisha kwamba anajitegemea, awatunze wazazi wake na yeye mwenyewe ajitunze. Lakini tukiishia kwamba kila siku kulalamika, tunajenga Taifa la walalamishi. Hili Taifa la walalamishi kwa kweli nina wasiwasi tunapoelekea huko siku za usoni. Kwa kweli tutakuwa tunajipalia mkaa ambao utakuja kutuumiza, sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana sasa hivi wafundishwe namna ya kujitegemea tangu wakiwa watoto wadogo shuleni, vyuoni na anavyomaliza elimu ya Chuo Kikuu, kijana awe ana uelewa mkubwa sana na upana mkubwa sana wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana nimeona katika mkataba huu, vijana wanaoishi nchi za nje wanatakiwa waendeleze nchi ambayo wametoka hasa katika nchi ya Tanzania. Utakuta baadhi ya vijana wanaoishi nje ya nchi, ukienda kwa mfano Marekani, China, Japan, na Uingereza, wale vijana wetu wengi ni kama watumwa, wanafanya kazi za kitumwa, na mchango wao mkubwa katika nchi hii ni mdogo mno. Nafikiri tuangalie namna tutakavyoweza kuita vijana wote ambao wanafanya kazi hata nje ya nchi, tuite hata *Tanzania Day* tukutane vijana wote tuweze kujadili mambo ambayo yanahusu Taifa letu. Tutapata ujuzi kutoka Mataifa wanakokaa na sisi kutoa mchango wetu na tukiunganisha pande zote hizo mbili tunaweza tukapata kitu ambacho kitawezesha tukawa na dira ambayo inaeleweka kwa vijana. Hilo linawezekana, kwa sababu hata ukiangalia kule China wanafanya vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naomba hayo yote yafanyiwe kazi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nyambari Nyangwine kwa mchango mzuri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Halima Mdee, na baadaye Mheshimiwa Zainab Kawawa na kama muda utaturuhusu, basi Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Azimio la Bunge muhimu sana kwa madhumuni ya kuridhia Mkataba wa Vijana Afrika.

Natoa mchango wangu kwa kuiambia Serikali kwamba ukiona mwenzako ananyolewa, unatakiwa utie maji. Waliopita wamezungumzia kuhusiana na harakati zilizotokea Barani Afrika, hususan nchi tatu za huku *Northern Africa, Egypt, Libya, Tunisia*, chanzo chake kilikuwa ni vijana kuchoshwa na Serikali na ahadi ambazo hazitekelezeki zinazosababisha maisha kuzidi kuwa magumu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunapopitisha Azimio leo, kama ambavyo vijana wengine toka CCM, CHADEMA walivyozungumza, yaliyomo humu tukayaweke kwenye mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepitisha mpango wa miaka mitano, lakini leo anaweza akaniambia Waziri yeyote hapo kwamba katika hiyo mipango ya miaka mitano, kuna hoja inayohusiana na kumkwamua kijana wa kitanzania kutoka katika umaskini? Nyingi ni blaa blaa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tuna uwezo wa ku-review, kila mwaka ukipita tuna-review mipango yetu, nina uhakika katika mipango yetu tukiweza kuangalia kilichomo humu na kujua kwa namna gani tukikiingiza katika mipango yetu kitamsaidia kijana, ni busara tukafanya hivyo. Lakini tukipuuza kuna hatari na sisi kunyolewa. Sisi kama vijana wa Kitanzania tunataka Tanzania yenye amani. Hatutaki tuje tunyolewe! Tunaomba watu ambao mmepewa dhamana, isiwe kama mazoea, tunaleta hoja tunazipitisha, inapokuja kwenye utekelezaji inakuwa ni yale yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia moja kwa moja kwenye mkataba wetu ambao pia umecainishwa kwa kifupi kwenye Azimio, Ibara ya 5(2) inazungumzia vijana kutokushurutishwa kujiunga na chama chochote cha siasa. Leo hii kwenye Vyuu Vikuu, kumekuwa na tabia mbovu sana ya kufukuza fukuza wanafunzi hovyo. Wanafunzi wanafukuzwa kwa sababu wanatekeleza wajibu wao wa kutetea maslahi ya wanafunzi wenzao, kama ambavyo watu wamekiri mapungufu ya Bodi ya Mikopo pamoja na vyombo vingine vinavyotakiwa visaidiane na Bodi ya Mikopo ili pesa za watoto wetu ziende kwa utaratibu unaotakiwa. Lakini pale inapotokea wanafunzi wanakwenda kudai haki zao za msingi, akionekana huyu mwanafunzi labda ana uhusiano ama ana mapenzi na Chama fulani cha Siasa, basi imekula kwake, anafukuzwa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kupitia Azimio hili, (Nchimbi naona anatabasamu) kupitia Wizara hii ambayo jukumu lake ni kutetea vijana, tutahakikisha tuna utaratibu ulio wa haki, siyo wanafunzi wanatetea maslahi yao, wapo wa CCM, wapo wa CHADEMA, inapokuja kuchukua hatua za kisheria wanapewa maelekezo kama CHADEMA arudishwe nyuma, *that is very wrong*, naomba hili Azimio tunalopitisha leo, na walimu huko Vyuoni, Wakuu wa Vyuu watusikie. Iwe ni mwiko kwa vijana wetu kufukuzwa Vyuu kwa sababu tu ana mapenzi na Chama fulani. Ni haki yake ya kikatiba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni Baraza la Vijana. Nchimbi anajua tokea na yeye yupo kijana, kama ambavyo Silinde amesema, hii imekuja akiwa mwanafunzi mwaka 1996 mchakato wa kuanzisha Baraza la Vijana, na iko kwenye Ibara ya 12 (i) - Vyombo vya kuratibu shughuli za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya leo tuna vyombo vya vijana vya Vyama vya Siasa, lakini ukiangalia asilimia ngapi ya Watanzania ni wanachama wa Vyama vya siasa? Kwa ujumla wake tupo milioni 46 hawazidi hata milioni kumi ya Watanzania ambao ni wanachama wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mtihani gani wa kuunda hili Baraza? Chombo ambacho kitakuwa kina mkusanyiko wa vijana kutoka kada mbalimbali watakaojadili mambo yao, watakaosaidia kupata sera ya Taifa ya vijana inayowazungumzia vijana na siyo inayozungumzia vijana wa CCM ama Vijana wa CHADEMA ama wa TLP na vyama vingine. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba, hili zoezi lilianza mwaka 1996 wengine tulianza kulizungumzia hapa mwaka 2006.

Nakumbuka Mheshimiwa Nsanzugwanko alikuwa anajibu hapa: "Ooh, litaundwa!" Sasa hivi ni mwaka 2012, ni aibu! Uzuri ni kwamba, hatujabadilisha utawala. Utawala ni ule ule wa Chama cha Mapinduzi. Ni aibu. Tutagharamika nini tukiunda hiki chombo kitakachosaidia kukusanya mawazo ya vijana, kujua vijana wanataka nini kwenye nchi hii ili tuweze kuviweka kwenye utekelezaji? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, naamini alikuwepo kwenye hizi harakati, naamini sasa amepewa jembe, anashikilia mpini. Afanye kazi yake, hili azimio liwe sehemu ya kuunda hilo Baraza letu la Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la elimu. Mheshimiwa Nyangwine amezungumza hapa kwamba Tanzania ya sasa elimu ni ya kibaguzi. Sisi ambao tuna kipato tutapeleka watoto wetu kwenye sijui *Saint* nini, wale ambao hawana kipato, watakwenda shule zinazoendeshwa na Serikali za Mitaa ama Shule za Kata. Tunaambiwa kuna fedha zinazopelekwa kama ruzuku. Mwaka jana kwenye bajeti hapa, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo kasema Shule za Sekondari 25,000, Shule za Msingi 15,000 kuweza kupunguza gharama za uendeshaji wa shule zetu kule chini, shule wanazosoma watoto maskini. Lakini leo nikimwambia anieleze kwa sababu mimi nimetoka Jimboni, uzuri naka Dar es Salaam, naka Jimboni, nafanya Mikutano na wananchi, fedha zimekuja, bajeti mwaka jana sasa hivi mwezi wa pili, tumeingia mwaka 2012 fedha hakuna. Fedha hazifiki. Michango haiishi, 200 kwa siku. Tunaambiwa watoto kusoma bure, Shule ya Msingi siyo pungufu Sh. 20,000/= mpaka Sh. 60,000/= wazazi wanachangishwa. Tumejenga Shule za Kata ili kupunguza gharama zisizokuwa na sababu.

Leo mtoto anatoka Kata 'A' anaka Msasani Shule ya Sekondari Goba wakati Msasani ameachwa mwanafunzi wa Goba. Kwa hiyo, haya mambo tunavyozungumzia elimu kupunguza gharama zisizo na sababu ndiyo hizi. Hatuwezi kuwaambia wazazi Sekondari, *Day* sijui Sh. 20,000/=, *Boarding* Sh. 70,000/= mzazi anakwenda analipa Sh. 300,000/=. Kwa hiyo, masuala kama haya lazima tuyafanyie kazi. Michango, ama tuwaambie ukweli Watanzania. Serikali ya CCM tumeshindwa kutoa elimu bure ili wale wenye uwezo wa kutoa elimu waje wapate fursa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba hili Azimio liwe chachu. Nchimbi shirikiana na Wizara nyingine, hivi vilivyoandikwa viwe vya kweli. Leo tunasema elimu bure, elimu zisizo na gharama, kesho kuna Sheria ya Bodi ya Mikopo inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitangulizi shughuli, lakini naweka angalizo kwamba Sheria ya Bodi ya Mikopo inafanyiwa marekebisho, kusema kwamba wanafunzi wanaopewa mikopo watatozwa riba kama itakavyoamuliwa na Waziri mwenye dhamana. Mkopo wa mwanafunzi wa Elimu ya Juu, leo akienda kulipa anatakiwa eti alipe riba. Sasa sijui ni elimu! Sijui imekuwa biashara! Sijui imekuwa nini! Kwa hiyo, naomba hili Azimio tukipitisha leo kama Bunge iwe ni chachu ya Wabunge kuungana na sisi Wabunge vijana kutetea vijana wenzetu kupinga pendekezo hili kandamizi linalotaka kuja kuhusiana na elimu. *(Makofi)*

Suala la mwisho kuhusiana na ardhi, Mheshimiwa Ester Bulaya amezungumza kwa mapana sana. Amesema kutolewa kwa msaada wa upatikanaji wa ardhi kwa vijana kama Taasisi za Vijana, nchi yetu leo kuna uvamizi wa mashamba ya watu usiokuwa na idadi. Kwa nini matajiri wamejilimbikizia ardhi? Vijana

wanahaha ardhi, inapambana vita dhidi ya wenye nacho. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ihakikishe kwamba ardhi tuliyonayo ambao ndio utajiri wetu mkubwa uliobaki unagawiwa pasipo upendeleo. (Makofi)

Nina ripoti ya CHC imefanya utafiti wa mashamba na viwanda ambavyo vilibinafsishwa. Katika mashamba waliyoyafanyia utafiti, 14 hayajaendelezwa kabisa, yana hekta zisizopungua 2000 kwenda 6000. 14 haijaendelezwa kabisa yapo humu. Kuna 19 ambayo yameendelezwa robo robo. Sasa kama hizi ni ripoti za Serikali, kwa nini washirikiane kuangalia hawa ambao walipewa maeneo makubwa wakashindwa kuendeleza? Tuna mpango gani wa kukusanya vijana kwa makundi? Mimi naamini hakuna kijana yuko Dar es Salaam anapenda kulala njaa kama kuna *opportunity*. Tunavyosema Kilimo Kwanza, tunataka tumsaidie nani kama asilimia 60 wapigike Mtaani? Kwa hiyo, vijana kukiwa kuna *incentives* za kilimo, watakwenda kulima, tusidanganyane. (Makofi)

Sasa mlipeana huku wakati tunakwenda kwenye ubinafsishaji, sasa mmeshaumbuka. Ripoti ya CHC ipo hapa. Sasa tutumie ripoti ya CHC kuangalia viwanda vilivyochakachuliwa wameshindwa kuvifanyia kazi, tuangalie mashamba yaliyochakachuliwa, wameshindwa kufanyiwa kazi, tuje na mpango muhimu wa kusaidia vijana wa Tanzania. Wenzenu hawakusikia wamenyolewa. Tusitake kunyolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri. Lakini nilitaka tu tuweke vizuri mambo hapa Kanuni ya 60 (16) inasema katika mjadala wowote Mawaziri watatajwa kwa majina ya nyadhifa zao na Wabunge watatajwa kwa kutumia neno Mheshimiwa kabla ya majina yao. Kwa hiyo, kwa faida ya baadaye, basi tunapotaja majina ya Mawaziri tuwataje kwa nyadhifa zao siyo Bwana Nchimbi, au nani. Kwa hiyo, nadhani tukiweka hivyo tutakuwa tunapata lugha ya kibunge zaidi.

Basi tunaendelea. Naomba nimwite sasa Mheshimiwa Zainab Kawawa na kama nilivyosema, muda ukituruhusu, basi Mheshimiwa Mkosamali atamalizia.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mada iliyoko mbele yetu. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomboleza vifo vya Mahayati Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wametangulia mbele ya haki, Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Sumari pamoja na Mtumishi wa Bunge. Nawapa pole familia za Marehemu. Najua kwamba wao aliwapenda Marehemu wetu lakini Mwenyezi Mungu aliwapenda zaidi na hivyo kama ilivyompendeza yeye akafanya vile ambavyo aliona inafaa. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono Azimio hili la Vijana la Kiafrika. Ukiangalia uhuishwaji wa vijana kwa rika kati ya umri wa miaka 15 hadi 35, ndio hasa vijana tunaowazungumzia leo. Lakini vijana hawa wa rika hili duniani kote ndio wanao-*determine* maendeleo ya Mataifa yao. Hivyo basi, Mkataba huu umekuja wakati muafaka japokuwa umechelewa na mimi naungana kabisa na vijana wenzangu kusema kwamba kwa kweli Azimio limechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vipengele vyote vilivyoainishwa humu, unapozungumzia afya unamzungumzia kijana; unapozungumzia elimu, unamzungumzia kijana kati ya rika fulani kwenda rika fulani. Kabla ya rika la miaka 15 kwenda mpaka labda 24 hivi wengine hata miaka 20, unapozungumzia ushirikishwaji wa maamuzi unamzungumzia kijana. Mimi nasema Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imekwishafanya mengi. Kama ni elimu imechukulia hatua kwa kujenga shule kadhaa; kama ni afya imechukulia hatua kwa kujenga Zahanati kadhaa; kama ni Miundombinu Serikali imechukua hatua kwa kujenga miundombinu ya barabara kadhaa. Sasa lazima tu-*invest* kwa vijana na ku-*invest* kwake ni kutekeleza hili Azimio pasipo na maneno yoyote, kwa kuwa sasa kwa kweli tumechelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyoko kwenye elimu ni mengi. Vijana wetu wa Vyuho Vikuu wana-*suffer*. Hivi juji juji palitokea habari ilinisitisha sana. Eti mtumishi wa Bodi ya Mikopo anadiriki kuiba fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi, vijana wetu hawa. Unamkwamisha mwanafunzi ashindwe kupata elimu iliyo bora, ashindwe kuelimika, matokeo yake anaamua kushiriki

kwenye maandamano, kwenye migomo, kwenye vurugu na wengine mpaka wanafikia mahali wanafukuzwa kwa sababu tu wewe tu mtumishi umeamua kuwa mwizi! Hatuwezi kuzungumzia elimu bora ya vijana kama sisi Watumishi hatuko tayari kuwajibika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia sana suala la ajira. Sitachoka kulizungumzia suala hili mpaka kieleweke. Duniani kote hata Marekani leo raia wanawapima viongozi wao kwa namna gani wameweza kukuza ajira kwa wananchi wao. Tunazo fursa nyingi za kutoa ajira, lakini vijana wetu wanalia hawana ajira. Usione vijana wanaandamana mkawachukia, wapeni kazi. Mtu mwenye kazi hawezi kwenda kuandamana. Wapeni kazi. (Makofi)

Hivi tuna viwanda vingapi ambavyo vimekufa leo ambavyo vingeweza kutengeneza ajira kwa vijana wetu? Tuna Kiwanda cha *General Tyre*, tena nilisema nitauliza swali kesho kwenye maswali ya Waziri Mkuu, hiki kiwanda kilifungwa tu. Ndio, kilifungwa na siyo kwamba mitambo ile haifanyi kazi, kimefungwa kwa sababu ya *mism anagement*. Sasa tuambiwe kiwanda hiki lini kitafunguliwa kwa sababu kikifunguliwa hiki kiwanda, tazama *network* iliyopo namna ambavyo kitaongeza ajira kwenye kiwanda tu pale. Kuna uhakika wa kupata ajira zisizopungua 1,500. Hizi ni takwimu zisizo rasmi. Lakini kile kiwanda tukiwa tuna mashamba ya *rubber* kule Muheza na Morogoro Kilombero kama sikosei.

MBUNGE FULANI: Mang'ola.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Ananisaidia, anasema Mang'ola. Tukiwa na mashamba ya *rubber* tuna-*produce rubber zenye quality* ya hali ya juu ambazo tukiweza kuzi-supply kwenye hiki kiwanda kwanza tutakuwa tume-supply ajira kwa vijana wetu walioko kwenye haya mashamba ya *rubber*, lakini pia na hiki kiwanda nacho kikifuliwa tutakuwa tumekuza ajira kwa vijana. Huo ni mfano mdogo tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa Serikali yetu, ninafahamu ime-*invest* kwa vijana, lakini lazima tu-*invest* kwa vijana kwa kuwapatia ajira. Hili ni bomu kubwa. Hakuna mtu ambaye yuko tayari kuamka asubuhi leo hajui anakula nini. Ukizungumzia afya katika Azimio hili vijana wa vijijini hawana ajira. Anatakiwa akajilipie afya. Hivi anajilipiaje kama hana ajira? Anajilipiaje zile huduma za hospitali kama hana kazi? Tunawawezeshaje vijana wetu wa vijijini kuwa na afya bora ili waweze kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nizungumzie suala la ardhi. Ardhi yetu ya leo kwa mazingira haya tuliyokuwanayo sisi vijana ni vigumu kupata, ni ndoto kupata. Yako maeneo ambayo watu binafsi tu wanauza mpaka Shilingi milioni 200. Hivi kijana mimi nitaweza? Haiwezekani! Nashukuru kwamba Azimio hili limeainisha hayo yote, lakini naomba wafanye utafiti wa kutosha, waweke mikakati ya kutosha kuhakikisha haya yote yaliyoainishwa kweli vijana wanayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa niwaombe vijana wenzangu kwamba na sisi kama vijana tuna wajibu wa kutii Sheria za nchi yetu. Tunao wajibu wa kujituma. Mheshimiwa Ester Bulaya asingefika leo kama asingejituma. Mheshimiwa Halima Mdee asingelifika hapo kama asingejituma na Waheshimiwa Wabunge wengine wote vijana, hata mimi nisingelifika hapa. Kama nisingefanya *efforts*, nani angenijua kama kuna Zainab Kawawa? Hakuna! Hata kama kuna maneno mengine huko, ooh, sijui Kawawa, lakini nasema hivi ni mfumo tu ambao umekuwepo duniani kote, tuna viongozi ambao watoto wao pia wamekuwa viongozi. Hata Marekani yuko George Bush, Zanzibar tunaye Karume, Kenya tunaye Uhuru Kenyatta, lakini wote hao wamejituma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono Azimio hili na naomba Wabunge wenzangu wote vijana tushirikiane kwa pamoja, tuunge mkono azimio hili. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Kawawa. Nilifurahi kidogo uliposema ningekuwa sikujituma, napiga picha ungekuwa umeolewa kule kijijini hali ingekuaje? (Makofi/Kicheko)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Mkataba huu wa vijana na mimi nikiwa Mbunge kijana kuliko wote humu ndani nilikuwa nasikitika kweli! Nasikitika kweli! Kwa hiyo, nashukuru sana Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba na mimi niseme kabisa kwamba mkataba huu umekuja kwa kuchelewa, lakini tunashukuru na tunafurahi kwa Serikali kuleta Muswada huu. Lakini wasiwasi wangu ni utekelezaji wa haya yalioko kwenye mkataba huu kwa sababu huu ni mwendelezo wa mikataba ya haki za binadamu mbalimbali ambayo imekuwa inasainiwa na kuridhiwa na Serikali yetu. Lakini mingi imekuwa haitekelezwi ipasavyo.

Katiba yetu ya nchi, Ibara ya (9) inatambua tamko la haki za binaadamu ambapo kwenye haki zile zinahusu pia vijana, lakini imekuwa haitekelezwi ipasavyo. Kuna mkataba *International Covenant on Civil and Political Rights* tumeuridhia, lakini vijana tumekuwa tunapuuzwa kwenye mambo ya kisiasa muda mrefu. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba tunaridhia mkataba, lakini tunaomba yaliyoko humu ndani yatekelezwe ipasavyo kwa sababu nchi ni ya vijana, wala wazee hili hamwezi kupinga. Ndiyo maana hata leo kama mmetuona vijana tunavyochangia, vijana wa vyama wote tumekuwa na lugha moja na hii inaonesha namna gani tuko makini na tumeweza kujipanga bila itikadi za Vyama. (Makofi)

Pia tunataka turudishe historia kwa sababu vijana ndiyo waliokomboa Bara la Afrika. Mwaka 1945 wakati inafanyika Manchester pale *Africanism Conference* ni vijana waliokuwa wanasoma Vyuu Vikuu Ulaya, akina Obote, Nkhuruma ndiyo waliokwenda kupanga namna gani wakomboe Bara la Afrika. Sasa mnavyoona tunachangia kwa namna hii, tunaeleza mambo yanayotuhusu, mfahamu kabisa kwamba tumeanza kujipanga.

MWENYEKITI: Mimi sio mzee bwana. Mimi kijana bwana! (Kicheko)

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 tunaomba vijana wengi sana wajitokeze kwenye Majimbo ili tuongeze kutetea vijana, maana sisi ndiyo wengi kwenye nchi hii na tunapaswa kuwa wengi pia ndani ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja mbalimbali. La pili, ajira. Hivi Serikali mimi naweza nikasema haifahamu ni vijana wangapi wana kazi na wangapi hawana kazi. Haifahamu! Haifahamu vijana wakulima wangapi wamelima mwaka huu, wangapi hawajalima, wangapi wamepata mbolea, haifahamu! Haijui waliomaliza Vyuu mwaka jana, wangapi wameajiriwa, wangapi hawaajiriwa, hawafahamu! Ndiyo nchi yetu ilivyo. (Makofi)

Sasa mimi ningependa kuwashauri kwamba Wizara ya Kazi na Ajira ilitakiwa ndiyo ishughulike na vijana, Habari, Utamaduni na Michezo ibaki Idara nyingine. Vijana sasa hivi wimbi la kukosekana kwa ajira ni kubwa sana, kwa hiyo, ni lazima tuwe na Idara. Huwezi ukaweka watu ambao wanatakiwa kuajiriwa, ni wengi! Unawaweka kwenye Wizara nyingine, halafu Wizara nyingine inashughulika na mambo mengine ndiyo maana haya yanatokea nchi hii inataka kuajiri wazee kuliko vijana. Unaposema mtu aajiriwe akiwa na uzoefu wa miaka 15, amemaliza Chuo ana 26, maana yake hutaki vijana waajiriwe. Ndiyo maana yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria zetu za Hifadhi ya Jamii, *Social Security* hazitambui namna gani ambavyo vijana ambao hawako kwenye ajira, wako kwenye *informal sector* kama waendesha boda boda hawa watanufaika wakati wa uzeeni kama zilivyo Katiba za wenzetu. Kwa mfano, Katiba ya Afrika Kusini, inatambua mifumo ya namna hii. Vijana hata ambao hawako kwenye mfumo rasmi wa ajira wanaweza wakajijwekea hifadhi yao na wakanufaika. Soma Ibara ya 27 ya Katiba ya Afrika Kusini. Kuna mfumo pale unaitwa Ubuntu, tunapashwa na sisi tuingize mambo haya katika mchakato huu wa Katiba. (Makofi)

Vijana wameachwa, wamepuuzwa huko, wanaendesha pikipiki, tena wengine wanaonewa kweli kweli! Mimi kule Jimboni kwangu kuna kijana mmoja amenunua baiskeli Sh. 100,000/=, amekamatwa na Polisi anaambiwa alipe fidia Sh. 80,000/=. Hayo ndiyo mambo ya kuwakandamiza vijana. Yaani baiskeli ya Sh. 100,000/= anaambiwa ana makosa manne, alipe Sh. 80,000/=! Ni mambo yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja nyingine ya tatu, kuhusu elimu. Mfumo wa elimu, kwanza utoaji wa mikopo unapaswa ubadilike sana. Mimi nimekuja hapa Bungeni nikiwa natokea Chuoni, nikiwa sijamaliza hata Chuo na nilikuwa kwenye Serikali ya wanafunzi.

Matatizo yanayoendelea ni makubwa sana. Kwanza Bodi ya mikopo hata tunavyobadilisha hii sheria, haina uwezo. Hata sheria ikibadilika kwa mapendekezo, yale matatizo yataendelea. Ku-access, kupima kujua kijana yupi apate mkopo asilimia ngapi, yupi apate asilimia hizi ni kwamba ule ni uwongo, hawana uwezo wa kupitia form zaidi ya 20,000 kwa kipindi cha miezi miwili. Haiwezekani! Hiyo ni Bodi gani? Form zaidi ya 20,000 wazipitie kwa miezi miwili, watu wa-apply mwezi wa Nne sijui wa Sita wawe wamemaliza! Sio kweli! Tengenezeni mfumo ambao utakwenda mpaka kwenye grass root kutambua hawa watu. Sasa hivi watu wanaopewa mikopo ni watoto wa matajiri. Watu wanajaza uwongo na wanapewa mikopo, watoto wa masikini wamekosa mikopo. (Makofi)

Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia mfumo namna ya kuwagundua watu hawa kuanzia chini mpaka juu. Lakini pia niliwahi kuuliza swali hapa, wanafunzi kwa mfano wanaosoma Shule ya Sheria (School of Law) hamuwapi mikopo, maana yake mnataka mawakili wawe watoto wa matajiri peke yao, ndiyo mnachotaka na ndiyo kinachoendelea. Wengi wameitwa pale hata mwaka jana watoto wa masikini wamerudi Muhambwe kule na maeneo mengine ya Tanzania kwa sababu hawana pesa. Sasa mkataba huu jamani iwe njia ya kupandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja nyingine. Kuna tatizo linaloendelea hapa nchini hasa nafasi za kuwateuwa vijana. Nafasi za uteuzi, tunaona Wakuu wa Mikoa wanaoteuliwa ni wazee watupu, Mabalazi wanaochaguliwa ni wazee wastaafu, Bodi mbalimbali zote na Tume, kama wewe sio mzee, wala hata usifikirie kuteuliwa. (Makofi/Kicheko)

Sasa mimi najiuliza, hapa kuna Mawaziri, akina Steven Wasira. Siku moja nilikuwa naongea naye Mheshimiwa Wasira, akaniambia Mwalimu Nyerere aliniteuwa nikiwa kama wewe Mkosamali, mbona ninyi hamwateui sasa hivi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Baraza la Mawaziri tunataka tuwaone vijana wako mle sio, kijana akionekana ana aibu, haiwezekani mbona sisi kule Muhambwe mmetuchagua? Tuna busara ndiyo maana tunataka hata umri wa Uraisi ushuke chini tufanye kazi. Mwalimu Nyerere amekuwa Mwenyekiti wa TANU ana miaka ishirini na kitu mwaka 1952. Vijana tuna uwezo, tuna busara, hatukurupuki kwenye mambo na tunafanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba Mkataba huu utekelezwe kwa umakini na watu watuamini wajue kweli wana vijana makini, madhubuti ndani ya Bunge na wataendelea kuwapigania vijana wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, tunaomba vijana waliofukuzwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam warudishwe. Wamefukuzwa kwa madai ya msingi na wameshaandika barua nyingine ziko kwa Waziri Mkuu, anazo, lakini amekaa kimya. Tunaomba warudishwe Chuoni kwa sababu ninyi wenyewe mmeunda Tume kwa kuafiki kwamba kulikuwa na matatizo kule. Sasa mmewafukuza vijana zaidi ya hamsini na kitu, watu bado miezi minne wamalize Vyuho mmewafukuza. Tunaomba mpitie maamuzi yale, walikuwa wanatetea mambo ya msingi. Kuna vijana zaidi ya 11,000 wamekosa mikopo, ndicho kitu walichokuwa wanaeleza. Sasa ni kosa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina watu wangu wa Jimboni kwangu, wengi wamekosa mikopo. Kwa hiyo, mnavyowafukuza wale viongozi wa wanafunzi mtakuwa mnawaonea. Najua Waziri wa Elimu yuko hapa na Naibu wake mnanisikia, warudisheni wale vijana, ni nguvu kazi ya Taifa. Vijana 50 inawezekana mle kwenye wale waliofukuzwa, kuna Rais makini sana mle ndani! Tunaomba muwarudishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. (Makofi)

MWONGOZO

MHE. ANTONY G. MBASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kupitia kanuni ya 47 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na hii inatokana na kwamba tumepewa ratiba katikati baada ya kuwa tumeshamaliza kipindi cha maswali na majibu. Lakini kuna swali lililoulizwa jana na Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kuhusiana na sakata linaloendelea la madaktari na tukapewa jibu kwamba tutapata taarifa, lakini katika ratiba tuliyopewa nilikuwa naangalia shughuli za mawasilisho ya taarifa za Serikali sikuweza kuona kwamba kuna sehemu ambako tutapata taarifa hii. Naomba kupata mwongozo wako ni lini Bunge litapata taarifa hii? Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli jambo hili jana liliombwa lijadiliwe kwa hatua za dharura na Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini Mheshimiwa Spika alitoa majibu kwamba Serikali inajipanga kwa ajili ya kutoa maelezo.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba jibu la Spika litabakia vile vile. Serikali ipo na kama hiyo taarifa itahijika wakati wowote, basi wanaweza kupewa fursa ya kuweza kutoa taarifa ya kinachoendelea. Kwa hiyo, jibu la Spika katika suala hili linabakia vilevile kama alivyolitoa siku ya jana.

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba hoja hii imepata msisimko mkubwa na kwamba kweli kabisa ni dhahiri vijana leo wamepata fursa nzuri ya kujifaragua na kwa kweli mmetia fora, mmeweza kuwakilisha hao watu walioko nje ya jumba hili la mzunguko.

Imani yangu ni kwamba, michango ya aina hii yenye afya, itaendelea kutolewa ingawa kwenye *Order Paper* mtaona kulikuwa kuna Azimio lingine la Marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambalo lilikuwa lifuate siku ya leo hii hii tumalize hii. Lakini ngoja kwa ladha hii ninayoiona na kwa afya ya mijadala ninayoona, shauku inanijia nichelewe kusema nini kitafuata jioni, lakini hebu tuwe na mawazo kwamba jioni tunaweza tukaendelea kidogo kabla Serikali haija-*wind up* hoja hii. Kwa sababu kwa kweli michango ina afya na kwa kweli vijana nawapongezeni, mmetoa michango mizuri.

Sio kwamba ni vijana tu, na wazee wameomba humu, kwa hiyo, na wazee nao wapo humu. Kwa hiyo, idadi ya wachangiaji ni wengi na wengi wakipata fursa, naamini Serikali mtapata michango mizuri kwa ajili ya kuboresha jambo hili. Basi baada ya kusema haya, nitaje tu kwamba jioni wale ambao mmeniomba kuchangia muwepo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, nilitaka tu kumkumbusha Mheshimiwa Dokta pale juu ya kile kilichosemwa jana kwa mujibu wa Kanuni ya 49, nilitaka tu asome Kanuni ya 49. Tulichomuandikia Spika sisi ni kile kilichomo kwenye Kanuni ya 49.

Kwa hiyo, asome tu masharti ya ile Kanuni ya 49. Kilichosemwa siyo kwamba tunaleta taarifa, sisi tutaleta kauli za Mawaziri kwa kifungu. Tumemwomba Spika atupangie kwa mujibu wa masharti yale kuleta kauli za Mawaziri. Sasa kauli za Mawaziri hizi kama Spika alivyosema zinatawaliwa na Kanuni ya 49. Nilitaka kuweka sahisio hilo. Tulichomwomba Spika, ni kuleta kauli za Mawaziri kwa mujibu wa Kifungu cha 49. Kwa hiyo, nilitaka tu asome masharti ya Kanuni ya 49 hayaingizwi kwenye ratiba.

MWENYEKITI: Nafikiri Mheshimiwa Waziri ameongezea tu kile nilichokisema kwamba jibu lile la Mheshimiwa Spika litabakia vile vile na Serikali itakapoleta kauli ya Mawaziri, nitajitahidi basi tuwasiliane na Spika tuone taarifa hiyo inatolewa mapema kwa sababu jambo lenyewe nalo ni la dharula vile vile.

Basi baada ya hayo niliyoyasema, naomba nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.58 m chana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mchana tulisema upo uwezekano pia tukaendelea kwa sababu hoja hii imevutia wachangiaji wengi na pengine hata kama tumewahi kupata fursa ya kujadili masuala ya vijana ni kwa muda mchache mchache kwa sababu ya mchanganyiko wa mambo mengine.

Kwa hiyo, kwa fursa hii ya leo inawafanya vijana wa nchi hii ya Tanzania ambao ni karibu asilimia 80 waweze kuwakilishwa vizuri sana wakati wa mjadajala huu kuliko pengine fursa nyingine yoyote iliyowahi kujitokeza. Kwa hiyo, tumedhani ni vizuri kwa siku ya leo tushughulike na Azimio hili tu na lile lingine litapata fursa nyingine. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Spika kukubali ushauri ambao tumeutoa. (Makofi)

Kwa hiyo, tutaendelea na wachangiaji. Tunao wachangiaji 11, katika muda wetu tutaangalia na tutajitahidi kwamba tuweze kupata fursa wote tuweze kusema. Sasa labda niwataje tu wachangiaji waliopo kwenye karatasi yangu, wa kwanza ni Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, wa pili ni Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo na baadaye Mheshimiwa David Zacharia Kafulila. Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika (The African Youth Charter) wa mwaka 2006

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Mshama, naona hayupo. Mheshimiwa John Mnyika ajiandaye, naona hayupo, Mheshimiwa Selemani Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii mchana huu wa leo kwa ajili ya kuujadili mkataba muhimu unaohusu vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu maana yake nafasi yangu ilikuwa nafasi ya tatu lakini nipewa nafasi ya kwanza. Sasa hii nadhani ni hekima ya Mwenyezi Mungu kwanza kusema kwamba Jafo saa hizi atakuwa mtu wa kwanza kwa ajili ya kuhakikisha kwamba katika ratiba hii ya jioni nami nakuwa miongoni mwa vijana ambao tunashiriki kwa pamoja kujadili mkataba huu wa vijana, pamoja na maridhiriano ya mkataba huu wa vijana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa watu kwa maana ya wanajamii wanatufahamu vijana ni akina nani, kwa kweli Taifa lolote ambalo lina nguzo kubwa sana ya uchumi, ambalo nguzo kubwa sana ya mchakato mzima wa maendeleo unaendeshwa na vijana na hili unaonyesha dhahiri ndiyo maana sehemu yoyote usipomtaja kijana ni kwamba hujafanya jambo lolote lile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikueleza hapa katika mambo ambayo katika salsafa ya dini naambiwa kwamba watu wataulizwa ikiwemo kipengele cha ujana, ujana wao watu wameutumia vipi. Hii ina maana kubwa sana kuona kwamba kijana naye ana sehemu kubwa ya kuulizwa swali la ujana wake ameutumia tumia vipi?

Sasa mimi nashukuru katika mjadala wa leo kuhakikisha kwamba katika ajenda hii ya Azimio hili kama vile Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuja hapa mezani kwa ajili ya kuujadili. Lakini nikichukua Tanzania kwamba nipende kushukuru katika Bunge hili nadhani Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla ni mashahidi. Wakiliangalia Bunge hili ambalo linaenda *very active* ni Bunge lenye mkusanyiko wa vijana wengi sana. Na vijana ambao wamechanganyika na kuchukua busara za wazee wakifanya kazi kubwa sana kwa ajili ya kutetea maslahi ya Watanzania. Wakati tukiwa hapa Bungeni kuna vijana mbalimbali wanaotutazama huko uraiani. Matarajio yao na matumaini yao kwamba Wabunge wao

wanasema nini katika mchakato mzima wa vijana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikienda moja kwa moja katika suala zima la uzoefu, bahati mbaya tumekumbwa na tatizo kubwa sana la kuwatenga vijana katika suala la uzoefu. Katika maeneo ya kazi ya aina mbalimbali vijana ambao wamehitimu wana elimu nzuri, lakini wakienda katika soko la ajira wanaambiwa kwamba wewe subiri kwamba huna uzoefu mpaka miaka mitano. Hii ninasema ni ajenda ambayo imejificha moja kwa moja ya kuwatenga vijana na mimi nikiwa kama kijana nasema kwamba jambo hili haliwezekani. Na kama Tanzania leo tunaridhia mkataba huu ningeomba moja kwa moja Serikali yetu sikivu ihakikishe kwamba kijana anapata nafasi yake kwa uhakika kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa siyo vyema vijana wetu leo hii wanamaliza vyo vikiu wengine tuna vijana wapo mtaani bado hawajapata kazi. Wengine juzi juzi wamemaliza vyo vikiu bado hawajapata kazi. Lakini tunaambiwa kwamba watu hawa wawezi kupata kazi mpaka wawe na uzoefu. Hili jambo ndugu zangu kwa Taifa la Tanzania tuseme haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lazima tulitekeleze kwa vitendo ndugu zangu, nadhani sasa hivi tuna Sekretarieti ya Ajira. Naamini hata matangazo yanayotangazwa na Serikali katika Sekretarieti ya Ajira kuna sehemu ya kitu cha uzoefu. Hivi kama tuna watu tunawalipia mamilioni ya pesa kwa kupata digrii zao halafu tunasema hawawezi kuajiriwa mpaka wapate uzoefu, kweli tunawatendea haki?

Mimi leo naiomba sana Serikali leo hii tunaporidhia mkataba huu twende na vitendo moja kwa moja kuhakikisha kwamba sasa hivi katika suala la ajira upana unapanuliwa kwa kiasi cha juu sana kwamba vijana waweze kuchukuliwa bila kulinganishwa isipokuwa *qualification* ili wawe na uwezo wao jinsi walivyomaliza digrii zao, lakini sio digrii peke yake mpaka kozi zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili naomba Wabuge wenzangu, naomba ndugu zangu tusilifumbie macho, tukilifumbia macho maana yake tunajijengea bomu kwa vijana wetu wa Tanzania. Hivi sasa vijana wengi wapo mtaani wanalia huko. Hili jambo leo hii tunaridhia naomba niseme kwamba hili tulipeleke kwa vitendo zaidi na mimi nina imani tutalipeleka kwa vitendo zaidi kwani kwa sababu tunaona sasa hivi jinsi gani wanaleta mabadiliko makubwa sana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyotekeleza vitendo hivi ninaiomba sana Serikali sasa hivi tunasema kwamba tuwaweze vijana, lakini kwa bahati mbaya sana Tanzania yetu hii suala zima la ajira tumelipeleka moja kwa moja katika Sekretarieti ya Ajira peke yake. Hili kutokana na suala hili linawakosesha vijana wengi kupata ajira waliokuwa katika maeneo ya mbali. Kwa nini Halmashauri zisiwezeshe katika ajira zingine za kada za chini kuhakikisha Halmashauri zenyewe zinapewa ajira hiyo? *(Makofi)*

Kuna watu wa kada mbalimbali nilizungumza katika Bunge la Bajeti, tuna madereva, tuna watendaji wa ofisi mbalimbali, makarani na kuna watumishi mbalimbali kama makarani na kuna watumishi mbalimbali mpaka watendaji wa vijiji. Ndugu zangu wakuu wetu waajiriwa na Sekretarieti ya Utumishi ya Ajira kwa kweli haleti afya. Haileti afya hata kidogo kwa sababu watu wengi ambao ni vijana tunaowakusudia wanakuwa hawapati kazi na hivi ni nini kinachotokea, kinachotokea ni kwamba ni watu wa aina fulani ndiyo watapata katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwaacha watu wengine wakikosa ajira katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba tunaporidhia mkataba huu naomba tuutekeleze zaidi kivitendo ili mradi kuhakikisha hawa vijana wa Tanzania wanaweza kupata fursa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la mikopo kwa vijana. Tuna vijana wamemaliza Chuo Kikuu lakini ni jinsi gani tunavyowawezesha, tuseme mara nyingi sana kwa nini cheti cha mwanafunzi wa Chuo Kikuu kisitumike kama vile ni kigezo kwa ajili ya kijana kuweza kupewa mkopo kwa ajili ya kuwezesha maisha yake, hivi kigugumizi kiko wapi?

Ndugu zangu haiwezekani hata kidogo kijana aliyemaliza leo Chuo Kikuu unamwambia kwamba wewe ukitaka kupata mkopo mpaka awe na nyumba, hicho kitu hakiwezekani. Kwa nini cheti chake kisiweze kumsaidia kwamba kiwe ni miongoni mwa kigezo ambacho kingeweza kumsaidia kupata mkopo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mtu huyo anaingia katika ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza suala hili naomba sana, leo hii tunaridhia tuhakikishe vijana wetu tunawapa nguvu ya kutosha ili mradi Taifa letu la Tanzania liweze kulingana na Mataifa mengine. Jambo lingine nazungumzia suala zima la kuwawezesha vijana hasa wanapokuwa vyuoni. Tunamtarajia kijana akiwa chuoni aweze kujifunza *theoretically and practically*. Bahati mbaya wanafunzi wengine wanapokwenda *field* wanakosa uwezo mzuri wa kuweza kuwawezesha kwamba jinsi gani atatoka baadaye kwenda kuingia katika soko la ajira kufanya kazi vizuri.

Naomba wakati tunaridhia mkataba huu tuweke mikakati ya kutosha kwamba vijana wa vyo vikiu ambao wapo sasa hivi vyuoni wakati wa *field practical* tuweke mianya mipana sana ili vijana hao waweze kuondoka katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata fursa ya kujifunza kazi vizuri, bahati mbaya ni wachache tu wanaopata fursa katika mashirika mbalimbali mazuri kwa ajili ya kwenda kujifunza kazi. Hii inatokana na ukiritimba, inategemea ni jinsi gani mtu wakati mwingine kaka yake au baba yake yuko katika nafasi fulani ndiyo anaweza kupata kazi ya kuweza kufanya *field* nzuri. Jjambo hili haliwezekani hata kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la ulinzi wa Taifa letu. Tuna vijana wengi sana katika Taifa letu, vijana wengine sasa hivi ndiyo wamekuwa wala unga. Naomba tunaposema kwamba leo tunaridhia mkataba huu naomba kujielekeza zaidi katika jinsi gani tutaweza kuimarisha Tanzania yetu hii na kuona inaenda kwa haraka katika suala zima la uimarishaji wa Jeshi la JKT. Jeshi la JKT litaweza kukuza uzalendo kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya Taifa letu hili na isitoshe tutaweza kutengeneza vijana ambao watasaidia katika uzalishaji mali wa nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza mengi sana, napenda kumalizia katika suala zima la ubaguzi. Suala la ubaguzi naiomba sana Serikali yetu kwamba kuna vijana wengine sasa hivi hawana fursa kama nilivyosema awali, wanajikuta wamekuwa *marginalized*, hawana *exposure* basi naomba Serikali wakati tunaridhia mkataba huu tuhakikishe tunawatengeneza wale vijana wengine mazingira hata ya kuingia katika fani za ufundi ili mradi na wao waweze kuwa na *access* ya ajira katika maeneo mbalimbali hata katika vyo vya ufundi. Tukifanya hivi tutatengeneza mkataba ambao hauwahusu vijana wachache isipokuwa mkataba ambao unahusu vijana wengi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba nimekuwa mtu wa kwanza na nimefarijika sana. Lakini mwisho nitakuwa si vyema kama nimesimama hapa bila kuwazungumzia vijana wa vyo vikiu. Tuna vijana wengi wa vyo vikiu, naomba ufanyike utaratibu mzuri, ibainike kwamba kuna vijana ambao wapo mtaani hivi sasa wanahangaika naomba sisi Wabunge tuwaangalie kwa jinsi gani tutawasaidia hawa vijana ili waendeleo kupata elimu zao. Tukiwaacha wabaki mtaani itakuwa ni tatizo kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naona busara ikitumika inawezekana kuna wengine watabainika dhahiri kwamba wamefanya makosa, basi naomba isichukuliwe kwamba makosa ya watu wachache i-*generalize* wanafunzi wote hivi sasa kuwa mtaani. Naomba Serikali yetu itumie busara katika jambo hili, wale vijana ambao watabainika kwamba hawana makosa basi waweze kuwezesha vyo vikiu ili mradi waweze kupata elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nipende kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhakikisha kwamba nami natoa mchango wangu katika suala zima la kuhakikisha mkataba wa vijana unaridhiwa katika Taifa letu la Tanzania. Ahsante sana kwa kunipa fursa hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jafo. Kwa kweli mjadala huu leo ni mtamu. Nimepata ki-*note* hapa hakina jina la mtu anasema vijana wana matatizo mengi sana, akiomba ajira anaambiwa awe na uzoefu, akiomba mkopo awe na nyumba, akiomba ndoa awe *tem bo card, master card*. Kweli vijana wana matatizo mengi sana.

Basi tunaendelea, sasa nitamwita Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, atafuatiwa na maana watu wengi naona hawajakaa vizuri basi nitamtaja atakayefuatia. Mheshimiwa Kafulila. (Makofi)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi jioni ya leo kuweza kuchangia mkataba huu wa Kimataifa kwa vijana wa Afrika ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia mkataba huu ambao tumeanza kuupigania tangu tukiwa Asasi za Kiraia kwa maana ya TYVA. Nakumbuka asasi hii ni miongoni mwa asasi chache ambazo zimetumia muda mrefu sana kupigania ajenda hii na tunamshukuru Mungu kwamba leo kwa mara ya kwanza sasa tunaanza kujadili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunajadili leo ajenda ya mkataba wa vijana wa Afrika ikiwa tumekamilisha miaka 50 tangu tupate Uhuru. Kwa maneno mengine ni fursa ya kutafakari pengine miaka 50 ya Taifa hili baadaye. Nasema haya kwa sababu duniani kote unapozungumza uhai wa Taifa unazungumza vijana. Mzungumzaji mmoja aliyetangulia amepata kusema kwamba unapozungumza hatima ya Taifa lolote duniani unazungumza hatima ya vijana. Kwa hiyo, unapata nafasi ya kuchangia mjadala huu pengine ni nafasi sasa ya kutafakari miaka 50 ijayo tunataka kutengeneza Taifa la namna gani? Ndiyo maana ya mkataba huu wa vijana wa Bara la Afrika ambapo Tanzania ni mojawapo.

Nilikuwa napitia pita baadhi ya vitabu nikasoma kitabu cha *Economist Pocket World in Figures* wanasema kwamba miaka 50 ijayo jumla ya Watanzania watakuwa milioni 109 kwa tafsiri nyingine Watanzania milioni 109 ni sawasawa wachukue watu wote wa Uganda, watu wote wa Kenya, uwachanganye na Watanzania halafu wote wakae Tanzania moja hii hii, kwa sababu nchi zote tatu zina jumla takribani watu milioni 110. Kwa hiyo, miaka 50 ijayo tutabanana kiasi kama cha watu wa nchi zote hizi tatu kwenye Taifa dogo kama la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapozungumza hatima ya vijana hatuzungumzi hatima ya vijana kwa leo tu, tunazungumza hatima ya vijana kwa miaka mingi mbeleni na pengine kwa sasa tunazungumza hatima ya vijana kwa miaka mingine 50 ambayo iko mbele yetu. Sasa kuna mambo mengi ya kuzingatia, kuna nafasi za vijana katika mustakabali wa utawala wa Taifa letu, kuna nafasi za vijana katika masuala mazima ya uchumi na kuna nafasi zao katika kufaidi fursa za kiuchumi ambazo nchi hii imejaliwa. Yote hayo ni mambo ambayo tunahitaji kuyatafakari kwa pamoja. Ningependa kuanza kuzungumzia nafasi ya vijana katika uamuzi wa utawala wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hii *charter* inaonyesha kwamba kijana ni kuanzia miaka 15, lakini kwa bahati sana kwamba vijana katika michakato ya kuamua utawala wa Taifa lao wametengwa. Leo wakati kijana ana miaka 15 ndani ya nchi hii hapigi kura, mwenye miaka 16 hapigi kura na mwenye miaka 17 hapigi kura. Lakini angalia hata kwenye sera ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu ya Tanzania inaonyesha kwamba umri wa miaka 15 ambao ni umri wa ujana ni umri ambao unatoshwa kabisa mtu kuwa amehitimu elimu ya msingi na kama misingi ya mtu kuhitimu elimu ya msingi ni kupata ufahamu wa maswali ya msingi ya kawaida yanayohusu maisha ya binadamu tafsiri yake ni kwamba kijana mwenye umri wa miaka 15 alipaswa kupiga kura, kijana mwenye umri wa 16 alipaswa kupiga kura na kijana wa miaka 17 alipaswa kupiga kura.

Kwa hiyo, kimsingi bado sheria zetu zinawabagua vijana kwenye kuamua hatima ya Taifa. Kwa hiyo, pengine changamoto kwa sasa Serikali ianze kufanya marekebisho mbalimbali ya kisheria na ya Kikatiba kuona kwamba vijana wenye miaka 15, 16 na 17 kama *charter* hii inasema kijana miaka 15 na kama sera ya elimu inaonyesha kwamba miaka 15 ni umri wa kutosha mtu kuhitimu elimu ya msingi *then* tukubaliane kwamba kuanzia sasa kuna umuhimu wa kurekebisha mfumo mzima wa uchaguzi kwa maana ya sheria inayo-govern nani apige kura nani asipige kura kwa upande wa umri. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa pili bado Katiba inawabana vijana, leo ukiisoma *charter* hii na maoni pengine ya Waziri na Kamati wamezungumza tu kwamba vijana washiriki kwenye uwakilishi kwenye nafasi za Udiwani, Serikali za Mitaa, Vijiji na Ubunge, wanaishia pale, lakini uwakilishi ni zaidi ya Udiwani na ni zaidi ya Ubunge. Tanzania kwa mujibu wa Katiba ili mtu apate nafasi ya kugombea Urais anahitaji awe na miaka 40 huu ni umri mkubwa mno na kwa Katiba hii vijana wamebaguliwa. Kwa hiyo, tunahitaji mabadiliko makubwa ili kuendana na *charter* hii ambayo leo tunaipitisha. Umri wa kugombea Urais ushushwe ili kusudi tuwe na Katiba ambayo mwisho wa siku tutapata siku moja Rais kijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaweza, Nyerere amekuwa Waziri Mkuu akiwa na miaka 39. Lakini kabla ya pale alipata nafasi ya kukiongoza Chama cha TANU mwaka 1954 akiwa na miaka 32. Lakini leo tunaambiwa tusubiri kwamba vijana ni Taifa la kesho tusubiri, hapana. Kwa hiyo, kuna umuhimu kwa kupitisha *charter*, Serikali itafakari masuala mbalimbali ya kisheria kuweza kufanya *reforms* ili kuweza kuendana sambamba na mkataba huu. (Makofi)

Kwa hiyo, hayo ningependa kuyachangia kwa maana ya nafasi ya ushiriki wetu sisi kama vijana kwenye nafasi ya uongozi. Lakini pia katika ushiriki huu huu, nimesema mwanzoni kwamba unapotafakari nafasi ya vijana leo, unapaswa kutafakari hatima ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takribani miaka 50 tangu tupate Uhuru Taifa hili linakwenda kombo na moja ya sababu kubwa ambayo inaashiria kwamba tunakokwenda siko ni nidhamu ya uwajibikaji ndani ya Taifa hili, inaporomoka siku hadi siku. Vijana wa zamani walioweza kulelewa na kutengenezwa waliweza kufundwa na Serikali ya Nyerere, nidhamu yao ya uwajibikaji ilikuwa kubwa kuliko leo na sababu mnazijua. Tulikuwa na JKT ambayo ilikuwa haiwezekani kupata kazi mpaka upitie JKT!

Mimi leo JKT ikianzishwa nitakwenda. JKT ni moja ya utaratibu, ni moja ya mfumo ambao unasaidia mambo mengi ya kujenga Taifa imara na kwa maana ya kuwaandaa vijana ambao baadaye watakuwa viongozi wa kisiasa, kuandaa vijana ambao baadaye watakuwa viongozi wa utumishi wa umma kwa maana ya watumishi wa umma na maeneo mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza kwamba kiwango cha uwajibikaji kimeshuka, watu hawatimizi wajibu wao, ni kwa sababu, hawaandaliwi. Ukienda maofisini watu wanasoma magazeti, wanapiga porojo tu, Taifa haliwezi kwenda namna hiyo. Kwa hiyo, tunahitaji kutengeneza mifumo ambayo itaweza kuandaa Taifa lenye kuwajibika na moja ya eneo kubwa ambalo tukilikubali ni kurejesha JKT mara moja. Tukubaliane kwamba mtu hapatilimwa mpaka apite JKT. Baba yangu mimi ni mwalimu, amestaafu juzi, lakini wakati ule ilikuwa saa 12 asubuhi anaamka, anajiandaa kwenda kazini, saa moja asubuhi siku zote yupo kazini. Leo kiwango cha uwajibikaji ofisini kinaporomoka kwa sababu watu hawaandaliwi kuwa watumishi! Elimu ni zaidi ya kuwa na *knowledge* kichwani! Elimu ni pamoja na nidhamu ya kutumika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ningependa kuzungumza kwa msisitizo kabisa na Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla muweze kuliangalia ni jambo muhimu sana. Lakini jambo lingine, leo Tanzania tupo kwenye mfumo wa vyama vingi. Moja ya changamoto kubwa ambayo itakwenda mbele yetu ni kuwapata viongozi walioandaliwa. Zamani wakati wa chama kimoja mlikuwa mnawaandaa watu kupitia chuo cha chama, wanaandaliwa waje kuwa viongozi wa baadaye. Sasa hakuna chuo cha kuwaandaa vijana kuwa viongozi! Kwa hiyo, matatizo mbalimbali ambayo baadaye yanaweza yakaja kuibuka ni kwa sababu, hakuna mfumo ambao unatumika kuweza kuandaa vijana wa Tanzania waje kuwa viongozi. Sisi wachache ambao tumepata kuingia ndani ya Bunge hili na wengine wamepata nafasi ya Udiwani, ni bidii binafsi! Ni jitihada na juhudi binafsi ambazo mtu anazitumia kujifunda mwenyewe kwa mazingira yake mwenyewe mpaka anafikia mahala anakubalika anakuwa Mbunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Taifa tunahitaji kupata chuo ambacho kinaweza kuwa-*train*, kuwa-*groom*, kuwafunda vijana bila kujali itikadi zao ili kusudi vyama vyote viwe na viongozi ambao wameandaliwa kwa sababu hakuna matumaini ya kwamba chama hiki kimoja kitaongoza milele. Sasa kama hawa walioandaliwa kwenye chama hiki kimoja watakapotoka na wengine kwenye vyama vingine hawajaandaliwa, hatima ya Taifa itakuwaje? Kwa hiyo, ni lazima kufikiria kwa mapana kwamba tunahitaji kuliandaa Taifa tayari kwa chama chochote kuingia na kwa hiyo, ni lazima vijana wote wa vyama vyote, waandaliwe kwa maana ya kuwa tayari kuongoza katika wakati na mazingira yoyote yale. Hilo ningependa Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kujumuisha, aweze kuliangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningependa kuzungumzia tatizo kubwa kabisa la ajira kwa vijana. Mheshimiwa Mkosamali ndugu yangu, amezungumza hapa kwamba ingeweze kabisa hii Wizara ikawa Wizara moja, Vijana na Ajira, kwa sababu wahanga namba moja, waathirika namba moja wa ukosefu wa ajira duniani kote huwa ni vijana. Leo utafiti uliofanywa mwaka 2007 (*Integrated Labor Survey*) na hata ripoti ya hali ya umaskini na uchumi Tanzania inaonesha kwamba takribani vijana 650,000 mpaka 750,000 wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka! Kwa hiyo, ni wastani wa vijana 700,000

wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Kwa miaka mitano, unazungumzia takribani vijana 3,500,000 wanaingia kwenye soko la ajira! Hawa vijana watapata ajira wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi ya mashirika na makampuni ambayo tumeyabinafsisha kwa lengo la kuongeza ajira, karibu mengi yamekufa! Mimi nina mfano wa nyumbani, tulikuwa na mgodi wa kuzalisha chumvi, mgodi mkubwa uliokuwa unaajiri watu zaidi ya 600 ajira rasmi, leo mgodi umekufa! Tumekwenda mwaka jana, Mheshimiwa Rais anautazama mgodi ule anakumbuka wakati yupo Nishati na Madini, haamini kama ule mgodi ndio mgodi ambao aliuona wakati akiwa Wizara ya Nishati na Madini, umekufa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kufufua, kuna haja ya kujenga uchumi huu upya! Na tunapojenga uchumi, hatuna maana kwamba ni lazima tuujenge kwa wawekezaji! Tufufue viwanda, tuongeze ajira. Hii ajenda ya Serikali ya kutengeneza ajira 1,000,000 kwa mwaka, tafsiri yake ni kuwaweka nje ya ulingo wa ajira za vijana 2,500,000 katika miaka mitano! Kwa hiyo, lazima tufikirie mambo haya kwa mapana. Wakati wa mjadala wa Tume ya Mipango, nilimuuliza Mheshimiwa Mpango kwamba unapozungumza kujenga uchumi kwa miaka mitano, unazungumza habari za uwekezaji mtupu na uwekezaji wenyewe kwenye maeneo mengine, lakini kwenye kilimo na biashara ndogo ndogo haionekani, tafsiri yake ni nini? Akanijibu ni gharama kubwa sana kujenga uchumi kwa kuzingatia sekta kama za biashara ndogo ndogo na kilimo. Lakini ukweli ni kwamba tunachokihitaji Tanzania sio takwimu ya ukuaji wa uchumi tu, lakini huo uchumi unawabeba akina nani? Ndio jambo la msingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninatamani kama ningeendelea kukupa muda lakini sina uwezo huo kwa sababu ulikuwa umefika kwenye utamu sasa wa mchango. Sasa nitamwita kijana mwingine maana sasa hapa ni vijana, lakini baadaye pia nitafungulia wazee ili ku-*balance* mambo.

Sasa nitamuita, sijui huyu ni kijana, Assumpter Mshama. *(Kicheko)*

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mimi ni kijana wa zamani. Kwanza ninachukua nafasi hii kukushukuru kunipatia nafasi na kumshukuru Mungu, kuwepo tena katika Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo na kunipatia nafasi kuchangia katika Muswada huu ambao unaongelea mkataba wa vijana katika Mkataba wa Kimataifa wa Vijana Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niipongeze kabisa Serikali kwa moyo wa dhati kwa muda mliochukua kwa umakini mkubwa, kukaa chini na kuutafakari mkataba huu na kuona kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuletwa katika Bunge hili Tukufu na hasa sisi wengine tukashiriki kuukamilisha, kwa hilo, naipongeza sana Serikali.

Katika suala lingine ambalo ningependa kuongelea ni suala la ulinzi, ulinzi wa maisha ya vijana unaosema kwa mtu binafsi, vijana wengi wanataka wawe na maamuzi yao binafsi; katika Ibara ile ya saba inataka kijana aachiwe nafasi ya yeye kuamua mambo yake mwenyewe. Mimi katika ushauri wangu ambao ninaona katika kupoteza utamaduni hasa wa kuwaonya watoto wetu, vijana wetu, katika kukosa ushauri muhimu na kutoangalia kwamba matendo unayotenda yanamuathiri mwingine, yamefanya vijana wengi waingie katika matatizo kwa sababu wanaamua mambo yao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninashauri vijana tuendeleo na utamaduni wetu wa kusikiliza wale watu waliowazidi umri. Zamani ulipokuwa upo kijijini, kama umetenda kosa hata mama mwingine anakuonya kwa sababu ameona umekosea. Leo hakuna mzazi anagusa mtoto wa mtu kwa sababu ni wakati wa vijana kuamua mambo yao. Mimi nilikuwa ninaishauri Serikali na ninawashauri wazazi, tuendeleo kuwaonya na kuwalea watoto na huku tukizingatia mambo muhimu yaliyoko katika mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara Namba 13, inahusu elimu na maendeleo ya ujuzi. Mkataba huu unataka mtoto wa kike ambaye amekatishwa masomo kwa kuolewa au kwa kupata mamba nje ya ndoa, arudi kusoma darasani na watoto wengine. Ninao ushauri ambao mimi nilikuwa ninafikiri ni vyingi tuangalie hili suala vizuri. Sisemi watoto ambao wamezaa wasiende shule lakini wanaenda shule kwa namna ipi? Kuna mtoto ameamua kujilinda na kujitunza ili kwamba afike wakati wa kuolewa aolewe; kuna

mwingine ameamua tu kutumia muda wake kwa mambo anayotaka na hatimaye amepata mimba! Leo mkataba huu unatutaka tuwaweke shule tena! Je, katika utaratibu upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda kushauri na wengine wanaweza kupinga, ni kweli! Lakini nataka niishauri Serikali, tunawatengenezea mazingira gani watoto wetu? Hivi leo watoto wengi wanazaa wakiwa shuleni ambapo tumeweka sheria! Je, tutakapofungulia mlango wa kwamba nenda uendako, beba ubebacho, utakaporudi utaendelea na kusoma!

Mimi nilikuwa naomba ni lazima wajutie dhambi ile, kwa sababu hata makanisani hatuwafukuzi kanisani, tunawaambia kaa mstari wa nyuma ili kusudi ujue kwamba tendo ulilolitenda halistahili ili tuwape watoto wetu ambao wamejilinda waweze kusoma vizuri na kuendelea kuogopa kwamba kubeba mimba wakati nasoma ni dhambi na tena haistahili kuonekana katika maisha yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalosema mimi nimezaa watoto wanne na wote ni wasichana; mtu anaweza akadhani ninasema hivyo kwa sababu ni watoto wa wengine, hapana! Katika dhambi siwezi kutetea, ninachotaka ni kwamba watoto wetu tuendeleo kuwaonya! Ikitokea bahati mbaya, tutengeneze utaratibu wa vyuo au wa masomo, kusoma peke yao na wakijua kabisa katika mfumo ule mzuri, wamekaa pembeni. Mimi nilikuwa nashauri kwa nguvu zangu zote na mtakapolipitisha hili, mimi nitanyoosha mkono wangu mbele ya Mungu kwamba sjaruhusu dhambi hiyo na sikubali kwamba watoto hawa wachangamane na watoto ambao hawajazaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongezee pia; nimeenda nchi moja kutembea, nimekuta *university* moja watoto wamepewa makopo yameonekana kama chupa ya kunyonya kwamba hata katika mfumo wa Serikali yao, hawapewi mkopo wa kusoma, wanaangalia kwamba wamewatengea shule zao lakini wanawachangisha watu kusaidia mabinti ambao wamekatishwa masomo yao. Kwa maana nyingine, wana *college* zao na wanaendelea kufundishwa namna ya kuondoa aibu ile waliyoipata usichanani mwao. Kwa hiyo, ninaomba tu tuangalie na tusiwatupe. Tuandae utaratibu mzuri, lakini tusi-spoil wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 12 imeongelea vijana kuishi maisha ya uwajibikaji, hili ni tatizo kubwa katika nchi yetu. Nataka niseme hivi hata katika maisha yetu ya kawaida au mfumo wetu, tumeanza na kitongoji, tukaweka kijiji, tuna kata tuna tarafa mpaka wilaya na vijana wengi wamekimbia vijijini wakiamini kwamba mjini kuna kitu na wakifika mjini wanakuta hakuna kitu! Lakini kwa kawaida, Serikali ni sawasawa na familia; unaamka asubuhi mtoto wako uliyemzaa tangu asubuhi hafanyi kitu mpaka jioni! Halafu baada ya muda anasema baba, hujanitengenezea mazingira!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninawaomba vijana wetu, wana maono gani? Niliweka mkutano katika kata yangu, nikawaita vijana nikawauliza, vijana wa kata hii mna mkakati gani wa maendeleo? Nikakuta vijana hawana mkakati wowote na hawana maono yoyote! Tangu asubuhi mpaka jioni Serikali haijatufanyia hiki! Serikali haijatufanyia hiki! Lakini wewe kama mtu, ndio Serikali haijakufanyia, wewe mwenyewe una mawazo gani? Ndio maana tukaweka kitongoji ili uende kwa Mwenyekiti wa Kitongoji; jamani sisi vijana tupo 10 tunaomba utusaidie, tumelima bustani yetu tunahitaji mbolea! Au tuna tanuri letu tunataka kuchoma matofali, vitu kama hivyo! Uwajibikaji, ndio utaisukuma na Serikali yenyewe kuwaongezea nguvu katika yale waliyoyapanga. Vijana wamepanga mambo gani ambayo Serikali imeshindwa kuwasaidia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye kata, tuna uongozi wa kata. Nani amekwenda kwa Mwenyekiti wa Kata au Katibu wa Kata kumwambia sisi vijana tunafuga samaki, tunahitaji kutuletea vifaranga vya samaki, akakosa msaada? Mara nyingi vijana kwa kuwa wanasikia wimbo wa kwamba Serikali haifanyi kitu, wanachukuliwa na mkumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuwashauri vijana, wako kata nyingine na Wilaya nyingine na Tarafa nyingine, zipo tayari kuwasikiliza vijana lakini watu wameingiliwa na *mob psychology*, wanapelekwa na upepo, Serikali Serikali! Mimi nasema Serikali ipo na ipo tayari kuwasaidia wale walio tayari kujisaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka tena niwaambie vijana kitu kingine; sio rahisi mtu akakukuta umekaa, kuna mmoja hapa amenifurahisha yaani wewe umekutwa umekaa chini Mbunge anakuja anakuuliza kijana nataka kukusaidia, sio rahisi.

Lakini kama Mbunge anatembelea, maana tumegawana Katibu Kata, nani, nani, anakukuta upo katika eneo la kufyatua matofali ukamwambia jamani tumekosa mashine ya kukaushia au tunahitaji mzigo wa kuni, kweli Mbunge atashindwa kukusaidia? Lakini vijana wapo asubuhi wimbo wa Taifa, hakuna kazi, hakuna ajira! Ofisi za kuajiri vijana wote tuliowazaa ziko wapi? Mtu anadiriki kuiambia Serikali, watafutieni kazi! Wapi? Wewe mwenyewe umeajiri watu wangapi? Mimi naomba niseme Serikali ni familia, Serikali inahitaji mtoto wa kujituma, Serikali inahitaji mtu aliyejitoa, Serikali inataka *vision*, maono yako yakoje? Na Serikali iko tayari kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nikwambie nimetembelea Kata zangu nimewafundisha kitu, nimesema nataka uniambie ulichoalemewa! Halafu na mimi niongeze nguvu ulipoalemewa. Kata zangu vijana wameweza kuchangamka, wengine wamesema sisi tunaomba utusaidie gari la kupeleka nyanya sokoni! Unapompelekea nyanya sokoni, tayari ana mtaji. Alikuwa labda anakwama *pick-up*, tayari ana kitu cha kufanya. Nimewaambia sitaweza kutoa pesa, lakini naweza kutoa mawazo na mawazo ni mtaji bora maana pesa za ku-*dish out* anaziweza Mheshimiwa Mapesa, lakini nadhani hata Serikali kutoa mapesa, mapesa, sio kitu rahisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachooomba na ninachosisitiza kuna miradi ya kufuga samaki, vijana mlio mjini mtu asiwadanganye! Vijijini tumeanza miradi na mikakati, njooni tupeane mawazo, leteni mawazo yenu na tuone kama hatutayashughulikia. Ninamuamini Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, nina imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayoyasema ni kweli na nina uhakika kwamba hamtaacha kutekeleza yale ambayo tunayapitisha leo. Labda moja tu niombe, tutakapokuwa tumepitisha tuwe waangalifu kupitisha mambo ambayo sisi wenyewe yanatujengea heshima na sio ili mradi kila kijacho chochote tunapitisha. Katika haya machache, Mungu awabariki sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Bila ya shaka mtakubaliana na mimi kwamba kumbe zee nao dawa. Kwa hiyo, vijana sio kutoa tu na hayo na yenyewe na sisi tuyapokee.

Sasa nitamwita Mheshimiwa John John Mnyika na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niseme tu kwamba dhana ya huu mkataba ni suala ambalo binafsi naliunga mkono; lakini naliunga mkono pamoja na mapendekezo ya mabadiliko katika Azimio ambayo nimeyawasilisha na ninaamini tutayajadili kwenye hatua ya Bunge litakapokaa kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwamba hatimaye Azimio hili limekuja Bungeni. Nimekuwa kwenye harakati za masuala ya vijana kwa takribani miaka 15 iliyopita; kwa hiyo, kama kwa kigezo cha uzoefu, naweza kusema kwamba mimi ni mzee kwenye masuala ya vijana. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kwamba tunavyozungumza leo kuhusu hili Azimio Wizara hii inayosimamia masuala ya vijana ipo chini ya Waziri wa Vijana Ndugu Nchimbi ambaye katika *corridor* za haraka za vijana kuanzia miaka ya 1990 mwishoni tulikuwa pamoja lakini najua vilevile kwamba Waziri wa Sera Uratibu na Bunge naye tulikuwa naye huko huko kwenye miaka hiyo ya 1990 mwishoni mpaka 2000 mwanzoni kwenye masuala ya vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakati huo taasisi za vijana zilikuwa zinapaza sauti sana kuhusu masuala ya vijana, ukianza na Taasisi ya Jukwaa la Vijana (*National Youth Forum*) ambayo baadaye ilikuja kufutwa na Serikali kwa sababu mbalimbali zilizoelzwa lakini kimsingi ilifutwa kwa sababu ya kisiasa na taasisi nyingine za vijana kama za Dira ya Vijana (TYVA), Vijana wa Umoja wa Mataifa (UNA), Mtandao wa Wanafunzi wa Tanzania (TSMP) na taasisi nyingine na vyo mbalimbali.

Sasa kati ya mambo ambayo kwa miaka yote toka Mheshimiwa Rais Kikwete alipokwenda kwenye mkutano Banjul, Gambia wa wakuu wa nchi na mkutano ule ukalipitisha hili Azimio mwaka 2006 toka wakati huo vijana kwa umoja wetu tulikuwa tunapaza sauti sana kwamba hili Azimio lije Bungeni na miaka

yote hiyo hilo Azimio halikuja Bungeni na nashukuru kwamba wakati tunajadili mkataba wa UNESCO niliomba Serikali kwamba kila Azimio linapokuja tu liletwe vilevile na mchakato na maelezo kuhusiana kusainiwa kwa Azimio husika. Walau Azimio hili tumeletewa kiambatanisho cha barua ambacho kinaonyesha mwaka 2008 *correspondence* kutoka ofisi yetu ya Addis kwenda kwa Wizara zinazohusika. Ingawa bado Serikali haijatumia kiambatanisho ambacho kinaweka sahihi na maelezo ya kutiwa saini. Sasa niseme jambo moja, nitaomba Wizara wakati inahitimisha hoja itoe maelezo ya kina, ni kwa nini toka ofisi yetu ya Umoja wa Afrika kule Addis Ababa, Ethiopia ipitie hili Azimio na kuona kwamba linaweza kuingia Bungeni, linaweza kuendelea kuridhiwa mwaka 2008 ni mpaka leo ndiyo Azimio linakuja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipojadili Mkataba wa UNESCO niliomba Serikali vilevile mambo matatu kuhusiana na utamaduni usiochikika. Niliomba mosi tuletewe huu mkataba wa vijana wa Afrika na nashukuru leo umekuja.

Lakini pili, tuwekewe utaratibu ili viongozi wetu wakuu wa nchi na Mawaziri wetu wanapokwenda nje kusaini mikataba yenye sura ya hitaji la Bunge kuridhiwa kwa mujibu wa Ibara ya 63 wakati mchakato ya Kiserikali ikiendelea Bunge lipewe taarifa kwamba tarehe fulani mwezi fulani kama tunavyopokea taarifa za hati zingine ambazo Serikali imepitia na maazimio mengine ya Kiserikali tuletewe taarifa tarehe fulani mwezi fulani nchi yetu imesaini mkataba fulani ili Wabunge kwa niaba ya wananchi waweze kufuatilia mara kwa mara kuhaji mikataba ije Bungeni mapema. Sasa kama huu mkataba ungekuja Bungeni mapema haya tunayoyazungumza leo tungeyazungumza takriban miaka mitatu iliyopita na tayari ingekwishakuanza utekelezaji mpaka tunavyozungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukajiuliza na hasa wazee wanaweza wakasema kwa nini vijana wanazungumza tu kuhusu vijana kama vile hakuna wazee kwenye Taifa hili. Mimi niseme tu kwamba hii kada ya vijana ina upekee wake, Bara la Afrika tofauti na mabara mengi duniani ni bara ambalo lina idadi ya watu wenye umri mdogo kuliko watu wenye umri mkubwa. Ukienda Japan na nchi nyingine za Mashariki ya Kati hata kidogo baadhi ya mataifa ya Ulaya utakuta wazee ni wengi kuliko vijana. Kwa hiyo, masuala ya wazee yanazungumzwa kweli kwa sababu wazee ni wengi kuliko vijana, kwa hiyo, masuala ya pensheni na mambo mengine yanazungumzwa sana. Lakini kwa Afrika kwa wastani, kwa Afrika nzima vijana kati ya umri wa miaka 15 mpaka 35 ni asilimia 35 ya mataifa, ukichanganya vijana na watoto yaani watoto wa miaka sifuri mpaka 15 na vijana wa 15 mpaka 35 kwa ujumla wake ni asilimia 60 ya wananchi. Sasa kama unazungumza kuhusu maendeleo unachopaswa kuzungumza kama jamii asilimia 60 ni watoto na vijana unapaswa mipango ya kimaendeleo, unapaswa mipango kimaendeleo ujikite kwenye kuyashughulikia haya makundi kwa sababu ya wingi wao na ukishayashughulikia haya makundi unaweza kulisukuma mbele Taifa kwa haraka zaidi. Lakini kwa vijana kuna sifa moja ya ziada na ya pekee sana, kwa sasa tulivyo kwenye Taifa letu vijana ni asilimia 60 ya nguvu kazi. Sasa kama una asilimia 60 ya nguvu kazi ambayo ni vijana lakini asilimia 60 hiyo ndiyo ina tatizo kubwa zaidi ya ukosefu wa ajira maana yake ni kwamba Taifa letu halitumii rasilimali vizuri na ndiyo maana tunashindwa kusonga mbele kimaendeleo. Kwa hivyo, wazee mkitusikia tunazungumza kuhusu masual ya vijana na kwa kweli katika hili tuinge mkono ninazungumza kuhusu mustakabali na maendeleo ya nchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli sitajieleza sana kwenye kifungu kimoja baada ya kingine kwa sababu hoja zinazojadiliwa hapa ni hoja ambazo tumekwishazungumza sana hapa Bungeni kwenye Bajeti zingine ikiwemo Bajeti ya Wizara husika. Mimi nijielekeze kwenye utekelezaji vifungu vinavyohusu utekelezaji, kwa sababu mwisho ya siku tusipoweka misingi ya utekelezaji, maneno mazuri tunayoyazungumza kuhusu ajira kwa vijana, elimu kwa vijana, maadili kwa vijana, uongozi kwa viongozi, ushiriki wa vijana, yataishia hapa bila kwenda kwenye utekelezaji wa vitendo wa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina tatizo na Azimio hili kwa sababu Azimio hili likipita kama lilivyo litakuwa kama maazimio mengine na mikataba mingine ambayo nchi yetu imeridhiwa lakini baada ya kuridhiwa mikataba hiyo imebaki kwenye makabati imebaki kuwa historia na nisingependa mkataba huu wa vijana wenye umuhimu mkubwa sana kwa Taifa letu kuwa mikataba itakayobaki kwenye historia. Na hapa najielekeza kwenye Azimio hili ambalo ukurasa wa pili wa Azimio kuna kifungu hapa ambacho Serikali imeleta kwenye Azimio kwamba hicho kifungu tusikiridhie kama Watanzania, tusikikubali kama Watanzania kifungu cha 12(1)(h) ambacho kinataka huu mkataba upitishwe au sera ya vijana ipitishwe kama sheria na itungiwe sheria ya utekelezaji.

Sasa nakubaliana na maelezo ya vijana kwamba sisi kwa Watanzania sera zinatungwa na Serikali, hazitungwi na Bunge, sheria zinatungwa na Bunge. Lakini kitendo cha kuacha kuridhia hiki kifungu ngoja tusikiridhie bila kuwa na Azimio maalum la kuilazimisha Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria ili sheria iagize sasa masuala gani yazingatiwe kuhusu huu mkataba, masuala gani yazingatiwe kuhusu masuala ya sera maendeleo ya vijana, masuala kuhusu ajira, masuala kuhusu elimu ili haya mambo yote kama tunavyozungumza vijana sijui wanakosa ajira kwa sababu ya vigezo vya uzoefu, sheria iseme kwamba ni marufuku kwa waajiri kuweka kigezo cha uzoefu kuwa ni kigezo cha lazima, maana yake kuna vigezo vya hiari vya nyongeza na kigezo cha lazima cha masuala ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iseme kwamba vijana watapatiwa mifumo maalum ya mikopo ya ardhi, mifumo maalum ya mitaji na kadhalika na hii italazimisha utekelezaji. Lakini kwa sasa ilivyo na Azimio likipita kama lilivyo Azimio hili linavua wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka kwa lazima mifumo ya kisheria kama ilivyo katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja ambazo kwa kweli ni maangalizo kwenye utekelezaji. Tumezungumza hapa kwamba masuala ya vijana yasiyo na itikadi na ni hoja nzuri na ni hoja muhimu lakini mambo mawili. La kwanza tusifikie wakati iwe ni wazee au vijana tukafanya kama vile wazee wote ni sawa na vijana wote ni sawa. Hapa kwenye vijana kuna tofauti ya hali, kuna tofauti ya uwezo, kuna tofauti ya kila kitu lakini zaidi kuna tofauti ya matendo, unaweza ukawa na kundi la vijana mafisadi, ukawa na kundi la vijana waadilifu hali kadhalika unaweza ukawa na kundi la wazee wa waadilifu na kundi la wazee mafisadi vilevile. (Makofi)

Sasa katika kujadili hili suala la vijana, tusichukulie tu kapu la ujumla kama vijana wote ni sawa na sisi vijana tunazungumza kama vile wote tunafanana na tunasimamia yote tunayofanana. Kwa hiyo, ni lazima na sisi vijana tuchujane tuchujane, vijana ambao Taifa linalopaswa kuwaweka mstari wa mbele ni vijana ambao wako tayari kutetea rasilimali za taifa, vijana ambao wako tayari kuwa na uadilifu na tukishafika hapa tusizingize masuala ya kivyama na hili niwaambie zaidi watu wa upande wa pili, sababu mimi nafahamu pamoja na kuwa tunazungumza hapa kwa maneno kwamba tusingize mambo ya kivyama lakini leo tumezungumza hapa kwa maneno kwamba tusingize mambo ya kivyama, lakini leo tumezungumza sana kuhusu matatizo ya vijana wa elimu ya juu na kadhalika. Nina ushahidi wa barua mbalimbali hapa *correspondences* kutoka kwa Chama cha Mapinduzi kwenda kwa viongozi wa Serikaliza Wanafunzi kuwapa maagizo maalum ya kichama, sasa huku tunazungumza kwamba vyama visitumie wanafunzi sijui visifanye nini vijana wasigawanywe kitiikadi, vijana wanaofukuzwa sijui ni wa chama fulani. Lakini tunayoyazungumza humu ukweli ni kwamba kwa maana ya vitendo hatuyatekelezi. (Makofi)

Lakini la pili, tumezungumza kuhusu haja ya kuundwa kwa benki ya vijana ambayo tumesema ihudumie vijana wote bila kujali itikadi, lakini hapa nina ushahidi wa barua pepe (*email*) inatoka inakwenda kwa kiongozi mmoja wa Chama cha Mapinduzi lakini inazungumza kuhusu hili suala la Benki ya Vijana na inatoa maelekezo maalum ya Benki kuundwa kitiikadi, chama cha CHADEMA wame-*invest* kwa porojo na nafiki sisi tunataka ku-*invest practically* kwa maana fedha maalum ya kuwaelekeza vijana wote kurudi kwetu, sasa Benki ya Vijana tunazungumza vijana Bungeni kuhusu masuala ya Benki ya Vijana bila kujali itikadi chini ya *carpet*, kunatolewa maelekezo maalum ya kisiasa na kadhalika kwa nafasi za umma. Sasa kama kweli tunataka kutekeleza mkataba wa vijana ni lazima tuweke haya mambo ya kivyama katika mambo ya kimaendeleo ili isije kama ikawa mradi wa wakati ule wa Dar es Salaam wa mabasi ya wanafunzi leo wanafunzi wa Dar es Salaam wanahangaika na usafiri lakini miradi ili uwawa kwa namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba tu tutangulize mbele masuala ya Taifa. (Makofi)

MWENYEKITI: Nilitaka tu tuweke mambo vizuri hapa uliwasilisha mabadiliko ya hoja lakini nikadhani unaelewa lakini ulivyoanza kuchangia ulisema wakati wa Kamati, nikajua pengine hujaiona sawa sawa ile Kanuni ya 57, 58 utaratibu pia wa upitishaji wa maazimio katika Bunge. Maazimio hayaingii katika hatua ya Kamati, kwa hiyo, tutakachofanya kwa sababu katika ile mabadiliko yako yale umesema moja unayo mawili lakini umelisema moja wakati ukichangia. Sasa kwa sababu hili la kwanza hujalisema nitakupua fursa ya kulisema tu ili Serikali iweze kulisikia tu waweze kulichukua na *Hansard* iweze kurekodi kwamba ni hoja ya kwako ili mambo yakae sawa sawa.

Sasa tunaendelea mchangiaji wetu anayefuatia ni Mheshimiwa Peter Serukamba na wengine nitawataja kadri tunavyoendelea. (Makofi)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jambo hili muhimu sana la vijana, kwa kweli mkataba huu wa vijana umekuja umechelewa. Ukisoma Ibara ya kwanza mpaka ya mwisho unaona ni mambo mengi na kwa kweli ndiyo ya msingi kwa ustawi wa vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwa mwaka naanza kwa kuwatajia mwaka mwema lakini pia niwape pole Waheshimiwa Wabunge kwa Wabunge wawili waliotutoka katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu la Tanzania ukiangalia *statistics* zilizopo, kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka 39 ni asilimia 80 ya *population*. Kwa kupiga hesabu hapa kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka 39 ni asilimia 80 ya watu walioko Tanzania. Kwa hiyo, unaweza ukaona Taifa letu ni changa sana, ni Taifa la vijana. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema ukienda kwa *statistics* hizo unaweza ukaona kwa nini nimshukuru Waziri kwa kuleta mkataba huu na kwa kweli umechelewa na naona mkataba huu umehangaika sana na kuhakikisha tunajua matatizo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo makubwa ya vijana na kweli mkataba umesema haki ya kupata elimu, afya, ulinzi na usalama mimi nitajikita kwenye mambo mawili makubwa ama matatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tunapofika mwaka 2020, nchi hizi ambazo ziko kwenye *horn* ya Afrika tutakuwa tunahitaji kazi mpya milioni 68, na kwa kuanzia mwaka 2010 mpaka 2015 kwa nchi hizi lazima ziweze kutoa kazi mpya 3,200,000 inapofika mwaka 2015 lazima tutoe kazi mpya 3,600,000 kila mwaka.

Kwa hiyo, unaweza ukaona changamoto iliyopo kubwa ni kwenye kazi. Na kwa kweli unapoongelea kazi mpya unaongelea vijana, na kama Taifa tunafanya nini hii ni changamoto kubwa kwa namna yoyote ile tunaporidhia mkataba huu lakini tuwe tayari kwenda kuyafanya yaliyomo kwenye mkataba huu. Tukiridhia kwa sababu tu wamekaa viongozi vya Afrika, wameona ni muhimu kama Taifa lazima tutumie *youth charter* hii katika mambo yetu kuhakikisha tuna solve matatizo ya vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira ni kubwa sana, sasa lazima tuangalie tunafanya nini kuanzia kwenye elimu tunayoitoa na namna tunavyoendesha uchumi wetu kwa ujumla wake. Lakini pia itategemea sasa na mipango yetu namna ya kuhangaika na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Malaysia walifanya jambo moja kushughulika na tatizo la vijana, ardhi yao Mungu aliwapa siyo kubwa sana lakini wakaamua kulima michikichi, nchi nzima imepambwa kwa michikichi vijana wakachukuliwa, haya maamuzi makubwa alifanya Mahathir Mohamad, mashamba yamelimwa kwa mkakati wa Serikali vijana wakapewa mashamba yale. (Makofi)

Sisi Mungu ametupa kwa kweli ardhi ya kutosha na ametupa maliasili na ametupa mali za kuweza kuwafanya kuwatumia vijana wetu. Wapo wanaosema lazima vijana na kwenye *charter* hii imesema washiriki kwenye ngazi za uongozi, wapate madaraka mimi nakubali, wakati tunahangaika vijana tuwe kwenye nafasi za uongozi, tuwe Serikalini lakini lazima tujue tunafanya nini ili kuweza kupata kazi kwa ajili ya vijana wetu, lazima tujue tunawasomesha kwenye vitu gani ambavyo itawafanya waweze kujiendeleza. (Makofi)

Mimi ninayo hakika kabisa Serikali haiwezi kutoa kazi zote lakini sasa lazima Serikali iandae mazingira, lazima elimu tunayoitoa iweze kuwafanya hawa vijana wetu waweze kujitegemea. Kwa hiyo, lazima tuangalie mitaala yetu upya, tuangalie tutakavyopanga mipango ya nchi yetu ili kuweza kuhangaika na hili tatizo la vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wenzetu wa Kenya na Uganda ambao wameanza kusafirisha kazi, wameanza ku-export kazi na sisi kama Taifa lazima tuanze, tukubaliane kila baada ya mwaka mmoja

tujiulize tumepeleka kazi ngapi nje? Zipo nchi ambazo zinatafuta wafanyakazi wa bei rahisi, wafanyakazi *skilled, non skilled*, lazima na sisi tuanze kuwa sehemu ya hao na tuweze kupeleka kazi nje kwa sababu zinazotakiwa ni nyingi sana. Kwa hiyo, changamoto yetu kwa sababu ni kubwa lazima tuanze kuangalia namna ya kupeleka kazi nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni lazima tuangalie *retirement* yetu. Watu wana-*retire* katika miaka mingapi? Je, kweli tunahitaji watu wastaafu (*retire*) katika umri wa miaka 60? Unapofika miaka 60 tukubaliane, hakuna haja ya kumuongezea muda mtu aliyefika miaka 60 wakati tuna Taifa la watu wengi ambao hawana kazi. Lakini *the trend* unayoiona leo watu wana miaka 60 unasikia kaongezewa miaka mitatu, kaongezewa miaka miwili, kwa nini na bado tuna Taifa la Vijana ambao hawana kazi mitaani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda leo kwenye Bodi za Serikali zote imekuwa ni sehemu ya kwenda kupumzika hawa wastaafu, mimi silikubali hili hata kidogo. Kila Mwenyekiti wa Bodi lazima awe mstaafu, kila nani lazima awe mstaafu! Hawa watoto hawa tunaowasomesha hawa tunawapeleka wapi? Watu hawa wameshamaliza maisha yao. Watu wengine wamekaa miaka 40 kazini, hamtaki wapumzike? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tulikuwa tuna-*retire* katika umri wa miaka 55 ikaonekana kwa kweli watu wengi tulikuwa kama hatujaandaa watu wetu, kwa uoga tukaamua kupeleka miaka 60. Lakini hata miaka hiyo 60 haijatoshwa, mtu amefikisha miaka 60 anaongezewa mkataba wa nini na huku tunao vijana ambao hawana kazi? Ndiyo maana nasema kama tumeamua kupitisha mkataba huu twende tukayatekeleze yaliyomo kwenye Ibara hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawafahamu wazee ambao hata kutumia kompyuta hawajui, lakini mnawapa vyeo kila kukicha. Vijana wa leo wanajua dunia inataka nini. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba tuanze kuandaa *plan* ya kuwa-*absorb* hawa vijana.

Nakishukuru chama changu na Serikali yangu, tumepeleka elimu mpaka shule za Kata, tumeanzisha Vyuho Vikuu vingi. Maana yake ni nini? Ndani ya miaka mitano ijayo Taifa hili litakuwa na wasomi wengi sana. Sasa namna ya ku-*deal* na hawa wasomi lazima tujiandae. Moja, nimesema na sisi tuanze kusafirisha kazi kwenda nchi za wenzetu, tusiogope! Watanzania ni wafanyakazi wazuri sana. Watanzania wanaweza wakafanya kazi popote, lakini tumekuwa na tabia ya kutopenda kusafirisha kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1970, Mazrui aliwahi kuandika kitabu akasema; "Watanzania wana ugonjwa hivi, wanaumwa ugonjwa wa kuipenda nchi yao." Ndiyo maana Watanzania wakawa hawatafuti kazi kwenye *UN agencies*. Wote tulikuwa tuko hapa kwa sababu tulikuwa tuna mapenzi makubwa na nchi yetu, ule ugonjwa umeisha na dunia imebadilika. Umefika wakati na sisi tuanze kusafirisha kazi, lakini pia tuangalie mipango yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuongelea suala la Mipango Miji na Ardhi. Ukiangalia namna ambavyo tunahangaika kukusanya ardhi, unajiuliza miaka 20 ijayo vijana hawa watakwenda wapi? Leo nchini Ethiopia kila unapoenda unakuta Addis Ababa imebadilika, maeneo yaliyokuwa kama Manzese yale wamefanya maamuzi wanaondoa watu wote, wanajenga magorofa, wanawarudisha wale na wengine ambao wangewatoa sehemu nyingine. Matokeo yake inabaki ardhi ambayo itatumika kwa ajili ya vizazi vijavyo. Leo ukiangalia mji kama wa Dar es Salaam, tunakaribia kuimaliza yote kugawa viwanja. Unajiuliza Taifa hili nalo baada ya miaka 20 inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba mkataba huu ni mzuri sana lakini unazo changamoto za kutosha. Ili tuweze kukabiliana na changamoto hizi ni lazima tuwe tayari kwenda kuyasimamia haya ambayo vijana wanatakiwa wayapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho wenzangu wamelisema, kupata kazi ni lazima uwe na *experience* ya miaka mitano, miaka mitatu, lakini wakati huo huo tuna vijana wetu vyaoni kule wanakwenda kufanya *studies* kila mwaka na Serikali inawalipia. Sasa leo kwenye kazi kwa nini watakiwa kuwa na *experience*, wanaitoa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya vijana ni kubwa na kama Taifa ni lazima tujiandae nayo. Changamoto ya kwanza nilikuwa nawaambia wenzangu hata vyama hivi, sisi ambao tupo kwenye vyama kitakachoamua chama gani kiendeleo kuongoza nchi yetu hizi za Afrika ni vijana. Hawa vijana wasio na kazi ndiyo watakaofanya maamuzi na inawezekana wasifanye maamuzi sahihi kwa sababu ya hali iliyopo. Kwa hiyo, kwa namna yoyote ile nchi hizi zinazoendelea ni lazima tuhangaikie na ku-solve tatizo la vijana hasa kwenye kutafuta kazi. Ili tuliweze hili narudia tena, lazima tuanze kuhakikisha tunaandaa mazingira ya vijana wetu kuwa na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimpongeze Waziri kwa kuleta jambo hili. Ni jambo kubwa lakini haya yaliyomo humu yanahitaji *commitment* na hasa ya kisiasa ili tuweze kuyatekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono jambo hili. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Hawa wazee nitawapa nafasi baadaye. Nitajitahidi kuweka muda wangu vizuri. Mheshimiwa Selasini ujiandae, Mheshimiwa Sanya ujiandae na Mheshimiwa Kilufi. Nitawaweka vizuri kwa wazee ili mambo haya yakae vizuri. Kwa sasa hivi mniache tu niendeleo na hii *facebook* kwanza ili ipumue kwanza halafu baadaye ninyi mtaweka mambo sawa sawa. Basi nitamwita Mheshimiwa Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa mwingine ambaye nitamtaja baadaye.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii muhimu. Japokuwa asubuhi nilipata nafasi ya kuongea kama Waziri Kivuli, lakini nashukuru kupata nafasi hivi sasa kwa sababu naongea kama Mbunge wa Mbeya Mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu na mimi pia nafurahia mkataba huu. Lakini pia naomba kutoa rai na kuisa Serikali kwamba mkataba huu yaliyomo inabidi yatekelezwe kwa maslahi ya vijana wa Taifa hili kwa sababu vijana wa Taifa hili wamepigika na kwa bahati mbaya bila kupinda pinda kama Taifa ni wazi kabisa tumeshindwa kuja na mikakati ya kuwasaidia vijana hawa.

Kitu hiki ni hatari sana kwa sababu matokeo yake vijana wengi wamekata tamaa na hata matumizi ya dawa hatari za kulevya yanaongezeka kati ya vijana wote, wawe wanafunzi, wasanii na wote. Lakini hii yote inachangiwa na hali ya vijana kukata tamaa hatua ambayo imewafanya wasiwe na imani tena na Serikali hii. Huo ni ukweli ambao ni lazima tuuseme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema vijana ni bomu linalosubiri kupasuka. Mimi nasema, vijana ni bomu la sumu ambalo tayari limeanza kuvuja taratibu na nchi inavuta hewa yake. Vijana ni *weapons of mass destruction (WMD)*. Ndiyo! Vijana siyo bomu linalosubiri kupasuka. Limeshaanza kuvuja kwa sababu bomu lile la sumu limehifadhiwa vibaya. Hii itakwenda kui-cost nchi hii, itali-cost Taifa letu. Kwa maana gani? Tunapoangalia nchi kama Somalia, wale magaidi wa *Al-shabab* wengi ni vijana. Sasa hivi kuna kundi la Boko Haram, Nigeria. Wanaotumika kupigana ni vijana. Vijana baada ya kukata tamaa wanafikia sehemu wanakuwa wako tayari kutumika kwa namna yoyote ile. Nigeria ni nchi ya Afrika, Somalia ni nchi ya Afrika, Tanzania ni nchi ya Afrika, yote yanawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa nchi hii wamekuwa na tatizo kubwa sana la ajira, hapa tunazungumzia *experience*. Wanaambiwa *experience, experience*, lakini ukweli ni kwamba hata hilo suala la *experience* linatumika kama *cover* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la ajira za kujuana katika Taifa hili na ndiyo maana watoto wa maskini wanaambiwa *experience* lakini mtoto wa kishua akimaliza *college* tu anapata ajira halafu anaambiwa utakwenda kazini mpaka saa 8.00, jioni utakwenda kusoma *Masters*, haya yanafanyika. Kwa hiyo, suala la ajira za upendeleo bado liko nchi hii na hili suala la kusema *experience* hiyo nadhani ni *cover* tu kwa sababu tatizo la ajira linashangaza sana kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia suala kama la walimu. Vijana wengi wanamaliza elimu. Kwetu kule *TECU* – Mbeya, wanamaliza *degree* yao ya ualimu, wanamaliza ualimu *UDOM* na katika vyo vyetu

vingi, lakini wamejazana mitaani bado wanakula ganja na vijana ambao hawaendi shule kwa sababu shuleni hakuna walimu. Sasa hii ni nchi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shuleni kuna matatizo ya walimu, lakini kuna walimu tena wana *degree*, kuna wakati hapa tulikuwa tunatengeneza walimu wa *voda faster*. Tulikuwa tunasema ooh, tuna shida ya walimu mpaka kukawa na walimu wanaitwa walimu wa *voda faster*. Sasa kulikuwa na haraka gani ya kuwapeleka wale walimu wa *voda faster* wakati sasa hivi kuna walimu wenye *degree* zao na wako mtaani tu tunashinda nao vijiwani wanashindwa hata kupata ajira? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili inabidi tuliangalie kama tunataka kweli kusema kwamba nchi hii au Taifa hili lina makusudi ya dhati ya kutatua matatizo ya ajira za vijana. Hata huko vyuoni mikopo yenyewe bado mpaka leo zengwe, mikopo haeleweki. Ndani ya Bunge hili tuliambiwa na Serikali kwamba Rais ameunda Tume Maalum ya Kurekebisha Bodi ya Mikopo, lakini mpaka leo hii simu, *text messages* 300 zinazolingia kwa siku moja, 180 zinahusu matatizo ya mikopo kwa wanafunzi kule jimboni kwangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vyo vya *TECU*, wanafunzi wa Mbeya ambao wanasoma vyo mbalimbali, malalamiko ya mfumo wa mikopo bado yako pale pale. Sasa sijui hiyo Tume iliyoundwa na Rais imefanya kazi gani? Ili kuondoa haya mambo inabidi hii Tume ivunjwe na iundwe nyingine. Nadiriki kusema kwamba Serikali haina vipaumbele vyovyote kwa vijana, kwa muda mrefu inapiga tu siasa na nadhani kipaumbele cha Serikali kwa sasa kipo kwenye Vazi la Taifa. Hata hili Vazi la Taifa vijana walikuwa wana sehemu yao pale, lakini matokeo yake Mheshimiwa Waziri ambaye naomba nimsifu kwamba hii kitu (Vazi la Taifa) ikipita leo kwa kweli ataacha *legacy* nzuri na itaacha *legacy* nzuri kwa hili Bunge pia. Ni kitu kizuri, lakini inabidi achukue maoni tunayoyaongea hapa ili aende akarekebishe kwa faida ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuanzisha mchakato wa Vazi la Taifa, hii nchi ina wasanii, wabunifu halafu unaenda kuchukua washikaji zako, unaenda kuchukua marafiki zako ndiyo unawaweka kwenye hiyo Tume kwamba waiongoze, unawaacha akina Khadija Mwanamboka, unaawaacha akina Mustafa Hassanali ambao ndiyo wabunifu wanaojulikana katika Taifa hili. Kwa nini usiwape hilo jukumu ili usonge, matokeo yake unakuja na mawazo ya kuleta urafiki katika mambo ya Taifa? (Makofi)

MWENYEKITI : Mheshimiwa Mbilinyi washikaji zako ni neno la Kiswahili cha kawaida?

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Yah, linatumika sana, ni la Kiswahili kwa maana ya marafiki wa karibu, mnashikana.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, *Hansard* ichukue lipi? (Kicheko)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Kama halina tafsiri potofu kwenu kwa sababu baadhi ya lugha zinaweza zisieleweke vizuri baadhi ya sehemu, lakini mimi sijihisi na kwa vijana wanaonisikiliza kule mtaani naamini wamenielewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitagusia sana suala la wasanii leo hii, lakini naomba nitumie fursa hii kuwapongeza wasanii wanaharakati wanaojulikana kama *Anti Virus Vinega* kwa sababu kazi wanayoifanya inatambulika na ninaomba niwajulishe kwamba wasanii wote wanaitambua na wanafurahia kwa sababu inaleta mabadiliko kwa baadhi ya wanyonyaji wanaoshutumiwa kuanza kubadilika katika suala zima la malipo kwa wasanii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nije kwenye suala la Wamachinga. Miaka 50 ya Uhuru Wamachinga bado wako vitani na Serikali yao, mpaka kesho kama Taifa kweli tumeshindwa kuweka mikakati ya kuwasaidia Wamachinga! Tena hili inabidi niliongee kwa sauti sana kwa sababu suala la Wamachinga halijasikika vizuri, lakini nikiwa kama mhanga wa eneo lililopata madhara ya Wamachinga (Jimbo langu la Mbeya Mjini), hili leo ninaomba nilizungumze vizuri sana. Kama Taifa tunatakiwa tuje na mkakati wa dhati kwa ajili ya Wamachinga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Jiji duniani lililokuwa na Wamachinga. Nilishawahi kulisema hili na ninalirudia leo tena. Nenda New York, London, nenda popote pale unakuta Wamachinga wamesimama

barabarani. Tena Wamachinga unaowakuta New York wale vijana wa Kisenegali hata *immigration status* yao katika ile nchi haihusiani, haijaka vizuri lakini hawaji kukamatwa kwa *immigration* na hawaji kukamatwa kwa Umachinga. Wanaachwa wafanye shughuli zao kwa sababu wameteteleza sheria za jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafanyaje? Badala ya kuwaambia Wamachinga watandaze viatu chini, labda mita 10 au 20, haya majiji yajenge *shelves* ambazo *pair* 50 hazitasambaa kwa kwenda hivi bali vitakwenda kwa juu kwenye ile *shelf*. Zile *shelves* zitawekwa sehemu maalum, zilezile zenye wateja kwa sababu Mmachinga hawezi kwenda sehemu ambayo haina wateja. Kwa hiyo, zile *shelves* ziwekwe sehemu maalum na majiji yetu yatachukua kodi ndogo ndogo kutoka kwa wale Wamachinga na hapo ndipo tunapozungumzia kuwaingiza Wamachinga katika mfumo wa uchumi wa nchi. Sioni kama kuna kitu kigumu hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si lazima nchi nzima iwe kama Mbeya Mjini. Siku mbili imepiganwa vita pale kati ya Wamachinga na Polisi, wakaja JKT, wakaja JWTZ wakashindwa. Mheshimiwa Waziri asubuhi amesema kwamba zile vurugu zilitulizwa na JKT. Kwa hili nitaongea, vurugu zile hazijatulizwa na JKT. JKT walishindwa, watu wa Mbeya wanajua nani alituliza zile vurugu. Kwa hiyo, basi walichofanya askari ambao Mheshimiwa Waziri anasema walienda kuokoa jahazi ni *negative*. W alipora Wamachinga simu, wakapora fedha, wakapora fedha za akinamama wanaofanya biashara eneo la Mwanjelwa kama Mama Mwakyoma *on gun point*. Unamwekea mwana mama wa Mbeya *on gun point* asiokote pochi lake la shilingi milioni nne chini, halafu hapa Waziri anakuja kuongea siasa kuhusu maisha ya watu! Kuhusu maisha ya Wamachinga, hiki kitu inabidi tukiangalie kama kweli tunataka kusonga kama Taifa, siyo vinginevyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili hili, pia naomba nitoe rambirambi au *RIP* kwa mara nyingine kwa kijana John Bosco Mwalingo ambaye aliuawa kwenye vurugu zile za Wamachinga Mjini Mbeya, Mmachinga mwendesha boda boda. Halafu leo hii tunaka kwenye Baraza la Halmashauri, Diwani wa CCM - Viti Maalum, anasimama anasema; "Mimi ni nesi nafanya kazi hospitali, nilikuwepo ile siku ya maafa, siku ya vurugu, hakuna mtu yeyote aliyepigwa risasi wala hakuna mtu yeyote aliyekufa." Katika Halmashauri Diwani aliyeketwa pale kwa mfumo wa Kikatiba uliokuwepo anakana mauaji! Sasa hivi katika nchi zote za Ulaya, ukikana mauaji ya halaiki (*genocide*) ya Israel unaenda jela. Huyu anayekana mauji ya Mwanambeya anatakiwa afanywe nini? Chama chake kinampa adhabu gani kwa sababu ana *support* ya Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri. Mwenyekiti wa Halmashauri anaka tu pale anatabasamu wakati Diwani wake wa CCM anakanusha kwamba katika vurugu za Wamachinga Mbeya hakuna mtu aliyekufa wala mtu aliyepigwa risasi! Sasa basi kwa sababu kuna utata katika hili, Serikali iunde *public inquiry* (Tume Maalum) kwenda kuchunguza suala hili Mbeya. Nani alimua nani na nani alifanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo natoa wito kwa Serikali kuwaacha Wamachinga nchi nzima wafanye shughuli zao kwa uhuru bila vurugu ili yasitokee mambo kama ya Mbeya mpaka pale Serikali itakapokuja na mkakati madhubuti kwa ajili ya Wamachinga. Tunaiga vitu vya Marekani na Uingereza, tunavileta hapa nchini, tuige Zambia. Rais Michael Sata, juzi ametangaza kwamba Wamachinga wasiguswe kwa miaka mitano atakayokuwepo mpaka pale Serikali yake itakapokuja na mkakati mbadala. Kama tunaiga Marekani, UK, sijui *programs* za uchumi na kila kitu, huu ni uchumi wa Wamachinga nasi tuige Zambia, tuwaache Wamachinga wa Taifa hili wafanye shughuli zao ili tuepuke kukabwa kwa sababu tukiwazuia Wamachinga kufanya shughuli ndiyo wanatupiga nondo kule Mbeya. Tuliseme mara ngapi ndani ya hili Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa wito, Wamachinga waachwe huru kufanya kazi zao nchi nzima kwa amani kama wanavyofanya. Halihitajiki Jeshi, halihitajiki nini. Mbeya ni mfano wa kuigwa na wakati huo huo wakati itakapoundwa hiyo Tume itakapokuja na matokeo, kuwe na kipengele cha fidia kwa wahanga wote wa vurugu za Wamachinga Mbeya. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mbilinyi a.k.a Mr. Sugu. Sasa nitamwita Mheshimiwa...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuweka sawa maelezo aliyotoa mdogo wangu Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Mbilinyi kwamba, Walimu waliomaliza Vyuu Vikuu wamepigika, wako mtaani, hawajaajiriwa. Labda kwa taarifa tu nimwambie kwamba, hivi sasa hata akisoma kwenye *Website* ya Wizara, Walimu wote wa namna hiyo wameshaajiriwa na wamepangwa vituo vya kazi nchi nzima. *(Makofi)*

Namshauri leo akaingie kwenye *Website* ya Wizara ya Elimu ataona, imeshaanza kutangazwa, labda kama ana tatizo na Mwalimu mmoja au wawili ambao anawajua lakini Walimu wote waliohitimu Shahada wameshapangwa na wameajiriwa na Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi taarifa hiyo unaipokea!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Siipokei na nitawasiliana na Mheshimiwa Waziri kwa sababu nina *text message* hapa na ndiyo maana imebidi nizame kutoa simu kuangalia *message* za baadhi ya Walimu ambao wako mtaani Mbeya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, naomba sana, shughuli za Bunge zinaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni na taratibu ambazo siyo wakati wote ni wakati wa mambo ya mzaha. Serikali inaposimama na kusema jambo ambalo sote tunafahamu kwamba limefanyika, Walimu wote wamepata ajira na kama unaikataa maana yake kwa uzito wa Kanuni yenyewe unaweza ukapaswa kuleta ushahidi kwa sababu siyo suala la mtu mmoja maana ukisema Walimu wote, ni jambo tofauti kidogo.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MWENYEKITI: Tunaomba kusiwe na ushabiki kwenye mambo haya kwa sababu tunazungumza na anayehusika. Kwa hiyo, nafikiri tusifike huko mbele, hiyo ndio taarifa ya Serikali, lakini kama wewe una taarifa ya watu wawili, watatu ambao wameachwa, ni vizuri ukaisaidia Serikali kwamba kuna hawa ninaowafahamu wameachwa, lakini kusema kwamba wote wako mtaani wameachwa si jambo linalokaa vizuri kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbilinyi!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema wote kwa sababu wote hawawezi kutuma *messages* kwenye simu yangu. Nimesema ni baadhi, siyo wote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, nafikiri imekaa vizuri. Tunaendelea na sasa nitamwita Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na baadaye nitamtaja anayefuata kwa sababu orodha ya wachangiaji imezidi kuongezeka, imekuwa kubwa, sasa nadhani nitumie tu busara ya Kiti.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Azimio hili muhimu la maendeleo ya Vijana katika Bara la Afrika lakini vilevile katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa niaba ya Serikali, wakati mwingine kumekuwa na mawazo ya mikataba hii kuchelewa kuletwa Bungeni kwa sababu mbalimbali lakini mimi kwa upande mwingine naona mkataba huu haujacheleweshwa sana. Wakati tukipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati, sababu kubwa ya kimsingi ilikuwa ni kuutazama mkataba wenyewe kwa undani wake mkubwa ili tutakapokuja kuulizia hapa Bungeni kweli uwe kwa maslahi ya Taifa na maslahi ya vijana wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri na Serikali, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakati nikisoma taarifa na nitayarudia, sote katika Kamati na mimi mwenyewe ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Peramiho, kimsingi ninakubali umuhimu wa vijana. Mahali

popote vijana ni nguzo na nyenzo muhimu sana ya maendeleo kwanza ya nchi lakini maendeleo ya jamii husika mahali popote. Hilo halina ubishi na mimi nakubaliana nalo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili kwa upana wake linatoa maelekezo yakiniifu ya nini nchi zitakazoridhia mkataba huu zinatakiwa kutekeleza majukumu gani katika kuhakikisha sekta ya vijana inashughulikiwa kwa hali inayotakiwa na hasa kwa wakati tulionao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili kabla sijaingia kwa undani wake lina pande zote mbili yaani upande wa kuikabili Serikali na kuikumbusha wajibu wake kwa vijana, lakini pia lina wajibu kwa vijana wenyewe kwa maisha yao ya kila siku. Kwa hiyo, ukilitazama Azimio hili unagundua kwamba linatupa mwelekeo sahihi wa jinsi ya kushughulikia matatizo ya vijana. Ni ukweli usiopingika kwamba vijana wana matatizo mengi na ya kimsingi na Azimio hili linaporidhiwa leo litatupa nafasi nzuri kama Serikali kujipanga na kuona namna gani sasa tunatatua matatizo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza kwamba yapo matatizo ya vijana lakini tunatakiwa kuyaangalia kwa pande zote mbili, yamezungumzwa sana matatizo ya vijana wasomi kwa kukosa ajira na masharti ya ajira yanayowakwamisha katika misingi hiyo ya ajira. Mimi nataka niwarudishe Waheshimiwa Wabunge nyuma, kwamba 80% ya vijana wa nchi ya Tanzania bado wanaishi vijijini na 80% ya vijana hao wanaoishi vijijini ni vijana ambao maisha na taratibu zao za maisha bado zinakabiliwa na changamoto kubwa ukilinganisha na 20% ya vijana wanaoishi mijini. Kwa hiyo, tunapoliangalia Azimio hili na kuishauri Serikali, nafikiri maamuzi yetu ya kuridhia leo yataisaidia Serikali yetu kuwatazama vijana hawa kwa idadi waliyonayo na matatizo waliyonayo.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, vijana waishio vijijini matatizo yao hayalingani na matatizo ya vijana waishio mijini, vijana waliosoma matatizo yao hayalingani na vijana wasiosoma. Kwa hiyo, hatuna budi leo kuishauri Serikali yetu tusijikite tu katika kutatua tatizo la vijana waishio mijini na kusahau 80% ya vijana wanaoishi vijijini ambao ni wengi sana na pia wanahitaji kusaidiwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba leo naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, vijana wetu wasomi angalau leo tunapewa taarifa hapa kwamba Walimu wote wameanza kujiriwa hata kama wapo wachache hawajaajiriwa basi naiomba Serikali kufuatilia hilo, lakini 80% ya vijana waliopo vijijini tumewaajiri kwa njia zipi? Tumewatafutia namna ya kujiajiri kwa njia zipi? Ni kweli kabisa upo msingi wa hoja kwamba ni lazima azma ya kujiajiri ianze kwa kijana mwenyewe lakini je, kijana huyu amejengewa mazingira na utaratibu wa kuweza kujiajiri? Hapo ndiyo kuna hoja ya msingi kabisa. Wapo waliosema kwamba wasomi wetu waangaliwe kwa namna wanavyoandaliwa, katika nchi zilizoendelea na nadhani sisi sasa ndiko tunakokwenda ni lazima tutazame huko, vijana wetu wasomi sasa hivi tuwaandae kwa mazingira yote mawili, tuwaandae waweze kujiajiri wao wenyewe na tuwaandae waweze kuajiriwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wasomi katika nchi hii inaongezeka, tumetengeneza utaratibu gani? Hiyo ndiyo hoja ambayo mimi nafikiri Serikali iangalie, inatoa mazingira gani kwa vijana wasomi kujiajiri na waweze kuajiriwa lakini wale ambao hawajasoma, 80% ya vijana waishio vijijini tunawatengenezea mazingira gani? Hawana elimu ya biashara, hawawezi kupata mikopo kwa sababu ya masharti magumu ya mikopo katika benki zetu na hakuna Sheria ambazo ni rafiki za kuwasaidia kujikwamua kiuchumi. Leo vijana wanaoishi vijijini wanakimbia maeneo ya vijijini na kuhamia mijini, nitakupa mfano. Leo hii wakulima wengi wa kahawa katika maeneo ya Jimbo langu wamebaki kuwa ni wazee kwa sababu vijana wengi hawaelewi mbinu za kilimo bora na jinsi ya kubadilisha kilimo kutoka kilimo cha kienyeji kwenda kilimo cha kisasa. Ukimwambia kijana sasa aende akalime anaona ni taabu sana, sasa hapa ndiyo mkakati mzito unatakiwa ufanyike. Hapa mimi nataka kuuliza utayari wa sekta nyingine mtambuka katika kutekeleza Azimio hili ukoje? Katika kuridhia Azimio hili wala tusiangalie Wizara moja tu ya Vijana, Habari, Utamaduni na Maendeleo ya Michezo, Wizara hii inawezesha kuridhia mkataba huu, lakini utekelezaji wake utaigusa Wizara ya Fedha, utagusa sekta ya mipango lakini pia utagusa sekta ya kilimo, sekta ya madini, tena umeleza vizuri kabisa suala la madini katika maeneo ya vijijini. Sasa tujulize ni namna gani tunaweza kutengeneza nyenzo za kuwezesha mkataba huu kutekelezeka. Hiyo ni changamoto kubwa sana na inatakiwa tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bado tunahangaika sana, Serikali yetu imejitahidi kuleta dhana ya Kilimo Kwanza. Mwaka huu vijana wangu wengi wa Jimbo la Peramiho walijitolea sana kulima, wamelima mahindi kwa wingi lakini wamepata shida kubwa sana ya soko. Sasa haya ndiyo mambo tunayotakiwa kuyatazama ili kuwapa nguvu vijana kwa sababu mkataba unasema waajiriwe ama wajiajiri wao wenyewe. Leo hii katika maeneo ya vijiji vyetu ufahamu wa vijana kuhusu mambo yao yanayowahusu ni kidogo sana na ndiyo maana unawakuta vijana wengi wako vijiwani toka asubuhi mpaka jioni. Mimi nafikiri kuna umuhimu kutilia mkazo Vyu vyetu vya Maendeleo ya Jamii ambavyo tunavyo kwenye vijiji vyetu. Vyu vile sasa vitumike kama vituo vya kuongeza stadi za kazi na maisha kwa vijana wetu. Ukiangalia bajeti ya kuviwezesha vyu vile ni ndogo sana, haiwezi kukidhi hata kuwasaidia vijana kule vijijini kujiondoa katika janga la umaskini. Sasa mimi nadhani tunaporidhia Azimio hili hakika ni lazima kuja na mpango mahsusi wa kujibu maswali yanayowahusu vijana kwa kuwaangalia wale 80% waishio vijijini na kuwatazama hawa 20% waliopo mijini na kuwaangalia kwa kadri ya mazingira waliyonayo yaani wasomi na wasio wasomi, wakulima, wafanyabiashara wadogowadogo na mambo mengine yote yanayowazunguka vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni lazima tujipange sawasawa na vijana, 35% ya Watanzania ni vijana na hawa ni vijana kuanzia miaka 15 - 35 lakini watoto ni asilimia kubwa zaidi ambao ni vijana wa kesho, kwa hiyo, kutoshughulika na vijana, naomba nikubali kwamba tunajitengenezea tatizo kubwa katika Taifa letu. Ni lazima suala hili la vijana leo lifungue ukurasa mpya na baada ya kufungua ukurasa mpya vijana hao sasa waanze kutazamwa kama ni sekta ambayo inatakiwa iangaliwe kama ni mchango mkubwa na tegemeo la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuridhia Azimio hili tumesema yapo maeneo tayaridhie kwa stara. Kwa mfano, suala la watoto wa kike kupata mimba, kuolewa na kuendelea na masomo. Agenda hii imechukua muda mrefu sana kujadiliwa katika nchi yetu, mkataba unataka watoto hawa waendeleo na masomo, bado Sheria zetu za nchi haziruhusu suala hilo yaani watoto hao hawaruhusiwi. Lakini mkataba unatutaka kuwa na uwiano wa 50% kwa 50% kati ya watoto wa kike na wa kiume katika elimu, leo katika Vyu Vikuu watoto wa kiume ni 65% na wa kike ni 35%, hiyo ni hali ya hatari, tukiendelea nayo huko mbele tutashindwa na kwa nini inakuwa hivyo? Ukiangalia kwenye shule za msingi uwiano upo sawasawa kwa hiyo hapa katikati kinachoendelea ni zile *drop outs*, watoto wanapata mimba, wanaacha shule na kadhalika, sasa tunasema nini katika kipindi hiki cha kati? Hapa kuna agenda na hoja ya msingi ya kufanyiwa kazi na kwa kweli ni lazima tuone tunafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanatakiwa wamiliki mali, lipo tatizo la Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi; Sheria ya Mirathi ni ya muda mrefu ninaomba ifanyiwe marekebisho katika kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa hakika ninapata shida ya muda na lazima tumuachie Mheshimiwa Waziri muda wa kutosha kwa sababu wachangiaji wamekuwa wengi, ni kinyume cha matarajio kabisa niliyokuwa nayo. Kwa hiyo, mtanisamehe wale niliokuwa nimewataja lakini nitajitahidi kidogo hapa, nitaomba nimwite mchangiaji wangu, maana hata muda wenyewe utakuwa hautoshi lakini wawili wanaweza wakaenea. Basi naomba nimwite Mheshimiwa Stephen Masele, atamalizia Mheshimiwa Selasini kwa sababu alikuwepo kwenye orodha tangu mapema.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nampongeza Waziri kwa kuleta mkataba huu Bungeni ili uweze kujadiliwa na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu una mambo mengi, lakini mimi nataka kujielekeza zaidi katika eneo hili la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye michango ya Bunge la bajeti niliwahi kuzungumza kwamba sekta nyingine zikiwemo za kitaalamu haziwezi kuwaajiri vijana wengi wa Tanzania ambao wengi wao hawana ujuzi wa kutosha na bado Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuwajengea uwezo na ujuzi ili waweze kujiajiri. Niliwahi kutoa ushauri kwamba Wizara ijielekeze katika maeneo ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama nchi za Afrika Magharibi na Afrika ya Kati, vijana wengi wameajiriwa katika sekta ya michezo. Ukisoma Ibara ya 22 ya mkataba huu inaeleza kwamba vijana wapate uhuru wa kuburudika na kupumzika na kufanya shughuli za michezo kama sehemu ya afya. Mimi nashauri kwamba Tanzania sasa ifike mahali tuchukulie michezo kama ni ajira, uchumi na ni sekta muhimu ambayo inaweza ikaleta uchumi katika Taifa letu. Mfano wacheza mpira na wanariadha wanaocheza Ulaya kutoka katika Bara za Afrika wanatoa ajira kubwa sana kwa vijana wanaoacha nchini mwao kwa kuleta fedha nyingi ambazo wanaweza kwenye nchi zao. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuanza kutazama uwezekano wa kuwa Chuo Kikuu cha Michezo na vijana wengi wapelekwe kusoma au kupata *training* ili waandaliwe kwenda kucheza michezo ambayo italeta uchumi katika Taifa letu na hii dhana ya michezo starehe na afya iwe ni dhana ya ziada tu lakini tujelekeze zaidi katika michezo kama ni sehemu ya kujenga uchumi wa Taifa na kutoa ajira kwa vijana walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo pia ndiyo sehemu kubwa ambayo inatoa ajira katika Taifa letu na mimi napenda kuona siku moja tunawa-engage vijana wanaohitimu kwa mfano Chuo cha Sokoina, ile miradi tunayoifanya ya Kilimo Kwanza, matrekta na kadhalika basi Serikali iweke utaratibu wa kuwa-engage Wasomi ambao ni Wataalamu, Serikali inawasomesha kwa fedha nyingi na wana ujuzi, iwape mitaji na nyenzo za kufanya kazi ili na wao wakaajiri vijana waliopo vijijini ambao hawana ujuzi wa kutosha. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumetengeneza ajira nyingi kwa vijana kuliko kutegemea kama Mheshimiwa Mshama alivyosema tuwatafutie ajira nyingine ambazo hatuwezi kuwatafutia vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma tena katika mkataba huu hasa kwenye Ibara ya 18, Ibara hii inaeleza kwamba uwepo usimamizi wa Sheria ambao utawalinda vijana hasa inapotokea wananyanyaswa, vijana wengi wa Taifa hili wananyanyaswa sana. Mimi niungane kabisa na Mbunge mwenzangu wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na nimekuwa nikipitia hotuba yake hapa amesema kwamba nchi yetu ni lazima tunapozungumzia vijana tuweke itikadi za kisiasa pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu kuona vijana wa jamii ya wafugaji haswa Wasukuma, Wamasai, wananyanyaswa ndani ya Taifa lao. Wanazuiwa kwenda kutembea maeneo mengine katika shughuli za uzalishaji eti kwa sababu wanakwenda kuharibu mazingira. Hii inatia uchungu sana kwamba leo kwenye Taifa letu Tanzania ukitaka kutoka Shinyanga, Mwanza, Tabora ama Arusha uombe pasipoti ya kwenda kuishi Mpanda, Rufiji au Ifakara. Hii haikubaliki! Naomba tunapozungumza na tunapojadili Mkataba wa Vijana, tutambue kabisa vijana ndio nguvukazi ya Taifa na tunapozungumzia wafugaji wale wanaoswaga ng'ombe kutoka Shinyanga na maeneo mengine ya wafugaji ni vijana ambao wanaoswaga ng'ombe kule njiani wananyanyaswa sana. Vijana wengine wanauawa, vijana wengine wananyang'anywa mali zao, wanateswa na wanaambiwa huku mnakuja kuharibu mazingira rudini kwenu, twende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukitazama hapa sisi Wabunge tuna afya njema ni kwa sababu ya mazao ya wafugaji, mazao ya ng'ombe. Ukienda kwenye baa asubuhi unasema naomba supu lakini supu ile inatoka wapi? Suala la ufugaji linatoa ajira kubwa kwa vijana lakini leo vijana wafugaji wakienda Rufiji wanaambiwa toka waende wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri akiwa anajumuisha ahakikishe kabisa anatengeneza mazingira mazuri haswa kwenye sheria ili kuhakikisha vijana wa jamii zote wanapata haki sawa katika kufanya shughuli zao za uzalishaji katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge hili, niwaombe Wabunge wenzangu, mwanzoni nilikuwa nadhani ni utani, lakini inaelekea kuwa ni *serious*, jamii ya wafugaji haitakiwi katika nchi hii, sielewi waende wapi. Ndugu zangu nazungumza hivi kuna kundi kubwa la jamii linanyanyaswa, wanapoteza fedha nyingi na wanatumia muda wao mwingi kushughulika na kesi ambazo hakuna mazingira ya kuwasaidia. Naomba Mheshimiwa Waziri anapojumuisha atueleze vizuri ili jamii ya wafugaji iweze kuelewa kabisa nafasi yao iko wapi kwenye Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi nilitaka kuzungumzia hayo na nimpongeze Waziri kwa kuleta Azimio hili na niwapongeze Wakuu wa Nchi kwa kuweka mkazo haswa kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi kilichofanyika Malabo ambapo ajenda kubwa ilikuwa ni kuwawezesha vijana katika nyanja za uchumi na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Selasini, huyo ndiye atakuwa Msemaji wetu wa mwisho.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa msemaji wa mwisho. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge vijana ambao wamechangia hoja hii. Ninawapongeza kwa sababu ya mshikamano waliouonyesha na ninawaoomba tu huu mshikamano uendeleo hata katika hoja nyingine zitakazoingia katika Bunge hili kwa sababu imeonyesha kweli ni Bunge linalojali maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, katika michango mingi ambayo imetolewa, vijana ambao nimeona mkazo mkubwa umewekwa sana kwao ni vijana wasomi, vijana wa Vyuo Vikuu na ambao wanategemea kupata ajira rasmi. Mimi naunga mkono sana hoja hizo lakini nataka pia tujielekeze katika kundi kubwa la vijana ambao wako mitaani, vijana ambao wanategemea ajira zisizo rasmi. Ukubwa wa tatizo la vijana hawa unaoongezeka siku hadi siku na kwa kweli nionavyo hapa ndipo bomu ambalo wengi wamelizungumza lilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita kwenye mitaa mingi na vijiji vyetu vingi, vijawe vimeongezeka sana vya hao vijana. Hawana matumaini na hawajui ni nini watakachokifanya au hawana matumaini ya siku inayofuata. Kwa sababu hiyo, vijana wengi wamejiingiza katika vitendo viovu. Wako vijana sasa hivi wanaendesha maisha yao kwa kujiuza. Hii sio siri kila mmoja anajua. Ndio maana naiomba Serikali na sisi kwa pamoja kuweka mkakati wa makusudi kabisa wa kuangalia namna ya kuwasaidia vijana hawa. Asilimia kubwa ya vitendo viovu katika nchi yetu ukiangalia vinafanywa na vijana kwa sababu ya ukosefu wa ajira au namna ambavyo wataendesha maisha yao. Kwa hivyo, wakati tukizungumza habari ya ajira za vijana kutoka Vyuo Vikuu, ajira zilizo rasmi, wakati tukizungumza habari ya vijana kuwa viongozi lakini naomba vilevile tuzungumze habari ya vijana kama nilivyosema walio wengi ambao wanaishi kwa kubaingaiza huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa kuna baadhi ambao wamejitahidi kupata namna ambavyo wataendesha maisha yao lakini pamoja na kupata nafasi hizo bado wananyanyaswa kwa kiwango kikubwa sana. Wewe na mimi tunapita kwenye sehemu za starehe, kwa mfano kuna hawa wahudumu wa mahoteli, wahudumu wa baa mbalimbali, hivi inawezekana vipi mtu akaishi kwa mshahara wa shilingi 7,000/= Sasa vijana wengi waliozungumza hapa sikuona kama wamewazungumzia vijana kama hawa ambao wanateseka sana. Kijana anaajiriwa baa mshahara wake ni shilingi 7,000/= halafu anaambiwa utajazia kwa namna unavyoona inafaa, haya mambo yapo katika nchi yetu na hawa watu ni watu ambao wana leseni, sheria za nchi zipo na kadhalika. Naomba sana mamlaka ambazo zinahusika na vijana pamoja na ajira ziangalie namna ya kulinda ajira za vijana hao ili waweze kufuzu, waweze kufanya kazi kwa sababu hizi kazi wengi wanaziacha tu, wenzao wananyanyasika basi wanaacha na katika kada hii wako wengi. Watumishi wa nyumbani, watumishi hawa wanaojajiri kama bodaboda na kadhalika. Mamlaka ziangalie namna ambavyo vijana kama hawa wanaweza wakasaidiwa ili shughuli zao ziweze kuwaletwa nafuu katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia pia suala la maadili kwa vijana. Wako wanaohimiza sana kurejeshwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa kama njia mojawapo ya kurejesha maadili na uzalendo kwa vijana. Kwa sababu tupo hapa watu wazima wengi niseme tu kwamba ninakubaliana kabisa na hoja ya kujenga uzalendo kwa wale watakaokwenda Jeshi la Kujenga Taifa lakini sikubaliani kwamba watakaokwenda Jeshi la Kujenga Taifa ndio watajengwa kimaadili. Ukienda Jeshi la Kujenga Taifa kama wewe ni mwizi utakuwa mwizi tu, kama wewe ni mhuni utakuwa mhuni tu. Kwa hiyo, ningehimiza Taifa liangalie namna ya kuhimiza maadili kwa vijana. Vijana wengi sasa hivi hasa wa mijini wanahimizwa kwenda shuleni, shuleni hawafiki wanaenda kwenye ma-internet na kwenye internet kule hawafanyi shughuli inayohusiana na masomo yao, lakini wanafanya shughuli ya kutafuta mambo ya ajabu ajabu tu. Kwa hiyo, nafikiria wakati vijana wanataka watendewe haki na Taifa, lakini wao pia watimize wajibu wao wa kujitahidi kujijenga kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina rafiki yangu ana hoteli pale Dar es Salaam, ni raia wa Kenya. Siku moja nilimuuliza kwa nini Wakenya wengi zaidi wako kwenye hoteli yako? Jibu alilionipa ni kwamba vijana

wa Kitzanzania ni wavivu, hawataki kufanya kazi na ukiwajiri wanazungukazunguka tu, sababu ni nyingi mara vifo, mara hivi na kadhalika. Kwa hiyo, vilevile vijana tuwahimize au tuhimizane wajijenge katika maadili kwa sababu kama ni kushindana na vijana wenzao wa Afrika, yako mambo mengi ambayo yanaangaliwa sio elimu peke yake. Anaweza kuwa na elimu, lakini akawa mvivu na asiajirike. Anaweza akawa na elimu nzuri, lakini mdokozi asiajirike. Kwa hiyo, wakati tunahimiza vijana kupata nafasi lakini vilevile nawausia vijana wajianganalie, je, maadili yao pamoja na elimu zao yanaweza yakawasaidia wakashindana vizuri katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yameshasemwa na kwa kuwa unahitaji muda wa kutosha naomba niishie hapa, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Kwa kweli nimepata *concern* ya upande huu huku, upande wa CUF. Naomba uniwe radhi, nitumie mamlaka niliyonayo ya kukalia Kiti hiki nimwombe sana Mheshimiwa Mnyaa hata kwa dakika tano.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa busara ulizotumia, nilikuwa nimeshasononeka na upande wangu wote wa CUF kuona Wabunge wengi upande wa CCM, upande wa CHADEMA wamechangia na sisi tumeomba kwa nguvu zetu zote lakini hatukupata nafasi. Kwa hivyo, busara uliyotumia hivi sasa nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba kitu cha kwanza Serikali inapoleta Mikataba au Maazimio yote ya kuridhia isitufanyie kinyemela kwamba mkataba wenyewe tunautambua siku hiyohiyo, unaletwa mkataba una kurasa nyingi na vipengele vingi, si rahisi wakati mwingine kwa mikataba mingine Mbunge aweze kupitia na kufahamu kila kitu kwa siku hiyohiyo moja. Mpaka hivi sasa ilikuwa ni utaratibu wa Serikali kwamba inaleta Maazimio, Mkataba wenyewe unaohusika Wabunge tunaupata siku hiyohiyo. Mkataba huu unajulikana toka mwaka 2006 na Serikali imekuwa ikitambua na kushiriki, leo mwaka 2012, miaka sita tunaletewa hapa hapa kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia Mkataba huu wa Vijana wa Afrika, ukiangalia maudhui yake kiujumla ni mazuri mno na hayapingiki lakini utakapokwenda kwa undani kabisa utagundua kwamba kuna Ibara ambazo hazifai kabisa kwa sababu ya mila, utamaduni wa Mwafrika au wa Tanzania na dini zao. Sasa leo tunapoambiwa na vijana wanapokuja juu wakawa wanataka kukubali harakaharaka na wakati Serikali yenyewe imeshaona kuna Ibara ya 12 na 13(4)(h) Serikali yenyewe imekataa, lakini pamoja na vipengele hivi viwili lakini ukiangalia humu kuna Ibara ya 6, 7, 8, 9, kuna vipengele ambavyo havikubaliki kwa utamaduni wa Mwafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, ukichukulia Ibara ya 7 kuhusu ulinzi wa maisha ya mtu binafsi, hakuna kijana atakayeingiliwa katika mambo yake binafsi, makazi au mawasiliano yake kwa kiholela au kinyume cha sheria au kuvunjiwa heshima au hadhi yake. Ukikitizama kwa undani kipengele hiki kinatupelekea kufuata mila za Wazungu maana yake nini? Tunataka haki ya huyu kijana, leo tukikaa kwenye ukumbi na mke wangu, binti yangu wa miaka 15 ananijia na kimini na huku juu amevaa wanachokiita mvuto halafu anakuja na *boyfriend* wake wanakaa kwenye *seat*, anasema *daddy this is my boyfriend*, katika mila zetu za Kiafrika haikubaliki na hapo kwa kipengele hiki ina maana wewe mzee huna la kumfanya. Ukimgusa kumkataza kipengele hiki kinakukataza, nchi inajifunga. Leo mnataka kutufikisha huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingine kuhusiana na kumiliki mali sawa. Hakuna anayekatazwa mwanamke au mwanamume kumiliki mali lakini inapokuja kwa mfano mzazi amefariki, kuna mali, unataka mwanamke na mwanamume wamiliki sawa, hiyo ni kinyume na kanuni ya dini ya Kiislamu. Leo tukisema tunapitisha hii ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo mengine tusivamie, tunapelekwa mahali ambapo siko. Kwa mujibu wa Mkataba huu ndio tutafikishwa mahali ambapo unamchapa mtoto wako mchanga au mdogo wa miaka mitano (5) au sita (6) kwa utovu wa nidhamu anapiga simu Polisi mzazi unakuja kuchukuliwa kwamba umemuonea mtoto, huko ndiko mnakotaka kutufikisha? Mkataba huu tukiuridhia, tukiukubali huko ndiko tunakoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ninachozungumza ni kwamba maudhui ya Mkataba huu wa Vijana wa Afrika utakuta mambo mengi yanayozungumzwa ni mazuri lakini ukienda kwa undani wake ndio inatupelekea pabaya na ndiyo hayo mambo ya David Cameroon yatakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali izingatie vipengele vyote hivi nilivyovizungumzia kama walivyovitoa hivi vipengele viwili basi na vipengele hivi vingine vitolewe, tusiweze kukubali kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru, ahsante angalau kwa kutufikiria na sisi upande wa CUF. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana kwamba sikukosea kutoa nafasi hii niliyoitoa mwishoni. Hata hivyo, muda wetu unatuacha sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwatakieni kheri ya mwaka mpya 2012. Niwatakie kheri na fanaka katika yote Mwenyezi Mungu atakayowajaalia vijana na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vijana hapa nchini limekuwa la kuangaliwa kimtaji na si kwa jinsi ya kuwasaidia. Vijana wengi wapo vijijini na wakati walihidiwa ajira, vijana wamemaliza vyo lakini ajira hakuna na matokeo yake wastaafu wanaomba mikataba ya kazi ili kuendelea kujaza nafasi hizo. Sasa vijana hawa watakata nafasi ya ajira lini na wapi? Leo hii katika maeneo mengi hakuna Vyu vya Ufundi, hakuna Vyu vya Maendeleo ya Jamii, hakuna msaada wowote kwa wale walio nje ya mfumo rasmi wa elimu. Vijana leo hii hawana kimbilio lolote kwa maana hawawezi kukopesheka na wala hawana mali ya kuweka rehani. Hii ndiyo inapelekea vijana wengi kujikita katika kundi la ulevi, kucheza karata asubuni na pool table, vijana hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naiomba Serikali sasa kufufua Vyu vya Ufundi ili kuwapatia vijana wengi taaluma na wajenge tabia ya kujijiri wenyewe. Leo hii tumetengeneza mfumo wa kutegemea kuajiriwa kuliko kujijiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarisha sekta isiyo rasmi kwa maana ya kuwahamasisha kujiunga katika vikundi ili wapatiwe elimu ya ujasiriamali na hatimaye waweze kujijiri wenyewe.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kuungana na wenzangu mwaka huu 2012 na wale wenzetu ambao wametutangulia, tunawaomba kwa Mungu aweke mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni muhimu kwa vijana ambao kwa sasa hawana mwelekeo hasa wanapokutana na changamoto nyingi ikiwemo ajira, nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunataka kuingia kwenye mchakato huu wa Katiba, basi ipo haja kubwa ya kuangalia vijana bila ubaguzi wala itikadi za kisiasa kama ilivyo sasa. Hivyo ni vizuri kufanya mikataba ya kitaifa kama huu leo kuanza utekelezaji wa Serikali pale inaposaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya kuboresha na kuwashirikisha vijana. Kimsingi wengi wao wanaishi vijijini na hawajui jinsi ya kujikwamua. Ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara ambayo imekuwa ikitokea sehemu nyingi hapa nchini, kuna hana Serikali kuliangalia vyema suala hili na kulipitia upya ili kujali vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Vijana iliyopita mwaka 2007 ina tofauti sana na masharti ya mkataba huu ambao unaridhiwa na Bunge hili Tukufu. Hivyo Sera ya Maendeleo ya Vijana ni muhimu sana kwani hata Serikali inapopitisha Azimio hili ili kuwalinda na wawe huru lakini tukiangalia iwapo sisi kwa sisi

tunawanyanyasa vijana kwa njia mbalimbali kwa kuwatenga katika makundi, kweli Mheshimiwa Waziri hata kama tunaunda Sheria hii ya kuwalinda vijana basi yahitaji kuangaliwa kuanzia ngazi zote, kuanzia wale maskini/wenye unafuu/wenye uwezo. Vijana wananyanyaswa na Serikali kwa maana ya Jeshi la Polisi/Magereza na kuzalilishwa bila huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri apitie maeneo mbalimbali kuanzia shuleni/vyuoni/ajira isiyo rasmi kama vile vijana wa kike na wa kiume kuwekwa kwenye madanguro /majumbani, hivyo ifike wakati liwepo Baraza la Vijana ili waweze kupata sehemu ya kutatulia matatizo yao.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Mheshimiwa Waziri mwaka mpya wenye kheri na fanaka pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Wizara yote. Nawapongeza kwa kazi nzuri, umahiri na *commitment* kwa masuala ya vijana ni wa kutukuka na unafahamika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu nyingi sana kwa kuletwa Azimio hili. Ni jambo jema kwetu sisi Tanzania ambapo 60% ya wananchi wake ni vijana, litatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio limeazimia masuala mengi muhimu na nyeti ambayo kimsingi ni dhahiri kwa sababu mengi hayajatekelezeka, ni vema tukajipanga upya na kuona uwezekano wa kutekeleza mambo muhimu kama katika *Afrika Chapter 4(l)*, (pg9) siyo rahisi sana kwani tayari tuna utaratibu ambao bado unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 4(a) na 4(b), hakuna *free education Tanzania*, kwani michango na gharama zinazohitajika zinazidi hata ada inayotozwa kwenye baadhi ya shule za binafsi. Aidha, matatizo ya ukosefu wa Walimu, vitendea kazi navyo vinabidi kuangaliwa endapo tupo *serious* kupitisha Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 4(h) ambayo kwenye hotuba yake pia amesisitiza kuwa haliendani na sera zetu, je, tunaposema tumepitisha Azimio hilo, nalo lipo kwenye *Youth Charter* itakuwaje? Kwa nini Watanzania waliohudhuria mkutano wa Afrika walishindwa kutetea suala hilo lisiingizwe? Ukisoma kwa undani utaona wanasema *Young Women*, yaweza kuwa *education* inayosemwa ikawa ni ya Chuo Kikuu, basi huwezi kuzuia kundi hili kwani hata walioolewa wanaweza kuwa masomoni, hivyo, ni vema kuainisha nini tunasema. Nashauri twende nalo baadaye tutatunga sheria na miongozo ya kulisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa vijijini nao ni ukweli usiofichika kuwa ni kama hawafikiriwi popote. Japo Azimio hili linazungumzia vijana wa vijijini ni vema kuwe na mwongozo wa wazi na usio wa jumla na wa mijini, kwani mazingira, kipato, fursa ni tofauti sana, ukiweka ushindani wowote kwa vijana, ni dhahiri wa vijijini watakuwa wanashindwa. Nasisitiza yale yote yanayohusu vijana wa vijijini, yaelekezwe kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 14(2)(a-d) kwa haraka mtu anaweza kudhani kuwa inahitaji miujiza kurudisha vijana hawa vijijini, si kweli, kwani unapomwambia kijana aliye mjini arudi akashughulike na kilimo, anawaza jembe la mkono na kadhalika. Kumbwe tukajipanga, tukafanya *mechanized farming* kwa maana ya kupeleka matrekta na pembejeo nyingi husika, maeneo ndiyo yanaisha kama mnavyosikia, wenye nacho wanachukua ekari kwa maekari, tujipange mapema tuchukue maeneo na kuyawekeka mazingira ambayo yatavutia vijana kurudi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Article 17*, ulinzi na usalama. Ni kweli vijijini kwenye kata zote nchi nzima, Serikali imeanzisha mafunzo ya mgambo, cha kushangaza baada ya mafunzo hawatumiki tena, wamebaki kuwa majambazi kwani wanajua kutumia silaha. Kama tuko *serious* katika hilo tuwasiliane na Polisi na Jeshi kuona tutawatumiaje kama ambavyo imeazimiwa katika mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nisisitize uwezeshaji wa ajira. Kwa taarifa, ni hivi punde nakusudia kuanzisha *Empowerment Agency for Youth*. Nitaomba Waziri aje kuzindua na nitaomba ushirikiano wa Wizara. Nawapongeza.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa hotuba ya mkataba wa vijana. Napenda kutoa mchango wangu kwenye eneo la ajira kwa vijana. Ajira ni tatizo la kidunia, kwa sasa nashauri Serikali kutafakari kuanzisha Chuo Kikuu cha Michezo ambacho kitafundisha vijana wengi zaidi na kujajiri katika sekta hii tajiri duniani. Michezo aina ya Mpira wa Miguu, Pete, *Basketball*, Riadha na kadhalika.

Tazama Mataifa ya Afrika Magharibi na Kati yanatoa ajira kubwa kwa vijana kupitia michezo na pesa nyingi zinarudi katika nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya Watanzania vijana hawana ujuzi wa kutosha katika sekta za kitaaluma. Nashauri wahitimu wa *SUA* wakopeshwe matrekta na mitaji ili wakawekeze katika kilimo na wao watatoa ajira kubwa kwa vijana wengi walioko vijijini. Ahsante.

MHE. THUWAIBA IDRISA MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wananchi ni vijana, ambapo wengi wao hawana wala hawajui mwelekeo wao ni upi. Hii inatokana na tamaduni na mila zilizokuwepo au iliyojiwekea nchi. Ni vyema sasa nchi iweze kubadilika kwa njia moja au nyingine lakini wakati huohuo kuangalia maadili ya dini yanazungumzaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Ndoa, Azimio linazungumza kijana awe na uhuru wa kuchagua mume au mke anayemtaka lakini, je, hata ikiwa mke/mume ni tofauti kidini? Ikiwa Azimio linazungumza hivyo na vijana wakapewa upenyo huo basi Taifa tutakalokuwa nalo kwa miaka 25 – 50 ijayo ni matatizo matupu na tutakuwa tumewajengea maisha mabaya, ni vyema Serikali kukaa na kufikiri vyema kwamba siyo kila Azimio likubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mirathi, Sheria hii ni vyema ikaangaliwa vizuri sana kwani ni moyo katika maisha ya binadamu. Kwa upande wa dini ya Kiislam kuna Sheria ya Urithi inayosema $\frac{2}{3}$ kwa wanaume na $\frac{1}{3}$ kwa wanawake na hii ina maana yake ukifanya vinginevyo huwa umekwenda kinyume na mirathi ya kidini ya Kiislamu. Sheria ya Mirathi ni vyema ikakaa kama ilivyo kwa wale Waislam na kwa wengine mtafanya inavyokuwa.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu bado inaenzi tamaduni, silka na kuheshimu dini ya kila mtu, ni jambo la kusikitisha kuona mkataba huu umetoa fursa nyingi bila kuangalia kwa undani hali halisi ya nchi yetu. Nashauri Serikali kuangalia upya Azimio hili katika misingi hiyo ya kuruhusu mjadala mpana zaidi ambao utahusisha kada tofauti na rika tofauti ili kutanua wigo wa kuuchambua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 1(2), inatakiwa nchi kuchukua hatua za lazima kimchakato wa Kikatiba kukubali Azimio hili. Hii ni changamoto kubwa kwa nchi yetu na ni lazima iwapo tutaridhia mkataba huu iwe tayari kama nchi tumeshajipanga, tuwe tumeshakuwa na tathmini ya uhalisia na majibu ya kweli juu ya matatizo yanayowakumba vijana wa Taifa hili kama vile masuala mazima ya ajira, afya na elimu. Vilevile kama nchi kuelewa thamani ya kijana, mipaka yake na haki zake na uhuru wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi siungi mkono Bunge letu kuridhia Azimio hili kwa sababu zifuatazo:-

1. Kucheleweshwa kuletwa Bungeni na kutunyima fursa wajumbe kuweza kupata muda muafaka wa kulitafakari;
2. Kwa kuwa Waziri husika ameshindwa kuonesha ni kwa namna gani Serikali imejipanga kukabiliana na utekelezaji;
3. Uhuru uliopevuka wakimagharibi umetawala mkataba huu; na
4. Kwa kuwa vijana ndio nguvu kazi ya kila Taifa, ni wazi tutawaondolea baadhi ya haki zao za malezi ya kimila na kidini kwa kutoa uhuru mpana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuandaa mjadala wa Kitaifa utakaohusisha kada zote kuupitia upya mkataba huu.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hoja hii, napendekeza yafuatayo:-

1. Vijana wapewe fursa ya kushiriki katika mchakato wa kujenga demokrasia ya nchi. Serikali ifanye marekebisho ya Kisheria na Kikatiba ili kijana mwenye umri wa miaka 15 – 18 apewe nafasi ya kupiga kura.
2. Katiba ifanyiwe marekebisho ili umri wa kugombea Urais, badala ya kuwa miaka 40, ushushwe ili vijana walio na miaka 15 na zaidi waweze kugombea Urais.
3. Kurudishwe mfumo wa uwajibikaji na nidhamu katika kazi kwa kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa ili kuandaa vijana katika Utumishi wa Taifa.
4. Zifanywe jitihada za dhati za kufufua viwanda ili kuwapatia vijana ajira.
5. Watoto wa shule za msingi na sekondari wanaopata mimba wakiwa shuleni wasiruhusiwe kurudi shuleni na kuchanganyika na wengine. Watafutiwe mfumo wa shule zao.
6. Wazee wa miaka 60 wasiongezewe muda wa kuendelea na kazi, nafasi hizo wapewe vijana.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia kama ifuatavyo. Ibara ya 4, sehemu ya pili, kijana atakuwa na uhuru wa kusambaza na kutafuta taarifa. Napenda kugusia katika masuala ya mitandao ya kijamii hususan *Facebook, Jamii Forum, Twitter, You Tube* na kadhalika, vijana wangejikita zaidi katika masuala ya maadili kuliko masuala yanayopotosha jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 2, sehemu ya pili, tungependu Serikali iondoe kipengele cha vijana wenye uzoefu kupewa kipaumbele katika masuala mazima ya kuomba kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 8, sehemu ya pili, inaridhia makubaliano ya mke na mume, vijana kwa hiari yao tu inatoshwa kuwafanya wafunge ndoa. Hii inatoa mwanya kwa vijana kujiamulia mambo yao wenyewe bila kufuata ushauri wa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana katika Ibara ya 16 wanatakiwa wawe watetezi wakubwa dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, kwa nini, kwani hakuna mateja watu wazima au wazee? Hatua za makusudi zichukuliwe kutunga sheria kali dhidi ya watumiaji wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 26 inazungumzia majukumu ya vijana, (a) *Youth shall have the duty to become the custodian of their own development*. Katika eneo hili ni lazima vijana wengi waajiriwe katika Wilaya na Halmashauri mbalimbali kama Maafisa vijana ili waweze kuwashauri vijana wenzao dhidi ya hatua muhimu za kuchukua ili waweze kujijajiri kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maeneo machache ningependa yazingatiwe.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa Azimio hili la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kuwa vijana ni kada muhimu sana kwa Taifa letu bali iliachwa bila kuandaliwa ili waweze kujitegemea na kutoa mchango wake kwa Taifa na kuwa na mfumo na tabia ya kuigwa kwa jamii inayowazunguka Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3, inahusu vijana kwenda kokote ilimradi wasivunje Sheria. Ni kweli vijana wana uhuru wa kwenda kokote ilimradi wasivunje sheria. Suala hili liko wazi bali vijana wetu uhuru huo wanautumia vibaya kwani wengi wao huharibika kitabia mfano kutumia madawa ya kulevya,

kuvaa mavazi ya kudhalilisha utu wao, kutumia lugha chafu na kutokuwaheshimu viongozi na watu waliowazidi umri hata wao kwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4, inayohusu uhuru wa kutoa mawazo yao, nami ninaridhia kabisa vijana kuwa huru katika kutoa mawazo yao bila kuvunja sheria za nchi zao. Hivyo basi ninaunga mkono ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuwa suala la kutunza maadili na utu wao wenyewe ni muhimu sana kwani uhuru bila mipaka ya kisheria basi sio uhuru tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5, kushirikiana na wengine na Ibara ya 6, uhuru wa kutoa maoni na kuamini dini aitakayo, ninaunga mkono Serikali kwa kuona vijana wanayo haki ya kushirikiana na wengine, uhuru wa kutoa maoni na kuamini dini aitakayo. Bali nisisitize Azimio liwe na vipengele vya kuwadhibiti vijana uhuru usitumike vibaya mfano vijana wa kiume kufanya mapenzi wao kwa wao au vijana wa kike kufanya mapenzi wao kwa wao. Kwani kufanya hivyo ni laana ambayo ni aibu kwa Taifa na haisameheki kwa Mungu. Vilevile kufundishana vitendo viovu mfano wizi, kutumia lugha chafu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana kupata elimu, ni kweli Serikali inatoa elimu kwa vijana bali elimu inayotolewa bado inawanyima haki vijana wengine mfano vijana waliotaka familia maskini, vijana wa kike wanaopata mimba bado Serikali haijaweka utaratibu wa kuwapa haki yao ya kupata elimu wakati aliyempa mimba anaendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kumiliki mali, bado vijana hawajathaminiwa na kupewa kipaumbele cha kumiliki mali hata kuaminiwa kushika nyadhifa kubwa. Ushahidi ni Maafisa wanapostaafu wanapewa ajira tena ya mkataba wakati vijana wengi wapo mtaani bila ajira. Napendekeza vijana wote wanapomaliza elimu ya juu au diploma Serikali ihakikishe inawapa ajira sio wao kuanza kutafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono Azimio hili nikiamini Serikali itazingatia mchango ya Wabunge.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Kama tujuavyo, vijana ni Taifa la leo na ndiyo nguzo kubwa katika ujenzi wa Taifa na nguvu kazi inayoweza kuongeza pato la Taifa na kukomesha umaskini uliokithiri. Ili kuweza kusaidia vijana hawa, lazima Taifa/Serikali izingatie baadhi ya mambo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi ni wasomi wazuri, wana ujuzi mwingi lakini ikija kwenye ajira, vijana wengi wanaulizwa au unakuta tangazo la kazi linasema lazima wawe na uzoefu usiozidi miaka mitano hadi saba. Hii hatuwatendei haki vijana hawa. Watapata wapi *experience* bila kuanza kazi? Ndiyo maana unakuta vijana wengi wanaishia kufanya umachinga wakati Serikali haiwaruhusu kufanya biashara hiyo, wananyanyaswa, wanafukuzwa ovyo, wanapigwa mpaka wengine kuuawa. Ni hatari kwa Taifa hili! Wakinyimwa hata kufanya biashara na ajira mpaka wawe na uzoefu, tunategemea kupata vijana wa aina gani wasiokuwa na ajira? Siku ya mwisho wataishia kuwa vibaka, hata majambazi au kutumiwa kufanya biashara za madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzoefu, kuna kazi za kiutawala mfano Mkurugenzi wa Halmashauri kuna haja ya kuongeza Mkataba kwa Mkurugenzi wakati kuna vijana wengi tu wapo mitaani waliomaliza vyo wenye kuweza kufanya kazi hiyo? Serikali ilifuatilie hilo. Je, ni kwa jinsi gani Serikali inaweza kuwasaidia vijana hasa wa vijijini zaidi ya asilimia 80 kuweza kujajiri. Je, wanaweza kupatiwa mikopo ya riba nafuu kama wapewavyo mikopo ya Elimu ya Juu pindi wanapoanza biashara hizo waanze kuzirudisha? Pia wapewe elimu ya ujasiliamali ili waweze kufanya biashara.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Azimio lililoko mbele yetu. Nami naungana na Wabunge wenzangu kwa kuchangia Azimio hili. Naaza kwa kusema, siyo vizuri msichana aliyebeba mimba kurudi shule na kusoma na wasichana ambao bado hawajabeba mimba. Kama tutawachanganya, hatutawatendea haki vijana/wasichana ambao hawajabeba mimba ni vizuri wasichana waliopoteza maadili kwa kubeba mimba waendeleo na masomo, lakini kwa shule ambazo zimetengwa tofauti na wasichana ambao hawajabeba mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kusema kuwa baadhi ya vijana sasa hivi wamekuwa wavivu wa kufikiri kupitia kwa watu ambao wanawadanganya. Hivyo basi, ni vizuri kuwaelimisha vijana waweze kujituma na siyo kukaa tu vijiwani na kutoa lawama tu kwa Serikali. Waelimishwe na ambao wanakubali kuelimika na kukubali kufanya kazi kwa heshima na nidhamu hawa wapewe kipaumbele na siyo wale ambao wanasubiri kutoa lawama bila kufanya kazi na kutoa lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kabisa kutoa kazi, mitaji na hata vyeo kwa vijana wenye maadili bila kujali ni mtoto wa nani, kabila gani, anatoka Chama gani. Cha muhimu tu awe Mtanzania. Pia kuna vijana ambao wamo katika viwanda vya watu binafsi, hali zao ni mbaya, malipo yao ni duni. Lakini hufanya kazi ngumu huko viwandani, kazi kubwa na ngumu, lakini mishahara ni duni sana. Hawa nao tuwaangalie kwani wanapoteza nguvu zao pasipo mafaniko ya kweli.

Vijana wetu wanatumika vibaya na wanatumika bila vifaa vya kuvaa wakati wa kazi ngumu na za hatari. Ni vizuri sana tuliangalie sana hili bila kujali kwamba hawa ni wawekezaji. Ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla mtalitazama hili kwa undani. Vijana wa Tanzania ni muhimu wawe na shughuli za kufanya, bila hilo Tanzania yetu kuna watu ambao wana nia tofauti ya kuwatumia vijana wetu.

MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuleta azimio hili.

Napenda kuunga mkono yote yaliyoainishwa katika Azimio. Hata hivyo, ningependa kushauri jambo moja linalohusu ajira ya vijana. Kwa kuwa kilimo ndicho chenye fursa nyingi ya kuajiri vijana wengi, ni muhimu tuwe na sera zenye uwezesaji na vivutio kwa vijana ili wakipende kilimo. Kwa hiyo, nashauri vijana wanaohitimu Vyu katika fani ya Kilimo waandaliwe mazingira ya kuwawezesha kupata ardhi na kuimiliki na kupewa mikopo ya kuendesha kilimo kama zana za kilimo, pembejeo za kilimo na kadhalika ili watumie elimu wanayopata katika uzalishaji. Sera hii inatekelezwa kwa mafaniko katika baadhi ya nchi kama Misri kwa mafaniko makubwa. Inawezekana hata katika sekta nyingine jambo hilo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta mkataba huu ili Bunge lipate kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki namba moja ya vijana katika Taifa lolote lile ni ile kupata elimu na ujuzi wa kazi vitakavyomwezesha kuelewa wajibu wake katika jamii na kujiajiri au kupata kazi. Tanzania tuko nyuma sana katika ajenda ya kuwapatia ujuzi vijana. Mikakati yetu mingi inalenga kutoa elimu ya darasani tu, yaani nadharia tu. Matokeo yake vijana hawa wakimaliza elimu hii ya nadharia wanabaki kurandaranda mitaani kwa sababu hawana ujuzi wa kazi katika fani yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kuiomba Serikali, kwanza, iturudishie utaratibu wa shule za zamani zenye michepuo ya ufundi, kilimo, biashara na kadhalika. Hii itasaidia hawa vijana kupata stadi za ujuzi na pindi wamalizapo wanakuwa na uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa na hivyo kupata haki ya msingi ya kupata kazi na kulijenga au kutumikia Taifa lake.

Pili, Serikali iharakishe kutekeleza mpango wake wa kujenga Vyu vya VETA katika kila Wilaya. Ifahamike kwamba vijana wanaomaliza Kidato cha Nne ni wengi sana na vijana hawa wanaingia kwenye soko la ajira bila ujuzi wowote ule, hivyo kuwa na nguvu za kazi ambayo haina *skills au competence* za kazi yoyote ile. Mafunzo katika vyu hivi yatawezesha vijana kupata *skills* za kazi na stadi mbalimbali. Hii pia itasaidia nchi kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi na hivyo kusaidia kutoa mchango wa kujenga nchi yao.

Tatu, kuhusu vijana wanaopata elimu katika Vyu vya Elimu ya Juu, Serikali iwe na mpango maalum wa kuwasomesha vijana katika maeneo ambayo yatalisaidia Taifa yaani vipaumbele vya uchumi vya nchi.

Mpango wa Taifa wa miaka mitano tulioupitisha hapa Bungeni unacainisha idadi ya wataalam katika kila fani za sayansi na teknolojia. Serikali ianze kuutekeleza mpango huu. Mpango huu ukitekelezwa

utawezesha vijana wanaomaliza elimu ya juu kupata ajira, kujijiri kwa urahisi kwani hizo fursa tayari zimeainishwa katika mpango huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Mkatoba huu upate kuridhiwa.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa naunga mkono Azimio la Kuridhia Mkatoba wa Kimataifa wa Afrika (*The African Youth Charter*). Iko haja ya kufanya kampeni ya makusudi kuzuia wimbi kubwa la vijana kukimbilia mjini badala ya kujiendeleza katika suala la kilimo. Kuna dhana ya kuwa vijana hawana kazi. Ni kweli, lakini kazi ambazo ni za uhakika ni kazi za kilimo, kwani vijana wengi wana haraka ya maisha na ndiyo maana hata tabia au utamaduni wetu umepotea kwa sababu vijana wengi wanaamini ya kuwa kuendelea ni lazima kuiga mila za kigeni na lazima nikiri kabisa ya kuwa hali ya sasa ya vijana wetu lazima wakubali kubadilika na kuheshimu mila na desturi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkatoba unaongelea juu ya tatizo la ajira. Mimi nashauri tuanzishe vikundi maalum vya vijana vijijini ili Serikali iweze kuwapatia mikopo ya matrekta au vifaa vyo vyote vya kuwasaidia katika kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, vijana lazima wafahamu kuwa wavumilivu na kuacha tamaa. Tamaa yoyote mwisho wake ni mbaya sana. Nashauri uletwe Muswada wa kuruhusu Wabunge kukaa Bungeni mihula miwili tu, yaani miaka kumi, na baada ya hapo, Mbunge asiruhusiwe kugombea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. MARGARET. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wizara yote kwa kuleta mkatoba huu.

Pili, bado kuna umuhimu wa kuangalia jinsi ya kuwapatia fursa vijana/wasichana ya kuendelea na masomo baada ya kupata mimba shuleni. Tunapoteza wasichana wengi ambao wangeweza kuchangia maendeleo kama wangepata fursa ya kuendelea na masomo.

Tatu, Vyuvo vya Ufundi viongezewe na vile vya ufundi vilivyopo viongezewe uwezo ili vijana wengi wapate ufundi wa kuwawezesha kujijiri na kuajiriwa na aina ya ufundi uongezwe kwa kuzingatia mahitaji ya maeneo walioko vijana.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni yangu kuhusu mkatoba wa vijana Afrika, Mkatoba ambao ni wa umuhimu mkubwa katika maendeleo ya maisha ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nielezee kipengele cha Ibara ya 21 inayohusu vijana wanaoishi nje ya Afrika (*Youth in the Diaspora*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wa Kitanzania wanaoishi katika nchi za nje, wengi wao wamekimbilia nchi za nje wakidhani hali yao ya maisha itakuwa na unafuu. Wengine wamedhani wataweza kusoma na kufanya kazi ili kujilipia ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake, vijana wetu ambao wameona hali ya maisha imekuwa ngumu nchini mwao na kuamua kukimbilia nchi za nje, wamejikuta wakiishi maisha magumu zaidi yanayofanana na utumwa kwa kufanya kazi zaidi ya moja ili kuweza kumudu maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ibuni nafasi mpya za ajira kwa kufufua viwanda vilivyokufa. Mfumo wa elimu uboreshwe na badala yake vijana wapatiwe elimu inayowaandaa vijana kiajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkatoba huu wa vijana Afrika, endapo utawekwa katika vitendo, vijana wengi ambao ndio Taifa la leo watakuwa wamefaidika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali yangu kwa uamuzi wa busara wa kuona umuhimu wa kuleta Azimio ambalo ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Azimio hili, mimi nitachangia katika maeneo yafuatayo: Elimu kwa vijana, ajira kwa vijana na nafasi za uongozi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa suala zima la elimu kwa vijana. Elimu ambayo inatolewa kwa vijana bado inahitajika kuboreshwa. Elimu ya vijana itolewe kwa vitendo zaidi kuliko nadharia. Elimu ya vitendo itawajengea maisha ya kujajiri zaidi. Elimu ya ujasilimali itawaanda vijana kwa maisha ya kujajiri badala ya kusubiri ajira za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana ni tatizo. Ajira kwa vijana ni kubwa sana na hasa pale ambapo ajira za Serikali zinawekewa masharti ya uzoefu wa miaka mitatu mpaka mitano. Sharti hili ni gumu sana na vijana linawapa taswira ya kuwa hawatakiwi katika Serikali ya nchi yao. Ni vyema sasa tukaliondoa sharti hilo kwa maslahi ya vijana wetu.

Nafasi za uongozi kwa vijana kwa kweli kuna haja ya kuwapa nafasi za uongozi na hasa katika Taasisi mbalimbali za umma kutokana na wepesi wa maamuzi walionao vijana. Kwa kweli Ofisi yangu inaongozwa na vijana na imekuwa na mabadiliko makubwa kiutendaji, lakini tuendeleo kuwafuatilia na kuwaongoza katika ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taathima kubwa naunga mkono Azimio kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kupongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili la Mkataba wa Vijana wa Afrika kwa kuridhiwa. Hata hivyo, ili Azimio hili liweze kuwa la manufaa, ni vyema sasa vijana wetu wakajitambua nafasi zao na wajibu na umuhimu wao katika jamii. Hivyo ni muhimu mkataba huu ukapatikana kwa urahisi ili vijana waweze kuusoma na kuelewa maana yake na vipi wanaweza kunufaika na mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya uzuri wa mkataba huu, bado kuna changamoto nyingi kwa Tanzania kuweza kunufaika na mkataba huu. Mfano, sasa hivi idadi ya vijana isiyo na ajira inazidi kuongezeka siku hadi siku. Lakini pia kuna vijana wengi tu ambao hawana elimu hata ile ya kuweza kujajiri.

Nikichukua mfano wa jimbo langu la Busega, mwaka jana vijana waliofanya mitihani wa Darasa la Saba ni kadri ya 7028 wakati waliochaguliwa kuingia Kidoto cha Kwanza ni 3,034 tu. Hii ni takribani asilimia 43 tu ya wahitimu wa Shule ya Msingi. Hebu fikiria zaidi ya vijana wa umri wa miaka 13 wanabaki hawana pakwenda, hilo ni jimbo moja tu. Sijui majimbo mengine hali ikoje. Jimbo lote hakuna Chuo cha Ufundi. Sasa tufanyeje? Hapa tunatengeneza bomu kubwa la miaka michache ijayo.

Hivyo, napenda kuishauri Serikali iwekeze katika Vyuvo vya Ufundi Stadi ili kuwapatia vijana uwezo wa kupata taaluma na pia kufundishwa ujasiriamali. Vijana hawa wakiunganishwa katika vikundi wawekewe pia mpango wa mikopo yenye masharti nafuu ili wakuze uchumi wao. Katika Mkataba huu, kuna fursa kwa vijana kwenda kwenye mataifa mbalimbali.

Hata hivyo, ili vijana na Tanzania waweze kutumia fursa hizo, lazima waandaliwe kupitia mitaala ya elimu ili kuwajenga kujiamini, Serikali iweke mpango maalum kwa kuwajenga vijana. Umuhimu wa vijana kwenda nje kuleta maarifa mapya nchini, kutafungua fursa kwa Watanzania nje lakini pia italeti rasilimali zaidi nchini na kuinua uchumi wao, familia zao na Taifa. Mfano, sasa fursa za walimu wa Kiswahili katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu pamoja na Sudan Kusini, vijana wetu wajengwe ushujaa kuchangamkia fursa hii. Hili litawezekana tu iwapo elimu ya ujasiriamali itakuwa sehemu ya mitaala kuanzia msingi hadi vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia Azimio hili la Mkataba wa Vijana wa Afrika. Naunga mkono Mkataba huu kwa asilimia mia moja.

Napenda nianze kuzungumzia suala zima la ajira kwa vijana wa Tanzania na Afrika kwa jumla. Hivyo basi, naendelea kuiomba Serikali kuwapatia mkataba huu uweze kuangalia suala hili kwa macho mawili. Vijana wa Kitanzania wengi wanalia kwa kukosa ajira. Wapo vijana wengi wasomi wanahangaika Mitaani kwa kukosa ajira. Ninaomba Serikali yetu iangalie upya muda wa kustaafu, kwa sababu zamani ilikuwa ni miaka 45 umri wa kustaafu kwa hiari, na miaka 50 kustaafu kwa lazima. Baadaye ikaenda miaka 60 mpaka 65, lakini bado mtu akistaafu anaongezewa mkataba. Je, kijana huyu wa Kitanzania atapata nafasi hii lini ya kuweza kujijiri?

Ninaomba Serikali kuwapatia mkataba huu iweze kuboresha hali ya maisha ya vijana vijijini, sababu asilimia kubwa ya Tanzania ni vijijini na huko kuna vijana wengi ambao kwa hali mbaya iliyo vijijini vijana wengi wanakimbilia mijini. Tuboreshe hali za maisha ya vijana wa vijijini ili kuweza kuwakwamua vijana hawa wa Kitanzania na hasa hili suala zima la Kilimo kwanza liguse vijana.

Napenda pia Serikali iangalie upya uzoefu wa kazi katika ajira, uzoefu unaohitajika katika kazi nyingi, chuoni atapata wapi uzoefu wa miaka 10 mpaka 15?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ipitie upya mtaala na kubuni vitu ambavyo vitampelekea kijana huyu wa Kitanzania amalizapo elimu yake awe na uwezo na dhana ya kujijiri *rather than* kujijiri. Hii pia itakuwa njia mojawapo ya kutatua tatizo la ajira.

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami nichangie hoja hii muhimu kwa Taifa letu.

Mkataba huu ni wa muhimu sana, kwani vijana ndiyo Taifa la sasa, wanakabiliwa na changamoto nyingi.

Mkataba huu utaleta mantiki zaidi endapo basi itatungwa sheria mahsusi kuhusiana na vijana. Aidha, ni vyema Serikali ikazingatia masuala ya nafasi ya vijana katika kushiriki katika uchumi, haki ya kumiliki mali na ardhi, haki ya kupata elimu kwa kuwapatia elimu ili vijana hawa wafahamu haki zao za msingi.

Ni vyema pia sera ya vijana ya Taifa ya mwaka 2007 ikaangaliwa upya ili ihuishwe kuendana na matakwa ya mkataba huu.

Bila ya kuyafanya niliyoeleza hapo juu, tutawafanya vijana wetu wasifaidi ujana wao, hususan wakati wao (*generation*) yao itarukwa.

Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Baada ya kuunga mkono hoja, naguswa na hali iliyojitokeza kwa vijana kutoshiki shughuli za maendeleo na hasa shughuli za kilimo na badala yake unakuta shughuli hizi zinafaywa na wazee na vijana kushinda vijiwani huku wakilalamikia hali ngumu ya maisha. Hali ngumu ya maisha haiondoki kwa kushinda vijiwani na kupiga kelele, ila ni katika kushiriki shughuli za kujibidisha kwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa, napata mashaka juu ya Taifa tunalolijenga, Taifa la watu wanaolalamikia hali ngumu ya maisha bila ya kufanya jitihada ya kuondokana na hali ngumu hii. Napata taabu juu ya Taifa baada ya wazee wa rika la umri wa watu wa kati kuaga dunia, hali itakuwaje? Hivi ile mikakati tuliyokuwanayo kama nguv ukazi imeishia wapi?

Hii tabia ya kutopenda kufanya kazi na hasa kazi za kilimo imetoka wapi, na hasa siasa zinazopandikizwa kwamba Serikali ina pesa nyingi na inaweza kupiga huku ikigawa raslimali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti ambao nimeufanya, napata taabu juu ya kukosekana na namna bora ya urithishaji na mwendelezo wa mali katika familia zetu za kitanzania na ukijiuliza ni nini kinachosababisha familia iliyokuwa ikijiweza kiuchumi mara baada ya kufa kwa waanzilishi kwa maana ya Baba na Mama, watoto wamekuwa kwenye lindi la umaskini? Yaani baada ya muda si mrefu, kama vile wazazi wao hawakuwaachia kitu!

Hapa kama Taifa lazima tufanye maamuzi yatakayonusuru Taifa.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba naunga mkono azimio hili asilimia mia moja, ila napenda kutoa maelezo yangu kwamba vijana ni nyenzo muhimu sana pale ambapo itatumika vizuri. Vijana wanaweza wakawa ni sumu katika jamii pale ambapo wataachwa bila kupewa ajira au njia yoyote ya kuwatafutia namna ya kujiajiri wenyewe.

Vijana wengi wanapokosa ajira, basi hukimbilia mijini, katika miji na kuna vijana wengi ambao wanazurura tu. Serikali inapaswa iangalie vyema sana pale ambapo vijana wanapojijiri wenyewe kwa mfano Wamachinga.

Wamachinga wanabughudhiwa sana na Askari wa Jiji. Hawa vijana nashauri sana kwamba Serikali iwaangalie, tena kwenye sehemu ambayo ina biashara na siyo kandokando ya Miji ili waridhike nao waweze kufaidika na nchi yao. Bila hivyo, hawa vijana wanaweza wakajishirikisha na makundi ya kihuni na wakaleta hasara katika nchi yetu.

Pia nashauri Serikali kwamba watoto wa kike wanapopata mimba wasitengwe na waachwe waendeleo na masomo yao.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mlitazame sana hili la kurudisha mtoto shule aliyepata mtoto mwenzake, mkiruhusu jambo hili yatakuwa mateso kwa sisi wazazi na hao watoto wetu nao wanaweza kuwapoteza watoto wao kwa asilimia kubwa kwa sababu ya matunzo hafifu tutakayotoa sisi wazazi kwa watoto hao na vifo hivyo vingi vitasababishwa na sisi wazazi kuwa na majukumu mengi yanayotuzidi uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiruhusu jambo ijue itakuwa imehalalisha uzinzi. Kama Serikali itaamua kufanya hivyo basi ijidhatiti kujenga mabweni mengi shuleni, wazazi hao wakae na watoto wao na Serikali ibebe msalaba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu alimpa Adam na Hawa bustani ya Edeni ili wailime na kuitunza, hawakupewa biashara. Serikali iwawezeshe vijana kuwapa msaada wataalamu wawafundishe jinsi ya kujitegemea, wapewe mashamba, wayalime na kuyatunza na Serikali iwasaidie kweli kweli kwa wale watakaonekana wameweka malengo yao kiutadam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Rais yeyote atakayeweza kutoa ajira za ofisini kwa vijana wote wasomi usiku na mchana hata katika nchi zilizoendelea haziwezi lazima wengine wajijiri. Pia Serikali iweke utaratibu wa nyuma wa miaka ya 1980 - 1981 kuanzisha vijiji vipya vya watu wanaokaa mjini bila ajira kama Baba wa Taifa alivyofanya kuanzisha vijiji vya Simbo na maeneo mengine mkoani Kigoma ili wale wanaokaa wana zuba mjini wakaishi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii nami kuchangia hoja hii kwa kuunga mkono Azimio hili kwa nguvu zangu zote. Ila ningependa kutahadharisha baadhi ya mambo yaliyomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sana suala la kuwaruhusu vijana wetu wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shuleni kuendelea na masomo mara baada ya kujifungua. Hili ni kosa kubwa kwani tunataka kuwajengea vijana wetu mazingira ya kuwapa uhuru usio na mipaka. Hofu yangu ni kwamba vijana hawa badala ya kusoma, watashughulika zaidi na mapenzi wakiamini kwamba baadaye watarudi

shuleni. Hapa ndiyo tunaliangamiza Taifa letu. Ni lazima tufikirie zaidi kwenye maadili yetu na pia sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za vijana ni jambo ambalo limetajwa kwenye mkataba huu. Bado nchi yetu tuna tatizo kubwa la ajira na sababu kubwa ni kwamba vijana wetu hatujawaandalia mazingira mazuri ya kujijiri wenyewe (ajira binafsi). Naiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuongeza vyo vya ufundi na kuhakikisha kijana anayetoka chuoni anawezeshwa ili aende akajijiri kwa kupewa zana. Hapo tutakuwa tumewatendea haki vijana wetu wa kike na wa kiume.

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya Tanzania imuwezeshe kijana kujijiri, ili tuweze kulikwepa mbali bomu kali litakaloweza kulitekeleza vibaya sana Taifa la Tanzania endapo Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itachelewesha kubadilisha syllabus zitakazotoa fursa za ajira ziwe za kuajiriwa na pia kujijiri, ni vyema tuweke wazi vipaumbele vyetu vya maendeleo ya M Tanzania na Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili, ni muhimu kuwa na malengo ya Kitaifa katika nyanja tofauti tukijua kwamba usemi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere aliposema; "Ili tuendeleo tunahitaji mambo manne:- watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora." Tujitizame na kujitathmini kwenye maeneo hayo na tujiulize tumejikwaa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maadili na malezi bora; tutajidanganya sana endapo tutasema eti ya kale leo hayana nafasi tena. Hili ni dhahiri limeturudisha nyuma kwa kiasi kikubwa. Nidhamu, heshima na adabu za mila na tamaduni zetu tumezipoteza. Hatuna budi kurudi tulikotoka kwa usemi kwamba isiyu kongwe haivuushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango mkakati wa Serikali, ni lazima Serikali ijenge mkakati wa makusudi ili tuweze kuitumia vyema rasilimali vijana tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkataba wa vijana wa Afrika, napenda kuchangia katika eneo la kuwapa uhuru vijana kuingia katika ndoa kwa kuzingatia sheria ya ndoa ya mwaka 1971 pamoja na sheria zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inamruhusu kijana kuanzia miaka 15 kuingia katika ndoa. Kijana wa miaka 15 bado katika nchi yetu anahesabika kama mtoto. Kumruhusu kuingia kwenye ndoa ni sawa na kumingiza mapema katika masuala ya mapenzi na hivyo kuweza kumsababisha ajikute akijitumbukiza katika maradhi kama vile UKIMWI na hivyo kusababisha kundi kubwa la vijana kuwa katika janga hilo na hivyo kupoteza nguvu kazi ya kutosha na hatimaye kusababisha uchumi wa nchi kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukumbuke kauli mbiu mbalimbali zinazowalinda watoto, kwa mfano; mtoto kuzaa mtoto. Hili ni hatari kwa Taifa kwani inaweza kusababisha Taifa kuwa la watoto wengi zaidi. Hivyo basi, nashauri na pia ninaiomba Serikali iweze kuangalia upya sheria hizo ili kuondoa mtafaruku katika kuzielewa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhia azimio hili.

MHE. FAKI HAJI MAKAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mungu kwa kutujalia amani. Aidha, nikushukuru wewe kwa kutoa nafasi kwa Wabunge kuchangia hata kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichangie Muswada wa Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika katika lugha ya mkataba wenyewe, ukurasa wa 5, Ibara ya 9 kuhusu mali. Ibara ya 9(3) neno "kiholela" liondoke kwa sababu watu wanaweza kunyang'anywa hata kama wamejitahidi kudhibiti haki zao. Kunyang'anywa kiholela ni pamoja na kuzembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata umri wa vijana unaotajwa katika mtakataba wa miaka 15 – 17 siyo mzuri kwa sababu baadhi ya nchi vijana wake wengi wamedhoofu kutokana na afya inayokosa chakula bora. Baadhi ya nchi zenye uchumi mzuri vijana wadogo wana umbo kubwa, hivyo wale wenye maumbo dhaifu watakuwa wadogo na umri mkubwa na wale wenye umri mkubwa na umbo dogo wanachanganyika na vijana halisi katika maisha ya kawaida. Ninapendekeza umri wa vijana uanzie miaka 15 – 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuridhia mkataba huu ni vyema tukazingatia malalamiko ya vijana katika nchi yetu kuhusu ajira. Vijana wengi wanapomaliza masomo yao wanatakiwa waombe ajira, lakini kikwazo ni uzoefu. Kwa kweli kama hujaajiriwa hupati uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na wanachama wa mkataba huu ni vyema zikaondoa kikwazo cha uzoefu kama sifa ya ajira. Tunapendekeza vizingatiwe vyeti tu, uzoefu utapatikana baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni katika nchi maridhiwa unatofautiana, leo mkataba huu unadai uhuru wa kuwaachia vijana watende watakavyo, maana ya neno uhuru hapa ni tatizo. Bila usimamizi, demokrasia ni fujo. Ni vyema nchi zikaachiwa mila zao maadamu zinawalea kwa maadili. Tutakuwa Taifa la wasio na adabu kama hakuna usimamizi wa wazee wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Turidhie mkataba na marekebisho yake.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii katika Bunge lako Tukufu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha japo kwa ufupi na mimi kupata nafasi hii adhimu ili kuchangia hoja hii ya Mkataba wa Vijana wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili ni suala la kihistoria hapa katika Taifa letu la Tanzania kwani suala hili lilikuwa linahitajika kwa muda mrefu, jambo ambalo Serikali yetu haikutoa kipaumbele. Kujumla tumechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni muhimu sana hasa wakati huu ambapo vijana wa Taifa hili wanakabiliwa na changamoto nyingi sana katika nyanja za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kiuchumi; kutokana na ukosefu wa ajira kwa vijana walio wengi katika Taifa letu la Tanzania kumesababisha vijana wetu walio wengi kuzurura ovyo na kusababisha wimbi la magenge maovu kama vile wizi, ujambazi na utumiaji wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuangalia upya taratibu za uajiri wetu, tuangalie muda wa kustaafu kwa watumishi wetu, ikiwezekana kama kuna haja ya kupunguza muda wa utumishi ili vijana wetu wengi waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja Serikali iangalie sana vijana wetu katika kutafuta mbinu mbalimbali kwa kuweka sera maalum itakayosaidia kuwapatia ajira kwa njia ya kuanda mikopo ya fedha kwa wale wanaomaliza masomo yao kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kisiasa, imekuwa ni mtindo kuwaondoa vijana walio wengi kwenye vyo kwa sababu za kusingiziwa kuwa wamefanya migomo. Naishauri Serikali iangalie sana suala hili la migomo kwani wengi wao huwa hawahusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri pia Serikali kupitia Bunge lako Tukufu kuwasimamia vijana wetu wale waliokumbwa na wimbi la utumiaji wa dawa za kulevya wahifadhiwe kwenye kambi maalum kwa muda ili wapate hifadhi ya malezi mema kwani wakiachiwa waendeleo kuongezeka, Taifa litapoteza vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya Taifa.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono maridhiano katika Azimio hili muhimu kwa vijana wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kuleta hoja hii muhimu katika kusaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii katika vipengele vifuatavyo:-

Kwanza ni ushirikishwaji wa vijana na ajira. Kwa kuwa nchi za Afrika ikiwamo Tanzania, vijana ni asilimia kubwa na kwa kuwa vijana ambao ni asilimia kubwa ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu la Tanzania, kwa maana hiyo inahitajika vijana wafunzwe maadili ya nchi yao pamoja na kupewa nafasi mbalimbali zinazohusiana na uchumi wa nchi kwa kushirikishwa katika nyanja mbalimbali ambazo zinaleta maendeleo kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika hili waweze kushirikisha vijana katika kupatiwa ajira katika sekta mbalimbali ili waweze kujipatia kipato kizuri na waweze kumudu maisha kwa ujumla hasa katika ajira binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na elimu. Kwa kuwa vijana hawawezi kushindana kiuchumi baina yao na vijana wa nchi nyingine, naishauri Serikali yetu iweke kipaumbele kwa vijana wetu wa Tanzania waweze kuendelea kuwapa nguvu ili waweze kupata elimu ya juu kwa kupatiwa mikopo bila ubaguzi maana vijana wengi hawana uwezo wa kujisomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwape nafasi kubwa katika elimu ili waweze kujitegemea wenyewe, maana bila elimu vijana hawataweza kubuni mambo yanayowasaidia. Elimu ni ufunguo wa maisha. Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vyo vya VETA vianzishwe kila Wilaya haraka iwezekanavyo ili vijana wetu waweze kujijajiri. Hili litawawezesha vijana kuongeza Pato la Taifa kutokana na shughuli wanazofanya. Ahsante.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa pamoja na kuwa vijana wanataka kuachiwa kuamua wenyewe, mimi nina wasiwasi kidogo kwani vijana wanakuwa na jazba sana na wanapokuwa wanaamua jambo lolote huwa hawafikiri faida wala hasara yake na ndiyo maana utaona vijana wanatumiwa kwenye kufanya maandamano kwa kuwa ni watu wa kukurupuka tu, wao huwa hawaangalii madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wale ambao walisema kuwa utaratibu wa kuwapatia mikopo ya elimu ya juu upitiwe upya na upunguzwe hayo masharti. Ni kweli vijana wengi hawana ajira lakini wengi wametoka vijijini na kwa nini hawajiendelezi kwa Kilimo Kwanza? Wengi huona ajira ni ya ofisini tu, lakini ukiangalia vijana ambao wamejiajiri wenyewe kwa kuuunda vikundi maisha yao ni mazuri sana kuliko wale walioajiriwa maofisini. Hata hivyo, naiomba Serikali ianze kufufua viwanda ambavyo hivi sasa havifanyi kazi ili hawa vijana wapate kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malezi mabaya ndiyo yanayofanya mabinti zetu kupata mimba. Kuna usemi usemao; "Mtoto umleavyo ndiyo akuavyo." Kwa hiyo, ninashauri hawa vijana ambao tayari wamepata mimba wasiruhusiwe kurudi shule ili iwe funzo kwa wengine na huu utaratibu wa kuwa na masomo ya ziada ya usiku ndiyo unaoharibu watoto wetu.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mungu kunijalia kupata nafasi kuchangia katika Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2012. Nachukua nafasi hii kuwatakia Marehemu Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, waliokuwa Wabunge na Ndugu Senge aliyekuwa Mtumishi wa Bunge, Mungu awalaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu ni muhimu kuridhiwa na kupitishwa na Bunge hili na ni muhimu kutungiwa Sheria na Kanuni zake ili uanze mara moja kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mimi si kijana lakini ni mdau na mwakilishi wa makundi yote katika jamii. Wakati tunapitisha kuridhia Azimio hili ninaguswa sana na maeneo yanayozungumzia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vijana wawe wazalendo na waipende nchi na watu wake, Serikali haina budi kuweka mazingira bora ya elimu kwa kuwawezesha vijana kupata elimu bora ambayo itaondoa malalamiko kwa watoa huduma (walimu) na wanafunzi hasa wa shule za sekondari za Kata na Vyuo Vikuu. Pia vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana ambaye anapata haki za kielimu na upataji wa kazi kwa mazingira magumu, hata atakapomaliza masomo na akabahatisha ajira hatakuwa mzalendo kutokana na mazingira aliyokuwa nayo huko nyuma ya kupata elimu na ajira. Matokeo ya hayo yote yanapelekea kujenga Taifa lisilo la uzalendo na ni hatari kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuliendeleza Taifa lenye uzalendo wakati umefika sasa kuwepo na somo la Utu kuanzia shule za awali mpaka elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana na ajira; ajira rasmi na zisizo rasmi, wapo vijana waliamua kujijaji baadhi wamepata mafanikio na wengine kutofanikiwa na vijana hao hawana vigezo vya uzoe fu katika sekta hizo binafsi.

Kuhusu ajira rasmi eneo hilo lina vikwazo kutokana na sheria na taratibu zilizopo ambazo zinawabana vijana hasa wasomi wanaoomba ajira Serikalini kupata vikwazo vya uzoefu au aliyebahatika kupata ajira atakaimu hadi miaka mitano au saba ndipo athibitishwe, hivyo, Serikali ipunguze muda wa kukaimu kwani kukaimu kunapelekea kutojamini na pia kushindwa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha uwekezaji kishirikiane na Wizara husika kuunganisha vijana kwa fani zao toka vyuoni na kutoa mitaji na kuwapa maeneo ya uwekezaji kwa mfano; migodini, kwenye kilimo na viwanda vya uzalishaji. Ahsante.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa mkataba. Ni haki ya vijana kuandaliwa vizuri ili wawe na ule uwezo wa kuwa wananchi bora na wenye tija kwa Taifa.

Kimalezi ni muhimu na wajibu kwa Taifa tukianza na wazazi kuhakikisha vijana wanalelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielimu ni wajibu wa Taifa kuwapa fursa ya elimu vijana kwa kiwango cha kufaa na pia ni wajibu wa vijana kufanya jitihada. Naipongeza Serikali ya CCM kwa hatua inayopiga katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ajira Taifa lijitahidi ili vijana wapate ajira. Serikali iendeleze uwekezaji wa ndani na nje ili kuzalisha ajira, lakini pia vijana wajitume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanatakiwa walindwe. Tujitahidi kuhimiza Sheria za kuzuia mambo yanayo *destroy* vijana kama vile tabia chafu, dawa za kulevya na kadhalika. Kama sivyo tutaisia kuwa na vijana wasiofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa wa kuonesha kwa vitendo namna ambavyo vijana wa Taifa hili watanufaika. Vijana wanahitaji ajira binafsi, Serikalini au katika mashirika, viwanda na makampuni mbalimbali. Ili haya yote yatimie ni muhimu kuimarisha uchumi wa Taifa kwa kuandaa vijana kuwa ni sehemu ya nguvu kazi ya Taifa kwa kufanyakazi (ajira) katika kada mbalimbali. Ili uchumi uimarike tunahitaji uwekezaji katika viwanda, migodi, makampuni binafsi na kuboresha sekta ya kilimo. Haya yote yatawezekana kama elimu wanayopata itakuwa yenye kutoa nafasi ya kujijaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu yafundishwe masomo ya biashara, kilimo, ufundi na ujasiriamali. Vijana wengi wamekuwa Wamachinga wakihangaika na biashara za mikononi, bila ujuzi wowote kibiashara. Tunazungumzia Kilimo Kwanza lakini kundi kubwa la vijana halijaandaliwa kushiriki kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye jitihada kubwa na kwa kasi kubwa kujenga Taifa lenye vijana walio tayari kujenga uchumi wa Taifa lao. Kwa ujumla wakati ni huu hatujachelewa.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wafanyakazi wa Wizara yako. Baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia na kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na malengo ya Mkataba, jambo la msingi katika Mkataba huu ni pale inapoeleza kwamba ni kutoa fursa kwa kuwepo mfumo wa Sheria wa kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika vyombo vya juu vya utoaji wa maamuzi katika maendeleo ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Waziri kama kweli tunataka Vijana wafanikiwe katika hilo lazima tuhakikishe kwamba:-

(a) Mitaa ya shule katika ngazi zote inahakikisha kuwawezesha kukabiliana na changamoto za Bara hili kisayansi, kielimu na kiteknolojia.

(b) Vyombo vya fedha nchini vinashawishiwa kuwapa fursa (kiseru) za masharti nafuu vijana ili waweze kukopa fedha za mitaji ya miradi.

(c) Vyuho Vikuu vinaongeza mafunzo ya Ujasiriamali (*entrepreneurship*) ili vijana wengi wapate mafunzo muhimu ya kuendesha miradi.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu ni Taifa la kesho. Wapo vijana ambao ni wasomi lakini hawana ajira, pia kuna vijana wengi waliopo vijijini ambao hawana ajira na miradi wanayoifanya siyo miradi endelevu. Ushauri wangu ni kwamba, vijana hawa tuwaandae kuanzisha miradi ambayo itakuwa endelevu. Hata ikiwa ni kilimo, ardhi tunayo, maji tunayo, tujipange ili tuwaweke makundi na kuwapa nyenzo za kilimo, pembejeo ili waweze kulima kilimo cha kisasa na wataweza kujijari wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vijana wa Afrika, *The African Youth Charter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mchango wangu, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta mbele ya Bunge kuridhia Mkataba huu. Ni lazima tukubali kwa dhati kuridhia mkataba huu, kwani Vijana ni Taifa la leo na kesho. Hivyo ni jambo muhimu sana kwa Taifa lolote. Kwa kutambua hivyo, ni vema basi kuwa na mipango madhubuti katika kuandaa mazingira bora katika kulea vema, katika makuzi bora, kuwalea katika maadili bora Kitaifa, Kimataifa na kijamii. Jukumu la kwanza ni kuwalea na kuwakuza kiafya, kuwapa elimu bora, kwa wale wote wanaobahatika kupata elimu. Kuwapa ajira kulingana na ujuzi waliopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, si vijana wote wanaobahatika kupata elimu, hivyo ni jukumu la Serikali kuandaa mazingira ya kufanya vijana wa aina hiyo wanajitegemea kwa kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira yao. Rasilimali kubwa ni kutumia vizuri ardhi yao kwa shughuli mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na uvuvi bora kutokana na bahari na maziwa tuliyonayo. Hivyo, jukumu kubwa kwa Serikali ni kutoa uwezesho kwa kupitia mipango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kuwatambua vijana waliopo nchini kwa makundi mbalimbali mjini na vijijini, walio na elimu na wasio na elimu na wasio na ardhi ili kutafuta njia bora ya kuwasaidia ni namna gani wataendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vijana wengi mijini na vijijini wamekuwa wakikaa vijiwani na mara nyingi kutokana na kukosa elimu au ajira, lawama nyingi zimekuwa zikielekezwa upande wa Serikali. Hivyo, ni jukumu la Serikali kutoa maelekezo ili kila mmoja wao ajue wajibu wake na sio kila jambo lawama zote ni kwa Serikali. Jambo ambalo sio sahihi, kazi kubwa ya Serikali ni kutengeneza mazingira mazuri ya

kumwezesha kijana kutumia elimu yake, ujuzi wake au nguvu zake na kazi yake na sio kila wakati kutoa lawama kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa nao kwa sehemu kubwa wanapotosha sana vijana kwa kudhani kila jambo linaweza kufanywa na Serikali bila kijana kufanya kazi. Wanasiasa wanaosema hivyo wawe wanachukuliwa hatua, vinginevyo Taifa letu litakuwa na vijana wengi wavivu na tegemezi kwa kila jambo. Mwisho wa siku tutakuwa na Taifa ombaomba, maskini, jambazi, wezi, lisilo na maadili, matokeo yake Taifa litakumbwa na vurugu ambayo italeta mapigano na mwisho ni vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kuipongeza Wizara na Mawaziri Dokta Emmanuel Nchimbi na Naibu wake Dokta F. Mukangara, kwa kuridhia na kuleta azimio hili muhimu katika Bunge. Hakika siwezi kulaumu kwa kuchelewa kuletwa kwa maana ni dhahiri zipo sababu za msingi zilizosababisha kuchelewa. Katika uchangiaji wangu, napenda kusisitiza kwa yote yaliyopendekezwa, yazingatiwe na yatekelezwe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo napenda nichangie kwa uchache katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2(1), ambayo imeainisha na kuzungumzia kuepuka ubaguzi kwa kusema: "Kila kijana atakuwa na haki ya kufaidi na uhuru uliotambuliwa na kuhakikishiwa katika mkataba huu bila kujali Utaifa, ukabila, rangi, jinsia na kadhalika. Naomba eneo hili lisilete mashaka mapya maana uhuru usio na mipaka ni hatari nene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(1) na (2), zote zimezungumzia uhuru wa kutoa mawazo. Hii ni heri ikaangaliwa kwa umakini, kwa maana yawe ni mawazo ambayo yatajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(2), ambayo inatoa uhuru kwa vijana kutoshurutishwa kujiunga na chama chochote. Naomba hili litazamwe kwa mtazamo yakini, maana si kila chama kina malengo mazuri na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja kwa kuiomba Serikali kuwa makini na mkataba huu, isije ikawa ni chachu ya vurugu na pia ikawa ndio kichocheo cha ghasia kwa vijana kuamini wamepewa hati ya uhuru mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Waziri, kuleta mbele ya Bunge hili, kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika. Pili, nitoe masikitiko kwa kuchelewa kuuleta Mkataba huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Mkataba huu umesainiwa toka mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanakabiliwa na tatizo la ajira. Wengi wao wanategemea Serikali iwapatie ajira katika Serikali. Mawazo haya ni lazima yaondoshwe kwani Serikali haina uwezo huo. Lazima vijana wapewe elimu ya ujasiriamali kwa azma ya vijana kujijiri wenyewe. Vile vile elimu ya kilimo itolewe kwa vijana ili waweze kurudi mashambani na kuendeleza kazi za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua madhubuti zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa wimbi la vijana kupata mimba linadhibitiwa kwa nguvu zote. Hivi sasa wanafunzi wengi wanapata mimba na kuacha masomo yao katika umri mdogo. Elimu juu ya hasara inayopatikana kwa wanafunzi kupata mimba itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanakabiliwa na tatizo la dawa za kulevya. Wengi wao wameingia katika janga hili kwa sababu ya kukosa ajira au wameacha masomo mapema au kukosa malezi bora. Serikali lazima ichukue hatua za dharura kuwatoa vijana wengi katika janga hili. Serikali ifungue vituo vingi vya kuwaweka vijana walioathirika na dawa za kulevya kwa ajili ya kupata matibabu.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii na imekuja kwa kuchelewa sana kwani vijana wako katika hali ngumu sana ya maisha kutokana na Sera mbaya zilizowekwa na Serikali. Naiomba Wizara husika ijikite sana katika mambo muhimu yanayowagusa sana vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu naomba lipewe kipaumbele zaidi hasa vijana wanaopata elimu ya Vyuho Vikuu ambao wanapata shida kubwa hasa kwenye Bodi ya Mikopo, ambako kuna manyanyaso makubwa sana kwa wale wanaosimamia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatima ya vijana wanaoishia elimu ya msingi na sekondari. Kundi hili ni kubwa sana ambalo lina vijana wengi ambao hawajui wapi wanakwenda. Ni vizuri Serikali ikaangalia kwa makini zaidi kwa kuangalia kundi hili kwa kuwatafutia miundombinu ya kuwawezesha vijana hawa ili washiriki katika zoezi la kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie pia kuhusu suala la ajira. Ajira ni tatizo kubwa sana kwa vijana ambao wengi wao wanaishi bila kupata kazi. Naomba Serikali iandae mipango mikakati ya kufufua viwanda ili vitoe ajira na ianzishe viwanda vipya hasa katika maeneo ya vijijini ambako vijana wengi wanaishi bila kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ardhi. Naishauri Serikali iangalie kwa upana wake juu ya uwezekano wa vijana hawa kuweza kujijaji wenyewe kupitia sekta ya kilimo. Eneo hili ni muhimu sana katika kuwaandaa vijana wawe na miliki za ardhi ambazo zitaisaidia vijana walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la madini. Eneo hili ni muhimu sana katika kuzalisha ajira kwa vijana. Naishauri Serikali kuwepo mpango maalum wa kuwasaidia kupata maeneo ya wachimbaji wadogowadogo ambao wananyanyaswa kwa kukosa maeneo ya kuchimba madini na kuangalia fursa za wageni wakipora mali katika maeneo yao ya asili ambayo yamewekezwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu. Naomba sana maoni ya Wabunge yafanyiwe kazi na Serikali isimamie vijana wafanye kazi na wajitume kwa shabby bila kufanya kazi hatuwezi kwenda mbele.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwako na kwa Bunge lote ikiwemo watumishi wa Bunge wote kwa kuhakikisha shughuli zetu kama Wabunge zinafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda leo kuona mkataba wa vijana wa Afrika wa mwaka 2006, japo muda umechelewa, lakini nashukuru angalau sasa tunaujadili na kuipitisha na napenda turidhie na tuipitishie kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vijana wa Tanzania kwa mkataba huu waendane na ushindani mzuri ulio sawa kwa vijana na wengine wa Afrika, basi ni vizuri sasa tuanze kuwaandaa vijana wetu kuwa na uwezo wa kujiamini hasa katika maamuzi yao na ya wategemezi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa kupunguza ugumu wa kupata elimu na mitaji ili baada ya Azimio hili la Afrika 2006 tuwe tayari tuna vijana ambao wanao uwezo wa kupambanua na kuchukua hatua sahihi za mustakabali wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili linamtaka kijana yeyote wa Afrika kwenda popote na kushiriki fursa za kiuchumi bila kuathiri sheria za nchi husika. Je, ni sheria zipi ambazo tayari tumezitunga kwa kulinda rasilimali ardhi kwa vijana pekee wa Kitanzania. Je, tayari tumewaandaa vijana wetu wa Tanzania kushiriki fursa ya kujenga na kujijengea uchumi?

Je, vijana wetu ni mikakati gani tumewawekea ili wajiamini na uzoefu wa kufanya kazi rasmi za kiutu zisizo na udhalilishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie vizuri sana mkataba huu na matokeo hasi au matokeo chanya kulingana na mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana basi tutumie fursa hii kupunguza makali ya upatikanaji wa elimu na ujuzi na kutoa dhana ya elimu ni bidhaa na kuifanya elimu ni huduma kwa vijana wote na tena ni lazima kwa kila kijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ni muda sasa wa kuwasamehe wote waliosimamishwa masomo vyaoni ili waweze kurudi kupata elimu ili waweze kujiandaa na kwenda sambamba na mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuhitimisha kwa kusema naunga mkono hoja.

MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mheshimiwa Dokta Emmanuel John Nchimbi na Naibu Waziri Mheshimiwa Dokta Fenela Mukangara kwa juhudi kubwa waliyofanya ili kuuleta Mkataba huu wa Kimataifa kwa maslahi ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni nguvu ya Taifa ili kuchangia maendeleo ya Taifa. Hivyo ni wakati muafaka kwa nchi yetu kuyapa kipaumbele mahitaji ya vijana ili kuwawezesha kielimu, kichumi, kiteknolojia, kijamii na kiutamaduni. Vijana wanahitaji elimu ya ushauri nasaha itakayowawezesha kujiamini na kujitegemea. Vijana wanakosa elimu ya ushauri nasaha ambayo ni kigezo muhimu sana kinachomwzesha mtu kujiamini. Bila elimu hiyo vijana wataendelea kulalamika kwa kukosa kujiamini.

Pili, mafunzo ya Jeshi ya Kujenga Taifa ni muhimu sana ili kujenga uwezo wa kujitegemea. Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yanaimarisha vijana, yanaleta ukakamavu, ukomavu wa akili, kujiamini na kujitegemea. Mafunzo hayo yatasaidia sana vijana kujijiri na kuwajengea maadili.

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Mkataba wa Kitaifa wa Vijana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wa sasa kwanza wamepoteza kabisa maadili ya kiutamaduni ya nchi yetu, wengi wanaiga mambo mengi ya kigeni. Kwa kufanya hivyo vijana wetu hawaambiliki au kufundishika kwa urahisi. Vijana wengi ni wavivu sana hawapendi kujituma siyo kama vitu vya kufanya hakuna, bali ni uvivu uliowajaa. Kwa mfano, michezo ni ajira kama vile kukimbia mbio ndefu, ngumi, mpira wa miguu na vinginevyo, lakini kuamka asubuhi peke yake ni kazi. Nchi yetu ni kubwa sana na ina ardhi kubwa sana, lakini vijana wengi hawajagundua kama kilimo kinaweza kuwafanya kuishi vizuri au kujijiri.

Nidhamu kwa vijana imepotea kutokana na uhuru mkubwa waliopewa maana kijana anaweza kupinga kitu kizuri ambacho mzazi au mkuu wake anamwona anapotea, lakini uhuru waliopewa wanadharau kabisa ushauri wa wazee. Vijana wetu wa leo pia ukakamavu umepotea lazima tuwe na sera kama ya zamani, lazima wapitie JKT ili wajifunze ukakamavu na uvumilivu.

Kwa hiyo, watakapopita hapo JKT wakimaliza kama hakuna kazi basi wawezeshwe na kupatiwa ardhi na zana za kilimo ili waweze kuzalisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu ambao ni wa kuridhia Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kuridha Mkataba wa Vijana wa Afrika (*Africa Youth Charter*) la mwaka 2006 kufika hapa Bungeni licha ya kuchelewa kwake lakini una umuhimu mkubwa kwa manufaa ya vijana na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu umezingatia nguvu kazi kubwa inayotokana na vijana lakini nguvu kazi hii haitumiwi inavyopasa juu ya uzalishaji na ukuzaji maendeleo na ukuzaji wa uchumi wa nchi yetu kupitia taasisi hii muhimu ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Azimio hili lina utata kutokana na kuwagawa vijana wa Tanzania kiitikadi hata katika sehemu za ajira. Sasa kuridhia Azimio hili lazima tujiangalie makosa yetu kama Taifa ili tuyasahihishe yale ambayo yanaligawa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama Tanzania kuridhia Azimio ili kwa kuwaweka vijana wa jinsia tofauti mahali pamoja katika sekta mbalimbali siyo mbaya lakini ni lazima liwe na mpango mkakati wa kuwawezesha vijana katika kujiletea maendeleo badala ya kuwaachia kushiriki katika biashara haramu, ambazo hatima nikulizalishia Taifa hili wezi, majambazi, ombaomba, ukahaba na magonjwa mengi ambayo hatimaye ni kulitwisha Taifa mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Tanzania tutakubali kuridhia Azimio la Mkataba huu vijana wa Tanzania watafaidikaje wakati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Wakenya na Waganda wananufaika zaidi kuliko W atanzania kutokana na kiwango chao kikubwa cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja na mshikamano wa Taifa unahitajika kuwajenga vijana kama Taifa na sio kiitikadi ya vyama wanavyotoka na hata wasiokuwa na vyama au kuzingatiwa maeneo wanavyotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ni sehemu yoyote ambayo itamwezesha kijana au vijana kujipatia pato la kuendesha maisha alimradi pato hilo liwe limepatikana katika njia halali. Serikali ina wajibu wa kuwapatia mikopo vijana waweze kuunganishwa katika sekta ya kilimo, biashara, ufugaji, uvuvi, viwanda vya maseremala, washonaji, viwanda vya nguo na mambo mbalimbali ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tutajie ni vijana wangapi wa Kitanzania ambao watapatiwa nafasi za ajira katika nchi wanachama wa umoja huu endapo Tanzania tutakubali kuridha Azimio la Mkataba huu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mkataba wa Vijana wa 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi tulionao hawana kazi, wale ambao wamepata elimu wengi wako mtaani, vijana ni Taifa la kesho. Maendeleo yoyote ya nchi yataletwa na nguvu kazi kubwa ya vijana.

Serikali ilibinafsisha Mashirika ya Umma na Viwanda vingi vilivyonunuliwa na wafanyabiashara wenye uwezo, ambao wametumia vibaya *opportunity* hiyo, kwa kutokufufua viwanda hivyo. Viwanda hivi vingeweza kutoa ajira kwa vijana wetu, Serikali imekaa kimya kuhusu mikataba ya viwanda na mashirika hayo. Wabunge wamepiga kelele kuwa mikataba iwe *revoked*, viwanda viuzwe kwa wengine wenye uwezo wa kuviondeleza ili mapato na ajira ipatikane. Serikali ifufue viwanda vilivyofungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja idadi kubwa ya vijana, Serikali ikubali kuwa-sponsor VETA angalau wakitoka waweze kujitegemea, wachache wanaokwenda kwenye *degree* waendeleo kutafuta na kujajiri hasa wakati huu wa soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki kazi zinaweza kupatikana pia katika mtandao, vijana wasi-*deal* tu na *facebook*, *twitter*, *jamiiforum*, watafute pia kazi katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezekano wa vijana wetu kuajiriwa pia katika michezo mfano mpira wa miguu, mpira wa pete, na kadhalika. Tunao vijana warefu hata *basketball* inawezekana, Serikali iwasaidie kujifunza michezo hii inawezekana kwa kutumia wafanyabiashara. Serikali iangalie mifumo ya mikopo ya benki zetu, benki zinavuna fedha nyingi lakini *borrowing interest* iko juu sana, Serikali iingilie kati ili vijana waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana Mkataba huu ukawa ngazi ya kupandia katika dira ya maisha mazuri kwa vijana. Vijana watumie fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mkataba uliopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Kwanza hitaji kubwa la vijana ambalo jamii huwa inajisahau, vijana wanahitaji kutambuliwa (*recognized*), wanapotambuliwa kwenye jamii inasaidia kuelewa kuwa jamii inawaona kuwa ni sehemu ya jamii.

Pili, vijana wanahitaji jamii kutambua mahitaji yao kadri wanavyokuwa kila ngazi ya ukuaji inahitaji mahitaji yake. Serikali itambue kila hatua ya ukuaji iwasaidie kulingana na mahitaji yao. Hata katika jamii za Kiafrika (Masai) walikuwa na mgawanyo wa vita katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie shughuli za kuwawezesha vijana kulingana na rika zao, kulingana na *interest* zao. Mfano, wanahitaji kujiunga na fani za michezo, sanaa, kilimo na kadhalika. Basi waendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni kipindi cha mpito (*transitional period*) kuelekea utu uzima. Serikali inahitaji kuwaelekeza na kuwaandaa kuwa watu wazima. Mfano, suala la elimu wanahitaji wote wapatiwe elimu ya kuwaandaa kuwa watu wazima, Serikali ikumbuke elimu ni ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Serikali inahitaji kuwatambua vijana, kujua mahitaji yao na kuwapatia elimu katika sekta mbalimbali ili waweze kupita kipindi cha mpito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ABDALLA HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote. Azimio hili la vijana ni suala zuri kujadiliwa. Vijana ndio tegemeo la kila nchi duniani. Naiomba Serikali kuangalia suala zima la nidhamu juu ya vijana, kwanza vijana wamekosa nidhamu kwa sababu hii wamekosa uzalendo wanathubutu hata kuwasemea ovyo viongozi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ikitoweka vijana hawana mapenzi ya kazi kwani kazi zozote za nchini huonekana ni za ovyo. Hivyo lazima taasisi ambazo kikifundisha nidhamu kama JKT lazima ziimarishwe na lazima vijana wadhibitiwe katika suala zima la nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ikikosekana hata mila, desturi na tamaduni zetu zinapotea. Tuangalie vijana kwa kukosa nidhamu wanafanya vitendo kwa kukosa nidhamu wanafanya vitendo kinyume na taratibu zetu. Mfano vijana wa kiume kusuka nywele, kuvaa herini, kuvaa vidani shingonmi kijana akiweza kufanya hivyo, hana jingine lolote atakalojali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilivalie njuga suala la nidhamu juu ya vijana kuondokana na uvivu wa kufanya kazi, kuacha tabia ya ulevi, kuvuta unga na kupenda mambo ya mapenzi, anasa na mengineo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nasisitiza suala la nidhamu pasipo nidhamu Taifa huyumba.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika, aidha, naomba kushauri kama ifuatavyo; vijana waendeleo kupewa fursa kwenye vyombo vya maamuzi kama vile Baraza la Madiwani, Bunge na Bodi mbalimbali?

Pia vijana wapewe fursa za kupata masomo ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali na wadau mbalimbali kwa kuwa vijana ni 60% ya nguvu kazi, naomba kushauri vijana wapewe fursa mbalimbali kama ajira, mikopo midogo midogo. Naomba Serikali iwawezeshe vijana katika elimu ya ujasiriamali ili kupunguza tatizo la ajira, vijana waweze kujijiri wenyewe. Vijana wapewe ajira kutokana na ujuzi wao bila kudai uzoefu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni la muhimu sana kwa mustakabali wa vijana wa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Tanzania na Afrika kwa ongezeko kubwa la vijana ambao ni asilimia 60 ya nguvu kazi na kwa idadi ya watoto na vijana kwa pamoja na asilimia 60 ya wananchi wa Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla.

Hata hivyo, vijana wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi kisiasa na kijamii. Changamoto hizi zinafanya vijana waonekane kama matatizo wakati ambapo ujana na vijana ni fursa za suluhisho la changamoto zinazowakabili vijana wenyewe na mataifa ya Afrika kwa ujumla.

Nashukuru kwamba hatimaye Serikali inaleta Bungeni mkataba huu kwa ajili ya kuridhiwa. Kati ya mwaka 2006 mpaka 2010, nimekuwa mstari wa mbele kushamiri kwa njia mbalimbali mkataba huu uletwe Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa. Baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge, nimechangia Bungeni kwa nyakati mbalimbali mkataba huu uletwe Bungeni. Hatimaye mjadala na mkataba huu umeletwa Bungeni.

Katika kuteleleza Ibara ya 15 ya mkataba, kwa upande wa jimbo la Ubungo Serikali iweke mkazo katika kufufua viwanda vilivyobinafsishwa lakini imeshindwa kuendelezwa ili kuongeza ajira kwa vijana. Viwanda hivyo ni pamoja na Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Kiwanda cha Ubungo Maziwa, Kiwanda cha *Ubungo Garments* na kilichokuwa Kiwanda cha Zana za Kilimo Ubungo cha (UFI). Aidha, Wizara ya Vijana iwasiliane na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji ili katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (EPZ/SEZ) katika Jimbo la Ubungo ili yaweke maeneo maalum ya wazalishaji vijana. Aidha, kama sehemu ya kuteleleza mkataba huu Wizara itoe kauli ya hatua iliyofikiwa kabla uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa. Izingatiwe kwamba ahadi ya kuundwa kwa Baraza la Vijana ilikuwepo katika Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 1996 na pia katika Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007. Mwaka 2003, aliyekuwa Waziri wa Vijana alituhidi vijana kwamba Baraza lingekuwa tayari mwaka huo lakini mpaka sasa mchakato haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izingatie kuwa mwaka 2009 – 2018 ni kipindi cha vijana wa Afrika (*African Youth Decade*) hivyo Serikali inapaswa kuandaa mpango wa hiari wa utekezaji. Katika kuondoa tatizo la vijana wengi kukimbilia mijini lazima mipango ya kilimo iwe na mikakati maalum kwa ajili ya vijana. Pia katika maeneo ya rasilimali mathalani madini, misitu na kadhalika, yahusishe kuweka kipaumbele miradi maalum ya vijana kwa ajili ya mustakabali wa nchi ikiwemo wa vijana ambao ni kizazi cha sasa na baadaye Serikali ianzishe mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya miaka 50 ijayo.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana ndiyo nguzo ya kujenga Taifa letu kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni, kwa maamuzi haya ya Mkataba wa Kimataifa wa Vijana wa Afrika ni jambo zuri sana. Hii itasaidia vijana kujulikana katika Taifa la Afrika. Mkataba huu utasaidia sana kuwaunganisha vijana wa Kiafrika katika sekta zote kama vile sekta ya kilimo, sekta ya utamaduni na michezo na sekta ya elimu.

Katika Ibara ya 13(4) elimu na maendeleo ya ujuzi, ni kweli kabisa vijana wanatakiwa kusoma kwa nguvu zote na kwa ujuzi wote ili kupata elimu sahihi na makini siyo bora elimu, maana yake vijana wanatakiwa kupata elimu bora ili wawe viongozi wazuri kwa Afrika. Kijana akisoma vizuri Bara la Afrika litapata uchumi ambao upo juu siyo kutegemea misaada kutoka nje.

Vijana wanatumiwa sana katika kuunganisha jamii yetu ya Kiafrika, pia ndiyo nguvu kazi na wenye changamoto nyingi na kubwa hivyo basi vijana wanapewa kipaumbele katika kujenga Afrika kwa ujumla ndiyo maana vijana wanapewa nafasi kubwa katika kupambana na changamoto za Kiafrika, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Vijana ndio wanaotumika katika masuala ya ulinzi, masuala ya nguvu kazi na utetezi wa sheria kwa masuala ya haki za binadamu.

Mwisho, naomba Serikali kuwapa vijana nafasi muhimu katika uongozi wa Kiafrika, vijana kumiliki ardhi, vijana kupata elimu sahihi, vijana kupata ajira na vijana kupata mikopo. Napongeza sana Serikali kwa kuleta Mkataba wa Vijana wa Afrika. Naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai huu na nafasi ya kuchangia juu ya hoja hii ya kuridhia Mkataba wa Vijana Afrika na hasa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu umechelewa kuletwa Bungeni, lakini basi napenda kuunga mkono Azimio hili na kwamamba yote yaliyopangwa/yaliyoelekezwa katika mkataba huu yatekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwaona wazee leo na wakitekeleza kazi zao kwa upendo na mshikamano na hatimaye kuleta maendeleo nchi hii ni kwa sababu wakati fulani vijana ndio waliokuwa wameandaliwa vizuri kielimu, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Hivyo basi ili Taifa letu kwa leo na siku za

usoni miaka 50 ijayo lisonge mbele zaidi kimaendeleo Taifa la Tanzania likishirikiana na Mataifa mengine halina budi ku-focus maendeleo ya vijana kielimu, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni wabunifu, wana nguvu wanachokitaka ni kuandaliwa na waliokwishaandaliwa wapewe nafasi ya utekelezaji katika nyanja mbalimbali nyuma yao wakiwepo wazee wapo na hekima na busara (kwa usimamizi) maana peke yao hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, vijana wapewe nafasi ya uongozi katika nafasi mbalimbali kuanzia shina hadi Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri atatumia dakika 15 kwa ajili ya kuchangia halafu Mheshimiwa Waziri naye atamalizia kwa kufanya majumuisho.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii kwa ruhusa yako, kwa niaba ya Serikali, niwashukuru Wabunge wote kwa mchango wao mzuri, lakini pia kwa kusaidia timu yetu ya Twiga na kuichangia vizuri. Nimeona nizungumze hili na nimshukuru pia Mheshimiwa Ummu Mwalimu kwa kutoa hamasa kubwa sana na kuhakikisha Wabunge wengi wanatuunga mkono mpaka timu yetu ya Twiga ikashinda.

Baada ya kusema haya ingawa umekwishatoa angalizo, najua Waziri Mkuu bado hajatoa, nimeona niliseme haraka haraka, kwa hiyo nawashukuru sana Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa maoni na ushauri wake hasa kwa kukubali turidhie vipengele kadhaa kwa stara kwa maana ya kuhimiza bila kusita umuhimu wetu kama Serikali na Wabunge kwa ujumla pamoja na wadau mbalimbali umuhimu wa kuzingatia sheria, mila na desturi zetu katika mengi tutakayoyapanga kuyapitisha na kuyaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja za Kamati ya Bunge, kuna moja ambayo niliona ni nzuri hasa suala la kuzingatia fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ngazi ya juu na hasa katika vyama. Ni mategemeo yetu kama Serikali, kwa vyama husika na jamii kwa ujumla itapokea hayo na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto mbalimbali zilizowasilishwa na Kamati ya Bunge, napenda kuchukua fursa hii kuelezea kuwa changamoto nyingi zimepewa mwelekeo wa kuzifanyia kazi kupitia Sera yetu ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo kwa kweli kuna mchangiaji mmoja aligusia hapa kwamba Sera hiyo haipo, nataka nitoe nafasi ya kuelezea hapa kwamba Sera hiyo ipo na mengi ambayo huu mkataba unazungumzia yamebebwa kwa kiasi fulani ndani ya Sera ile. Labda kwa sasa hivi mpango utaweza kuja wa kuanza kuibadilisha au kui-review Sera hiyo kuweza kuchukua masuala mapya ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kukubaliana na yale yaliyopendekezwa kuridhia kwa stara Ibara ya 13,(4)(h) na Ibara 23(1)(g), kuhusiana na wanafunzi wajawazito kuendelea na masomo baada ya kujifungua na ile ya mfumo wa kuwaruhusu wanafunzi wajawazito kuendelea na masomo. Hili kuna ambaye alilizungumzia kiasi na kuonyesha *reservations* mbalimbali. Kwa kifupi, Serikali inachosema ni kwamba tunaridhia kwa stara kwa maana tutazingatia Sheria na Kanuni lakini pia na desturi na mila zetu ili kuhakikisha kwamba hatuendi nje ya utaratibu ambao umewekwa. Pamoja na hayo, Sheria ya Elimu, Na.5 ya mwaka 1978 kama ilivyo sasa hivi hairuhusu, ndiyo maana tunasema kwamba tunataka turidhie kwa kuzingatia stara. Hata hivyo, Wizara ya Elimu ina mipango mbalimbali kwa mfano Mpango wa MEMKWA ambao kwa kiasi fulani unachukuliwa na kuanza kuwazingatia wale vijana mbalimbali ambao wanapata mimba kuweza kuwastiri na kuwapatia nafasi ya kuweza kusoma hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Sugu, kwa mchango wake na hoja mbalimbali alizoziweka na nyingi zimeonyesha umuhimu uliopo wa kuridhia Mkataba huu. Hata hivyo, hoja zingine za ndani zaidi nadhani Mheshimiwa Waziri Nchimbi ataendelea kuzitungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo labda kwa uchache nijibu kidogo hoja za watu mbalimbali waliochangia hoja hii. Kwanza, nianze kwa hoja ile inayohusu elimu bora kwa vijana vijijini na pia kuhakikisha kwamba vijana wanamilikishwa ardhi. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Zainabu Kawawa, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Kakoso pamoja na wengine wengi ambao siwezi kuwataja wote kwa sababu orodha ni ndefu lakini nataka tu watambue hiyo hoja yao ambayo wameizungumzia kuhusu elimu bora lakini pia kuhakikisha vijana wanapata rasilimali ya ardhi ili kuhakikisha kwamba wanaweza kujikwamua kwa kutumia ardhi hiyo. Sisi kama Serikali tunasema kwamba utekelezaji wake ni mtambuka na tutahakikisha kwamba tunautangaza na kuoanisha na sera zetu ili tuwe na mpango mkakati wa kisekta kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kuna elimu bora kwa vijana vijijini lakini pia kuhakikisha kwamba wanamilikishwa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa kwamba Mkataba huu umecheleweshwa sana kuridhiwa tangu uliposainiwa mwaka 2006 na hoja hii kwa kweli imezungumzwa na watu wengi tena kwa uzito kabisa, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Peter Serukamba na wengine wengi. Kwa taarifa tu, kwanza, naomba kusahihisha kwamba Mkataba huu umesainiwa mwaka 2008 na sio mwaka 2006. Aidha, Mkataba umecheleweshwa kuridhiwa kwa sababu Serikali kupitia vyombo vyake mbalimbali vilihitaji kupitia kwa umakini tu, kujiridhisha na Mkataba huu, je, mkataba huu unatekelezeka kwa mujibu wa sera na Sheria za nchi yetu? Pia ule mchakato mzima kupitia Serikalini huwa kidogo ni mrefu ili kuhakikisha vitu vinafanyika sawasawa, lazima utoke Waraka uende kwenye MTC, uende kwenye Baraza la Mawaziri na sasa hivi ndiyo umefika Bungeni. Kwa hiyo, hicho ni kipindi kiasi na katika kila ngazi kuna masuala mbalimbali ambayo yanakwenda, yanarudishwa kama sasa hivi hapa Bungeni tunaendelea kuchangia na kuanza kuomba mabadiliko tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilijitokeza ni suala la ajira na imesemwa kwamba vijana ndiyo waathirika wakuu katika upatikanaji wa ajira. Katika hili, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Nyangwine, Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Mhagama wote hawa wamezungumzia masuala haya na mimi napenda nichukue nafasi hii niseme kwamba Serikali na Wizara yangu inatambua kuwa vijana wanaouwezo mkubwa na ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Hivyo Wizara yangu inaendelea kuthamini mchango wa vijana na itaendelea kuwajengea uwezo katika maeneo yote yakiwemo maeneo ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la ajira ni kweli tatizo ni kubwa, Wizara yangu inafuatilia kuhakikisha kwamba kila Wizara yenye mlengo wa kuzalisha ajira wanafanya hivyo kwa nguvu na kwa makusudi kabisa kuanzia masuala ya kilimo, masuala ya uvuvi, viwanda, ardhi, habari, michezo na utamaduni. Nataka nirudie hili wakati tunapogusia Wizara ya Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni, kuna wenye wasiwasi kwa nini vijana iko upande huo. Nadhani ukitaka kuangalia kabisa suala la ajira kama ni suala la msingi katika masuala ya vijana basi tutambue kabisa kwamba masuala ya utamaduni na masuala ya ajira, habari, michezo hasa katika mlengo wa masuala ya maadili na utamaduni na kuwajengea masuala ya uwajibikaji, Wizara yangu inakuwa ndiyo mhimili mkubwa zaidi wa kuweza kuwafikia vijana kama ikiwezesha. Katika hili, nataka nichukue nafasi hii niwaombe Wabunge kwa nafasi yao wakati wa Bajeti tuhakikishe Wizara inapata nafasi ya kupewa nyenzo za kutosha pamoja na miundombinu ikiwemo rasilimali watu pamoja na fedha za kuhakikisha Idara ya Vijana inaweza ikafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana kushiriki katika mchakato wa uongozi, Serikali itaendelea kuwahamasisha vijana kushiriki katika masuala yote ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kushiriki katika uzalishaji.

Pia Mheshimiwa Silinde amezungumzia uanzishwaji wa Benki. Nataka kusema kwamba suala hilo liko katika mkakati kupitia Serikalini na kuna mchakato kupitia Idara ya Vijana na Wizara yangu kuhakikisha kwamba vijana wanapata Benki yao kwa misingi itakayowekwa ambayo itaonekana inatoshleza kuhakikisha kwamba Benki inakuwepo na inaendeshwa kwa misingi ya *Market Principles* sio kwamba kwa vile imeanzishwa na Serikali basi iende tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kwa kusema kwamba vijana ni rasilimali kubwa ambayo kama Taifa tunayo, vijana wanategemewa kuendeleza na kulinda nchi yetu lakini pia ni muhimu tuhakikishe tunalea vijana wenye kutambua wajibu wao kwa Taifa, lakini pia wawe vijana wenye mienendo na mitazamo chanya ya kupenda nchi yao, vijana wenye kutambua kabisa wana juhudi ya kupenda kazi lakini pia kujitolea na kutambua kabisa kwamba katika kutafuta kazi vijana wanatakiwa kujiimarisha na kuweza kutengeneza kazi mbalimbali na kuhakikisha wanaajiri vijana wenzao. Tuhakikishe hatuna vijana ambao wapo katika vijawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Sasa nitamwita Mtoa Hoja, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Kambi ya Upinzani na Wabunge wote waliochangia kwa mdomo na maandishi. Napenda kuwathibitishia Wabunge kuwa maoni na michango yao tumeipokea na tutaifanyia kazi kwa kushirikiana na sekta nyingine. Aidha, tumepokea kwa heshima kubwa pongezi zilizotolewa kwa Wizara yetu na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja kwa kuzungumza ambao jumla yao ni kumi na nane. Waheshimiwa hao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Eng. Habib Mnyaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni 63, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Godluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Faki Khamis Haji, Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Salome Mwandu, Mheshimiwa Murfaza Mangungu, Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Ester Matiko. (Makofi)

Wengine ni Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Nassib Omar, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Haroub M. Khamis, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Moza Abeid na Mheshimiwa Rashid Ali Omar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka niwapitishie kwenye maoni ya Kamati. Hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii zimepokelewa na Wizara na itaendelea kuzifanyia kazi kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ambazo hazitoi fursa kwa vijana kujijaji au kuajiriwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara husika itahakikisha kuwa zinafanywa maboresho kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la vijana kutumia madawa ya kulevya ni tatizo linalowakabili baadhi ya vijana wetu hivi sasa. Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa hizi na kushirikiana na vijana wenyewe kubadili vijawe vya vijana kuwa vikundi vya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la ajira kwa vijana Wizara yangu inaendelea kuboresha programu mbalimbali zitakazosaidia katika kuongeza ajira kwa vijana. Programu hizo ni pamoja na programu za vijana za uzalishaji mali, programu za ujasiliamali ambazo zinafanyika hivi sasa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Shirika la Kazi Duniani (ILO), programu za uwezeshaji wa vijana kupitia taasisi mbalimbali za fedha (*microfinance institutions*) na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao unatekelezwa kupitia ushirika wa programu za utamaduni wa kuweka na kukopa na programu nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa haraka nitaomba nzipitie baadhi ya hoja zilizowasilishwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza alijenga hoja ya umuhimu wa kuwepo kwa Sheria rafiki kwa Vyombo vya Habari. Utakumbuka kwamba Serikali katika bajeti iliyopita iliweka wazi msimamo wake wa kuwa na Sheria ya Vyombo vya Habari mapema inavyowezekana na nilitaarifu Bunge lako kwamba kwa mazingira ya sasa ya nchi yetu tunao uhuru wa kutosha wa vyombo vya habari ambao hauandikiki. Lakini hata hivyo ni muhimu bado kuwa na maandishi ambayo yanaongelea Sheria hii ya Vyombo vya Habari ambayo ni rafiki kwa Vyombo vya Habari. Tupo katika mchakato huo, hivi karibuni tutatoa taarifa ya kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliongelea kuhusu vurugu za Wamachinga. Nataka nitumie nafasi hii kuwataka viongozi wote wa Serikali na Vyama vya Siasa kutambua kwamba wana wajibu wa pekee kwa jamii. Ukitambulika kama ni kiongozi, moja wa wajibu wako ni kuhakikisha kwamba vijana wanakaa katika mazingira mazuri, wanaishi kwa amani, wanapendana na hawafanyi vurugu. Kwa hiyo, ni wajibu wa Vyama vya Siasa, wajibu wa Serikali na wajibu wa jamii kushirikiana kuona kwamba Wamachinga wanapata nafasi ya kushiriki katika shughuli za maendeleo bila kuwa na fikra za kupenda vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kufufua viwanda vilivyobinafsishwa, tunakubaliana na hoja hii ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Tunatoa wito kwa Watanzania wenye uwezo kuanzisha viwanda kwa sababu hatuwezi kuendelea kutoa kilio cha viwanda vilivyoanzishwa miaka ya 1970, mabadiliko ya teknolojia ni makubwa mno, sio busara kutegemea mitambo ya zamani ya wakati ule lazima sasa tutoke huko kwenye kulialia, twende mbele sasa tutafute namna ya kujikomboa kwa kuwa na viwanda vya kisasa katika mazingira ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni aliongelea hoja ya wanafunzi kufukuzwa katika vyuo kwa sababu za kisiasa. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwakemea wale wote ambao wanafanya shughuli za kisiasa katika vyo vyetu vya elimu. Tunapeleka watoto wetu wakasome, si halali kwa CCM, si halali kwa CHADEMA, si halali kwa CUF, si halali kwa chama chochote kuendesha shughuli za kisiasa kwa kisingizio chochote cha kudai haki. Lazima vijana wapewe nafasi ya kusoma na kuandaliwa kulitumikia Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwepo na hoja kutoka katika Kambi ya Upinzani kuhusu umuhimu wa kuwa na Benki ya Vijana isiyo na ubaguzi. Nakubaliana nao moja kwa moja na huo ndiyo mkakati wa Serikali. Serikali makini haiwezi kuanzisha Benki ambayo inafikra za kutengeneza utaratibu wa Chama cha Siasa. Ukiona Serikali makini inafanya namna hiyo ujue hata aliyepewa dhamana ya kuendesha Wizara hiyo ni mwepesi mno kifikra na sidhani kuwa nina wepesi wa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kupitia upya Sera ya Vijana imeshaongelewa na Naibu wangu na ameilezea vizuri lakini suala la kuanzisha Baraza la Vijana la Taifa, naomba nirudie dhamira ya Serikali

kuhakikisha Baraza hili linaundwa. Nataka nikubaliane na mdogo wangu John Mnyika alipokuwa akichangia alisema nilikuwepo katika harakati za kuhakikisha Baraza hili linaundwa. Ni kweli tumeshiriki sana harakati hizi na ni vizuri nikatumia nafasi hii kutambua Wabunge wengine ambao tulishirikiana nao sana katika jambo hili. Yupo Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa John Mnyika mwenyewe na wakati tukiyafanya haya hatukuwa Wabunge. Ninayo nia ya dhati ya kuona kwamba jambo hili tulilolianshisha kwa juhudi kubwa linafikia tamati. Kazi kubwa ambayo rafiki yangu Mnyika utakuwa nayo ni kuhakikisha unaniombea dua ili Mheshimiwa Rais asibadili mawazo kabla sijakamilisha jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja kuhusu maeneo ya stara, kuhusu wajawazito kuendelea na masomo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni ametutaka tueleze tulitumia vigezo gani kwenye kikao hicho cha Afrika kujenga hoja ya kuweka stara katika jambo hili. Vilevile ametaka Serikali iseme ni kwa nini mikataba haianzi kutumika baada tu ya kusainiwa na kuendelea kusubiri muda unapita mpaka kuja kupitiwa na kuridhiwa na Bunge. Katika jambo hili labda niseme tu kwa ufupi kwamba jambo hili ni la kisheria zaidi. Tunaweka stara katika maeneo ambayo tunaridhika kwamba Sheria zetu kwa sasa hazikubaliani na utaratibu huo na wakati huo mnajipa nafasi ya kupitia kama jambo lenyewe mnalikubali inabidi kutengeneza upya taratibu zenu za kisheria ili jambo hili liweze kuchukuliwa na kufanyiwa kazi katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu kwamba huwezi kuanza kutekeleza Mkataba kabla haujaridhiwa na Bunge. Upo mchakato wa kubadili Katiba. Ni bahati mbaya tu katika uongozi hatujui kila kitu. Lazima wakati mwingine tuwaone wenzetu ambao wanajua mambo fulani fulani. Hata katika CHADEMA tunatambua wapo Wanasheria waliobobea, yupo Mheshimiwa Tundu Lissu lakini vilevile yupo Mheshimiwa Halima Mdee na mimi nimekuwa nikiomba ushauri mara kwa mara wa kisheria kwa watu hawa. Kwa hiyo, rafiki yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi asisite kuomba ushauri kwa wataalam hao kabla hajafika mbele ya Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia hoja za Upinzani, sasa kwa haraka nipate nafasi ya kuzipitia kwa haraka baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge mtanivumilia sitaweza katika utaratibu huu kutaja majina yote, nitajaribu kuzichukua hoja zilizohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza ni hoja ya wasiwasi kuhusu utekelezaji. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu imeleta Azimio hili bila shinikizo lolote kwa sababu ya dhamira ya uongozi wake na watendaji wake kuona kwamba jambo hili linatekelezwa. Naomba niwahakikishie kwamba jambo hili tutalisimamia kikamilifu. Tunayo nia ya kuona jambo hili linatekelezwa na tunayo dhamira ya kulitekeleza. Tupeni nafasi tulifanye jambo hili. Kwa hiyo, msiwe na hofu yoyote kwamba tunapitisha tu kwa nia ya kuridhia halafu tuwe tumemaliza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la wasichana wajawazito kuendelea na masomo, nilisema pale mwanzo na nitarudia kulisema tena kwamba kwa sasa Sheria Na.5 ya mwaka 1978 haikubaliani na jambo hili. Mchakato unaendelea wa kulitazama upya jambo hili. Tujipe nafasi ili tuendee kulitazama na kushirikishana. Baada ya hapo, tutapata nafasi ya kuamua vizuri utaratibu bora wa kutumia ambao utafanya siyo tu tuweze kuwafanikisha vijana, lakini kufikia malengo tuliyoyakusudia katika nchi yetu ya kupata maendeleo kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuimarisha fursa za vijana Vijijini ni hoja ambayo Serikali inaizingatia na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya vijana waliopita Mgambo kukosa ajira, niseme tu, vijana wengi ambao wamepata mafunzo mbalimbali wamekuwa wakikosa ajira na msingi wake ni kwamba vijana wengi wanahangaika sana kutafuta kazi za kuajiriwa. Kila mtu anazunguka kutafuta kuajiriwa. Hakuna ambaye anafikiria wakae wawili/watatu wakubaliane utaratibu wa kuanzisha chombo chao cha umoja hivi. Kwa mfano, Mgambo wanaweza kuanzisha chombo chao 'ushirika wa kuzalisha mali', wakanza kuomba kazi za kulinda sehemu mbalimbali wakiwa na umoja wao. Katika mazingira hayo, hata wanapongelea kuomba mkopo wakiwa na umoja uliosajiliwa, mtu anaweza kuwaona hawa ni watu waaminifu na wakaaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajaribu kuona namna ambavyo tunaondoa vijana wetu katika akili za utegemezi, za kufikiri muda wote namna ya kujajiriwa sehemu, lazima vijana wetu waanze kutafakari namna ya kujajiri. Hakuna nchi ambayo Serikali yake inaajiri vijana wote na hakuna nchi ambayo mashirika yake ya sekta binafsi yanaajiri vijana wake wote lazima tufike mahali vijana wetu waanze kuwa na fikra za kutaka kujajiri wao wenyewe. Tukifika hapo, tutaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vijana kupewa nafasi za uongozi, Wizara ya Vijana ingefarijika sana kama vijana wangepewa zaidi nafasi za uongozi na kwa kweli wanapewa kwa kiasi fulani ingawa bado haijatoshesheza. Nakumbuka miaka michache iliyopita tulifanya kampeni kubwa ya kutaka zitengwe nafasi maalum za vijana Bungeni na wakati ule ndani ya Chama cha Mapinduzi tulifanikisha kuipitisha mpango ule lakini baadaye nikaambiwa kwenye kikao fulani, mtu alijenga hoja akasema "ukumbi wa Bunge ni mdogo". Sasa nikaambiwa una majibu gani? Nikawajibu kwamba vijana wana uwezo wa kukaa nje, wanasikiliza kwenye TV, halafu muda wao wa kuchangia ukifika, watarudi ukumbini kuchangia. Kwa hiyo, tatizo la sehemu ya kukaa si tatizo kwa vijana. Kwa hiyo, nadhani hoja hii imebaki vilevile kwamba kuna umuhimu wa kuwapa nafasi, maana tusipowapa nafasi hatuwaandai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanafika ghafla wamekuwa Wabunge bila kupata maandalizi ya awali, ninyi wenyewe ni mashahidi kwamba wanapata misukosuko mingi sana na wakati mwingine Vyama vya hata haviwasamehi wakiteleza kwa sababu ya kukosa tu uzoefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu tukajenga mazingira, hata tunapokuwa na Bunge jipya, vijana wanawekwa mahali, wanafundishwa, wanaelekezwa namna ya kuishi na wenzao na kadhalika. Vilevile na wale viongozi wa Vyama vya Siasa wakafundishwa namna ya kujenga uvumilivu kwa vijana hawa, wanateleza mara nyingi lakini ndiyo sehemu ya mafunzo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge waliongelea tatizo la vijana kupewa uhuru kupita kiasi kwamba linaweza likaleti madhara kwa Taifa. Niseme hivi kwa vyovyote vile, tunapoongelea vijana kupewa uhuru mkubwa wa kuamua mambo yao, dhamana ya mzazi, dhamana ya jamii, dhamana ya Taifa kwa malezi ya vijana haiondolewi. Asiye mtu akatoka hapa, Mheshimiwa Mbunge umetoka hapa umeenda nyumbani kwako unasema kuanzia leo siwajibiki na mwanangu, wewe utakuwa zezeta wa kiakili. Lazima ujue ukishaamua kuwa na watoto, ukiamua kuwa na familia, una wajibu nao mpaka wanapoanza kujitegemea. Kwa hiyo, nasema jamii isijiondoe, wazazi wasijiondoe katika malezi ya watoto kwa sababu ya kusema tunawapa uhuru. Uhuru ni sehemu tu ya kumfanya mtu ajenge tabia ya kujitegemea, unamtengenezea mazingira taratibu. Kama unavyoanza, mwanzo mtoto unamzuia hata kutoka nje ya nyumba, baadaye unamruhusu kwenda kusalimbia kwa mjomba peke yake, anakwenda anakua anafundishwa. Kwa hiyo, nafasi yetu kama jamii, nafasi yetu kama wazazi haiondoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilizungumziwa ni vijana kupewa kipaumbele katika kumiliki mali na hili nilisemee vizuri. Tunasema vijana wapewe kipaumbele katika kumiliki mali, ni kutambua nafasi yao katika kuzalisha na kuzimiliki. Maana tusipitishie Azimio hapa, kesho asubuhi tukakuta vijana wako kwenye maduka siyo yao wanasema limepitishwa Azimio, tuna haki ya kumiliki mali, kuanzia leo hili duka ni langu, siyo tunachokiongelea hapa. Tunaongelea haki yako ya kuzalisha na kumiliki ulichokizalisha kwa njia halali, hakuna haki za njia ya mkato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wameongelea hapa kwamba tunalo tatizo la baadhi ya watu wetu kutopenda kufanya kazi, kutumia muda mwingi wa kazi kwa shughuli zingine zisizo na uhusiano na kazi. Hili ni tatizo kubwa, lazima tushirikiane kulimaliza, lazima tusione haya kulikemea. Ndiyo maana ukifika kila sehemu katika nchi yetu ukipita, hapa unaombwa na lugha ya vijana "Mheshimiwa sijala". "Mheshimiwa sijala"! Haiwezekani kujenga Taifa la "Mheshimiwa sijala" Lazima kujenga Taifa la watu wanaopenda kufanya kazi na kutaka kuridhika na kipato ambacho wamekipata kwa jasho lao. Tabia ya kufikiria mwingine afanye kazi, wewe utumie, ni tabia potofu katika jamii na hakuna Taifa linaweza likaendelea kwa utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda wa kustaafu na mikataba kuongezwa, hii niseme ni changamoto kwa Serikali. Kwa kweli jambo lenyewe halina mvuto sana wala mimi sina maelezo mengine ya kusemea kwamba unapotaka kuongeza nafasi za ajira kwa vijana, huwezi kuwa unaendelea kutoa mikataba. Kwa hiyo, nikisema vingine, nasema uongo. Jambo hili halina mvuto! Kwa hiyo, sisi kama Serikali

tumelipokea, tutalifanyia kazi ili kwamba iwe hivyo tu kwa wale ambao ni kweli tunakosa aina ya taaluma ambayo wanayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine tatizo kubwa sana ambalo tunalo ni watu wetu kutoandaliwa au kutokujiandaa kustaafu. Ukifikisha miaka 40, unajua bado una miaka 20, ukifikisha miaka 50 unajua una miaka 10, halafu ukifikisha miaka 55 unaanza kuzunguka zunguka, "jamani mimi ni mtu muhimu sana kwenye taasisi hii, jamani nipeni nafasi tena miaka miwili mingine", *that's bad*. Hii ni matokeo ya kutojiandaa kiakili na kisaikolojia, lazima watu wetu wajenge utaratibu wa kujiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzoefu wa kazi miaka 10 mpaka miaka 15, nimetaarifiwa kwamba kimsingi nafasi nyingi za ajira za Serikalini zikiwemo za Wagani, Madaktari, Wahandisi na Maafisa Tawala hazihitaji uzoefu lakini lazima tutoe changamoto kwa taasisi mbalimbali zinazohusika na jambo hili la ajira, hii hoja si ya kupuuza, lazima ifanyiwe kazi. Kwa sababu ni kweli kwamba ukisoma magazeti, unaona uzoefu miaka 15, uzoefu miaka 20, kama kuna mtu ulishaamua kumpa kazi si umpe bila kutangaza! Ukianza uzoefu miaka 20, uzoefu anafanyia nini huyo? Maana uzoefu wa miaka 15 na 20 ni maandalizi ya kustaafu. Sasa lazima taasisi zetu za binafsi na za Serikali zinazohusika na ajira zione kwamba zina wajibu wa kuwaandaa vijana. Kuna kitu kinaitwa *succession plan* (maandalizi ya kurithishana) hatuwezi kuyafanya kwa kuzungushiana nafasi sisi wote wenye rika moja lazima tukubaliane rika mbalimbali ziwepo. Ndiyo maana taasisi zingine zinafika hatua katika muda ambao zinataka kwenda mbele, unakuta asilimia 90 ya watumishi wake wanastaafu halafu inapoteza mwelekeo kwa sababu hakuna anayejua kinachoendelea, hakuna anayejua kilichopangwa awali, hakuna anayejua mkakati wa maendeleo unatakiwa uende wapi. Wote wana-*retire*, wanabaki tu kuandika barua za kuomba kuongezewa mkataba kwa sababu wao ndiyo wanalijua shirika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengine wamezungumzia haja ya vijana wetu kuheshimu mila na desturi zetu. Nataka nikubaliane nao kwamba tunazo mila na desturi zetu, hatuwezi kuzipuuza hata wenzetu wanazo desturi zao. Wako Waheshimiwa wengine wameandika kwa uchungu sana kuhusu watu wetu kupenda kuvaa *vi-min* bila kuangalia wako wapi. Mheshimiwa Mwenyekiti, *vi-min* ni sketi fupi na ninyi mnajua wenzetu wale wa nchi zilizoendelea, kule kwao kuna baridi sana, wakifika huku wanalazimika kuvaa nguo za namna ile kwa sababu joto linawatesa. Wewe mwenzetu unakuta jasho linakutoka, umevaa nguo ya ajabu, Mbeya huko, wapi, lakini haliwezi kutokuwa jukumu la wazazi. Lazima liwe jukumu la wazazi kujua wapi, unavaa nini, wakati gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nasoma kwenye mtandao wa Facebook, nikakuta Mheshimiwa Mbunge mmoja ana miaka kama 35 hivi, anaalika watu kwenye shughuli yake. Anasema "enyi mabinti wa Vyuho Vikuu vyote mje kwenye shughuli na visketi vifupi". Jamani, wewe Mheshimiwa Mbunge, ona aibu! Ukishakuwa wewe ni Mbunge, wewe ni mzazi, wewe ni kiongozi katika Taifa, chagua vitu unavyoandika kwenye mitandao. Watu wazima wanapokutazama umeandika vitu vya hovyo, mtu uliyechaguliwa na wananchi na hapa unanitazama wakati nasema maneno haya, tafadhali acha! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara mwenzenu nimekabidhiwa ngumu sana, inahusu utamaduni wa nchi, mila zake na maadili yake ambavyo vinapambana na utamaduni wa kimagharibi. Ukifika mahali unasoma vitu vya namna hii, unakuta aliyeandika ni Mbunge, ukitoka hapo unaenda kuomba *Asprin* tu, kichwa lazima kikuume kwamba hii vita tutafanikiwa kweli kama wasimamizi wake ni Waheshimiwa Wabunge! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imetolewa na Wabunge ni kuhusu umuhimu wa kada za watumishi kuajiriwa katika ngazi zinazohusika. Naomba kulitaarifu Bunge lako kwamba tayari utaratibu huu umeanza kufanyiwa kazi na watumishi wa ngazi ya Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, Madereva na Wahudumu wanaajiriwa katika ngazi za Halmashauri kwa utaratibu mpya ambao umeanza na Serikali itafanya kila inavyowezekana kuhakikisha kwamba utaratibu huo unaboresha zaidi ili kwanza, nafasi za ajira zipatikane zaidi kwenye maeneo yanayohusika, maana inapunguza gharama ya Serikali. Pili, watu wanaoishi nao ndiyo wanaowajua. Ukisema leo anatakiwa Dereva wa Mbeya Mjini, anakwenda kufanyiwa *interview* na Tume ya Utumishi Dar es Salaam, hata mtu yeyote mwenye akili timamu akiona mchezo mnaoufanya, anasema hawa jamaa hawajatulia. Kwa hiyo, nasema ni kweli, kama Serikali tumeliona, tumechukua hatua na imeanza kutekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja za vijana kuruhusiwa kupiga kura kuanzia miaka 15 na kugombea nafasi mbalimbali kuanzia umri fulani. Ni bahati nzuri kwamba Tume ya Marekebisha ya Katiba na mjadala wa Katiba utakuja karibuni. Mfanionea sana mkitaka mimi nilijadili hili. Kwa hiyo, nadhani muda wa mabadiliko ya Katiba watu watoe maoni yao yatazingatiwa. Halahala tu msije mkatuletea Rais awe na miaka 16! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni umuhimu wa kuwa na Chuo cha kuandaa vijana bila kujali itikadi. Tunakubaliana kwamba hili ni jambo muhimu sana lakini pia uwezekano wa kuandaa mitaala katika shule zetu za sekondari au za msingi ambayo inaweza kuwaandaa vijana, maana kiongozi siyo lazima uwe umechaguliwa, uongozi unaanzia katika ngazi ya familia, mtu aanze kujijua kuwa ni kiongozi tangu katika ngazi ya familia. Atambue wajibu wake binafsi na wajibu wake kwa jamii yake na kwa Taifa lake. Hili ni jambo ambalo tunaweza kuanza kulitazama ili tujenge Taifa la maana zaidi siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamezungumzia mitandao ya kijamii kama *Facebook, JamiiForum, Twitter, Youtube* kwamba Watanzania ambao wako kwenye mitandao hii wajitahidi kutoa michango yao kwa kuzingatia maadili ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Watanzania wenzetu popote walipo. Kila nafasi unayoipata ya kutumia mitandao hii, utambue kwamba unatoa mchango wako katika makuzi na malezi ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba utoe michango ambayo haina madhara kwa ndugu zako, watoto wako na Watanzania wenzako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vita ya dawa za kulevya tumelielezea kwa kiasi fulani lakini niseme hili ni tatizo kubwa, bado tunalo. Uko utaratibu wa kupambana kwa mujibu wa sheria kwa kukamata na kuchukua hatua zingine. Wizara yetu tunajenga utaratibu wa kuwa na utaratibu na mafunzo na uelimishaji ili watu walione kwamba hili tatizo ni kubwa na waone uwezekano wa kuliacha kwa jinsi ambavyo halina tija kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mkataba kuchelewa, mpaka sasa hivi tukifanikiwa kuridhia mkataba huu, tutakuwa nchi ya 23 kati ya nchi 53. Kwa hiyo, tutaingia kati ya wale watakaopewa heshima ya kuwahi. Nirudie tu kusema, mikataba mingi imekuwa ikichelewa kuja Bungeni kwa sababu ya kupitiwa kikamilifu ili turidhike na maudhui yake. Kwa maana ya Wizara hii, maana ya mimi kuletwa Wizara hii, moja ni kuileta hii mikataba. Sasa, mimi naomba ninapokuwa naleta mikataba msinigonge sana habari ya kuchelewa, mtapunguza kasi yangu ya kuileta maana kazi yangu ni kuitafuta kokote iliko ambayo ina maslahi na nchi yetu. Maana ile ya kwanza miwili, niliileta mwaka jana mkanigonga sana kuchelewa, nimeleta mwingine, naomba mnivumilie nitaendelea kuileta. Ila hii hoja ya kuchelewa jamani mnanipunguza kasi. Naomba mniunge mkono niendeleo kuileta kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni vijana wetu kutozingatia mila na desturi na kutowasikiliza watu wazima. Hili nimeishalizingumzia kwa kirefu, naomba tuendeleo kulifanyia kazi kwa utaratibu ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika, baada ya kujenga hoja kwamba Azimio limechelewa alishauri Bunge liwe linapewa taarifa mara tu baada ya kusainiwa. Jambo hili si baya linaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu alitoa mapendekezo, katika aya ya saba anapendekeza neno "hayakubaliki" liondolewe na neno "hayatekelezeki" liingie katika eneo hilo. Serikali haina pingamizi na jambo hili, tunakubali kwamba tufanye marekebisha hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya ya nane, alipendekeza kuingiza sentensi ambayo inataka Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa masharti ya mkataba huu pamoja na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana. Kama ambavyo nimesema kuna utaratibu wa kuleta mapendekezo ya Marekebisha ya Sheria na haifiki Bungeni kabla Wizara haijashirikiana na wadau katika jambo hili na tusingependa tutumie njia ya mkato katika kulifikia jambo hili. Tunataka tutumie njia ya ushirikishaji ambayo ndiyo utawala bora. Kwa hiyo, Mheshimiwa utuvumilie wakati tunalifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Benki ya Vijana na mawasiliano ya *E-mail* ambapo imeonyesha kwamba kuna watu wanafanya mawasiliano kwamba Benki hii itekwe na CCM. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mnyika kwamba hiyo *E-mail* aliyoipata ni zile ambazo kwenye utalaam wa mle ndani ya *E-mail* wanasema *spam*. Zile *E-mail* za hovyo hovyo ambazo zinatunwa na watu wasiojulikana kwa malengo yasiyojulikana. Kwa hiyo, nenda tu kaifute na ujue haikutoka kokote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuandaa mazingira ya vijana kujitegemea, tutalifanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nirudi tu kwenye hoja ya Vazi la Taifa. Kwanza, naomba niseme Wizara katika kuanza mchakato wa Vazi la Taifa inatekeleza maagizo ya Bunge. Bunge kupitia Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ni mjumbe na kupitia Bunge hili katika michango ya Wabunge ya Bunge lililopita la bajeti, mliagiza mchakato huu uishe. Wizara yangu inatekeleza jambo hili. Hakuna mwaka ambao hakujawa na kilio cha Vazi la Taifa na michango ya wananchi kwenye magazeti na vyombo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaomba tunapotekeleza maamuzi ya Bunge, Wabunge wawe wa kwanza kutuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kamati tuliyoiunda kwa ajili ya jambo hili haijateuliwa na Mheshimiwa Nchimbi peke yake, ni mchakato wa Wizara ambapo Waziri anafanya maamuzi ya mwisho baada ya kupita kwenye mchakato. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba haya majina ninayoyataja ni ya watu makini, siyo suala la ushikaji hapa. Kama mtu anaweza kusema Joseph Kusaga si mtu makini, Ndesambuka Merinyo, Habibu Gunze, Mustafa Hassanali, Kayenga Makwaia, Joyce Mhaviile na Anjela Ngowi, hawa ni watu makini, hamna rafiki yangu hapa. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba nilianza wakati muda bado, kwa hiyo nina dakika kama saba hivi, ninaangalia saa pale.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa, una dakika saba.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumefanya utafiti makini na kupata timu hii. Ila tu tunalo tatizo moja katika nchi yetu ambalo nalo lazima liishe kwamba ukiwa unataka kuteua watu katika Kamati mbalimbali lazima uanze kujiuliza, pale nani adui yake fulani, au ukikaa unateua watu kwa misingi hiyo kwamba kwa sababu fulani ni adui wa Waziri Kivuli, sitamteua, hatuwezi kuendesha nchi, hatuwezi kuendesha nchi. Utakuta mtu amekazana matusi mengi kwenye mitandao "ooh washenzi hawa" na matusi ya nguoni anapiga mle lakini wewe mtu mzima fika mahali tambua mambo ya msingi yenye maslahi kwa nchi yako, siyo ugomvi binafsi, ugomvi miaka 10, ugomvi hauishi! Jamani, tuombe Mungu atusaidie tuache tabia za kubeba visasi. Tabia ya kisasi si ya kiongozi. Wanasema kiongozi makini au mtu *strong* ni yule ambaye anaweza kusamehe. Kama unalala na jambo bila kusamehe, wewe siyo kiongozi. Nawaombeni wote tujenge utaratibu wa kusameheana. Kama mtu alikuudhi mwaka juzi, mwaka jana, msamehe, kiongozi songa mbele, anza upya, hesabu siku kuanzia leo, achana na mambo ya jana. Tusipofanya hivyo, tutakuwa na Taifa la ajabu la watu kununiana, kugombana kila sehemu kuimbiana nyimbo za ajabu, nchi itakwenda kweli! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuwa na mikakati ya dharura ya kusaidia Wamachinga kwa mfano ya kutumia teknolojia ya *shelves* za kisasa mitaani, ni hoja nzuri na nadhani siyo kwenye *shelves* peke yake, inabidi tuitafakari vizuri zaidi ili tuipanue iwe na tija zaidi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu suala la Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi kwa ajili ya kuchunguza yaliyotokea Mbeya, Serikali bado haijaona umuhimu wa jambo hilo, itakapoona itafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameongelea umuhimu wa kuiboresha michezo kuwa sehemu ya uchumi, nakubaliana na michango hiyo, ni jambo muhimu ambalo linaweza kutekelezwa katika nchi yetu. Tukishirikiana, tunaweza kupiga hatua katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu baadhi ya Waheshimiwa wameongea kwa hofu sana kuhusu mkataba huu kama utazingatia sheria zetu mbalimbali, kwa mfano, Sheria za Kiislam. Naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba unapoanza tu na utangulizi wa sheria hii, inasema moja ya mambo ya msingi kwa sheria hii ni kuzingatia sheria zilizopo za nchi husika. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba hakuna sheria iliyopo sasa inayotenguliwa na jambo hili. Kwa hiyo, sheria zilizopo zitaendelea kuwepo na hamasa ya sheria mpya itaendelea kuwepo lakini hatuathiri jambo lolote ambalo lipo tayari kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nitumie nafasi hii kwa mara nyingine kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa michango mizuri sana mliyotupa ambayo imetufikisha hatima ya jambo hili. Kipekee niishukuru Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa ambao imetupa mpaka kufikia hatua hii. Kipekee sana pia nimshukuru Waziri Kivuli, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa ushauri mwingi ambao amekuwa akiutoa nje ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kama nilivyosema awali kwamba kwenye Maazimio hatuendi kwenye hatua ya Kamati. Kwa hiyo, hivi sasa ni kupiga kura tu na kura yenyewe ni ya kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iam uliwe)
(Hoja iliam uliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika
(The African Youth Charter) wa mwaka 2006 liliridhiwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Niwapongeza sana Wabunge, michango ilikuwa mizuri na yenye afya na mimi naamini kabisa kwamba Serikali pengine imepata zaidi ya kiwango ambacho ilitarajia. Maeneo mengine yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge, naamini yatazingatiwa, ukizingatia jambo linalohusu ajira kwa vijana, yote yakizingatiwa tutakuwa tunapunguza matatizo.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 2 Februari, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*